Mzimu wa Kichaa

E. B. Mahelo

Kimechapwa na;

Mahelo Book Centre
S. L. P 10703
Mwanza, Tanzania
Simu: +255 (0) 756 972 099
Barua pepe: info.mbc.2015@gmail.com

© **E. B. Mahelo**

ISBN: 978 – 9987 – 814 – 47 – 3

Hakimiliki © 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kuiga, kunakili, kupiga chapa, kurudufu, kuzalisha nakala au kukitoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila ruhusa ya mwandishi.

Yaliyomo

Utangulizi ..... *iv*

Shukrani ..... *vi*

Sehemu ya Kwanza 1

Sehemu ya Pili 33

Sehemu ya Tatu 105

Sehemu ya Nne 174

Sehemu ya Tano 195

Sehemu ya Sita 216

Sehemu ya Saba 252

Sehemu ya Nane 289

Sehemu ya Tisa 323

Sehemu ya Kumi 330

Sehemu ya Kumi na Moja 338

Utangulizi

Mzimu wa Kichaa ni kitabu chenye hadithi ya kubuni yenye mkusanyiko wa masimulizi yanayohusu ulimwengu wa kawaida wa maisha ya watu na ulimwengu usioonekana kwa macho ya kawaida. Riwaya hii ni ya kipekee kwa kuwa imezungumza mambo ambayo jamii nyingi haziyaweki wazi. Mambo ya uchawi na ushirikina yamefichwa sana, na watu wengi hawapendi kuyajadili kwa uwazi na undani. Mambo hayo yanathibitishwa kuwepo katika maandiko ya kiimani kama vile Koran na Biblia tangu karne na karne na jamii nyingi zinazungumza uwepo wa uchawi, ushirikina na majini.

Kitabu hiki kinasimulia kwa kina jinsi uchawi na ushirikina unavyoleta maumivu na huzuni kwa wanajamii wasio na hatia. Kuna simulizi na matukio ya aina mbalimbali ambayo huonekana ni ya kawaida au bahati mbaya katika jamii, lakini katika kitabu cha **Mzimu wa Kichaa**, utapata picha nyingine adimu usiyoijua kuhusu anga na mifumo ya ardhini, majini na chini ya bahari.

Kina mafundisho mengi ikiwa ni pamoja na mwenendo na tabia njema ya utu, upendo,

ushirikiano na kutokukata tamaa. Miujiza mbalimbali iliyomo itakupa msisimko na kukufanya uelee katika tafakuri ya kina kuhusu maisha na matukio katika ulimwengu halisi na ule wa kimazingara. Utapata maarifa adimu ambayo hayazungumzwi kirahisi katika jamii. Utafurahi, utahuzunika, utashangaa, utakasirika, utatafakari na utapata pia ujasiri katika safari ya maisha yako.

Mtiririko wa masimulizi unakufanya kutaka kujua tukio litakalofuata, hivyo ukianza kusoma kitabu hiki, hutatamani kukiweka chini. Ni kitabu kinachoonesha uwepo wa mambo ya nuru na giza katika jamii, ambayo hasa kizazi cha sasa hakiyafahamu; mambo ya jadi na tamaduni za jamii. Nakuachia jukumu la kufanya uchambuzi wako pia baada ya kusoma kitabu hiki cha kusisimua.

Shukrani

Napenda kukiri kuwa, kukamilika kwa kitabu hiki haikuwa kazi nyepesi naya muda mfupi, bali kwa neema ya Mungu aliye mweza wa mambo yote ikiwemo kunijalia afya njema mimi pamoja na familia yangu, wazazi wangu, ndugu pamoja na marafiki zangu. Pia natambua na nathamini sana ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwa watu mbalimbali hapa nchini akiwemo ndugu Ngenda Frank Sebahene na Dkt. Zena I. Machinda (PhD) kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Mwanza. Si rahisi kuwataja wote kwa majina kutokana na wingi wao, lakini kwa namna ya pekee ningependa kuwashukuru sana mlivyojitoa kwa kunipa ushirikiano mwanzo hadi mwisho wa uandaaji wa hiki kitabu. Mwenyezi Mungu azidi kuwalinda na kuwafanikishia kwa wepesi hitaji la mioyo yenu.

Edwin B. Mahelo
Mwanza, Tanzania.

Sura ya Kwanza

Kijiji cha Kitale ni mojawapo ya kijiji kinachopatikana katika kisiwa cha Upendo ndani ya ziwa Pwezi lililoko Mashariki mwa bara la Afrika. Ukiachilia mbali makazi ya kudumu na ya muda mfupi kwa wanakijiji, shughuli kuu ya kiuchumi ambayo hutamalaki katika kijiji hicho ni uvuvi ambao huendeshwa kwa njia ya asili. Chakula chao cha asili hutokana na kilimo cha mkono kinachoendeshwa na wanawake pamoja na watoto kwani wao huamini kuwa mtaji na utajili mkubwa ni kuzaa watoto wengi ili watumike kama nguvu kazi katika shughuli mbalimbali hasa kilimo.

Mbali na hayo, amani na upendo ni hali inayotawala kwa kiasi kikubwa kwa wakazi wa kijiji cha kitale licha ya kuwa wengi wao wana elimu isiyo rasmi. Mzee Utulivu ni mmoja wapo wa wakazi ndani ya kijiji hicho anaetumiwa na wanakijiji wengi kama mshauri na mtatuzi wa mambo mbalimbali yawahusuyu ingawa hakufanikiwa kupata hata chembe ya elimu ya darasani. Mateso na misukosuko aliyoipitia mzee huyo katika makuzi yake ambayo labda ilisababishwa na maisha duni aliyoyapitia, hakuweza kukata tamaa katika kufanya kazi kwa

bidii na hatimae kumiliki pesa na mali nyingi. Ama kweli shida huleta maalifa.

Ipanga ni mtoto pekee katika familia ya Mzee Utulivu. Sio kwamba hakuwahi kupata watoto wengine, La hasha! Mtoto wa kwanza alikuwa wa kiume ingawa alizaliwa akiwa amekufa. Mtoto wa pili alikuwa wa kike ambaye alizaliwa akaishi kwa muda wa miaka saba kisha akafariki dunia. Chanzo cha kifo chake ni kwamba, alijikwaa kwenye jiwe dogo akadondoka chini kwenye mchanga sehemu iliyo tambarare na kuaga dunia ingawaje mwili wake haukuwa na jeraha lolote. Mtoto wa tatu pia alikuwa wa kike. Yeye alifariki akiwa na miaka minne na chanzo cha kifo chake ni kwamba, aliamka asubuhi mwili mzima hasa mgongoni ukiwa na alama za kuchapwa kwa fimbo, huku nywele zake zote kichwani na nyusi zimenyolewa. Alikuwa analalamika kuwa kuna watu anawaona wanakuja kumchukua, wakati mwingine alijaribu kurusha mikono na miguu akidai wasimshike ingawa wazazi wake waliokuwepo nae, ila walikuwa hawawaoni hao watu. Baadaye ilipofika jioni alifariki ghafla. Mtoto wa nne ni wa kiume ambaye kwa sasa ni kijana, yupo hai na anajulikana kwa jina la Ipanga.

Ipanga aliponea chupu chupu kwani miaka sita baada ya kuzaliwa aliugua sana miguu na mikono hadi kupelekea kushindwa kutembea na kuishi kwa muda wa wiki moja bila kunywa wala kula kitu chochote. Miguu na mikono yake ilikuwa mithili ya mtu aliyeungua kwa mafuta ya moto na hivyo kupelekea vidonda vyake kuvuja majimaji yasiyokauka muda wote usiku na mchana. Wazazi wake walimpeleka zahanati ya Katu iliyo jirani na kisiwa hicho cha Upendo kutibiwa, ikashindikana na baadaye kupelekwa hospitali kubwa ya Geremo kwa matibabu. Kwa miaka miwili hakufanikiwa kupona wala kupata nafuu na hatimaye kuamua kumpeleka hospitali ya kitaifa ya rufaa Muhibi iliyoko Jijini Dazo.

Wazazi wa Ipanga waliamua kufunga safari na kumpeleka kijana wao kwenye hospitali hiyo ya kitaifa ya rufaa kwa uchunguzi zaidi. Walipomfikisha hospitalini hapo alipokelewa na wauguzi ambao walimpeleka moja kwa moja kwa daktari aitwaye Nzoka aliyekuwa katika kitengo cha wagonjwa wa dharura kwa ajili ya uchunguzi kutokana na hali mbaya aliyokuwa nayo Ipanga. Kabla daktari hajafanya chochote kile aliwaomba wazazi wa Ipanga waingie kwenye ofisi ndogo

iliyomo humo kwenye kitengo cha wagonjwa wa dharura na kuanza kuwauliza chanzo cha ugonjwa wa Ipanga. Walianza kumueleza daktari huku wakitoa vielelezo vya zahanati na hospitali alizotibiwa Ipanga bila mafanikio yoyote. Walimueleza kuwa alianza kuwashwa mikononi na miguuni na baada ya wiki vikaanza kutokea vipele vikubwa vilivyojaa maji mfano wa mtu aliyeungua kwa mafuta ya moto. Baadaye, vilianza kupasuka na kuwa vidonda.

Baada ya maelezo hayo daktari aliangalia rekodi za matibabu katika zahanati na hospitali alizotibiwa. Daktari Nzoka aliwaruhusu wakapumzike nje kwenye viti vya wagonjwa, wakisubiri. Daktari Nzoka alimpima Ipanga kila aina ya kipimo alichoona kinafaa ili aweze kunusuru maisha yake kutokana na hali aliyokuwa nayo. Baada ya muda wa saa sita majibu ya vipimo vyote yakawa yametoka ambayo yalimshangaza sana daktari kwani kila kipimo hakikuwa na ugonjwa. Daktari alionyesha sura ya mshangao sana kwa kuwa vipimo vyote vilionesha hakuna ugonjwa. Hali hiyo ilipelekea wazazi wa Ipanga kushituka na kutaka kujua kijana wao anasumbuliwa na nini wakidhani kuna tatizo

limegunduliwa. Daktari Nzoka hakutaka wazazi wajue nini kimejiri katika majibu ya vipimo vya mtoto wao, badala yake daktari aliwaambia kuwa kijana wao hana budi kulazwa.

Daktari Nzoka alimwita muuguzi wa kike na kuamuru Ipanga apelekwe wodini na yeye atawafuata muda si mrefu. Muuguzi alimwamsha Ipanga ambaye alikuwa kishapitiwa na usingizi na kumbeba akisaidiana na wazazi wake wakamkalisha kwenye kitoroli cha kubeba wagonjwa wasiojiweza na kumpeleka wodini. Alipofika wodini alilazwa kwenye kitanda na kusubiri tena maelekezo ya daktari. Baada ya muda si mrefu daktari alifika wodini huku akiongozana na madaktari wenzake watano. Wazazi wa Ipanga walishituka sana kuona jopo la madaktari wanakuja kwa ajili ya kijana wao. Madaktari hao walipofika walimwomba mwuguzi na wazazi wa Ipanga watoke nje ya wodi kwani wana mazungumzo ya faragha. Mzee Utulivu na mkewe walianza kufuta machozi kwa kutumia vidole vya mikono yao huku mwuguzi akiendelea kuwatia moyo wakati huo huo akiwatoa nje ya wodi.

Daktari Nzoka aliufunga mlango wa chumba cha wagonjwa binafsi alipokuwa amelazwa Ipanga na kuanza kujadiliana na madaktari wenzake. “Huyu ndiye mgonjwa niliyewaeleza, majibu ya vipimo vyote haya hapa na hayaoneshi ugonjwa wowote! Hii ndiyo hali iliyonishtua na kunifanya niwaite hapa ili tujadiliane zaidi.” Alieleza daktari Nzoka. Wakajadiliana kwa nusu saa huku wakirejea kumbukumbu mbalimbali za wagonjwa wa aina hiyo, hatimaye mmoja wao akatoa ushauri kuwa wamuache hadi saa nane usiku ndipo warudie tena kuchukua vipimo vingine. Wote wakaafiki kisha wakashauriana kuwa wampatie mgonjwa vidonge aina ya panadol ili apunguze maumivu kwani alikuwa akilalamika sana kila wakati kuwa vidonda vinamwuma sana.

Baada ya muda madaktari wale wakiongozwa na daktari Nzoka ambaye alifungua mlango wa wodi na kutoka nje, wakamwachia mwuguzi maelekezo kuwa aendelee kumtazama mgonjwa kwa ukaribu sana na amwandae kwani saa nane usiku atachukuliwa na kupelekwa maabara kuu kwa ajili ya kuchukuliwa vipimo kwa mara nyingine. Vile vile, daktari Nzoka aliwasihi wazazi wa mgonjwa kuwa watulivu na wajitahidi

kumpatia mgonjwa chakula anachokihitaji. Wazazi wa Ipanga waliendelea kupata hofu ya kumpoteza kijana wao kipenzi na wa pekee anayewafuta machozi kila mara wanapowakumbuka watoto wao wengine waliopoteza maisha. Mzee Utulivu alianza kuwaza moyoni, katika familia yetu tulizaliwa watoto kumi na moja, lakini wazazi wetu walishindwa kutupatia huduma za msingi kama vile elimu, malazi na afya bora. Sio kwamba nawalaumu wazazi wangu kwa kutotupatia hizo huduma, la hasha!, walishindwa kwa sababu tulizaliwa wengi sana na wakashindwa jinsi ya kututimizia hizo huduma kutokana na kipato kidogo walichokuwa nacho. Sasa mimi na mke wangu tuliamua tupate watoto wachache ili tuweze kuwatimizia huduma za msingi, lakini mbona sasa Mungu anatupa pigo hili! Ni kweli yeye ndiye anapenda tukaadhirike kiasi hiki mbele ya jamii na uzee wetu huu?"

Mama Ipanga nae akawa anawaza moyoni mwake, hiki ni kitu gani jamani!, mwanangu ndiye kila kitu kwangu. Nimefunga na kuomba usiku na mchana ili mwanangu asipatwe na chochote kibaya maishani mwake na aweze kuishi maisha ya kumpendeza Mungu aishie juu mbinguni kwani

ndiye kijana wa pekee niliye naye baada ya wenzake kutangulia mbele ya haki.” Wote wawili walijikuta wako kwenye dimbwi kubwa sana la mawazo mithili ya rubani aliyepoteza mwelekeo wa ndege anayoiongoza baada ya kukumbwa na dhoruba ya mvua kubwa inayoambatana na upepo mkali.

Ilipofika usiku wa manane, mwuguzi alikuja kutoka jengo la maabara kuu na kumwamsha Ipanga kisha akamchukua hadi kwenye jengo la maabara kama alivyo amriwa na daktari. Mwuguzi alimwingiza ndani na kumlaza Ipanga kwenye mtambo maalumu na ndani ya dakika kadhaa hivi liliingia jopo la madaktari wanane wakaanza kumwandaa kwa ajili ya kuchukua vipimo. Baada ya dakika chache huku wakiendelea kumwandaa, Ipanga akapitiwa na usingizi. Baada ya Ipanga kusinzia, kila daktari alishughulika kupima kipimo chake hadi saa kumi na mbili alfajiri. Ilipofika saa moja asubuhi, Ipanga alizinduka kutoka kwenye usingizi mzito sana na kujikuta akisafishwa vidonda vyake na daktari ambaye hakumfahamu. Daktari huyo alimsemesha Ipanga akisema, pole Ipanga, unaendeleje kwa sasa?” Ipanga alijibu kwa sauti ya mbali, “ahsante! kuwashwa kumepungua.”

Daktari alimwambia, “usijali, utapona haraka. Naomba nimalizie kukusafisha ukapumzike.” Ipanga akajibu kwa unyonge, “haya.”

Baada ya kumaliza kusafishwa Ipanga alirudishwa wodini akamkuta baba yake akiwa amekaa kitandani akimngoja mwanae kutokana na maelekezo aliyopewa na mwuguzi kuwa ataletwa saa moja asubuhi. Ndani ya dakika chache baada ya Ipanga kufikishwa wodini, mama yake nae alifika huku akiwa na chai kwenye birika lililofungwa kwa ustadi ili lisipoze chai pamoja na vitumbua. Walisalimiana huku kila mmoja akitaka kujua nini kilijiri huko maabara kuu. Ipanga aliwaeleza, Walinifikisha nikalazwa kwenye mtambo ambao hata mimi sikuufahamu ila pande zote nikiwa nimezungukwa na taa nyingi sana na zenye mwanga mkali kiasi. Baadaye waliingia madaktari wanane wakiwa wamevalia mavazi meupe na wamejifunga makofia meupe na kila mmoja alifika na kuanza kufanya alichokifanya kwani wote walikuwa kimya. Ila kuna mmoja tu miongoni mwao alikuja na kibakuli akaniambia nikitemee mate na nikafanya hivyo. Baadaye nilipitiwa na usingizi mzito sana nikalala na niliposhtuka kukawa na daktari ananisafisha na baadaye ndio

kuletwa humu. Baada ya hayo maelezo wote walitulia kwa dakika chache huku kila mmoja akitafakari yake ya moyoni na hatimaye mama Ipanga akamwuliza kijana kama angependa kunywa chai muda ule. Ipanga aliomba apumzike kwanza na kwamba atakunywa chai baadaye na wote walimuacha akawa kapitiwa usingizi.

Ilipotimu asubuhi, Ipanga alizinduka usingizini na kuomba apatiwe chai ili anywe kwa sababu ya njaa kali aliyokuwa nayo. Wakati anaandaliwa chai aliwasihi wazazi wake nao waandae chai wanywe kwa pamoja nao walifanya hivyo huku wakimwongelesha kijana wao maneno ya kumtia moyo. Waliendelea kunywa chai huku wakizungumza na wakati mwingine kucheka kutokana na maneno mbalimbali waliyokuwa wakiyazungumza. Ilipotimu saa nane mchana, Mzee Utulivu aliitwa na mwuguzi akaambiwa kuwa daktari Nzoka anamuhitaji ofisini kwake. Mwuguzi akampeleka Mzee huyo mpaka ofisini kwa daktari Nzoka kisha kumwacha humo. Daktari alimpa pole Mzee kwa mara nyingine na Mzee akashukuru. Baadaye daktari akaanza kumweleza majibu ya vipimo walivyompima mwanae usiku. Daktari akasema, “mzee, tumejaribu kupeleka

wataalamu tunaowategemea kuhusiana na ugonjwa alionao Ipanga ili wampime tuone ni nini kinachomfanya awe hivyo lakini vipimo vinaonesha hana tatizo yeyote. Tumepima kila kinachoweza kusababisha ugonjwa huo lakini kwake hatukuona kitu chochote. Sasa tushauriane kitu, tulitaka kukuandikia barua umpeleke mgonjwa nchi ya mbali kwa uchunguzi zaidi lakini tumeona gharama ni kubwa sana ukijumlisha na gharama za kwetu hapa ambazo unadaiwa. Kama kuna uwezekano, tutume vipimo vikapimwe upya huko kisha watutumie majibu tuone kama wanaweza kugundua tatizo. Kwa huu ushauri unasemaje mzee?" Mzee akajibu, "mimi sina neno ila sijui gharama ninazodaiwa hapa ni kiasi gani na hizo za kutuma vipimo nchi ya mbali ni kiasi gani." Daktari akajibu, "gharama za hapa ziache kwanza ila gharama za kutuma vipimo nchi ya mbali ni milioni kumi na tunapata majibu ndani ya wiki mbili. Milioni tatu tutapata majibu ya vipimo ndani ya miezi mitatu." Mzee akajibu, "kutokana na hali ya mwanangu ilivyo mbaya, naomba tufanye utaratibu wa wiki mbili." Daktari alishangaa sana kwa uamuzi wa mzee na kumweleza kuwa pesa hizo huwa zinalipwa taslimu. Mzee alimuomba daktari ampatie siku tano atakuwa amekikamilisha

kiasi hicho. Basi daktari alimruhusu na kumwambia kuwa kijana wake ataendelea kuwa hapo wodini kwa ajili ya uangalizi zaidi hadi majibu yatakapotumwa.

Mzee Utulivu alirudi wodini akamsimulia mkewe juu ya majibu aliyopewa na daktari kisha akaomba aondoke siku hiyo hiyo akalale kwenye kituo kikuu cha mabasi ili kesho yake aanze safari ya kurudi kijijini kukusanya pesa ili amletee daktari. Ilipofika saa kumi na moja jioni, mzee Utulivu aliruhusiwa na mkewe aondoke kwa ajili ya maandalizi ya safari kesho yake. Mzee Utulivu alimwaga mwanaye na kumwachia mkewe pesa ya matumizi na ziada kisha akaondoka kuelekea kwenye kituo cha mabasi. Kesho yake alipanda basi na kuelekea nyumbani kwake. Siku iliyofuata mzee alifika kijijini kwake na kupokelewa na ndugu, jamaa, marafiki na wafanyakazi wake. Alipata muda wa kupumzika kidogo kwa ajili ya uchovu wa safari aliokuwa nao na ilipofika jioni alianza kuwasimulia kile kilichojiri kuhusu kijana wake kipenzi Ipanga kwani wanakijiji walikuwa tayari wamefika nyumbani kwake kujua kilichojili huko na wengine walikuwa na hofu sana kuona amerudi peke yake.

Baada ya kuwasimulia walipatwa na mshangao sana huku wakijiuliza maswali mengi yasiyo na majibu. Aliwaeleza lengo la kurudi kijijini ghafla hivyo na kumwacha mkewe na mtoto wao huko, ilikuwa ni kutafuta pesa kwa ajili ya matibabu zaidi. Baada ya kusikia hivyo, mwenyekiti wa kijiji aliomba ruhusa na kuondoka kwenda kuchukua ngoma ipigwe kijiji kizima ili kuwakusanya wanakijiji nyumbani kwake. Ilipofika saa kumi na mbili jioni, wanakijiji walikuwa tayari wamekusanyika nyumbani kwa mwenyekiti.

Mwenyekiti wa kijiji cha Kitale alisimama mbele ya umati ule huku akiwa ni mtu mwenye huzuni. Aliwasalimia wanakijiji na aliwatangazia, kwa kusema, “wanakijiji wenzangu, kwanza poleni kwa majukumu! Nimewaita hapa kwa jambo moja tu, wengi wenu mnafahamu kuwa mzee Utulivu hakuwepo hapa kijijini kwa muda sasa na hiyo yote ni kwa sababu ya ugonjwa unaomsumbua mwanae kwa muda mrefu sasa. Mwanae yuko hospitali kubwa huko jijini Dazo anatibiwa na bado hali yake siyo nzuri. Daktari anayemtibu ameshauri vipimo vyake vichukuliwe vikapimwe nchi ya mbali kwa uchunguzi zaidi. Sisi uongozi wa kijiji tumeona si vema suala la gharama za kutuma vipimo huko

limuhusu mzee Utulivu peke yake. Tumeona tuitane hapa ili mwenye kiasi chochote cha pesa achangie ili tumsaidie mwanakijiji mwenzetu. Kwa hili suala ninyi mnasemaje?" Wanakijiji kwa ujumla wao wakajibu, sawa mwenyekiti. Mwenyekiti akaendelea, "sasa utaratibu utakuwa kama ifuatavyo, kesho tutafungua ofisi saa moja kamili asubuhi tukiwa na jukumu moja tu la kupokea michango hadi saa kumi na mbili jioni. Naombeni muwataarifu wote ambao hawajapata fursa ya kuhudhuria hapa kwa muda huu hususani, wenzetu waliokwenda kuchanja kuni na wavuvi ambao bado wako ziwani." Baada ya hapo wanakijiji walitawanyika na kuendelea na shughuli zao na wengine ambao walikuwa hawajaonana na mzee Utulivu walielekea kwake kumsalimu.

Ilipofika kesho yake wanakijiji na watu kutoka vijiji jirani walijitokeza kwa wingi sana kwenye ofisi ya mwenyekiti wa kijiji kwa ajili ya kutoa michango. Walitoa michango na ilipofika jioni wanakijiji walikuwa wamechanga kiasi cha shilingi milioni tatu, laki nane, elfu tisini na tisa mia mbili na hamsini. Mwenyekiti na wazee wawili walizifunga pesa hizo kwa ustadi na kuziweka kwenye mfuko kisha wakaongozana moja kwa

moja hadi nyumbani kwa mzee Utulivu. Wakati huo mzee Utulivu alikuwa akijiandaa tayari kwa kuanza safari kesho yake. Mwenyekiti wa kijiji alimuita mzee Utulivu, "mzee upo?" Mzee Utulivu alijibu, "nipo karibuni na ingieni ndani moja kwa moja." Mwenyekiti na wale wazee waliingia moja kwa moja ndani na kumwomba wamkabidhi kiasi cha pesa kilichochangwa na wanakijiji wenzake pamoja na waliotoka vijiji jirani. Walimkabidhi hicho kiasi cha pesa na akawashukuru sana kwa jinsi walivyojitoa kumsaidia katika wakati huo mgumu alionao. Baada ya kumkabidhi waliomba waondoke ili wampishe aendelee kujiandaa kwa safari ya kesho yake. Mzee Utulivu aliwaruhusu wakaondoka kwani nje alikuwa akisubiriwa na wasimamizi wake wa uvuvi ili apewe taarifa ya maendeleo ya uvuvi pamoja na kukabidhiwa pesa iliyokwisha kusanywa. Mwenyekiti na wazee aliokwenda nao wakaondoka na wasimamizi wake wa uvuvi wakaingia ndani. Kwanza wote kwa pamoja walimpa pole kwa kuuguliwa na kisha kuanza kumpa taarifa ya maendeleo ya kazi inavyokwenda ikiwemo na kumkabidhi pesa iliyokusanywa kwa kipindi chote ambacho hakuwepo. Mzee Utulivu aliwashukuru kisha nao akawaruhusu waondoke ili naye awahi kulala

kwani alipaswa kuanza safari kesho yake alfajiri sana. Nao waliondoka kisha akafunga mlango na kulala.

Kipindi yupo usingizini, mbwa wa Ipanga aitwae Fujo alibweka sana hadi kupelekea mzee Utulivu kushtuka usingizini na alipotazama saa yake ya mkononi akakuta ni saa kumi na moja kamili alfajiri. Fujo ni jina la mbwa wa Ipanga, mbwa wa ajabu, mbwa wa miujiza. Kupatikana kwake kulikuwa kusikoelezeka. Alikuwa mbwa mdogo lakini sasa amekua mkubwa kiasi. Fujo ana rangi ya kahawia na ukubwa wa wastani. Miguu yake ya mbele na ya nyuma imejaa manyoya mengi. Uso wake una manyoya mengi pia. Hakuwa na sura ya kutisha sana ukimzoea, lakini mwanzoni ukimwona lazima upate hofu kidogo. Amezoea kukaa au kujilaza nje, upenuni mwa nyumba wala usingemsikia akibweka ovyo. Kamwe hakuondoka nyumbani kuelekea mahali popote bila kuongozana na mwenyeji wake.

Mzee alijiuliza sana kwa nini mbwa anabweka kiasi hicho, kaona nyoka, mtu au mnyama wa hatari!. Akachukua tochi na kutoka nje kujua nini kinamfanya mbwa kubweka hivyo. Mbwa alipoona mzee Utulivu anafungua mlango na kutoka nje,

akaelekea sehemu anapotengewa maji ya kunywa akang'ata bakuli analowekewa maji ya kunywa na kwenda uelekeo alipokuwa mzee Utulivu kisha akalishusha chini. Ndani ya hilo bakuli kulikuwa na kiasi kidogo sana cha maji, mbwa alinyoosha miguu yake ya mbele akaichovya mara moja kwenye bakuli kisha akalinyanyua na kuanza kupaka yale maji kichwani. Ghafla likamwijia wazo mzee Utulivu kuwa anatakiwa aoge na kuanza safari mapema alfajiri. Baada ya hilo tukio, mbwa alienda pembeni ya mlango akajilaza na mzee Utulivu akaanza kujiandaa kwa ajili ya safari.

Baada ya maandalizi mzee Utulivu alitoka nje tayari kuanza safari lakini kabla hajaondoka mbwa alimsogelea huku akitingisha tingisha mkia wake. Mzee Utulivu alimshika mbwa wake kichwani kisha akaanza safari kuelekea kuvuka ziwa kwa boti ili apande basi la asubuhi kuelekea Jijini Dazo. Alifika ng'ambo ya pili na kupanda basi kisha safari ikaanza. Alifika Jijini usiku sana ila hakuweza kwenda moja kwa moja hospitali kwa sababu asingeweza kuruhusiwa kuingia getini usiku huo. Badala yake alichukua chumba katika nyumba ya kulala wageni iliyoko jirani na hospitali ili kesho yake alfajiri awahi hospitali. Usiku wa manane

alishtuka kutoka usingizini akakuta mlango wa chumbani kwake alipokuwa amelala unatikiswa kwa nguvu sana. Hali hiyo ilimtia hofu sana na kujiuliza kimoyo moyo, nani huyo na mbona anataka kubomoa mlango!. Hatimaye ilibidi aulize kwa sauti ya juu, "nani wewe?" Ile anauliza tu, mlango ukabomolewa na watu watatu waliovalia mavazi ya kufunika nyuso zao wakiacha macho tu wakaingia ndani huku wakimwamuru asipige kelele na alale chini kifudi fudi. Watu wale watatu walikuwa warefu, na wenye nguvu. Mikono yao ilionekana kama imejaa misuli, pengine kutokana na mazoezi ya mwili na misuli ili kuwa imara na nguvu katika uhalifu wao. Mmoja wa wale watu akamwambia kwa sauti ya chini, "ukipiga kelele tu, tunakuua!" Mzee Utulivu hakuwa na budi bali afanye hivyo kunusuru roho yake wakati huo hao watu wakiendelea kumkagua kwenye mifuko ya suruali.

Baada ya dakika chache watu hao walitokomea kusiko julikana na alipoinuka kutahamaki hakuona begi lake lililokuwa na nguo zake pamoja na pesa kiasi cha shilingi milioni kumi na tano. Mzee Utulivu alipiga kelele kwa sauti kubwa ya kuomba msaada jambo ambalo lilisababisha wafanyakazi na

wateja waliokuwemo ndani ya hiyo nyumba ya kulala wageni kuamka na kuingia chumbani kwake. Walishangaa kuona mlango wake umevunjwa na kuanza kumhoji jinsi tukio lilivyotokea. Baada ya maelezo ya mzee Utulivu, mhudumu wa nyumba hiyo ya kulala wageni alipiga simu polisi na ndani ya dakika chache askari polisi wakawa wamefika. Askari polisi waliwahoji mzee Utulivu, wageni vyumba jirani, mlinzi na mhudumu wa nyumba hiyo ya kulala wageni kwa saa moja na dakika kadhaa. Mzee Utulivu aliwajibu huku akitetemeka kuwa wamemwibia begi lake lenye pesa kiasi cha shilingi milioni kumi na tano pamoja na nguo zake. Baada ya hayo maelezo, askari polisi waliomba kuondoka na mzee Utulivu, mhudumu wa nyumba hiyo pamoja na mlinzi wake kuelekea kituo cha polisi.

Wakati wanajiandaa kuanza kutoka nje, wale watu watatu walirudi mbio sana hadi kwenye ile nyumba ya kulala wageni huku wakiomba msaada kwa sauti kubwa kuwa wanang'atwa na mbwa. "Jamani nisaidieni mbwaaa! Ayaaa mbwaaa ananig'ata!" Aliyekuwa amebeba begi alikimbilia miguuni mwa mzee Utulivu kisha akamwambia, "chukua begi lako hili hapa." Mzee Utulivu

akaogopa kulishika begi, huyo jamaa akaliweka chini na wote watatu wakaendelea kugalagala chini huku kila mmoja akilia mbwa ananiua. Mzee Utulivu, askari polisi na wengine walitaka kukimbia kwa jinsi wale jamaa watatu walivyokuja kwa kasi na woga wa kinachoendelea hapo. Baada ya dakika chache askari polisi mmoja alichukua hilo begi na kulifungua kuona kama vitu vya mzee Utulivu vimo vyote ikiwemo pesa. Alivikuta vitu na pesa vyote vipo salama kisha akampatia mzee Utulivu ahakikishe zaidi. Mzee huku akiendelea kutetemeka akalipokea na alipolipokea tu begi lake wale wezi wakatulia na kila mmoja akashangaa sana.

Baada ya muda mchache, askari polisi walimwomba mzee Utulivu ahakiki kila kilichomo ndani ya begi kama kiko sawa na alifanya hivyo na kukuta kila kitu kipo sawa ikiwemo pesa zake. Polisi waliwahoji wale jamaa, “nyie, hao mbwa mmewaona wapi mbona hapa hakuna mbwa?” Mmoja wao akajibu, “mbwa amenig’ata sana ebu oneni alivyoning’ata!” Watu wakaanza kuwatazama hao jamaa na kuwakuta na vidonda vya kung’atwa miguuni, mikononi na mgongoni. Askari mmoja akahoji tena, “hao mbwa wametokea

wapi?" Mmoja wa hao jamaa akajibu, "baada ya kuiba, tumetoka tu nje ya hili jengo tukaanza kufukuzwa huku akibweka sana. Mwanzoni alionekana ni mmoja lakini alipozidi kusogea wakaonekana watatu na kila mmoja akaanza kumfukuza mmoja mmoja." Askari akamwuliza tena, kwa hiyo hao mbwa wameenda wapi?" Jamaa akaendelea kueleza, "tulipoingia tu humu ndani akaonekana tena ni mmoja na amepotea tu ghafla." Mmoja wao kati ya wale askari akawaambia wale wezi, "mkome kuwa na tabia mbaya za wizi zinazowaaibisha na kuwavunjia heshima kwenye jamii. Simameni twende kituoni." Mmoja wa wale vijana akaongea kwa sauti ya upole na unyonge huku akimtazama mzee Utulivu, "Mzee wangu, tusamehe sana, kuanzia leo tumekoma kabisa tabia hii ya wizi. Nasema ukweli toka moyoni mzee, tusamehe na tunaomba tusiende kituo cha polisi."

Hatimaye mzee Utulivu akatulia na kupata nguvu kisha akawaambia wale askari polisi, mhudumu wa hiyo nyumba ya kulala wageni pamoja na wateja wa vyumba vingine kuwa hakika toka azaliwe na hadi sasa ana huo umri hajawahi kuona wala kusikia tukio lililompata na

linamshangaza sana. Pia akawasihi askari polisi wawaachie wale vijana waende zao kwani kikubwa pesa zake amezipata na ziko salama. Baada ya askari polisi kusika maelezo ya mzee Utulivu, waliwasamehe hao jamaa ila wakawaamuru kulipa pesa kwa ajili ya mlango waliouvunja. Walitoa kiasi cha pesa walichoambiwa na mhasibu wa hiyo nyumba ya kulala wageni kisha wakaachiwa na kuondoka huku wote wakiwa wanatembea kwa kuchuchumia. Baada ya hapo, askari polisi nao waliondoka na kurudi kituoni. Mhudumu wa nyumba ya kulala wageni alimhamishia mzee Utulivu kwenye chumba kingine kwa kuwa kile cha kwake kilikuwa kimevunjwa mlango, akapumzika.

Ilipofika alfajiri, mzee Utulivu alianza kujiandaa ili aelekee hospitali kumwona mwanae anayeumwa na baada ya kumaliza kujiandaa alianza safari yake. Alipofika hospitali aliwakuta mke wake na mwanae kipenzi ingawa alikuwa bado amelala. Alisalimiana na mkewe huku wakiulizana habari za kijijini na hospitalini. Mzee Utulivu alimwuliza mkewe, “habari ya maendeleo ya kijana tangu nilipondoka?” Mkewe akamjibu, “hali yake ni ile ile ila amekuwa akikuulizia mara kwa mara kuwa unarudi lini. Nadhani atafurahi sana akikuona leo.”

Baada ya maelezo hayo kutoka kwa mkewe, mzee Utulivu alimwomba mkewe aondoke akaonane na daktari ili amkabidhi kile kiasi cha pesa alichomwambia. Alifika ofisini kwa daktari Nzoka ingawa hakumkuta daktari kwa kuwa mlango wa ofisi yake ulikuwa umefungwa ila nje ya ofisi kulikuwa na mwuguzi amesimama akimsubiri daktari. Mwuguzi akamsalimia mzee Utulivu, “Shikamoo mzee!.” Mzee Utulivu akaitikia, “Marhaba kijana. Daktari hayupo leo?” Mwuguzi akamjibu, “hapana mzee, yupo ila kwa sasa katoka kidogo kaelekea kuwaona wagonjwa wodini. Muda wake wa kurudi umekaribia kwani hata mimi ninamsubiri yeye.” Mzee Utulivu akamwambia, “Ahsante kwa taarifa kijana. Ngoja nami nimsubiri.”

Baada ya dakika kadhaa kupita daktari alirudi ofisini kwake na kuwakuta mwuguzi na mzee Utulivu wanamsubiri. Daktari Nzoka akamsalimia, “Shikamoo mzee Utulivu!.” Mzee Utulivu akajibu, “Marhaba daktari.” Daktari Nzoka akaendelea, “karibuni ila mzee naomba unisubiri kidogo nimhudumie kwanza huyu kijana.” Mzee Utulivu alibaki nje ya ofisi, baada ya dakika chache mwuguzi alitoka ofisini kwa daktari huku amebeba

mafaili kisha akamwambia mzee Utulivu aingie ofisini. Mzee aliingia ofisini na kumkabidhi daktari kiasi cha shilingi za kitanzania milioni kumi. Daktari alizichukua na kuanza kuzihesabu, baada ya kumaliza kuzihesabu alimuomba mzee Utulivu waelekee chumba cha malipo ili daktari akaziwasilishe zile pesa kisha wapewe risiti.

Walipofika katika chumba cha mhasibu walikabidhi kiasi hicho cha pesa na kupewa risiti ambayo alikabidhiwa mzee Utulivu. Waliondoka wote na kuelekea tena ofisini kwa daktari. Wakiwa njiani ilibidi daktari Nzoka amwulize vizuri mzee Utulivu juu ya shughuli anayoifanya kwani sio jambo la kawaida kwa mzee wa kawaida sana kama mzee Utulivu kugharamia matibabu ya namna hiyo tena kwa kulipa pesa taslimu. Daktari Nzoka akamwuliza, “Mzee Utulivu, unajishughulisha na shughuli gani za kiuchumi?” Mzee Utulivu akajibu, “ninavua samaki aina ya furu, sato, dagaa na sangara. Pia ninajishughulisha na kilimo cha mkono kwa ajili ya mazao ya chakula kama vile mpunga, mihogo, viazi vitamu na maharagwe.” Daktari alipatwa na mshangao sana kwa kuona jinsi mzee Utulivu na mkewe wanavyojishughulisha kimaisha. Daktari akasema, “hongera sana mzee na Mungu

azidi kuwatia nguvu. Una watoto wangapi mzee?" Mzee Utulivu akajibu, "mtoto niliye naye ni huyu huyu Ipanga, wengine walishatangulia mbele ya haki." Daktari akajibu kwa huzuni, "pole sana mzee ila Mungu atamsaidia Ipanga na atarudia hali yake nzuri aliyokuwa nayo awali. Tuwe wavumulivu tu kwani baada ya siku tatu tutapata majibu ya tatizo linalomsumbua."

Hatimaye walifika ofisini kwa daktari kisha mzee Utulivu akahitaji kujua pia gharama za hapo hospitalini ili aanze kuzilipa lakini daktari akamweleza asubiri kwanza majibu ya kutoka hospitali ya kimataifa Indosi kisha atamweleza kiasi anachodaiwa. Mzee Utulivu alikubaliana na maelezo ya daktari kisha akaaga na kurudi wodini akamwone Ipanga kwani hakusalimiana nae mwanzoni, alikuwa bado kalala. Alipofika wodini alimkuta Ipanga ameamka na alifurahi sana alipomwona baba yake kisha wakasalimiana huku wote wakiwa na furaha kubwa. Baada ya kusalimiana Ipanga alimwuliza baba yake kuhusu mbwa wake kama yuko salama. Mzee wake alimjibu yuko salama wa afya njema. Baba yake akamwuliza, "unaendeleaje mwanangu?" Ipanga akajibu, "ninaendelea vizuri baba kwani hali ya

kuwashwa sana imepungua ila bado vidonda vinaniuma." Baba yake akasema, "Pole sana, utapona tu haraka. Tuko hapa tunakuhangaikia ili upone mapema." Ipanga akasema, "sawa baba." Waliendelea kuongea mambo mengine mengi huku wakifurahi kwa pamoja wakimliwaza kijana wao mpendwa.

Baada ya siku tatu daktari Nzoka akapita wodini asubuhi kumwona Ipanga kama kawaida yake kisha akamwomba mzee Utulivu waonane ofisini kwake baada ya nusu saa. Ulipofika muda huo mzee Utulivu alielekea ofisini kwa daktari Nzoka na kumkuta yumo ndani. Daktari alimkaribisha kisha akamwomba aketi amsubiri kidogo kuna faili anamalizia kulijaza. Wakati daktari anajaza faili hilo pia alikuwa anafikiria jinsi ya kumweleza mzee Utulivu kwani majibu ya kutoka Indosi yameletwa na kijana wake anaonekana hana tatizo lolote. Ugonjwa alio nao Ipanga unapimwa kwa vipimo vidogo sana na unaonekana lakini vipimo alivyopimwa ni kuanzia vidogo na vikubwa lakini ugonjwa huo hauonekani kwenye vipimo. Masharti ya huo ugonjwa alionao Ipanga ni kupewa dawa kulingana na kiasi cha wadudu waliopo kwenye mzunguko wa damu. Hivyo lazima kwanza

mgonjwa apimwe ili kujua kiasi cha wadudu walioko kwenye damu ndio apewe dawa kwani kinyume na hapo mgonjwa anaweza kupoteza maisha.

Hatimaye daktari alimaliza na kuanza kumwelezea mzee Utulivu juu ya majibu ya kijana wake yaliyotoka Indosi. Daktari akaanza kwa kusema, “pole sana kwa kuuguliwa mzee wangu. Majibu ya kutoka Indosi yamekuja ila bado yanashangaza kwani bado ugonjwa hauonekani. Tulivyotuma vipimo, tulituma pia na picha ya kijana jinsi anavyoumwa lakini na wao imewashangaza sana kutokuona ugonjwa kwenye vipimo. Ilibidi waitane madaktari bingwa watano wa magonjwa ya namna hii, walikaa kikao na kuamua kuvipima tena mara ya pili lakini hawakuona tatizo lolote. Ilifika hatua wakapima magonjwa yote yanayopatikana kwenye damu, mate, haja ndogo na haja kubwa lakini vipimo vyote vinaonesha hakuna tatizo lolote. Lakini baada ya kupata haya majibu tuliitana tena kuyajadili na tulifikia mwafaka kuwa kuna madaktari wawili wanakuja mwezi ujao toka Chibu kwa ajili ya kutembelea na kutibu wagonjwa walioko katika hospitali kubwa kama hii hapa nchini. Watakaa

kwa muda wa miezi mitatu, hivyo tumesajili jina la kijana wako ili naye awe kwenye orodha ya kukutana nao." Wakati daktari anazungumza maneno hayo huku akimwonyesha vielelezo vya upimaji wa mwanae nje ya nchi, mzee Utulivu alikuwa akimsikiliza kwa makini sana huku akiashiria kuishiwa nguvu mwilini. Daktari Nzoka akamwuliza, "Unaonaje kuhusu wazo hilo mzee wangu?" Mzee Utulivu akajibu, "Ni sawa daktari." Daktari aligundua kuwa mzee hakuwa sawa baada ya kupokea majibu hayo. Alijitahidi sana kumwelimisha na kumtuliza ili hilo jambo alipokee kama la kawaida na juhudi kubwa inafanywa na madaktari pamoja na uongozi mzima wa hospitali hiyo ili kuokoa maisha ya kijana wake mpendwa.

Daktari Nzoka aliendelea kumweleza, "Mzee wangu, kwa sasa itabidi niwaruhusu mwende nyumbani lakini utamrudisha tena kijana hapa hospitalini baada ya siku ishirini na nane ili apewe kitanda tayari kwa kukutana na hao madaktari kutoka nchini Chibu. Ila nitakupatia dawa ya kumwogeshea na kumpaka asubuhi na jioni kila siku. Pia nitakupatia vidonge vya panadol kwa ajili ya maumivu. Jitahidi sana asimeze vidonge vya aina yoyote ile isipokuwa panadol tu." Mzee

Utulivu akajibu, “Sawa daktari nitajitahidi. Gharama za hao madaktari kutoka Chibu ni shilingi ngapi na kwa sasa nadaiwa shilingi ngapi toka tumekuwa hapa hospitalini?” Daktari Nzoka akamjibu, “Tumekaa na uongozi wa hospitali na tumekubaliana usitoe gharama zozote zile tofauti na gharama ya kufungulia faili ambayo mliitoa siku mnafika hapa hospitalini. Pia hao madaktari kutoka Chibu wanagharamiwa na uongozi wa hospitali pamoja na serikali.” Mzee Utulivu akajibu, “sawa daktari, nimekuelewa na ahsante sana kwa msaada wako mkubwa toka tumefika hapa hospitalini.” Daktari akamwambia, “Usijali mzee wangu, huo ni wajibu wangu kuhakikisha kijana anapona haraka.” Mzee Utulivu akauliza, “Tunaweza kuondoka leo?” Daktari akajibu, “Ndiyo mzee wangu. Ila baada ya saa moja nitakuja wodini kukuletea hizo dawa na kumwaga kijana pamoja na mama.” Mzee Utulivu akajibu, “Sawa daktari. Ngoja tukajiandae ili jioni tuelekee stendi ya mabasi.”

Mzee Utulivu alirudi wodini na kumwambia mkewe kilichojiri huku wakizungumza kwa makini sana ili kijana wao asijue juu ya utata mkubwa wa vipimo vya ugonjwa anaoumwa. Baada ya hayo mazungumzo mzee wake alimsogelea Ipanga na

kumweleza kuwa daktari amempatia dawa na kuwaruhusu waende nyumbani na watarudi tena baada ya siku ishirini na nane. Kijana wao alifurahi sana kusikia taarifa hiyo na kuanza kuwaeleza wazazi wake kuwa amepakumbuka nyumbani kwao hasa mbwa wake aitwaye Fujo. Alipokuwa akiendelea kuwaelezea, mara daktari Nzoka akagonga mlango kisha akaufungua na kuingia ndani huku ameshikilia dawa mkononi mwake na kumkuta Ipanga akielezea huku akionekena na uso wa furaha sana. Daktari akamwuliza, "Ipanga, mbona leo umefurahi sana?" Ipanga akajibu, "Baba kasema tunakwenda nyumbani leo." Daktari na wazazi wa Ipanga kwa pamoja wakatabasamu. Daktari akaendelea, "Umepakumbuka sana nyumbani?" Ipanga akajibu, "Ndiyo, nimepakumbuka." Basi daktari akamwambia Ipanga kuwa ni kweli ameruhusiwa kwenda nyumbani na atarudi tena hospitalini hapo baada ya siku ishirini na nane. Akamkabidhi mzee Utulivu dawa za kijana wao na utaratibu jinsi ya kutumia kama alivyomweleza awali kisha akawaaga na kuwatakia safari njema.

Ilipofika jioni, Ipanga alibebwa mgongoni na baba yake huku mama yake akibeba mizigo

mingine hadi stendi ya taksi wakitokea hospitalini. Walikodi taksi na kuelekea stendi ya mabasi na kulala hapo. Kesho yake alfajiri walipanda basi na kuanza safari kurudi nyumbani. Walifika jioni wakavuka mto kwa kutumia boti na kufika kijijini kwao Kitale na kupokelewa na wanakijiji wenzao. Wanakijiji walisaidiana kumbeba Ipanga hadi nyumbani kwao kwani kwa ugonjwa wake alikuwa hajiwezi kutembea wala kujisogeza. Walipofika nyumbani kwao Ipanga alifurahi sana wakati huo mbwa wake alionyesha hali ya furaha pia huku akitaka aje karibu kwa Ipanga aliyekuwa amekalishwa kwenye kigoda kilichowekwa chini ya mti wa mwembe ili apate hewa nzuri lakini aliogopa umati wa wanakijiji waliokuwa tayari wameanza kuja kuwasalimia wazazi wa Ipanga na Ipanga mwenyewe. Wanakijiji wengi walishangaa sana upole wa huyo mbwa kwani sio kawaida yake kuwa mpole vile sababu huwa ni mkali sana. Baada ya muda mchache wanakijiji walitawanyika kwa ahadi ya kurudi kesho yake kuwajulia hali kwa mara nyingine. Wanakijiji walipoondoka, mzee Utulivu na familia yake wakapata chakula cha usiku kisha wakapumzika.

Kesho yake wanakijiji waliendelea kumiminika nyumbani kwa mzee Utulivu ili kuwasalimia na kujua zaidi hali ilivyokuwa huko hospitalini. Ilipofika saa nane baada ya kupata chakula cha mchana, mzee Utulivu alianza kuwaeleza baadhi ya wazee wenzake na wengine waliokuwepo hapo jirani jinsi majibu ya vipimo vya kijana wao kutoka Indosi yalivyokuwa. Kila mmoja alipatwa na mshangao mkubwa na kuwaza ni tatizo gani hilo ambalo halionekani kwenye vipimo. Mzee Utulivu alipomaliza kuwasimulia kila mmoja alimpa pole na wengine waliaga kuondoka kuendelea na shughuli zao. Maisha ya Ipanga yaliendelea kuwahuzunisha wazazi wake na wanakijiji wenye mapenzi mema kwa muda mrefu sana.

Sura ya Pili

Siku moja majira ya asubuhi, Ipanga alitolewa nje na kukalishwa kwenye kigoda chini ya mti wa mwembe ambapo alikuwa anapenda kupumzika yeye mwenyewe. Mama yake akamuaga na kwenda kuchimba viazi vitamu kwa ajili ya chakula cha mchana. Baada ya dakika chache tena, baba yake pia akamuaga na kwenda kumtafutia maziwa ya mgando kwani siku hiyo Ipanga aliomba kula viazi vitamu na maziwa ya mgando wakati wa mchana. Baba yake aliondoka na kusahau kumfungia mbwa chini ya mti uliopo nyuma ya nyumba anapofungiwa siku zote. Baada ya muda mfupi, Ipanga akapitiwa usingizi akiwa amekaa kwenye kigoda huku kaegemea mti wa mwembe. Fujo alikuja taratibu na kuanza kulamba vidonda vya Ipanga akianzia mikononi.

Ipanga alishituka kutoka usingizini na kumkuta mbwa wake akimalizia kumlamba mguu wa mwisho. Ipanga alimfukuza mbwa kwa sauti ya mdomo kwani hakuweza kunyanyuka wala kushika kitu ampige nacho. Mbwa wake alisogea pembeni yake kidogo na kujilaza chini kwenye ardhi huku akimtazama Ipanga. Ipanga aliendelea kujiuliza kwa nini huyu mbwa kamlamba kisha

akapuuza na kuachana na hilo wazo. Baada ya dakika kadhaa Ipanga akaanza kuhisi muwasho na maumivu kwenye vidonda yanapungua. Wakati huo mbwa wake bado kajilaza na huku akiendelea kumkazia macho Ipanga. Baada ya dakika kadhaa tena, maumivu na muwasho wa vidonda vya Ipanga vikaisha kabisa, Ipanga akapata nguvu ya ajabu sana na maji maji kwenye vidonda yakakauka. Akajaribu kuinua juu mkono wake wa kulia ukakubali, wa kushoto ukakubali, akainyoosha miguu yote ikakubali. Akajaribu kunyanyuka asimame, akaweza na kuanza kutembea. Mbwa wake nae akasimama na kuanza kufurahi na kumsogelea Ipanga huku akichezesha mkia wake.

Ipanga alifurahi sana na kujiuliza ni miujiza gani iliyompata. Akataka kumwuliza mbwa wake akashindwa kwani mbwa hawezi kuongea. Ikabidi aingie ndani na kuchukua kitenge kingine ajifunike. Mara tu alipotoka nje akamwona baba yake akiwasili nyumbani. Baba yake alipomwona Ipanga anatembea akataka kukimbia arudi alikotoka huku moyo ukimwenda mbio sana. Alivumilia sana na kujikaza kutokana na sauti ya mwanaye alivyokuwa na furaha ingawa naye furaha yake

ilikuwa furaha ya mshangao mkubwa. Baba yake akamsogelea mwanaye kwa kunyata huku suruali yake ikiwa imeloa mkojo uliopita ghafla kwa ajili ya mshituko pamoja na maziwa yaliyomwagikia baada ya jagi alilokuwa amelishikilia kudondoka chini na maziwa kumrukia. Alimshika mwanaye mkono na wote wakakaa chini kwenye vumbi kwa sekunde kadhaa bila kuzungumza chochote huku baba akimtazama mwanaye kwenye vidonda vilivyokauka.

Walipokuwa wanajiandaa kunyanyuka wakae kwenye viti, ghafla mama yake Ipanga naye akafika nyumbani akitokea shambani kuchimba viazi vitamu alivyokuwa amejitwisha kichwani. Ipanga alipomwona mama yake, alinyanyuka na kumkimbilia akampokee, mama yake alishangaa kuona kijana ananyanyuka na kumkimbilia. Alipiga kelele ya mshituko mara moja na kudondoka chini kisha akapoteza fahamu. Mzee Utulivu alijikaza na kunyanyuka haraka kwenda kumpepea mkewe kwa kutumia shati lake alilolivua. Baada ya sekunde kadhaa alimwambia Ipanga aendelee kumpepea mama yake ili yeye akawaite majirani wamsaidie.

Mzee Utulivu alikimbilia ndani kwake kuvaa suruali nyingine na shati kisha akakimbia kwenda kwa majirani zake ambao nyumba zao ziko mbalimbali kidogo ili kuomba msaada. Wakati Ipanga akiendelea kumpepea mama yake, Fujo alikuja kwa kasi sana akitokea nyuma ya nyumba yao na kuanza kumlamba mama yake Ipanga nyayo zake za miguuni mara moja kisha akasimama pembeni ya Ipanga. Kile kitendo cha mbwa kumlamba mama yake Ipanga kilikuwa cha kushitukiza sana ambapo kutahamaki Ipanga anataka kumfukuza, mbwa alikuwa amemaliza kumlamba. Mzee Utulivu akafika kwa jirani yake mmoja huku akihema sana na kuwakuta majirani zake wengine wapo hapo wanazungumza. Mzee Utulivu akasema kwa hofu "Jamani!, jamaaan! Msaada nyumbani kwangu." Wakakimbia wote kuelekea nyumbani kwa mzee Utulivu huku wakidhani hali ya Ipanga imebadilika na kuwa mbaya. Wote kwa pamoja walikimbia kwa kasi akiwemo mzee Utulivu kuelekea nyumbani kwa mzee Utulivu na kumkuta Ipanga akiendelea kumpepea mama yake. Wale majirani walipomwona Ipanga ambaye alikuwa ni mgonjwa hajiwezi anafanya kazi ya kumpepea mama yake

wakasimama ghafla na kurudi mbio walipotoka huku wakipiga kelele.

Mzee Utulivu alihisi kuchanganyikiwa huku akitafakari nini cha kufanya baada ya kukimbiwa na majirani zake ambao alitegemea msaada kutoka kwao. Wakati akitafakari ghafla mkewe akazinduka na kufumbua macho na kuanza kuwatazama. Kila mmoja aliendelea kupigwa na butwaa asijue nini cha kufanya. Baada ya dakika chache, Ipanga alimwita mama yake kisha mama akaitika na kunyanyuka na wote wakakumbatiana huku wakimtazama kwa wasiwasi Ipanga. Walipomaliza wakaelekea ndani huku mzee Utulivu akionekana kutembea kwa kuchechemea kwani mguu wake ulishituka alipokimbia kwa kasi kwenda kuwaita jirani zake. Wote waliingia ndani sebuleni na kukaa kwenye viti wakati huo wazazi wake Ipanga wakiwa na shauku ya kutaka kujua nini kimetokea hadi akaanza kutembea wakati huo zimebaki siku nne warudi hospitali.

Kabla hawajaanza kumwuliza, majirani walianza kuja mmoja mmoja kwa kunyata na kuchungulia mithili ya mtu anayeingia kwenye nyumba aliyomo nyoka mwenye sumu kali. Baba yake akaanza kumwuliza, “Mwanetu, hebu twambie kwa maana

hadi sasa hatujui nini kimetokea ama kimekukuta hadi umeanza kutembea na vidonda vyako kukauka ghafla kiasi hiki." Mama yake akaongezea, "Ipanga, tuelezee vizuri kwani hadi sasa tunaona ni miujiza hii." Ipanga akajibu, "Hata mimi bado siamini kama ni mimi. Mliponiacha nimekaa hapo nje kwenye kigoda nimeegemea mti wa mwembe, nilipitiwa na usingizi mzito sana. Ila ghafla nilishituka na niii…kaaaa…ooooo…! Naombeni kwanza nilale nahisi usingizi mzito sana." Ghafla Ipanga akasimama na kuelekea chumbani kwake kulala. Wazazi wake na majirani waliokuwa wamefika walijiuliza sana ila hatimaye wakakubaliana wamwache kwanza apumzike atawaambia baadaye. Wote walibaki wakitazamana wasiwe na hata cha kuongea kwa muda huku kila mmoja akiwa na mtazamo na mawazo yake.

Baada ya muda mfupi walikuja wanakijiji kadhaa kujua habari kamili juu ya Ipanga baada ya habari kuanza kusambaa. Wanakijiji walipofika, wazazi wa Ipanga na majirani zao walitoka nje na kuwakaribisha huku wamepooza kama vile wamenyeshewa na mvua ya mawe. Wanakijiji wakiongozana na mwenyekiti wa kijiji pamoja na baadhi ya wazee walichukua viti na kuketi huku

akili na masikio yao yote yakiwa kwa wazazi wa Ipanga wasikie kilichojiri lakini macho yao wakiangaza huku na kule wamwone Ipanga. Baba yake Ipanga alipokuwa akijiandaa kuanza kuwasimulia kilichojiri, mara kukasikika kishindo kidogo cha watu wakifukuzana kutokea nyuma ya nyumba kuja uelekeo wa walipokaa karibu na kona ya nyumba. Kile kishindo kilipokaribia kwenye kona ya nyumba ghafla baadhi ya wanakijiji wakiwemo jirani zake mzee Utulivu wakakimbia na wengine kuanguka ovyo kwenye viti, kile kishindo kilipokuja kutokeza wakawa ni bata wakubwa wawili wa jirani yake mzee Utulivu ndio wanafukuzana. Wale wanakijiji huku kila mmoja akirudi kukaa mahali pake wakaanza kutazamana usoni kwa aibu. Mzee Utulivu akawapa pole akisema hiyo yote ni tafrani iliyosababishwa na kijana wao Ipanga.

Mzee Utulivu alianza kuwasimulia jinsi ilivyokuwa kuhusu kijana wao ingawa ukweli kamili jinsi alivyopona bado haujajulikana kwani mara tu kijana alipotaka kuwasimulia akapatwa na usingizi mzito na bado kalala hadi muda huu. Wazee wenzake walimshauri mzee Utulivu amwache kwanza kijana apumzike ila awe

anamwangalia kwa ukaribu kuona maendeleo yake. Naye alikubali kisha wakaaga na kuondoka. Ilipofika alasiri, Ipanga aliamka na kuomba chakula kisha akala huku akiwa ni kijana mwenye nguvu na furaha tele. Baada ya kumaliza kula alimpelekea rafiki yake Fujo chakula naye akala kisha akaomba maji ya kuoga ili akajioshe mwenyewe kitendo ambacho hajawahi kukifanya kwa muda wa miezi kadhaa. Mama yake alimwandalia maji ya kuoga, akaingia bafuni na kuanza kuoga mwenyewe.

Baada ya kumaliza kula chakula cha usiku walimwuliza tena ili awaelezee ilivyokuwa, alipotaka kuanza kuwaelezea ghafla alipatwa tena na usingizi mzito na kuomba akalale kidogo. Walimruhusu akalala na hata hakuweza kuamka kwa ule muda aliowaahidi kuamka awasimulie. Ilibidi wamwache tu aendelee kulala huku wakiwa wanamwangalia mara kwa mara wanaposhtuka usingizini. Ipanga alishtuka usiku wa manane na kuanza kutafakari mwenyewe kwa jinsi alivyokuwa anaumwa hadi akapona. Alijua fika kuwa kupona kwake kumesababishwa na mbwa wake, lakini kwa nini mbwa ndiye amponyeshe na huyo mbwa alikuwa na nini. Aliwaza jinsi alivyompata huyo mbwa akiwa mdogo na kuanza kumfuga. Alikuwa

akicheza peke yake nyuma ya nyumba hapo kwao kabla hajaanza kuugua. Alicheza kwa kutumia vijiti na kamba za katani kwa muda wa masaa kadhaa.

Muda wote huo mazingira ya nyumbani kwao yalikuwa matulivu sana kwani hapakuwa na kelele ya aina yeyote ile isipokuwa sauti za ndege kwa mbali. Mama yake alikuwa kalala kwenye mkeka mbele ya nyumba na baba yake hakuwepo kwani alikuwa amekwenda kuangalia maendeleo ya vijana wake wanaomvulia samaki. Alipokuwa akicheza akili ilimwambia atazame nyuma yake. Alipotazama nyuma yake aliona mbwa mdogo amejilaza karibu yake huku akimtazama. Ipanga alishtuka na kumfukuza huyo mbwa lakini kila alipokuwa akimfukuza mbwa alikwenda mbali kidogo kisha alirudi kujilaza. Hatimaye mama yake Ipanga akasikia mwanaye anamfukuza mbwa, akanyanyuka kisha akaenda kumtazama huyo mbwa. Alipomwona akamwambia mwanaye amuache ataondoka mwenyewe kisha akamchukua wakarudi mbele ya nyumba kukaa. Wakiwa wamekaa, akili yote ya Ipanga ikahamia kwenye mbwa. Akaingia jikoni kuchukua mabaki ya chakula akampelekea kwa kujua kwamba labda anahisi njaa na anatafuta chakula. Alipompatia

chakula huyo mbwa hakuonyesha kukijali, Ipanga ilibidi amwache. Mbwa akaendelea kuwepo pale nyumbani kwa siku kadhaa mfululizo na kupelekea Ipanga kumzoea na kuanza kucheza naye. Baba yake alichukua jukumu la kutangaza kijiji kizima aliyepotelewa na mbwa mdogo aende kumchukua kwani yupo kwake bila mafanikio.

Hatimaye, Ipanga alijimilikisha mbwa huyo na akampa jina Fujo kwa sababu katika kucheza kwake na wakati mwingine kukimbizana na mbwa huyo alionekana kutopenda fujo. Hivyo hadi leo Ipanga hajui huyo mbwa alitokea wapi na hadi sasa ni mkubwa na amekuwa mlinzi mzuri wa familia pamoja na mali zao. Baada ya kufikiria hayo pasipo majibu yoyote, Ipanga aliamua kuyaacha na kusinzia hadi asubuhi alipoamshwa na baba yake amsalimie alipotaka kwenda kuangalia mavuno ya dagaa waliovuliwa usiku huo. Baada ya siku tatu wazazi wa Ipanga walipanga na kuamua wasimpeleke kijana wao hospitali kwani watakapofika hospitali itakuwa vigumu kwao kumweleza daktari jinsi kijana wao alivyopona kutokana na hali mbaya aliyokuwa nayo Ipanga. Wakati wakijadili hayo zilikuwa zimebaki siku nne kukamilika siku ishirini na nane walizopewa na

daktari ili wamrudishe Ipanga hospitali aonane na madaktari kutoka Chibu. Kadri siku zilivyokwenda mbele, wazazi wa Ipanga walizidi kufurahi kwani afya ya kijana wao ilizidi kuimarika.

Siku moja mchana mama yake Ipanga akiwa kwenye mwamba anaponda udaga uliotokana na mihogo ili apate unga, sauti ilimwijia ikamwambia, “Endelea kumuomba sana Mungu kila wakati bila kuchoka kwani binadamu wenye roho mbaya hawapendi kuiona familia yako ikiwa na furaha hata kidogo. Pia mpelekeni kijana wenu shule aanze kusoma.” Kisha ile sauti ikapotea. Mama Ipanga alishangaa sana na kuogopa kutokana na sauti na maneno aliyoyasikia. Akamwuliza jirani yake aliyekuwa pembeni yake akimsaidia kuponda udaga kama amesikia sauti yoyote ile. “Jirani, umesikia nini muda si mrefu?” Jirani akamjibu, “hapana jirani, sijasikia chochote kile ila nimekuona wewe umeduwaa. Kwani nini kimetokea ama umepatwa na shida gani?” Mama Ipanga akajibu, “Hapana jirani, tuendelee tu na kuponda udaga.” Mama Ipanga alijiuliza maswali mengi sana moyoni mwake, “Hii ni ndoto? Kama ni ndoto, mbona sikupitiwa na usingizi hata kidogo?” Lakini hakuwa na majibu. Baada ya kumaliza kazi zao,

mama Ipanga alimshukuru jirani yake kwa kumsaidia kisha kila mmoja akaelekea kwake. Sauti na maneno hayo ya kushangaza yalimtesa mama Ipanga kwa muda mrefu sana na hakuweza kumwambia mumewe mzee Utulivu kwani alishindwa aanzie wapi. Lakini jambo lililomjia kichwani mwake wakati wote huo ni la kumuomba Mungu hususani kimoyo moyo na alifanya hivyo bila kuacha kila alipokuwa akipata nafasi ya utulivu.

Afya ya Ipanga iliendelea kuimarika zaidi na zaidi kwa muda wa miezi michache tu, jambo lililowafanya wazazi wake kukubaliana kwenda kumwandikisha shule ya msingi ili aanze kusoma darasa la kwanza ingawa alikuwa na miaka tisa. Kwa kawaida alitakiwa kuandikishwa darasa la kwanza akiwa na miaka saba lakini ilishindikana kwa sababu ya ugonjwa aliokuwa akiugua kwa muda mrefu. Wazazi wa Ipanga walimpeleka mtoto wao katika shule ya msingi Dodo kumwandikisha ili aanze kusoma darasa la kwanza. Ipanga na wazazi wake walipofika shuleni walipokelewa na walimu kwa furaha kubwa sana kwani wengi wao wanaifahamu vizuri familia hiyo. Licha ya hayo, walimu walivutiwa sana na Ipanga kutokana na

kujibu maswali vizuri waliyokuwa wakimwuliza kama usaili wa kumwandikisha darasa la kwanza. Walipokamilisha usajili wa kijana wao wote walirudi nyumbani kwa maandalizi rasmi ya kijana wao kwani alitakiwa kuanza shule kesho yake.

Ipanga alianza masomo na maendeleo yake yakawa mazuri kwani kila mitihani aliyoifanya alishika namba moja darasani. Siku moja Ipanga akiwa darasa la tano, yalitokea malumbano kati ya wanafunzi wawili (Iba na Ibe) wa darasa alilomo Ipanga, huku kila mmoja akimtambia mwenzake kuwa hamwezi. Malumbano hayo yalianzia darasani kipindi cha kujisomea halafu yakaendelea kipindi cha mapumziko huku kila mmoja akiwa na wapambe wake. Ipanga na rafiki zake akiwemo Masha waliendelea kuwashangaa huku wakila viazi vilivyokaushwa maarufu kama michembe, mbute pamoja na kabaragara walizonunua kutoka kwa akina mama wanaochuuza hapo shuleni kipindi cha mapumziko. Masha ni mvulana wa rika moja na Ipanga. Ipanga na Masha walitokea kuwa marafiki sana. Masha ni mrefu wa wastani, maji ya kunde mwenye macho ya wastani na masikio makubwa. Masha ni kijana mwerevu na pia mwenye kujimudu darasani. Wazazi wa Ipanga

walimfahamu Masha vizuri kwani baada ya kuanza urafiki wao, walikuwa wakitembeleana.

Hatimaye kengele ya kuingia darasani iligongwa na wote walielekea darasani huku malumbano yakiendelea. Wakiwa darasani kabla mwalimu wa kipindi kuingia, Iba na Ibe walikubaliana wakaonyeshane ufundi wao jioni baada ya kutoka shule na wakutane eneo la Itongo. Itongo ni eneo ambalo lipo kando kando ya ziwa, pembeni sana mwa kijiji cha Kitale na lenye mawe na miamba iliyotoka nchi kavu hadi ziwani. Pia kuna miti mikubwa inayofanya ndege kama bata maji, tai na wengineo kujenga viota vyao pamoja na makazi ya wanyama kama fisi maji, nyoka (chatu, kijani, weusi, koboko, swila n.k), mijusi, kenge, n.k. Serikali ya kijiji cha Kitale ilikuwa imekwishawatangazia wanakijiji kuwa eneo hilo ni hatari sana kwa maisha yao, wasipendelee kwenda eneo hilo ingawa lilikuwa lina sifa ya kupatikana samaki wengi sana aina ya sato, mumi, kamongo na sangara. Na hata kama wanakijiji wanataka kwenda eneo hilo, watembee wakiwa watatu kwa pamoja au zaidi kuepuka kushambuliwa na wanyama wa hatari.

Iba na Ibe walisitisha malumbano yao baada ya mwalimu wa somo la uraia kuingia darasani na kuanza kufundisha. Vipindi viliendelea na ilipofika saa nane na nusu kengele ya usafi iligongwa na wanafunzi wote walitoka darasani na kwenda kufanya usafi maeneo waliyopangiwa chini ya usimamizi wa viranja wao. Wakiwa nje wanafanya usafi, Masha alikwenda kwa Ipanga na kumkuta anafanya usafi eneo lake. Masha akauliza, “Ipanga, nasi tutakwenda kuwatazama Iba na Ibe?” Ipanga akamjibu Masha kwa mshangao, “Mbona msichana anaweza kupigwa na kuumizwa!” Masha akamjibu, “Hawaendi kupigana ila wanakwenda kuoneshana ufundi na kuona nani anamzidi mwenzake ufundi.” Ipanga akahoji, “Ufundi gani huo wanaokwenda kuoneshana?” Masha akajibu, “Sijui ni ufundi gani, ningependa kuona nini kitajiri.”

Baada ya maelezo hayo, Ipanga naye akashawishika kujua nini kitajiri huko Itongo. Ipanga akauliza tena, “Rafiki zetu wengine wanasemaje juu ya jambo hilo?” Masha akajibu, “Wamekubali na ndio maana wameniambia nije nikuulize na wewe unasemaje.” Ipanga akahoji, “Nyumbani tutaaga tunakwenda wapi ilhali wazazi wanasema eneo hilo linatisha?” Masha

akasisitiza, “Hapo kweli ni mtihani!” Ipanga akatoa wazo, “Nimekumbuka, tuage twende kwa mwalimu anayetufundisha masomo ya ziada na tukifika kwake tumwombe asitufundishe badala yake atupe maswali tukafanyie nyumbani. Ila tumwambie kuna sehemu tumeagizwa ili aturuhusu mapema twende. Unalionaje hilo wazo?” Masha akatikisa kichwa na kusema, “Ni wazo zuri. Ninaomba niende nikawaeleze na wenzetu.” Ipanga akajibu, “Sawa Masha.” Masha aliwatafuta haraka haraka rafiki zao wengine akawaeleza wazo kutoka kwa Ipanga na wote wakaafiki.

Kengele ya kutawanyika kwenda nyumbani ilipigwa na wanafunzi wote wakajipanga mstarini na baadaye mwalimu wa zamu akawatawanyisha kuelekea nyumbani kwao ingawa wengi wao walio darasa la tano walikuwa na shauku ya kwenda kuona nini kitajiri kwa wale waliokuwa wakitambiana. Ipanga na rafiki zake walikutana kabla ya kutawanyika na wakakubaliana wakabadilishe nguo na kula haraka haraka ili wakutane kwa mwalimu anayewafundisha masomo ya ziada na safari yao itaanzia hapo ili wawahi kurudi nyumbani. Ipanga alifika nyumbani kwao akawasalimia wazazi wake halafu akaingia

chumbani mwake kubadilisha nguo kisha akaingia jikoni kula chakula. Alipomaliza kula chakula na akaanza maandalizi ya kuelekea kwa mwalimu lakini kabla hajaanza safari mbwa wake alibweka sana ambapo siyo kawaida yake kubweka hivyo muda wa mchana. Ipanga aliona mbwa wake anamsumbua na kumchelewesha kuondoka, hivyo aliamua kumfunga kamba kisha akamwacha akiendelea kubweka kisha akakimbia kuwahi.

Ipanga na rafiki zake walifika kwa mwalimu, walimwomba mwalimu asiwafundishe ila awapatie kazi kwenda kufanyia nyumbani kwani kuna sehemu wameagizwa. Mwalimu alikubaliana nao, akawapa kazi kisha aliwaruhusu waondoke ingawa hakujua wanaelekea wapi. Wakiwa njiani kuelekea Itongo, walikutana na wanafunzi wenzao waliowasaidia kuwaelekeza njia kwani wao hawakuwahi kufika maeneo hayo. Walipofika Itongo waliwakuta baadhi ya wanafunzi wa darasani kwao tayari wamefika huku Iba na Ibe nao wakiwa wamefika tayari ingawa kila mmoja alikuwa kimya. Baada ya muda mchache kupita Iba akamwambia Ibe, “Anza sasa nikujibu, wewe si unajifanya mtaalamu sana!” Ibe akamwambia, “Wewe subiri kidogo, namalizia nije nikuoneshe.”

Ibe aliongea hivyo huku akichezesha mdomo kuonyesha anazungumza maneno bila kutoa sauti. Alipomaliza kuzungumza kimya kimya alinyanyua mkono wake wa kulia na kumnyooshea kidole mbwa aliyekuwa amesimama pembeni ya wanafunzi.

Baada ya kumnyooshea kidole, mbwa alilia kwa maumivu makali sana na kujigalagaza chini akiashiria kuwa anachapwa fimbo kali sana. Ipanga na rafiki zake waliogopa na kushangaa sana huku wengine wakicheka kuona mbwa anavyohangaika huku akilia. Wakati huo Iba alikuwa akicheka kicheko cha dharau huku akimtazama Ibe. Baada ya dakika mbili hivi, mbwa alilala chini huku akiwa amechoka sana na baada ya muda mfupi alitokewa na alama za mijeredi mwili mzima. Iba alicheka tena huku akimtazama Ibe na kusema, "Siku zote huwa ninakwambia kuwa huniwezi kwani hiyo ni ya kitoto sana." Iba naye akamwambia Ibe amtazame kenge mkubwa aliyekuwa amejilaza juu ya jiwe lililojitokeza juu ya maji akiota jua la jioni. Wote waligeuka kumtazama huyo kenge. Iba aliinua mkono wake wa kulia na kumnyooshea kidole yule kenge kwa kidole chake cha kati, ghafla yule kenge akaanza kuvimba, akajaa na kupoteza

fahamu. Baada ya sekunde chache, kenge alilipuka mithili ya mtu aliyelishwa bomu na kuchanika vipande vidogo vidogo. Wakati huo Ipanga na wenzake waliendelea kuogopa na wachache kushikana mikono kwa nguvu kwa ajili ya woga na hofu kubwa lakini walishindwa jinsi ya kuondoka peke yao kutokana na hayo matukio. Hata hivyo miongoni mwa wanafunzi waliokwenda nao, baadhi walikuwa wakifurahia na kushangilia kila kilichofanywa kati ya Iba na Ibe.

Wakati huo, Ibe hakuonesha kushangazwa na tukio hilo alilolifanya Iba badala yake akamwambia kuwa yeye bado sana. Ibe alitazama ziwani akaona mashua ya wachuuzi wa samaki wanatoka kuvua samaki kisha akamwambia Iba aitazame. Wote waliitazama ile mashua, ghafla Ibe alipikicha mikono yake na kuzungumza maneno bila kutoa sauti kinywani mwake. Punde si punde upepo mkali sana ulivuma na mawingu yakatanda eneo hilo na kupelekea kunyesha mvua kubwa sana ya mawe. Haikuwa mbali sana na eneo wanapoegesha mashua. Waliiona ile mashua inazama na watu kuanza kuelea juu ya maji huku wakionyesha ishara ya kuomba msaada. Mashua ilipozama, Ibe aligeuka haraka na kugonolea upande mashua

ilipozamia mvua na upepo ukakata ghafla pakawa shwari.

Wavuvi waliokolewa wote pamoja na samaki wao kwani palikuwa karibu na kando kando ya ziwa. Iba alipoona tukio alilolifanya Ibe ilimshangaza kidogo na kuamua kuongea huku akitoa sauti lakini maneno yasiyoeleweka kuwa ni lugha gani. Huku akiongea hivyo, ghafla alitokea ndege aina ya mwewe mdogo, na kumbeba yule mbwa aliyekuwa bado hajapata fahamu na kumpeleka juu sana kisha akamrudisha kwa kumdondosha toka juu kidogo umbali wa mita kadhaa hivi hadi pale chini alipokuwa kajilaza. Ibe hakuonesha kushangaa bali aliwaambia wote watazame ziwani. Kipindi wametazama ziwani ulitokea mnyororo mnene sana kwenye mawingu ukadondoka ziwani na baada ya sekunde kadhaa, huo mnyororo ulitoka ziwani ukiwa umenasa nyoka aina ya chatu mkubwa sana na kupanda naye juu kisha vikaishilia kwenye mawingu. Baada ya kuona hivyo Iba naye akawaambia wote watazame ziwani na walipofanya hivyo, ilitokea meli kubwa sana. Ukubwa wake na urefu ilikaribia kugusa mawingu huku ikiwa inaunguruma na kupiga honi ikija uelekeo wa kando kando ya ziwa

walipokuwa wamesimama. Meli hiyo ilikuwa imebeba abiria wa mataifa mbalimbali. Matukio hayo ya mwisho yaliwapelekea Ipanga na wenzake kupiga kelele kwa nguvu sana kuomba msaada. Iba na Ibe waliwasihi wasiendelee kupiga kelele kwa ahadi kuwa wanasitisha hilo zoezi kwa masharti ya kwamba wasimwambie mtu yeyote yule waliyoyaona hapo. Walisitisha zoezi hilo na kutawanyika kurudi nyumbani huku Iba na Ibe wakiendelea kutambiana.

Ipanga alifika nyumbani kwao jioni sana baada ya kuachana na marafiki zake huku akiwa na sura ya woga. Alipofika nyumbani aliwafungia kuku kwenye mabanda yao na kwenda kumfungulia mbwa ambaye ni rafiki yake ingawa hakuwa na furaha kabisa kutokana na matukio alioyaona. Baada ya mama yake kuona hana furaha ikabidi amwulize, “Mwanangu umekuwaje leo? Mbona unaonekana ni mwenye huzuni na pia sijakuona ukiandaa maji yako ya kuoga?” Ipanga akajibu, “Hakuna kitu mama ila nahisi baridi tu.” Mama akasema, “Basi subiri niivishe chakula cha usiku kisha uchemshe maji ya kuoga” Ipanga akajibu, “Sawa mama.” Ipanga alichemsha maji kisha akaenda kuoga na alipomaliza kuoga mama yake

aliandaa chakula, wakala na baada ya kumaliza kula Ipanga aliondoa vyombo halafu aliwatakia wazazi wake usiku mwema kisha akanyanyuka kuelekea chumbani kwake kulala. Kipindi anajiandaa kufunga mlango wa chumba chake, baba yake alimwuliza kama ana tatizo lolote lililomsibu kwani si kawaida yake kumaliza kula na kuelekea kulala. Alimjibu baba yake kuwa hakuna tatizo lolote lile ila amechoka na kuna muda alihisi baridi iliyompelekea kuoga maji ya moto. Baba yake alimruhusu afunge mlango wa chumbani kwake ili alale apumzike.

Hakika Ipanga hakuwa katika hali nzuri kwani aliwaza na kujiuliza mambo mengi sana kichwani mwake kama vile Iba na Ibe ni watu wa namna gani hadi wanafanya matukio ya kutisha kiasi hicho. Vile vile kwa nini waliwazuia wasimwambie mtu yeyote matukio waliyoyashuhudia huko Itongo, na wakisema ni nini kitatokea. Maswali yote hayo ambayo hayakuwa na hata chembe ya majibu yalimfanya Ipanga auone usiku kuwa mrefu sana kwani alipata usingizi wa mang'amung'amu tu. Kesho yake asubuhi Ipanga aliamka na kujiandaa tayari kuelekea shule ili awahi kuhesabu namba. Aliwasalimu wazazi wake kisha akaondoka.

Alipofika shuleni alihesabu namba na kuelekea katika eneo lake la kufanya usafi akaanza kufagia ingawa alikosa tena raha baada ya kuwaona Iba na Ibe kipindi cha kuhesabu namba. Hali hiyo ya hofu na kukosa raha ilimchukua muda mrefu sana hadi kuizoea ingawa hakuweza kumueleza mtu yeyote yule.

Baada ya miezi kadhaa kupita, akiwa shambani, muda wa jioni na baba yake, Masha alijikuta ghafla anaanza kumsimulia matukio ya Iba na Ibe yaliyotokea Itongo. Alifanya hivyo kwa sababu mashua iliyozamishwa kwa upepo na mvua ya mawe ni ya baba yake na kaka yake ni mmoja kati ya watu walio okolewa kutoka ndani ya hiyo mashua. Baba yake Masha alikasirika sana aliposikia maelezo hayo na kuahidi kuwashitaki hao wanafunzi (Iba na Ibe) kwenye uongozi wa shule ili hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao.

Siku iliyofuata baba yake Masha alikwenda shuleni kutoa taarifa kwa uongozi wa shule juu ya hayo matukio yaliyotokea Itongo na kuusihi uongozi huo kuchukua hatua kali dhidi ya hao wanafunzi. Mwalimu mkuu aliwaita walimu wenzake wakakaa kikao cha dharura kujadili suala

hilo. Waliwaita Iba na Ibe kwenye kikao hicho ili kuthibisha matukio hayo waliyoyafanya Itongo nao wakakiri kuwa ni kweli ingawa mwanzoni walianza kwa kukataa. Walimu walishtushwa sana na hayo matukio na kuamua kuitisha kikao cha wazazi ili kujadili suala hilo kwani lilifananishwa na matukio kadhaa yaliyowahi kutokea hapo kijijini. Baada ya siku mbili kiliitishwa kikao cha wazazi huku wazazi wa Iba na Ibe wakihusishwa kwa asilimia kubwa kuwa wanajua vizuri juu ya matukio mazito wanayofanya watoto wao.

Wakiwa ndani ya kikao, kulitokea mvutano mkubwa sana kwani wanakijiji wengi walitaka Iba na Ibe wafukuzwe shule na wazazi wao wafukuzwe hapo kijijini. Lakini yote hayo yalipokuwa yakiendelea ndani ya kikao, wazazi wa Iba na Ibe hawakuonesha ushirikiano wowote mzuri jambo lililomfaya mwalimu mkuu kuwasimamisha masomo Iba na Ibe kwa muda usiojulikana na kuahirisha kikao ili suala hilo lipelekwe kwenye serikali ya kijiji kwa maamuzi zaidi. Baada ya siku tatu mwenyekiti wa kijiji aliitisha kikao cha wanakijiji wote ili wajadiliane kwa pamoja na kufikia mwafaka kuhusu suala la wanafunzi Iba na Ibe pamoja na wazazi wao. Kikao

kilianza alasiri na kumalizika jioni sana na kilihudhuriwa na wanakijiji wengi sana na wengine kutoka vijiji jirani kwani walitaka kusikia mwafaka kutokana na wao kushtushwa na hayo matukio ya akina Iba na Ibe.

Mwafaka wa kikao cha wanakijiji wote ukawa ni kukubaliana kwa pamoja kuwa wazazi wa Iba na Ibe waombe msamaha kwa wanakijiji, watoe ngo'mbe wawili wawili kwa kila familia na watoto wao wasimamishwe masomo kwa muda wa mwezi mmoja. Wazazi wa Iba na wazazi wa Ibe walikubali hiyo adhabu na wakaahidi kuwa watawakanya watoto wao kwa matukio hayo ingawa wao waliendelea kukataa kuwa hawahusiki na matukio ya watoto wao. Kabla mwenyekiti hajawatawanya wanakijiji aliwaeleza familia ya Iba na familia ya Ibe kuwa ingawa wamewasamehe lakini wasirudie tena na endapo kesi yoyote ile itajitokeza juu yao inayohusu tukio kama hilo basi watafukuzwa katika kijiji hicho.

Baada ya wiki chache hivi Masha akaanza kuhisi kizungu zungu kikali na kupelekea kutohudhuria shule kwa siku kadhaa kwani alikuwa hawezi hata kusimama peke yake mpaka ashikiliwe. Wazazi wake walimpeleka zahanati ya kijiji akapata

matibabu lakini hakuhisi nafuu yoyote ile. Hali yake ilizidi kuwa mbaya kwani alianza kuumwa kichwa sana huku akivimba tumbo, macho na miguu. Wazazi wake waliamua kumvusha hadi ng'ambo ya pili ya mto ili kumpeleka hospitali kubwa achunguzwe zaidi. Walipofika hospitalini, Masha alilazwa kisha akapimwa vipimo vyote vya mwili wake lakini majibu yakatoka kuwa ana virusi vya ukimwi jambo ambalo liliwashangaza sana wazazi wake. Baba yake alijiuliza, "Kijana wetu kavipata wapi virusi vya UKIMWI! Mbona kijijini kwetu hakuna taarifa yoyote kuwa kuna aliyewahi kuathirika! Licha ya hayo, kijana wetu bado hajawajua wanawake, nani kamwambukiza virusi vya UKIMWI!"

Ilibidi daktari awaeleze wazazi wa Masha kuwa kijana wao atalazwa hapo kwa siku moja na kesho yake ataruhusiwa kurudi nyumbani akatumie dawa na baada ya mwezi mmoja watamrudisha tena hospitali kuona anaendeleaje. Baba yake Masha akamwuliza daktari, "Mimi na mke wangu tunaweza kupima kama tuna virusi vya UKIMWI?" Daktari akamjibu, "Ndiyo, mnaweza, pia hakuna gharama yoyote ile. Daktari akawauliza, "Mnataka kupima na mko tayari kupokea majibu?" Mama

Masha akajibu, “Ndiyo daktari, tuko tayari.” Basi daktari akawaandikia fomu kisha akawaambia waipeleke maabara wakapimwe na akawaeleza warudi kwenye chumba chake baada ya saa mbili. Walipimwa kisha wakarudi wodini kumtazama kijana wao ambaye tayari alikuwa ameanzishiwa dozi ya dawa za kufubaza virusi mwilini ingawa yeye binafsi alikuwa hajaambiwa kuwa ana Virusi vya Ukimwi (VVU) kwani wazazi wake walishindwa jinsi ya kumwambia. Baada ya saa mbili walirudi kwa daktari na kumkuta akiwasubiri kwani muda wake wa kuwahudumia wagonjwa ulikuwa umekwisha na alitakiwa kumkabidhi daktari mwingine wa zamu ya usiku.

Daktari aliwapa hongera kisha akawaambia kuwa hawana virusi vya UKIMWI, waendelee kuaminiana na kulindana maisha yao yote. Pamoja na kupewa majibu mazuri yahusuyo afya zao, hawakuonyesha furaha yoyote ile kwani swali lao kubwa ni namna gani kijana wao amepata virusi vya UKIMWI. Basi daktari aliwaruhusu kuelekea wodini na akawatakia safari njema kurudi kijijini kwao endapo hatawakuta kesho yake asubuhi. Kesho yake asubuhi walirudi kijijini huku Masha akiwa amebebwa mgongoni na baba yake kwani

alikuwa hawezi kunyanyuka wala kukaa na kila mara alikuwa akilalamika maumivu mwili mzima hasa kichwa.

Ilipofika jioni, Ipanga na wazazi wake walikwenda nyumbani kwa akina Masha ili kumjulia hali Masha kwani walikuwa na taarifa kuwa wamefika nyumbani kwao kijijini muda wa mchana wakitokea hospitali. Masha alipomuona rafiki yake Ipanga aliangua kilio kwa uchungu sana kilichopelekea Ipanga naye kuanza kulia baada ya kuona hali ya rafiki yake kipenzi ilivyo. Hali ya simanzi ilitawala nyumbani kwa akina Masha na baada ya muda mfupi wazazi wa pande zote mbili walianza kuwanyamazisha vijana wao huku nao wakiwa na huzuni mioyoni mwao. Baada ya dakika kadhaa vijana walinyamaza hali iliyopelekea baba yake Masha kuwakaribisha wageni sebuleni kuanza kuwaeleza kilichojiri hospitalini huku Ipanga akibaki chumbani na rafiki yake.

Kipindi anaelezea kilichojiri hospitalini, Ipanga alikuwa akisikia mazungumzo yote yaliyokuwa yakiendelea sebuleni na aliposikia rafiki yake ana virusi vya UKIMWI, alianza kulia tena kwa huzuni kubwa. Wazazi wake walimfuata chumbani kumtoa nje kisha wakambembeleza na kumsihi

asilie bali aendelee kumwombea rafiki yake kwani tayari amepewa dawa zitakazomsaidia. Baada ya muda Ipanga alinyamaza, wakaingia ndani na hatimaye waliaga kurudi kwao kwani muda ulikuwa umeenda sana. Walinyanyuka na kijana wao ambaye alishindwa hata kumuaga rafiki yake kisha wakaondoka.

Masha alishindwa kabisa kuhudhuria masomo shuleni kutokana na hali yake kiafya kuendelea kuzorota jambo lililowafanya rafiki zake akiwemo Ipanga kwenda takribani kila siku kumjulia hali walipokuwa wakitoka shule. Hali hiyo ilimpa faraja sana Masha. Jumamosi moja mama yake Ipanga alimwambia Ipanga aende shambani kulinda, ndege wasile mpunga kwani yeye alihitaji kwenda kwenye shamba la mihogo kwa ajili ya kufanya palizi. Ipanga alijiandaa asubuhi hiyo na ilipofika saa moja alianza safari kuelekea majalubani kwenye shamba lao kulinda ndege wasile mpunga. Alifika shambani na kuendelea kuamia ndege huku akitembea tembea kulizunguka jaluba lao, joto lilikuwa kali sana huku likizidi kuongezeka kadri saa zilivyokwenda.

Ilipofika saa sita mchana, Ipanga aliendelea kuhisi joto kali, mti wa kivuli ulikuwa mbali na

eneo la jaluba lao hivyo asingeweza kwenda kujikinga na jua. Alipita kijana mmoja karibu na jaluba alipokuwa Ipanga huku akipiga mluzi. Ipanga alimtazama lakini hakumfahamu kijana huyo. Kutokana na hali ya joto aliyokuwa nayo Ipanga, ilibidi amsimamishe huyo kijana kisha akamwomba amtazamie ndege wasitue kwenye shamba kula mpunga kwa dakika chache ili aende kando kando ya ziwa akajimwagie maji kichwani kwani joto limemsumbua sana. Kijana huyo alimkubalia na Ipanga akaanza safari kuelekea kando ya ziwa lililopo mita chache tu kutoka kwenye jaluba lao.

Alipofika kando kando ya ziwa alivua malapa na kukanyaga maji ili achote kwa mikono yake ajimwagie kichwani. Alifanya hivyo mara ya kwanza, alipotaka kuchota maji mara ya pili alisikia sauti pembeni yake ikisema “Ipanga, usiogope na wala usihofu kwa chochote.” Ipanga alishtuka sana na kutazama pembeni yake, ghafla akamwona mamba mkubwa sana akiendelea kumsisitiza asiogope.

Mamba yule alikuwa amesogea kidogo ufukweni, nusu ya kiwiliwili chake kikiwa majini na nusu nyingine kwenye mchanga. Ipanga aliweza

kuyaona meno makali na makubwa ya mamba yule. Hakuwahi kumwona mamba mkubwa kiasi kile, akiwa mzima. Mshangao mkubwa zaidi ni pale mamba yule alipokuwa akizungumza kama mwanadamu huku akimwonesha Ipanga kuwa ni mwema na kwamba hakuwa na madhara yoyote. Ipanga kwa ujasiri, alipiga hatua kinyume nyume akirudi nyuma na kisha akatoka ndani ya maji na kusimama nchi kavu. Yule mamba aliendelea kumsihi asiogope na aendelee kumsikiliza. Mamba akaendelea, "Ninaitwa Amani, jina langu linaakisi tabia yangu kwani mimi ni mtu ninayependa amani."

Ipanga aliendelea kumsikiliza kwa mshangao mkubwa hatimaye ujasiri ukamwijia na akataka kumhoji yule mamba. Ipanga akaanza kwa kuuliza, "Wewe ni Amani wa wapi na umejuaje kuwa ninaitwa Ipanga?" Amani akajibu, "Mimi nipo hapa kisiwani kwa miaka mia mbili sasa. Watu wote waishio katika vijiji vya kisiwa hiki ninawafahamu kila mmoja na sifa zake. Wewe ni mtoto wa mzee Utulivu na mama yako mzazi anaitwa Mema. Mama yako ndiye aliyekuagiza uje kuamia ndege kwani yeye kaelekea kwenye palizi shamba la mihogo lililoko jirani na Itongo." Wakati huo

Ipanga alimsikiliza yule mamba kwa makini sana na baadaye alishangaa sana kwani mambo yote aliyoelezwa yalikuwa ya kweli. Ingawa alikuwa kasimama kando kando ya maji lakini roho ya woga ilikwisha kabisa, akapata shauku ya kuendelea kumsikiliza yule mamba na kutaka kujua nini hasa lengo lake. Mamba aliendelea, "Ipanga, nataka nikueleze kitu juu ya familia yako na rafiki yako Masha."

Ghafla moyo wa Ipanga uliripuka na kumwenda mbio huku mwili wake ukijawa ubaridi mwembamba. Mamba akaendelea kusema, "Wazazi wako hawako salama kwani wanatafutwa na kusumbuliwa sana na watu wabaya. Kuna siku nilimwambia mama yako akiwa anaandaa unga wa udaga mwambani kuwa asali sana kwa imani yake kwa sababu yeye ndiye mwenye nafuu kuliko baba yako." Ipanga alihoji, "Mwenye nafuu kivipi?" Mamba akamjibu, "Baba yako ana ndugu zake wa karibu sana, ingawa yeye kawahangaikia na kuwasaidia mambo mengi sana katika maisha yao hadi hapo walipo lakini shukrani yao kwake ni kumtesa na kumuhangaisha ikiwemo kumfunga fikra zake za ufahamu kwa kutumia michezo michafu waliyonayo. Ila kupitia mama yako kusali

na kumuomba Mungu kwa imani yake ya kweli, baba yako anapata ahuweni kwani yeye binafsi kishafungwa ufahamu na hao ndugu zake wanaojifanya wanampenda kwa dhati na hata hawezi kutambua vizuri kitu cha kumletea madhara yeye binafsi na familia yake. Kuna mambo mengi sana ila kwa leo sipaswi kukuelezea zaidi yahusuyo familia yako. Jambo lililonileta leo ni moja tu lihusulo rafiki yako Masha."

Ipanga alimkatiza Mamba na kusema, "Kuna kijana nimemwomba anisaidie kuamia ndege shambani, naomba nikimbie nikamwombe aniongezee muda wa kunisaidia kuamia ndege kisha nirudi unielezee hayo." Mamba akamjibu akasema, "Uliniomba mimi na nilikuja nikiwa napiga mluzi, hata hivyo usiwe na shaka kwani hakuna ndege wa kuweza kutua na kula mpunga, hadi sasa ninapalinda." Ipanga alishituka sana ingawa yule mamba aliendelea kusema, "Nimeamua kuja kwako ili nimsaidie rafiki yako, naona jinsi anavyoumia na kuteseka bila kosa lolote. Haijapata kutokea ndani ya vijiji vya hiki kisiwa mimi kujitokeza na kumsaidia mtu yeyote ila kwako imenibidi kwa sababu wewe ni mstaarabu, mnyenyekevu, msikivu, mvumilivu na

mpenda amani kama mimi nilivyo. Tuyaache hayo, rafiki yako anaumwa kama nilivyokwambia lakini ugonjwa wake ni wa kimazingara. Binadamu wengi wamekuwa na tabia mbaya sana, inafikia hatua wanamtengenezea binadamu mwenzao ugonjwa unaofanana kabisa na uhalisia wa ugonjwa huo kitaalamu. Ugonjwa wa UKIMWI alionao ni ugonjwa wa kutengenezwa."

Ipanga akadakia na kuuliza, "Ugonjwa wa kutengenezwa! Kwani unatengenezwaje?" Mamba akajibu, "Ugonjwa wa kutengenezwa ni ugonjwa unaotengenezwa kimazingara na hasa hutengenezwa na wachawi, unakuwa na dalili sawa na ugonjwa wa ukweli kitaalamu. Madaktari wenu hutoa majibu ya mgonjwa kwa kutazama matokeo ya vipimo kwenye maabara ama kwa kumtazama mgonjwa anaumwaje na ana dalili gani. Daktari anaweza kupokea majibu kutoka maabara yasithibitishe ugonjwa unaoumwa lakini yeye akahitimisha kwa kukupatia dawa za huo ungonjwa kwa kutazama dalili ulizonazo zinazohusiana na ugonjwa huo. Hizo ndizo changamoto mnazozipitia kwa baadhi ya madaktari wenu ninyi mnaowaita wataalamu. Kipindi mpo Itongo, mlipewa masharti ila Masha aliyakiuka

masharti hayo na ndio maana akatengenezewa ugonjwa wa UKIMWI alionao."

Ipanga aliwaza na kupata majibu kuwa ni kweli walipokuwa Itongo walipewa masharti tena kwa msisitizo kuwa wasije wakamwambia mtu yeyote yule juu ya kilichotokea huko. Ipanga akauliza, "Wachawi ndiyo watu gani? Kwani Iba na Ibe ni wachawi?" Mamba kajibu, "Ndiyo, Iba na Ibe ni wachawi walifundishwa na bibi zao wakishirikiana na mama zao. Ninaweza kusema kuna aina nne za uchawi ambazo ni kama ifuatavyo; kwanza, kuna uchawi wa kuzaliwa nao. Mtoto ananuiziwa maagano ya kichawi akiwa tumboni mwa mama yake na yote hayo mama yake ndiye anayehusika na ni lazima na yeye awe mchawi. Pili, kuna uchawi wa kupewa. Mtoto mchanga hupewa vitu vya kichawi kiganjani, akifumba mkono anakuwa ameupokea uchawi na kuukubali. Mama ama baba ama ndugu yeyote anayeujua uchawi anaweza kumpatia uchawi mtoto akiwa bado mchanga na kitovu chake hutumika sana kumwandaa kuwa mchawi. Tatu, kuna uchawi wa kufundishwa. Mtoto anaweza asiujue uchawi ila akafundishwa na mtu yeyote yule ama mzazi/wazazi ama ndugu wa karibu pasipo hata wazazi wake kujua. Mtoto

anaweza kufundishwa kupitia michezo ya kichawi ama kutazama picha ama mambo ya kutisha tisha yahusuyo uchawi. Mtu mzima pia anaweza kufundishwa uchawi iwapo yeye mwenyewe anataka kufundishwa na wakati mwingine mtu hutoa vitu vya thamani, mifugo ama pesa ili afundishwe. Nne, kuna uchawi wa kununua. Mtu anaamua kununua tu ili naye awe mchawi. Mara nyingi uchawi wa kununua hununuliwa na watu wenye roho mbaya, wenye wivu na maisha ya watu ama maendeleo ya watu. Inapofikia kiwango kikubwa cha wivu wa maisha ama maendeleo ya mtu ama watu, anakuwa hana namna ya kufanya zaidi ya kutengeneza chuki na mazingira ya kuwaharibia watu. Inapofika hatua hiyo, ndipo hujikuta anakwenda kununua uchawi. Ila uchawi wa Iba na Ibe ni kunuiziwa maagano wangali tumboni mwa mama zao."

Muda wote huo Ipanga alikuwa akimsikiliza mamba huyo na kuonesha kushangaa sana kutokana na maelezo aliyokuwa akiyasikia. Mamba akaendelea kueleza, "rafiki yako Masha amebakiza siku chache sana atachukuliwa kichawi ila ninyi kwa macho ya kibinadamu mtaona amekufa, ila ni wewe pekee mwenye uwezo kuokoa maisha yake."

Ipanga alishituka sana kuambiwa rafiki yake atakufa na ni yeye pekee wa kuweza kuokoa maisha yake. Ikabidi amuulize vizuri yule mamba, “nawezaje kuokoa maisha ya Masha?” Mamba akamjibu, “Kuna kazi nitakupatia ukaifanye, ukifanikiwa kuifanya, na kwa ufasaha utakuwa umeokoa maisha ya Masha. Kufanya kazi hii inatakiwa uwe makini sana kwa sababu utachukiwa sana na watu wenye roho mbaya na wakati mwingine vita hiyo inaweza kuhamia kwako. Lakini usijali, kikubwa zaidi sali sana na fuata nitakachokuelekeza, ukifanye kwa sababu Mungu yupo pamoja nawe. Uko tayari kuyaokoa maisha ya rafiki yako?”

Ipanga alijibu kwa woga huku akifikiria ni kitu gani ataambiwa akifanye ili kuokoa maisha ya rafiki yake, “Ndiyo, nipo tayari.” Mamba aliendelea kusema, “Kesho asubuhi uje hapa hapa utakuta kikopo kidogo kikiwa kinaelea majini, utakichukua na ndani yake kutakuwa na dawa ya maji. Ukibebe vizuri na kwa umakini mkubwa sana hadi nyumbani kwa akina Masha. Ila hakikisha usikute mtu mwingine nyumbani kwao tofauti na Masha pekee yake. Kwa vile unakifahamu vizuri chumba anapolala Masha, ingia ndani bila kubisha hodi

wala kupiga kelele huku ukitazama uelekeo alipolala. Mmwagie hayo maji yenye dawa kwa kumshitukiza. Hakikisha hiyo dawa inampata vizuri hususan kichwani. Akikitazama tu hicho kikopo kabla hujammwagia dawa hiyo haitafanya kazi na atapata nguvu za ajabu sana ambazo sio za kwake, ni nguvu za kichawi na roho za mauti alizonazo kwa sasa na atakufa katika siku hizo nilizokueleza. Nasema hivyo kwa sababu inachukua muda mrefu sana kuiandaa dawa hiyo, ila hii ni kushukuru imeandaliwa siku nyingi kwa ajili yake."

Ipanga alikubali na kuahidi kuwa atafuata maelekezo yote ili amwokoe rafiki yake Masha. Mamba akaendelea kumweleza Ipanga, "Pia jitahidi kuwa makini njiani ukiwa unaelekea kwa akina Masha kupeleka dawa, njiani utaona vitu vya ajabu sana na vya kutisha ama kuogopesha ili uimwage hiyo dawa na ukimbie ila usivijali kwani hivyo ni vitisho tu vya kichawi. Unaweza kuona nyoka wengi wako chini na wametanda njia nzima, ama unaweza kuona mnyama mkubwa sana anakufukuza akitokea mbele yako, ama unaweza kuona maiti za watu mbalimbali zikiwa zimelazwa chini njiani, ama unaweza kusikia sauti ya watu

wakikuzomea na kukuchekelea kwa sauti kubwa na vitu kama hivyo. Kikubwa usiogope na usikwepe kitu chochote njiani, kama kikikukaribia wewe kikanyage ingawa hutakikanyaga kwani kitapotea na utajikuta unakanyaga chini tu kama kawaida."

Ipanga alikubali kisha akaendelea kumhoji mamba huyo mambo mengine mengi, ila mamba akamjibu kwa kusema, "Siku ya leo nenda kwanza kwani kuna mambo mengine ya kuandaa kwa ajili ya hiyo kesho na hayo mambo mengine nitakuelezea siku nyingine." Pia yule mamba alimsihi Ipanga asimweleze mtu yeyote juu ya suala hilo kisha akapotea. Ipanga alibaki anashangaa na hakuwa tena na hamu ya kujimwagia maji kichwani licha ya joto la jua kuwa kali. Alitoka na kutembea taratibu kuelekea shambani kwao huku akijaribu kutafakari kuhusu huyo mamba na yale yote aliyomwambia likiwemo suala la kumponya rafiki yake Masha. Ilipofika jioni Ipanga alirudi nyumbani kwao na alipofika nyumbani aliwakuta wazazi wake wameketi nje ya nyumba huku wakizungumzia hali ya Masha ilivyo mbaya kwani alianza pia kupata kwikwi kali sana. Aliwasalimia kisha akaingia ndani na kujiandalia maji ya kuoga.

Baada ya kumaliza kuoga alikuta tayari chakula kimeandaliwa mezani na mama yake kisha wakaanza kula huku wazazi wake wakiendelea kujadili kuumwa kwa Masha na jinsi hali yake inavyozidi kudhoofu kila kukicha. Muda wote huo Ipanga hakutia neno lolote, alikuwa kimya tu akiwasikiliza kwani aliambiwa na yule mamba kuwa asije kusema kwa mtu yoyote kinachoendelea. Walipomaliza kula Ipanga alitoa vyombo na kusafisha meza iliyokuwa imeandaliwa chakula na baada ya hapo aliwatakia wazazi wake usiku mwema kisha akaelekea chumbani kwake kulala. Kabla hajapitiwa na usingizi alisikia mbwa wake akibweka kwa sauti kubwa sana ambavyo siyo kawaida yake. Ipanga aliogopa sana kusikia mbwa wake anabweka hivyo, ilibidi atoke nje kutazama mbwa wake amepatwa na nini.

Alifungua mlango na kutoka nje, mbwa wake alimkimbilia na kumsukuma arudi ndani huku akitoa sauti ndogo ya uchungu ingawa Ipanga hakuelewa. Ghafla mbwa wake alibadilisha sauti na kuunguruma kama simba dume huku akiendelea kumsukuma arudi ndani. Ipanga aliogopa na kukimbilia ndani kisha akafunga mlango huku akitetemeka. Baada ya kufunga mlango, alikimbilia

dirishani chumbani kwake, alifungua dirisha taratibu kisha akatazama kuona nini kinajiri nje. Alimuona mbwa wake akiendelea kubweka kwa sauti ya kawaida huku akitazama juu ya mti wa mwembe uliopo hapo nyumbani kwao. Ghafla aliona moto mkubwa sana uliozungukwa na vibuyu vidogo vidogo vingi ukiwa umeambatana na moshi mzito ukipaa juu kutokea kwenye huo mti. Baada ya huo moto kuishia juu, mbwa wake aliacha kubweka na kuanza kutembea tembea huku na kule akiizunguka nyumba yao.

Muda wote huo mazingira ya nje yalikuwa matulivu huku mwanga mweupe wa mbalamwezi ukiangaza kila mahala. Baada ya muda mfupi, Ipanga alifunga dirisha na kuelekea kwenye mlango wa chumba cha wazazi wake kisha akaanza kuita, “Baba, mmeshalala?” Baba yake akajibu, “Hapana, bado hatujalala. Unashida gani?” Ipanga akajibu, “Nimesikia sauti kama ya mnyama mkubwa ikiunguruma nje ya nyumba. Nilitaka kujua kama ni ya kweli nanyi mmeisikia ama nimesikia vibaya tu.” Baba yake akajibu, “Hapana, hatujasikia sauti yoyote kubwa tofauti na sauti ya mbwa aliyekuwa akibweka na baada ya muda mfupi akanyamaza.” Ipanga akasema, “Sawa baba,

nilitaka kujua hilo tu. Niwatakie usiku mwema kwa mara nyingine." Wazazi wake wakamjibu, "Ahsante, nawe pia." Ipanga alielekea chumbani kwake kulala pasipo kuwaeleza wazazi wake kilichojiri nje huku akitafakari pia tukio lililompata siku hiyo la kukutana na mamba kisha kuelezwa mambo mazito kadha wa kadha likiwemo la kumsaidia rafiki yake Masha ili apone.

Kesho yake asubuhi, Ipanga aliamka akawasalimia wazazi wake kisha akaanza kujiandaa kuelekea shambani ili akatimize ahadi ya kumponyesha rafiki yake Masha. Alipofika shambani, alihifadhi vizuri chakula chake alichoandaliwa na mama yake kwa ajili ya kula mchana na baadaye kuelekea kando kando ya ziwa ili akachukue dawa ya kumtibu rafiki yake. Alipofika kando kando ya ziwa aliona kikopo kidogo cheupe kinaelea juu ya maji bila kusogea ingawa kulikuwa na upepo mkali kiasi pamoja na mawimbi. Ingawa Ipanga aliingiwa na hali ya taharuki na woga, lakini alipiga moyo konde na kuanza kuvua kandambili zake na kisha kuingia ndani ya maji kuchukua dawa iliyoko ndani ya kikopo. Alikishika hicho kikopo kilichokuwa wazi kwa juu, akakibeba na kuanza safari kuelekea

nyumbani kwa akina Masha. Kipindi yupo njiani, alisikia sauti kubwa sana masikioni mwake ya bibi vizee ikiangua kicheko cha dharau. Nywele na mwili wake vilimsisimka sana ila akakumbuka maneno ya yule mamba kuwa atakutana na vitisho vingi na kwamba asijali na wala asigeuke nyuma.

Baada ya muda mfupi sauti hiyo ikatoweka na akaendelea na safari. Alipokaribia kufika nyumbani kwa akina Masha, ghafla aliona gari moshi kubwa sana likiwa limebeba abiria likitembea barabarani wakati hakuna hata njia yake likifuata uelekeo wake likitokea anakokwenda. Moyo wake uliripuka sana, akapatwa na kizungu zungu kikali kilichopelekea kushuka pole pole ili akae chini huku kashikilia kikopo chake cha dawa. Kabla hajafika chini ghafla alishikwa mikono na mtu ambae haonekani, akanyanyuliwa na kusimamishwa tena. Gari moshi lilizidi kumsogelea ila lilipofika karibu naye likapotea. Baada ya kupotea, Ipanga aliendelea na safari yake hadi nyumbani kwa akina Masha.

Alipofika nyumbani kwa akina Masha alikuta nyoka wengi sana wa rangi ya kijani wametanda uwanjani, wengine wakiwa kwenye ukuta wa nyumba na wengine wanatembea tembea

kuizunguka nyumba ingawa hakukuwa na mtu yeyote kwa nje. Ipanga alipiga moyo konde na kutembea haraka haraka kuelekea ndani. Lakini kila alipokuwa akikanyaga nyoka wanapotea anajikuta akikanyaga chini. Akafanikiwa kuingia ndani na moja kwa moja akaelekea chumbani kwa Masha na kukuta amelala huku kajifunika shuka mwili mzima. Alimwita akaitika, akajifunua shuka usoni ajue ni nani anayetaka kumsalimia na hapo ndipo Ipanga akammwagia dawa ikampata kichwani, usoni, kifuani na mikononi.

Masha aliishiwa pumzi kwa muda mfupi. Ghafla akapitiwa na usingizi mzito sana. Hali hiyo ilimfanya Ipanga aogope na kuhisi kuwa labda rafiki yake kapoteza maisha kama alivyokuwa akisikia watu wengi wakimjadili kuwa angekufa. Ilibidi atoke nje kuona kama anaweza kupata msaada zaidi. Alitoka nje kwa tahadhari kubwa sana kutokana na nyoka aliowaona, lakini alipofika nje hakuona nyoka hata mmoja na wala hakuona mtu yeyote wa kuweza kumsaidia kwa haraka. Ipanga alizidi kuchanganyikiwa, ikabidi akimbilie tena ndani kumtazama rafiki yake Masha.

Alipofika ndani, Masha alipiga chafya mara tatu kwa nguvu sana kisha akafumbua macho na kumtazama Ipanga. Ipanga akamwita rafiki yake na kumwuliza, “Masha, unajisikiaje kwa sasa?” Masha akajibu kwa sauti ya chini, “Najisikia vizuri ingawa ninahisi njaa kali. Ninaweza kupata chakula?” Ipanga akajibu, “Ngoja nikamwite mama yako akupikie chakula haraka. Amekwenda wapi?” Masha akajibu, “Sijui alipokwenda. Basi nenda jikoni kanichukulie mhogo mbichi nitafune.” Ipanga akaelekea jikoni, akamenya mhogo wa wastani kisha akamletea rafiki yake atafune. Masha alianza kutafuna mhogo ule mara ghafla akaanza kuwashwa mwili mzima na kuanza kujikuna. Baada ya muda mfupi alipata nguvu za ajabu na kunyanyuka kitandani kisha akasimama huku akipepesuka kutokana na kukonda. Aliposimama aliendelea kujikuna mwili mzima kwa dakika kadhaa na kila sehemu ya mwili wake alipokuwa akijikuna palitoka vitu vyeupe mithili ya unga wa udaga ulio laini.

Baada ya muda kidogo alitulia kisha akamwuliza rafiki yake, “Ipanga, kuna nini kimetokea? Mbona najisikia vizuri mwili mzima na nimepata hadi nguvu?” Ipanga akamjibu, “Masha,

nitakuelezea siku nyingine kwani ninatakiwa kurudi shambani muda huu kwani hakuna mtu." Masha alikubali na kumruhusu aondoke kuelekea shambani. Ipanga alitazama sehemu alipokiweka kikopo kilichokuwa na dawa akakiona na alipopeleka mkono kukichukua kikatoweka. Alihisi kama yupo usingizini anaota na kuanza kufikicha macho kama atakiona kikopo bila mafanikio. Aliamua kuondoka huku akiwaza mbona kikopo kimepotea na kama ataulizwa na yule mamba atamjibu nini. Wakati huo wote Masha hakujua kinachoendelea tofauti na kujishangaa vile mwili wake ulivyobadilika. Ipanga alipoondoka, Masha naye ikabidi atoke nje kuota jua kwani alihisi kiubaridi kwa mbali. Wazazi wake waliporudi kutoka shambani, walimkuta akiwa nje anaota jua huku amekaa kwenye kigoda. Mama yake alitupa chini jembe na kutaka kukimbia kwani aliogopa sana huku akijiuliza iweje Masha awe nje tena kaketi kwenye kigoda peke yake na hali mbaya ya kutojiweza waliyomuacha nayo. Mumewe alimshika mkono na kumtuliza huku naye mapigo yake ya moyo yakimwenda mbio.

Wakati wote huo Masha alikuwa akihisi kutapika na alipowaona wazazi wake akaanza

kutapika. Ilibidi baba yake asogee hadi alipokuwa. Mama naye alimfuata mmewe kwa nyuma na wote kwa pamoja wakamfikia Masha na kumtazama kwa makini sana huku akitapika. Masha aliendelea kutapika na hatimaye akaanza kutapika matapishi yenye mchanganyiko wa kila aina ya vyakula na baada ya muda mrefu alianza kutapika mabonge meusi ya nyama, vitu vidogo vidogo vilivyofungwa kwenye vitambaa vyeusi kwa kamba nyekundu. Aliendelea kuvitapika huku akipiga kelele kwa maumivu makali aliyokuwa akiyapata. Alipomaliza kuvitapika alilala chini kwenye mchanga kisha kupitiwa na usingizi mzito sana. Mama yake alifuata mkeka ndani, wakautandika pale chini kisha wakambeba na kumlaza juu yake.

Ipanga alipofika shambani, ilibidi akae chini kwa muda mrefu sana akitafakari kilichotokea huku akijihoji maswali mengi juu ya huyo mamba pasipo kupata majibu. Pia alijihoji ni kwa namna gani ataweza kuwaeleza wazazi wake pamoja na rafiki yake Masha jinsi alivyoonana na yule mamba, mambo aliyoambiwa na mamba pamoja na mlolongo mzima wa kumponyesha Masha. Huku akiendelea kuwaza na kujihoji, alikumbuka kuwa yule mamba alimsihi asije akamweleza yeyote juu

ya hayo matukio ingawa hakumwambia hadi kwa muda gani. Alijiuliza tena kuhusu kile kikopo cha dawa kilivyopotelea hewani na ni nani aliyefanya kipotee kati ya wachawi aliokuwa akisimuliwa na yule mamba ama ni mamba mwenyewe. Baada ya muda mrefu kidogo, Ipanga aliamua kukusanya vifaa vyake na kuelekea nyumbani kwao. Kipindi anaanza safari kuondoka lilimuijia wazo la kupita nyumbani kwao na rafiki yake Masha ili akamwone anaendeleaje. Alipofika alimkuta Masha bado kalala usingizi mzito, aliwasalimia wazazi wake kisha akaondoka kuelekea nyumbani kwao bila kuwaeleza neno lolote. Alifika kwao na kumkuta mbwa wake kasimama kwenye njia ya kuingia nyumbani huku akiwa na furaha sana akiruka ruka huku na kule. Mbwa akaanza kumfuata huku akimrukia rukia kwa kucheza. Ipanga hakumjali sana mbwa wake kwani alianza kujiandaa kwa ajili ya kesho asubuhi kuelekea shule.

Ilipofika jioni Masha akiwa kaketi nyumbani, alihisi kiu ya maji ya kunywa. Alinyanyuka akachukua kata na kuelekea kwenye mtungi kisha akachota maji na kunywa. Muda wote huo wazazi wake walikuwa wakimtazama huku wakiwa na shauku ya kujua ni namna gani aliweza kupata

nafuu ya ugonjwa wake hali ambayo inampelekea kupona kabisa. Alipomaliza kunywa maji wakaanza kumhoji nini kilimtokea hadi akapata nafuu hivyo. Baba akauliza, “Masha, nini kilikutokea hadi umepata nafuu kubwa kiasi hicho?” Masha akajibu, “Kichwa ni kizito sana na pia sijui nini kimenitokea.” Mama akamwuliza, “Kuna mtu kaja hapa nyumbani kwa muda ambao sisi hatukuwepo?” Masha akajibu, “Sikumbuki chochote mama.” Basi ilibidi wazazi wake waache kumsemesha zaidi. Baada ya muda kidogo akawaambia wazazi wake, “Mimi kesho nitakwenda shuleni kusoma.” Wazazi wake walipigwa na butwaa kusikia hivyo lakini yeye baada ya kuwaambia hivyo alinyanyuka na kutembea kuelekea bafuni kuoga huku akitembea vizuri bila ya kupepesuka. Walikubaliana na uamuzi wake wa kwenda shule huku wakishauriana kuwa baada ya muda atatulia ili awasimulie vizuri kilichotokea hadi kupata nafuu kiasi hicho.

Kesho yake asubuhi, Ipanga alianza safari kuelekea shuleni. Alipofika shuleni alimkuta rafiki yake Masha amekwishafika huku akionekana kutengwa kwa kuogopwa na baadhi ya wanafunzi

wenzake kwani walimwona kama siyo binadamu wa kawaida kupona ghafla kiasi hicho sababu ilipita siku mbili tu toka wanafunzi hao waende kumjulia hali na akawa hajiwezi na wala hajitambui. Alimsogelea, akamsalimia kwa kumkumbatia huku wote kwa pamoja wakiwa na furaha kuonana tena wakiwa wazima. Baada ya muda mfupi walimu nao walianza kufika shuleni na walipomwona Masha walipigwa na butwaa. Mwalimu aliyekuwa zamu hiyo wiki akamwita ofisini ili asalimiane na walimu wengine. Mwalimu Ngere (mwalimu wa zamu), akasema kwa mshangao, “Huyu ni Masha! Masha, njoo ofisini walimu wanakuita wakusalimie.” Masha akajibu, “Sawa mwalimu, nakuja.” Alipofika ofisini aliwasalimia walimu salamu ya pamoja na wote wakaitikia. Mwalimu Ngere akasema kwa huruma, “Pole sana Masha kwa kuumwa!” Masha akajibu, “Ahsanteni sana walimu.” Mwalimu Kipipi akauliza, “Kwa sasa unaendeleaje Masha?” Masha akajibu, “Ninaendelea vizuri mwalimu kwani sisikii maumivu yoyote yale na nina nguvu hata za kuweza kukimbia.”

Muda wote huo Masha anasalimiana na walimu hapo ofisini, kuna mwalimu mmoja hakuitikia

salamu ya Masha na alichukia ghafla kumwona Masha. Alishindwa kujizuia kuificha chuki yake kisha akajikuta amesema kwa sauti ya chini huku akifyonza, “Nani sijui kamponya kuharibu sherehe yetu!” Kipindi anazungumza hivyo, mwalimu Ngere alimsikia kwani alikuwa kasimama karibu naye kisha akamwuliza taratibu, “Mwalimu Bisya, unamaanisha nini kusema maneno hayo?” Mwalimu Bisya akashituka kama vile ametoka usingizini, akamtazama mwalimu Ngere kwa kumkazia macho kisha akajibu, “Hapana mwalimu, mbona mimi sijasema neno lolote!!” Mwalimu Ngere hakuongeza tena neno lolote na badala yake alitoka nje ya ofisi huku akimpuuza mwalimu Bisya. Baadaye kengere iligongwa wanafunzi wote wakaelekea mstarini na baadaye kwenye madarasa yao kuendelea na masomo.

Mwalimu Ngere ni mwalimu kijana. Urefu wake wa wastani na uso wa mviringo, macho makubwa na nywele fupi. Anapenda kunyoa mtindo kama wa kiaskari. Ni mwalimu mtanashati ambaye huvalia maridadi kila siku. Suruali na shati la viboma ambalo hupenda kuvaa humkaa sawasawa na kumfanya aonekane nadhifu. Ngere ni mwalimu mkakamavu anayeipenda sana kazi yake.

Amejenga uhusiano mzuri na wanafunzi wake. Pamoja na kutumia chaki mara kwa mara kufundishia, usingemkuta akiwa na vumbi la chaki hata mara moja iwe mikononi, usoni au kwenye nguo zake.

Mwalimu Bisya ni mtu wa makamo akiwa na umri wa kukaribia kuacha utumishi yaani kustaafu. Uso wake umekunjama kidogo. Nywele zake na ndevu zinaonekana kuwa na mvi kwa mbali. Mrefu mwembamba, na uso mrefu pia na macho yaliyoingia ndani, na masikio madogo ndio mwonekano wake wa nje. Kwa nje anaonekana pia kama mtu mtulivu na mwungwana, lakini kwa ndani alificha moyo wa kisasi na chuki kwa mafanikio ya watu wengine wakiwemo walimu na wanafunzi. Jambo kama hilo lisingetarajiwa kwa mtu ambaye ana elimu na maarifa katika malezi. Ama kweli kuna tofauti ya kupata elimu na kuelimika.

Ipanga na rafiki yake Masha waliendelea na masomo hadi wakafika darasa la saba huku Ipanga akiwa kimya asiweze kumsimulia mwenzake kilichojiri hadi akapona kabisa. Walipokaribia kufanya mitihani ya kuhitimu darasa la saba, wote kwa pamoja walisoma kwa bidii sana ili wafanye

vizuri katika mitihani yao. Siku chache kabla ya kuanza kufanya mitihani hiyo, Masha alikuwa ndani chumbani kwake akijisomea ghafla daftari lilitoka juu ya meza lenyewe likapaa hewani hadi usawa wa kichwa chake kisha likaanza kumzungukazunguka karibia chumba kizima na hatimaye likapita dirishani na kudondokea chini nje ya nyumba. Masha alipiga kelele kisha akakimbilia nje kwa wazazi wake walipokuwa wameketi. Walimwuliza kaona nini, na kipi kimetokea ndani? Lakini hakujibu kitu kwa sababu alikuwa akihema kwa nguvu sana. Walimwacha apumzike kwa muda lakini wakati huo huo baba yake alielekea ndani taratibu hadi chumbani kwake akihisi labda kaona nyoka mkubwa, hata hivyo hakuaona kitu chochote kile.

Baada ya muda mfupi alitulia na akawaambia kuwa alikuwa anajisomea ila daftari moja lililokuwa kwenye meza limepaa lenyewe likaanza kuzungukazunguka humo ndani kisha likatoka nje kupitia dirishani. Baba yake akatembea haraka kuelekea kwenye dirisha lililoko kwenye chumba cha Masha akalikuta daftari limedondoka chini akaliokota akaja nalo walipokuwa wamekaa. Baba yake akamwuliza tena kwa sauti ya upole, “Masha,

hadi sasa mimi na mama yako tunajiuliza uliponaje lakini hatuna jibu! Uliona mwenyewe daktari alikupima mara tatu kwa siku tofauti tofauti lakini ni kweli alithibitisha kuwa huna tena virusi vya UKIMWI kitendo kinachomshangaza hadi sasa. Bado leo unatueleza kuwa daftari limepaa juu na kudondoka nje kupitia dirishani. Hebu tueleze vizuri, kuna nini zaidi?" Masha akajibu, "Baba, ninachokikumbuka ni kutembea kutoka nje, kukaa kwenye kigoda na kuanza kutapika hayo niliyoyatapika baada ya kuwaona nyie. Zaidi ya hapo hakuna ninachokifahamu ama kukikumbuka. Siku zote kila ninapotoka shule huingia chumbani kwangu kujisomea, lakini leo nimeshangaa kuona daftari langu limepaa lenyewe huku likizunguka ndani na hatimaye likatoka nje kupitia dirishani!" Mama yake akamwuliza, "kwa sasa unausikiaje mwili wako?" Masha akajibu, "Tangu ile siku nitapike hadi sasa najisikia vizuri sana." Baba yake akasema, "Sawa Masha, tumekuelewa ila kuwa na amani, ngoja tulifanyie kazi hilo suala tuone nini tatizo." Masha akajibu, "Sawa baba nimewaelewa." Masha alinyanyuka alipokuwa amekaa akaelekea ndani baada ya kutulizwa na wazazi wake. Alipoelekea ndani, wazazi wake walianza kushauriana nini cha kufanya kutokana na matukio

yanayompata kijana wao ingawa hawakufikia mwafaka vizuri.

Siku ya kufanya mitihani ilifika, Ipanga na Masha walianza kufanya mitihani yao ya kuhitimu darasa la saba na kuimaliza salama. Walipomaliza mitihani walifanyiwa sherehe ya kuwaaga darasa la saba ambapo walimu wengi walifurahishwa sana na nidhamu pamoja na tabia njema waliyoionesha Ipanga, Masha pamoja na wenzake na walipewa zawadi mbalimbali. Wazazi wao walifurahi sana watoto wao kuhitimu salama elimu ya msingi. Sherehe ilipomalizika, wahitimu, wageni waalikwa, walimu na wanafunzi kwa ujumla walitawanyika kurudi majumbani kwao huku kila mmoja akiwa na furaha. Muda wote huo wazazi wa Iba na Ibe waliendelea kuwa na kinyongo, chuki na hasira ya kwa nini Masha amepona na nani kamponyesha. Pili. kwa nini watoto wao wasimamishwe masomo na kutakiwa kurudi kufanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba siku za mtihani tu. Mwisho, kwa nini Masha, Ipanga na rafiki zao wapewe zawadi nyingi kiasi hicho ikiwemo pongezi na zawadi kwa wazazi wao kwa kuwalea watoto wao vizuri.

Ilibidi walifikishe suala hilo kwa bibi Kikavu. Kikavu ni jina la mkuu wa wachawi katika kijiji hicho cha Kitale. Wachawi wenzake walimpatia jina hilo kwa sifa moja tu, akihitaji kumwua mtu hazipiti hata dakika tano mtu huyo anakauka. Walipoanza kumweleza, Kikavu akawacheka sana na kusema "Ninyi ni watu wa ajabu kabisa, siku zote kwenye vikao vyetu mbona hamjawahi kusema. Basi tusiongee sana, tuonane usiku kwenye kikao chetu." Baada ya kupewa hayo majibu waliondoka kwenda kujiandaa kwa ajili ya kikao cha usiku cha kichawi.

Kikavu ni mwanamke ambaye uzee ulikwishaanza kumnyemelea, kwa maana kwamba alikuwa hajawa ajuza. Hakuwa mrefu wala mfupi. Ngozi yake nyeusi inaonekana bado ni laini katika umri huo. Macho yake makubwa ambayo ni mekundu kiasi fulani, pengine kwa ajili ya moshi uliotokana na matumizi ya kuni ya muda mrefu katika kupikia. Kikavu ana kichwa kidogo naye hufunga kilemba cheusi wakati wa shughuli zake za kichawi au wakati wa vikao vyao. Mtu yeyote angekutana na bibi Kikavu wakati wa mchana, asingedhani kuwa alikuwa mwanamke katili

ambaye kwake, kuutoa uhai wa mtu au kumpoteza kichawi ilikuwa jambo dogo kabisa.

Ilipofika usiku, Kikavu alimwamuru msaidizi wake kupiga mbiu ya kichawi na kila mchawi akakimbia haraka kuwahi kikao na baada ya muda mfupi kikao kikaanza. Kikavu alianza kikao kwa kuwapa salamu nyingi sana za wachawi wenzao kutoka mataifa mbalimbali na akawakumbusha kuendeleza vema zoezi la kuwafundisha watu uchawi hususan wenye roho mbaya pamoja na watoto wadogo ili wajiunge kwa wingi pamoja na kuendelea kuua watu kwa wingi kwa ajili ya kupata mafuta ya binadamu kwa ajili ya shughuli za kichawi pamoja na misukule kwa ajili ya kuwafanyisha shughuli zao za kilimo, uvuvi na ufugaji. Akafafanua hapo, "Ukileta huku kuzimu watu ambao siyo kizazi chako ama watu wasio wa familia ama ukoo wako kujiunga nasi nakupandisha cheo tu. Lakini ukileta kuzimu ama ukiua kizazi chako ama watu wako wa familia ama ukoo wako hapo nakupandisha cheo mara mbili na kufanyiwa sherehe kubwa huku ukipata ofa ya kutembelea sehemu mbalimbali za kula raha na kukutana na wenzetu ikiwemo wa mataifa mbalimbali. Kwa hayo machache nadhani

tumeelewana vizuri. Haya sasa tuwasikilize wenzetu wanaoomba msaada, karibuni."

Mama Iba na Ibe walisimama, mama Iba akaanza kueleza, "Heshima mkuu wetu Kikavu, sisi kuna watu wanatunyima amani na raha kabisa. Walisababisha watoto wetu wakasimamishwa masomo kwa muda na kwenye sherehe ya mahafali wao wamesifiwa sana pamoja na watoto wao. Tunataka tuwalete huku kuzimu wawe wanatuimbia kabla ya vikao kuanza huku wakisubiri msimu wa mvua kuanza kutulimia mashamba yetu. Kikavu, libariki hili ombi langu." Kikavu akaagiza, "Hebu wavuteni wote kwenye kioo kikuu tuwaone hawa washenzi wanaotuletea jeuri." Baada ya hilo agizo kutoka kwa mwenyekiti wao wakaanza kuzivuta taswira zao zikaja. Kila familia ilionekana kwenye kioo mfano wa runinga kubwa sana isipokuwa familia ya mzee Utulivu yenyewe ilionekana ikiwa imetega mgongo na familia ya akina Masha walionekana wengine wote isipokuwa Masha alionekana akiwa chenga chenga. Hiyo hali ilimwudhi sana Kikavu na kuwauliza kwa hasira kuwa ni nani anayewafanya hao watu ambao hawaonekani sura zao na huyo anayeonekana chenga chenga kuwa hivyo?

Kikavu alijiinamia kwa dakika kadhaa huku akiwaza kwa kina kisha akakumbuka kitu na ikabidi aweke wazi na kusema, "Nisikilizeni! Tena mnisikilize kwa makini sana. Binadamu aishie juu ya hii ardhi kuna nguvu moja pekee ambayo anaweza kujivunia na nguvu hiyo ni ya maombi. Akifanya maombi thabiti na ya kutoka moyoni mwake kwa Mungu aishiye juu mbinguni na zoezi hilo likawa ni la mara kwa mara ndani ya maisha yake yote bila kujihusisha na dhambi yeyote ile, hakika anatufanya sisi kuishiwa nguvu tukiwa kazini na usipokuwa makini utakufa kabisa. Haidhuru anafanya maombi akiwa kwenye nyumba yao ya kuabudia, nyumbani ama kwenye shughuli zake za kila siku. Anaweza kuwa anafanya maombi kwa kutoa sauti ama kimya kimya. Sasa, ni nani huyo anayewafundisha haya yote! Tungekuwa na kikao kirefu kidogo ikiwemo kula nyama za binadamu, lakini ninaahirisha na ninagawa majukumu muda huu tutawanyike ili mimi nikamfuate huyo mshenzi na ikiwezekana kesho tumle nyama."

Kikavu aliinama tena chini kwa muda wa dakika chache huku akiomba sala na dua zake za kichawi kisha akaanza kugawa majukumu. Mmoja

miongoni yao akauliza, “Mkuru, kabla hujagawa majukumu, hawa ambao hawaonekani tunafanyaje?” Kikavu akajibu, “Kila siku ninapowaambia mtuletee kuzimu vizazi vyenu pamoja na watu wa familia na ukoo wenu huwa hamnielewi! Lengo kuu ninataka mpande vyeo na unapopanda cheo unafundishwa mbinu nyingine za juu zaidi. Kipindi ninainama hapa kuna watu nilikuwa ninawaomba waje kuwasaidia hilo suala ambalo ni dogo na kabla sijamaliza kugawa kazi watakuwa wamefika hivyo msihofu.” Kikavu alianza kugawa kazi kama ifuatavyo; “Mama Iba na Ibe wapelekeni watoto kundi la wanafunzi wakawachezee walimu pamoja na wanafunzi ambao sio wenzetu. Hakikisheni wanawachezea kweli kweli hususan walimu, kesho tukipita shuleni kuwasalimia kila mmoja alalamike mwili mzima unamwuma. Mkishawafikisha watoto nendeni kwa wazazi wa Masha, hakikisheni mnawapa magonjwa ya homa na kichwa kiwaume lakini sio sana sababu tunataka kuwapa miezi kadhaa ya kuishi ndipo waje huku kuzimu. Ninyi wawili mtaungana na watakaokuja mkashughulike na Masha pamoja na baba yake Ipanga. Jivu kashughulike na rafiki zake Ipanga wengine, hawa ninawahitaji huku kuzimu haraka sana.”

Kikavu alipokuwa akimalizia kugawa majukumu mara upepo mkali wa kimbunga ukavuma huku ukizungukia eneo walilopo, mara wakashuka baba wawili wa makamo na upepo ukakata. Kikavu aliwakaribisha kisha akawakutanisha na wale wawili waliokuwa wakiwasubiri. Walipeana ishara za vidole na vichwa kwa muda mfupi tu kisha wote wakapotea na kwenda kwenye shughuli waliyopangiwa. Kikavu alikwenda moja kwa moja nyumbani kwa mzee Utulivu na alipofika akatua kichawi juu ya paa la nyumba kubwa. Muda wote huo mbwa wake Ipanga alikuwa akishuhudia hilo tukio huku akiwa kimya.

Mama yake Ipanga alishtuka kutoka usingizini na kusikia juu ya paa la nyumba mchanga unamwagwa huku nafsi yake ikiwa na mfadhaiko mkubwa sana. Kwa vile hali hiyo haikuwa ya kawaida kwake, ilibidi ashuke taratibu kutoka kitandani hadi chini kisha akapiga magoti na kuanza kuomba. Aliomba kwa dakika chache tu nafsi yake ikatulia na kurudi kwenye hali yake ya kawaida, pia mchanga uliokuwa ukimwagika kwenye paa la nyumba nao ulikata. Kipindi mama Ipanga anaendelea kuomba, Kikavu aliishiwa

nguvu hadi kufikia hatua ya kutaka kudondoka chini. Wenzake walipata taarifa kupitia ishara zao za kichawi wakaja mbio ili waweze kumuokoa mwenyekiti wao. Walipofika walipitiliza na kurudi walipotoka baada ya kuona eneo lote la kiwanja cha Mzee Utulivu linawaka moto huku wakimshuhudia mwenyekiti wao akihangaika juu ya paa kwa kuungua moto. Aliendelea kuungua na hatimaye akadondoka chini kutoka kwenye paa la nyumba. Kishindo hicho cha kudondoka kiliwastua Ipanga na baba yake wakati huo mama yake alikuwa bado yupo macho ingawa alikuwa kisha panda kitandani.

Baba alitaka kunyanyuka kutoka kitandani atoke nje ila mke wake alimzuia na kumwambia asitoke nje sababu ya ile hali aliyoisikia. Mbwa alimsogelea Kikavu lakini Kikavu hakumwona kwa umbo la mbwa bali alimwona kwa umbo la tembo, kisha akamwambia kwa sauti kubwa, “Umefuata nini hapa? Usiponiambia ama ukinidanganya utakuwa majivu.” Kikavu, kwa sauti ya upole akajibu, “Ninahitaji roho ya Ipanga.” Mbwa akamwuliza, “Uipeleke wapi?” Kikavu akajibu, “Nimwue kichawi ili nimpeleke kuzimu akatusaidie kazi.” Mbwa akauliza, “Kazi gani mnayohitaji Ipanga

akawasaidie huko kuzimu?" Kikavu akajibu, "Yeye ana akili sana kwa hiyo tunataka akatufundishie vijana wetu huko kuzimu kwani tumeanzisha shule." Mbwa akauliza, "Kakukosea nini hadi umfanyie hivyo?" Kikavu akajibu, "Hajafanya kosa lolote na ni kijana mwema sana, ila familia yake ina majivuno sana hasa mama yake." Mbwa akauliza tena, "Kwa nini una roho mbaya kiasi hicho?" Kikavu akajibu, "Nisameheni tu kwani shinikizo kubwa la kufanya hivyo linatoka kwa ndugu wa kike wa damu upande wa baba yake. Ninaomba usiniue, ninaahidi kuacha tabia hii kuanzia sasa hivi." Mbwa akasema kwa hasira, "Uiache tabia hii na usije ukarudia tena. Jitahidi usimame na uondoke mara moja." Kikavu akajibu, "Ahsante na ninaondoka."

Kikavu aliondoka usiku huo kwa kutembea huku mwili wake ukiwa mtupu. Alipofika nyumbani kwake aliingia ndani na alipofika ndani alihisi kuishiwa nguvu mikono na miguu na baada ya muda mfupi tu vikapooza. Kutokana na hali hiyo ya kupooza, Kikavu alishindwa kabisa kuendelea na uchawi hali iliyopelekea wachawi wengine kukosa mwelekeo na hatimaye

kutawanyika kutafuta utawala mwingine wa kichawi.

Baada ya miezi kadhaa, matokeo ya kuhitimu darasa la saba yalipotoka, Ipanga na rafiki yake Masha walikuwa miongoni mwa wanafunzi waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ingawa walipangiwa shule tofauti. Ipanga, Masha pamoja na wazazi wao walifurahi sana kwa ufaulu huo. Wazazi walianza maandalizi ya vijana wao kujiunga kidato cha kwanza. Lakini kipindi hicho chote cha maandalizi ya kwenda shuleni, Ipanga aliwaza sana jinsi atakavyomwacha mbwa wake kwani alimzoea na alimpenda sana. Muda wa kwenda shule ulikaribia na kuwafanya wazazi wa pande zote mbili kukamilisha mahitaji ya vijana wao. Kipindi wakiwa kwenye maandalizi ya mwisho, baba yake Ipanga hakuwa na mashaka atakapoishi kijana wake kwani alikuwa na ndugu zake wa damu mjini wanaoishi kwenye nyumba yake ambayo ameijenga mwenyewe na kuwaruhusu waishi humo hadi watakapopata makazi yao. Pia kwa upande wa wazazi wa Masha hawakuwa na wasiwasi kwani kijana wao alipangiwa shule ya bweni.

Siku chache kabla ya shule kufunguliwa, Mzee Ipanga alifunga safari kwenda shuleni kumchukulia kijana wake fomu ya kujiunga ili aandae mahitaji yake. Alipomaliza kuchukua fomu, alipita kwa ndugu zake aliowapatia makazi kwenye nyumba yake sababu ni muda mrefu sana hajawatembelea, pia awaeleze na kupanga utaratibu ili kijana wake aishi hapo wakati wa masomo yake. Ndugu zake wote waliokuwa wanaishi kwenye nyumba yake walikuwa wanawake ambao ni dada zake. Dada yake mkubwa aliitwa Kuchi, wa kati aliitwa Nzile na wa mwisho aliitwa Gufa. Kuchi alikuwa mwanamke wa makamo, mrefu, mnene, rangi ya chokoleti na mwenye umbo pana. Kichwa chake kilikuwa kikubwa. Alipenda sana kusuka nywele zake. Kwa kuwa alikuwa mnene, hakuwa mwepesi katika kutembea. Mwendo wake ulikuwa wa taratibu. Alikuwa na tabia ya ukali, uongo na unafiki. Nzile ambaye alimfuata Kuchi kuzaliwa, naye pia ni mtu mzima. Nzile ana umbo dogodogo, kiasi kwamba usipomwangalia kwa makini, utadhani bado ni kigori. Kichwa chake kidogo, macho madogo na masikio madogo viliendana na umbo lake dogo. Anapenda kuwa na nywele fupi za kuchana. Hakuonekana kujipenda kama Kuchi. Tabia yake ni

ya upole na mara nyingi hakuwa msemaji sana. Gufa ni mwanamke wa makamo pia, mwenye umbo la kati. Hakuwa mrefu sana kama Kuchi. Ana macho ya wastani na kifua kipana. Ana nywele ndefu za asili kwa hiyo mara nyingi huzinyoosha na kuzifunga kwa nyuma. Nywele zake nyeusi, nzuri ziliviringana kama za kisomali. Kuchi, Nzile na Gufa walikuwa wakiishi pamoja katika nyumba ya kaka yao, yaani mzee Utulivu.

Walipomwona kaka yao walifuhi sana kwani ilikuwa ni kitambo sana hawajaonana. Kuchi akasema, "Karibu sana kaka, wewe ndiye ndugu yetu wa kiume pekee uliyebaki na tunajivunia sana kuwa nawe. Karibu sana." Mzee Utulivu akajibu, "Ahsante sana dada, ni muda mrefu sana hatujaonana na nimefurahi sana kuona mnaendelea vizuri." Gufa naye akasema, "Nasi tumefurahi sana ndugu yetu." Muda mfupi tu baada ya kaka yao kumaliza kunywa chai aliyotengewa, Kuchi alimwomba kijana anayeishi nyumba ya jirani amsaidie kumkamatia bata mmoja na kumchinja kwa ajili ya kitoweo cha mgeni wao. Kijana huyo alifanya hivyo na baada ya saa chache chakula (ugali na nyama ya bata) kilikuwa tayari mezani na mzee Utulivu akakaribishwa kuanza kula.

Mzee Utulivu alipomaliza kula, aliwaelezea dhamira kuu iliyo mpeleka hapo. Wote kwa ujumla wao walifurahi sana na Kuchi akasema, “Kaka jamani, ni vema umlete hata kesho.” Mzee Utulivu akajibu, “Hakuna shaka dada, ngoja niende kwani ninahitaji kupita mjini kwa ajili ya kununua mahitaji ya kijana kisha nirudi kijijini.” Alipotaka tu kunyanyuka, Nzile akamsihi, “Usiondoke kwanza kaka, kuna jambo ninataka nikwambie. Kuna mpangaji mmoja anatusumbua sana kulipa kodi ya nyumba.” Mzee Utulivu akawaeleza, “Jamani dada zangu, ninyi niliwakabidhi majukumu yote ya hapa nyumbani ikiwemo kupangisha hivyo vyumba ili hizo pesa zinazopatikana ziweze kuwasaidia kwa mahitaji yenu ikiwemo chakula. Licha ya hilo, wapangaji wenyewe hata siwafahamu na wao hawanifahamu kwani sikuwapangisha mimi. Mimi ninadhani cha kufanya, kama anawasumbua ulipaji wa kodi ya chumba, umeme na maji basi mtoeni tu ili mpangishe mwingine. Mie sitaki kabisa mpate shida yoyote ile nikiwa bado nipo hai. Nadhani mmenielewa vizuri!” Kuchi akajibu, “Ndiyo kaka, tumekuelewa. Unajua wewe ndiye ndugu yetu pekee na tulikuwa tunajaribu tu kukueleza ili utushauri.” Mzee Utulivu akasema, “Sawa dada

nimewaelewa ila jaribuni kufanya hivyo. Ngoja mimi niende."

Aliposimama na kuanza kutembea, Kuchi akasema, "Sawa kaka, mwanetu asijali kabisa kwani hapa ni kwao. Uliyotutendea na unayoendelea kututendea ni makubwa sana na kila siku huwa tuna kuombea kwa Mungu akupe maisha marefu wewe pamoja na familia yako yote." Mzee Utulivu akajibu, "Ahsanteni sana na ninafurahi kusikia hivyo kwani hata nasi huwa tunawaombea kila siku yaliyo mema maishani mwenu."

Mzee Utulivu alisindikizwa na ndugu zake kisha wakamwacha akaondoka. Baada ya kuondoka, dada zake walirudi nyumbani na walipoingia ndani ya nyumba wakaangua kicheko kikubwa cha furaha. Mmoja wao akasema, "Yaani hako katoto kake kamekwisha kutusumbua sana kuwafuata ndugu zake kuzimu. Kila mitego tunayoiweka inaharibika na kusambaratika kabisa. Sasa leo tunaletewa mikononi mwetu, Mungu wetu atupe nini kama siyo gunia la chawa, hahahahaaaa!!." Mwingine naye akasema, "We acha tu, tena tuangalie kama mboga imepungua tuchinje bata mwingine kwa ajili ya furaha kubwa tuliyonayo kwa ujio wa huyo mtoto." Mwingine naye akasema,

“Hebu tusifurahi sana tukapitiwa, tusubiri siku ya kikao chetu tutajadili vema hilo suala kwa sababu si mnaona hata kaka yetu (baba yake Ipanga) naye alivyo mgumu kuwafuata kaka zetu wengine walio kuzimu. Tumekwisha jaribu huku na kule lakini bado mambo hayaendi kama tunavyotaka. Lazima tutathimini vizuri huwa tunakosea wapi na ndiyo maana nawaambia haya ni mambo ya msingi sana lazima tuyajadili kwenye kikao tukiwa na wenzetu.”

Baada ya hilo wazo la mwenzao wote walikubaliana nalo ila kabla hawajatoka nje, mkubwa wao akawauliza, “Ratiba ya chakula chake na maji ya kunywa imekwenda kama kawaida?” Mmoja akajibu, “Ndiyo, kila kitu kimekwenda sawa. Bora kusahau kuweka chumvi kwenye mboga kuliko kusahau hicho kitu.” Mkubwa wao akafurahi na kusema, “Tunaendelea kusisitizwa sana na wakubwa wetu juu ya suala hilo. Mtu tunayemuhitaji kuzimu cha kwanza lazima alishwe na aendelee kulishwa chinuzi (dawa ya kumpumbaza akili) kupitia chakula tunachomwandalia ama maji ya kunywa. Hii inamkata nguvu ya kuwaza zaidi ikiwemo na nguvu ya kufanya maombi kwa Mungu wao aliye

juu mbinguni.” Baada ya kuhitimisha mazungumzo hayo, wote walitoka nje na kuendelea na ratiba zao za kawaida. Mzee Utulivu alifika mjini, akanunua baadhi ya vitu vya nyumbani kwake kisha akavuka kuelekea kijijini kwake. Alipofika kijijini aliikuta familia yake inaendelea vizuri kisha akamwambia kijana wake Ipanga ajiandae baada ya siku mbili ataenda shuleni kuripoti ili aanze masomo yake ya sekondari na atakuwa anaishi kwa ndugu zake muda wote huo wa masomo yake. Ipanga alianza maandalizi ya kwenda shuleni huku akimwazia mbwa wake jinsi ya kumuacha.

Hatimaye siku iliwadia, mzee Utulivu alimuaga mke wake tayari kwa safari. Ipanga naye alimuaga mama yake kwa kumkumbatia kisha akaelekea kwa mbwa wake kumuaga. Alipomkaribia mbwa wake, mbwa akapiga magoti huku akimtazama Ipanga usoni kisha akadondokwa na machozi. Kitendo hicho kilimshangaza sana Ipanga pamoja na wazazi wake. Ipanga alimshika kichwani kisha akaondoka huku akiwa na huzuni kwani alikwisha mzoea sana. Alipopiga hatua chache tu mama yake akamwita, “Ipanga mwanangu!!” Ipanga akaitika, “Naam mama.” Mama akaendelea kuzungumza, akasema, “Ipanga, ujitahidi sana katika masomo

yako na usiache kumwomba Mungu akusimamie." Ipanga akajibu, "Sawa mama, nimekuelewa vizuri." Mama Ipanga akasema, "Ahsante kwa kunielewa mwanangu, niwatakie safari njema." Wote kwa pamoja wakaitikia, "Ahsante na ubaki salama."

Walianza safari kuelekea mjini na walipofika walikwenda moja kwa moja hadi shuleni kukamilisha taratibu zote ikiwemo malipo ya ada. Walikamilisha malipo yote hapo shuleni kisha wakaelekea nyumbani ili mzee Utulivu amkabidhi kijana wake kwa ndugu zake. Walifika na kukaribishwa kwa furaha na bashasha kubwa. Walianza kumsifia sana kijana kwa jinsi alivyokuwa mkubwa na mwenye akili sana wakati huo wakiandaa taratibu za chakula ikiwemo kuchinjiwa bata kwa ajili ya kitoweo. Mmoja wao alimwita Ipanga, akisema "Ipanga, wewe ni Ipanga kweli kweli! Njoo huku mwanangu nikuoneeshe chumba chako." Ipanga akanyanyuka na kuelekea kwenda kuoneshwa chumba alichoandaliwa. Alipofika chumbani akaambiwa ajiandae akaoge kwani maji ya moto ya kuoga yamekwisha andaliwa kwa ajili yake kutokana na hali ya mawingu iliyokuwa imetanda siku hiyo.

Moyoni mzee Utulivu alifurahi sana kuona ukarimu anaooneshwa mwanaye. Wakati huo huo mmoja wao akauliza tena kwa sauti, “Jamani mtu wa jikoni umefikia wapi kuhusu chakula? Kijana wetu atakuwa ameanza kuhisi njaa, ninataka amalize kuoga tu ale chakula kwani yuko kwao hatakiwi ajibane bane mambo ya chakula.” Mzee Utulivu akamwambia, “Kijana atakula tu, kwanza ndio katoka kunywa uji na sasa ndio mchana unafika.” Kuchi akamjibu, “hapana kaka, inatakiwa ale muda huu kwani nyie mmezoea mambo ya kijijini kwenu ya kijibanabana kula chakula lakini huku mjini mambo yetu ni chapu chapu.

Sura ya Tatu

Ipanga alipomaliza kuoga walikaa dakika chache tu chakula kikawa kimeiva. Kipindi chakula kinapakuliwa, mkubwa wao akasema kwa sauti, “Pakueni mapaja yote ili Ipanga naye ale paja.” Muda wote huo Ipanga alikuwa akisoma mazingira ya hapo nyumbani atakaposomea pamoja na upendo mkubwa anaooneshwa na ndugu wa baba yake. Walitengewa chakula wakala na baada ya kumaliza kula Ipanga akanyanyuka kutoa vyombo avipeleke jikoni, mara sauti ya mmoja wao ikasikika, “Mwenetu, acha kwanza. Tunamalizia kukukaangia mayai ule kabisa.” Ipanga akasema, “Sengi, nahisi nimeshiba.” Mkubwa wao akasema, “Hapana, tulipewa taarifa yako kuwa uliugua sana, hivyo ni lazima ule sana vyakula vya kuujenga mwili wako ili ukae vizuri. Pia huku utakuwa unakula vyakula hivyo mara kwa mara.”

Ipanga hakuwa na pingamizi ingawa alikuwa anajihisi kushiba sana lakini ilibidi ale mayai aliyoletewa. Huku akiendelea kuyatathimini pole pole mazingira ya mji huo wa baba yake, aliendelea pia kufurahia ukarimu wanaomuonesha. Baada ya kumaliza kula mzee Utulivu aliaga tayari kwa kuanza safari ya kurudi kijijini kwake. Mzee

Utulivu akaaga kwa kusema, “Ahsanteni sana kwa chakula na ninaombeni niende kuwahi usafiri wa huko kwetu kijijini.” Kuchi akauliza, “Kaka mbona haraka hivyo, usafiri wenu upo tu utaukuta.” Mzee Utulivu akajibu, “Hapana dada, bado nina safari ya kupita mjini kununua vitu vya huko kwangu.” Pia akamwambia kijana wake Ipanga, “Kwa chochote utakachohitaji kuhusu shule ama matumizi binafsi, mwambie dada mkubwa atakutimizia.” Ipanga akaitikia, “Sawa baba.” Kipindi mzee Utulivu anasindikizwa na ndugu zake alimwachia Kuchi pesa nyingi kwa ajili ya matumizi ya mwanaye kisha akaondoka.

Alipofika nyumbani kwake kijijini alimweleza mkewe alivyokamilisha taratibu za shuleni kwa kijana wao na upande wa ndugu zake. Pia akaongeza, “Mke wangu, sijui nikwambie nini! Hao ndugu zangu huwa wanatupenda sana na pia ni watu wenye moyo wa pekee kabisa. Kijana wetu ataishi hapo kwa amani na raha sana. Niliwahi kukueleza jinsi nilivyowasaidia. Mzee wetu alifariki mimi nikiwa kijana mdogo kwenye familia kwani kaka zangu walikuwa wamekwisha anza maisha ya utafutaji na walikuwa wamekwisha toka nyumbani. Mara nyingi nilikuwa bega kwa bega na baba

hususan kwenye shughuli zake za kila siku ambazo ni kilimo na uvuvi. Lakini kabla baba hajafariki (kipindi anaumwa), alinieleza kuwa mimi ndiye kijana nitakaye linda mji wake na nihakikishe ninawasaidia hawa dada zangu. Hivyo baada ya baba kufariki, nilihakikisha ninawasaidia kupata elimu kwa wale waliohitaji akiwemo yule kaka yangu aliyefariki miaka mingi iliyopita. Wapo waliosoma kweli lakini wakaishia njiani na wengine hawakuweza kusoma kwa ajili ya umri kuwa mkubwa.

Lakini haikuishia hapo, nilihakikisha ninawapa matunzo hadi ikafikia hatua ya kupata waume na hatimaye wote wakaolewa na kuanza maisha yao. Baada ya kuhakikisha dada zangu wapo kwenye miji yao na kaka yangu yupo chuoni ndipo nilipoamua kutoka nyumbani kwenda kutafuta mali sehemu ya mbali na ndipo nikaja kuanzisha makazi hapa tulipo. Baada ya muda nilipata taarifa kuwa dada zangu wapo kijijini Mizeye tulipokulia, ilibidi niende kujua nini kimewasibu kwani ni muda mrefu ninasikia wapo hapo kijijini. Nilifika na wakanieleza kuwa wameachika kutokana na manyanyaso ya waume zao na walikuwa wanahangaika huku na kule. Mizeye ni kijiji

kingine katika Kisiwa cha Upendo ndani ya ziwa Pwezi. Kilikuwa umbali kama wa kilometa kumi hivi kutoka Kijiji cha Kitale.

Niliwaonea huruma sana kwa hizo changamoto kisha nikaamua kurudi kwangu. Wakaja kwangu tena kila mmoja kwa nafasi yake wakinililia kuwa wana shida, kwani wamekuwa wa kuzurura tu, ndipo nilipoamua kutoa wapangaji wote kwenye nyumba hiyo ya mjini nikawakabidhi wao wajichagulie vyumba waishi hapo. Vyumba vilivyobaki niliwaambia wavipangishe ili pesa ya kodi waitumie kwa matumizi madogo madogo ya kila siku. Pia kila mmoja nilimpatia pesa nyingi tu ili kuanzisha maisha ama shughuli ya kujipatia kipato. Sikuishia hapo, bado nikawaeleza yeyote atakayekwama sehemu kuhusu pesa asisite kunieleza ili nimpatie pesa nyingine." Mama Ipanga akajibu kwa mshangao, "Kumbe mme wangu! Mengine nilikuwa nimekwishayasahau na umenikumbusha. Huo ni upendo mkubwa sana kwa ndugu zako na inatakiwa iwe hivyo kwani maisha ya leo ni kusaidiana kwa nia na lengo moja la kukuza na kuimarisha undugu." Mzee Utulivu akasisitiza, "Kweli kabisa mke wangu. Pia unaona hapa kijijini tunavyowasaidia watu mbalimbali

kulingana na kipato chetu kilivyo." Mama Ipanga akaongeza, "Kweli mume wangu, ninaona hata hubagui jinsia, rangi wala kabila. Ndiyo maana watu wanakuheshimu sana. Karibu ukaoge mume wangu, maji yapo tayari bafuni." Mzee Utulivu akajibu, "Sawa mke wangu, ngoja nijiandae kwani nimechoka sana kwa sababu ya safari."

Ndugu zake mzee Utulivu walipanga kukutana na kufanya kikao chao cha kichawi pamoja na washirika wao wengine. Kwa kuwa kikao hicho kilikuwa cha kufunga mwaka wao, walihitaji kuhamasishana ili wasitishe shughuli nyingine zote za kichawi wahudhurie kwa wingi kwani walihitaji kujadili ajenda zote za mwaka na utekelezaji wake. Kikao hicho kikubwa kinapofanyika huwa kinahitaji uwanja mkubwa, chakula cha kutosha pamoja na viburudisho vya ngoma.

Usiku huo walikutana kwanza wajumbe wa kamati ya maandalizi wakiongozwa na mwenyekiti wao ambae ni Kuchi. Mwenyekiti akasema, Nimewaiteni hapa kwa dharura ili tupange kikao chetu kikuu tunakifanyia wapi na tunakiandaaje kwani wajumbe ni wengi sana na hadi tumealika wageni wengine kutoka mataifa mbalimbali." Mjumbe mmojawapo aitwae Zaza akasema,

“Mwenyekiti, ni vizuri kikao tukifanyie kwenye uwanja wa Mateso.” Mwenyekiti akadakia, “Nimepita jana nimeona kuna vijishenzi vimeweka hapo mahubiri ya Mungu wao, havitatubughudhi?” Mjumbe mwingine aitwae Didi akajibu, “Mwenyekiti, nimekwisha kwenda kuwapima imani juu ya Mungu wao aishie juu na kukuta haiko thabiti sana, hivyo kuwatawanya ni kazi ndogo tu.” Mwenyekiti akauliza, “Kazi ndogo kivipi?” Didi akajibu, “Mwenyekiti, hao nitawaachilia kimbunga tu, kitawatawanya na uwanja utabaki wazi.” Didi na Zaza ni watu wa rika moja. Katika umri wao wa kati, wakiwa wameolewa karibuni, isingekuwa rahisi kuamini kuwa walikuwa tayari ni wachawi waliokubuhu. Ni wanawake wanaojiamini sana na walipenda kuonekana kuwa wanajituma katika shughuli zao za kichawi.

Mwenyekiti akasema, “Kuna mmoja alitaka kuniaibisha, alisema kuwa ataachilia kimbunga na mwisho wake hakufanikisha kama tulivyokuwa tumepanga. Ilibidi nitumie nguvu ya ziada nikaongeza utaalamu mwingine wa radi ndio tukafanikiwa. Unanihakikishiaje kuwa hutaniangusha?” Didi akajibu, “Mwenyekiti, Juzi tu

nimetoka kuongeza utaalamu juu ya kimbunga na jaribio la kwanza ni lile la kusambaratisha nyumba za ule mtaa wa mzee Uchovu pamoja na shule iliyopo jirani. Sasa sembuse hako kamkutano na anayetoa neno hana hata imani thabiti! Mwenyekiti, hapo sihitaji hata msaada wa aina yeyote ile."

Mwenyekiti akasema, "Nilikuwa ninakupima, ninaona sasa umekomaa. Kikao ni kesho na kitaanza saa tano usiku, wageni wanaanza kufika saa kumi na mbili jioni. Hakikisha hao watu wanatawanyika uwanjani hapo mapema jioni ya hiyo kesho. Vipi kuhusu kitoweo? Maana yake inahitajika nyama ya siku hiyo hiyo kutokana na heshima ya wageni tutakaokuwa nao." Zaza akajibu, "Mwenyekiti, kuhusu kitoweo, tukipata watu watano watatutosha." Mwenyekiti akauliza, "Tutawapataje?" Zaza akajibu, "Mwenyekiti, kwenye orodha yetu tuna watu ishirini. Tutakata watano kwa njia za dharura kama ifuatavyo; wawili kwa ajali ya gari, mmoja kwa kujikwaa na kuangukia kichwa na kufa hapo hapo, mmoja ajinyweshe sumu na mmoja atapike damu." Mwenyekiti akatikia kwa kichwa na kusema, "Sawa, nimekuelewa ila hakikisha ni wale wenye afya nzuri na wanono. Mafuta ya kupikia tutapata

wapi?”Akauliza. Zaza akaendelea, “Mwenyekiti, mafuta hayana shida, wenzetu walio wauguzi katika hospitali kubwa watatuletea watoto kumi wachanga waliozaliwa siku hiyo hiyo ili tupate mafuta yaliyo safi.”

Mwenyekiti akakubaliana nao kwa kusema, “Sawa, nimewaelewa vizuri. Kuna kitu nilitaka kusahau, viti vya kukalia je?” Didi na Zaza wakatabasamu kisha Didi akasema, “Mwenyekiti, hilo nalo ni swali la kuuliza? Kila mjumbe atapita katika kaya mojawapo usiku huo huo na kunyanyua hao binadamu kwa ajili ya kuwakalia migongoni wakati kikao kinaendelea kama ambavyo huwa tunafanya tunapokwenda kulima mashamba makubwa. Vichutu (misukule) vyetu vitakuwa na kazi za hapa na pale kuhakikisha kuni, maji, n.k vinakuwa sawa.” Mwenyekiti akasema, “Sawa nimekuelewa. Lakini nitaendelea kuwaambia na mkawaambie wajumbe wengine pia kuwa wawe makini ili wasije kudondoka ama kuganda ama kuishiwa kabisa nguvu na kudondoka ambapo inaweza kupelekea kupoteza maisha. Ndiyo maana huwa ninawaambia kabla hujaingia kichawi kwenye kaya ama nyumba yoyote ile ukiwa kazini, ni vizuri kujenga mazoea

na wanafamilia wa hiyo kaya ama mji ukiwa katika hali ya kiubinadamu ili upime uzito wa imani ya wanakaya hao kwa Mungu wao." Didi na Zaza walitii maelekezo ya mwenyekiti wao na kutawanyika kuendelea na majukumu mengine waliyokuwa nayo usiku huo ya kuhakikisha kila kitu kinakuwa tayari kwa ajili ya sherehe yao ya kufunga mwaka.

Kesho yake maandalizi yalizidi kupamba moto na ilipofika saa kumi jioni kila kitu kilikuwa kipo tayari wakati huo anga likiwa limetapakaa wenyeji na wageni kutoka sehemu mbalimbali. Wakati huo kwa hali ya kawaida wageni (wachawi) hao waliotapakaa angani walikuwa wanaonekana kama ndege wa aina mbalimbali ingawa wengi wao walikuwa mbayuwayu na mwewe huku anga likiwa na hali ya mawingu mepesi. Ilipofika saa kumi na moja jioni wakati uwanjani pale mahubiri ya neno la Mungu yakiendelea, ulivuma upepo wa kimbunga mkali sana ukiambatana na mvua kubwa na kusababisha jenereta kukatika umeme, watu waliokuwepo pale uwanjani walikimbia na kusababisha mahubiri ya neno la Mungu kuishia hapo. Hapakuwa na maandalizi yoyote juu ya kujikinga na mvua kwa sababu ya msimu wa

kiangazi kwa wakati huo. Mvua iliendelea kunyesha eneo hilo la uwanja kwa muda wa dakika kadhaa tu wakati maeneo yote yanayouzunguka uwanja huo yakipata manyunyu na upepo kiasi.

Wakati huo wote mwenyekiti na wajumbe wake wa kamati ya maandalizi walikuwa wakiwasiliana kwa haraka sana mithili ya umeme usafirivyo kuhakikisha ratiba inakwenda kama ilivyopangwa. Mwenyekiti akasema, “Didi, kazi nzuri sana. Sasa ni saa moja kamili na ninazidi kupokea wageni wapya, nina wasi wasi na kitoweo kinaweza kupungua. Inabidi mtembelee bucha zilizopo hapa mjini kuongeza nyama ya ng’ombe waliochinjwa leo. Kwenye karakana ya nyama kuna nyama ya vichutu na mbwa mwitu za jana?” Didi akajibu, “Ndiyo mwenyekiti ila ni chache sana.” Mwenyekiti akaamuru, “Agiza haraka wenzako watano wakazibadilishe huko mabuchani, wachukue za ng’ombe na kuwaachia hizo. Pia hakikisha hao binadamu wanakuwepo wengi kwa ajili ya kuwafanya viti vya kukalia. Nadhani tumeelewana?” Didi akajibu, “Ndiyo mwenyekiti na ngoja niondoke muda huu nikashughulikie suala hilo.”

Baada ya kutoa hayo maagizo, mwenyekiti alirudi nyumbani kwa ajili ya kujiandaa kwa kikao kwani muda wa kuanza kikao ulikuwa unakaribia. Alipomaliza kujiandaa, alijaribu kumchukua Ipanga kichawi ili naye akawe kiti chake cha kukalia akashindwa kwani ghafla Ipanga alibadilika na kuwa mbwa. Kitendo hicho kilimkasirisha sana kwani alijaribu kila aina ya utaalamu wake wa kichawi alionao lakini ilishindikana kumchukua na kuamua kuondoka kwa hasira. Ilipofika saa sita kamili usiku, mwenyekiti alifungua kikao akiwa na ajenda kuu mbili tu ambazo ni kuongeza idadi ya wanachama wachawi na kuwapandisha vyeo waliofanya matukio makubwa na ya kutisha ndani ya mwaka huo. Hizo ajenda zilifuatiwa na sherehe ya kula nyama pamoja na kunywa damu za watu na mwisho kutawanyika na kuondoka.

Mwenyekiti alianza na ajenda ya kwanza kisha akaruhusu mjadala kuchangia hiyo ajenda. Mjumbe mmoja akanyoosha mkono na kuruhusiwa kujadili, akasema “Mwenyekiti mtukufu, binafsi naona tuongeze jitihada kubwa sana kwa watoto wadogo wakiwemo wanafunzi. Sababu watu wazima walio wengi wamekuwa wakitusumbua sana.

Wanapomwomba Mungu wao tunapata shida sana ikiwemo kuishiwa nguvu na wakati mwingine kupoteza maisha. Pia wanakuwa na malaika wao ambao wakati mwingine wanatuunguza na kutupotezea mwelekeo hata kupelekea kudondoka ovyo tunapokuwa angani kwenye kazi zetu. Lakini watoto wadogo wanakuwa hawawezi kujisimamia kwani wanategemea maombi ya wazazi wao ambao wanakuwa na shughuli nyingi za kimaisha na hawapati muda wa kuwaombea."

Mwenyekiti akawauliza wajumbe kwenye hicho kikao, "Ndugu wajumbe, mnasemaje kutokana na hiyo hoja?" Wajumbe kwa wingi wao wakasema, "Mkuru, hoja imepita." Mwenyekiti akawauliza tena, "Tutumie mikakati gani kuwaingiza kwenye uchawi?" Mjumbe mwingine akajibu, "Mkuru mwenyekiti, kwanza tuhakikishe tunaitekeleza vema kanuni yetu isemayo kila mtoto wa mwanachama lazima awe mwanachama mwenzetu huku kuzimu na mtoto atakayekataa lazima atengenezewe mikosi yaani awepo wepo tu kwenye ulimwengu wao bila kufanikiwa kwa chochote hadi hapo atakapojifia mwenyewe ama hadi hapo atakapohitajika kutusaidia shughuli zetu huku kuzimu." Mjumbe mwingine tena akajibu, "Mkuru

mwenyekiti, tuongeze jitihada za kuwakatalia ama kuomba mtoto ama watoto hata kwa kulaghai na kulazimisha tukitumia njia ya kuwalea. Watakapokuwa nyumbani kwako ni rahisi sana kuwafundisha uchawi na hatimaye kuwaunga kuwa wanachama wa huku kuzimu."

Mjumbe mwingine tena akajibu, "Mkuru mwenyekiti, hata kama tukikosa kabisa mtoto ama watoto wa kuwalea basi tujitahidi kujifanya kuonesha ukarimu na upendo wa hali ya juu kwa mtoto ama watoto wa jirani zetu ili tuwe nao karibu kwa kuwatembelea kwenye kaya zao ama wawe wanakuja kwenye kaya zetu. Muda huo ni fursa kubwa kwetu kuchota nyayo zao za miguu pamoja na vitu vingine kutoka kwenye miili yao tayari kwa kumlainisha ama kuwalainisha na hatimaye kumchukua usiku kutokea kwao na kuanza kumfundisha mambo yetu ya kuzimu ili awe mwanachama." Mjumbe mwingine naye akajibu, "Mkuru mwenyekiti, tutumie watoto wetu walio wataalamu ili kuwafundisha wenzao mambo yetu ya kuzimu hususan wanapocheza pamoja mtaani ama shuleni ama kwenye kaya zao. Kwao ni vyepesi sana kuwapata watoto wenzao na kuanza pole pole kuwachezesha michezo yetu ya kuzimu."

Baada ya mikono iliyonyooshwa kuisha, mwenyekiti akasema, “Nadhani kwa sasa hakuna tena mawazo mapya. Naomba niwaulize wajumbe, mnayaonaje haya mawazo ya wenzetu?” Wajumbe wote kwa pamoja wakasema, “Heshima iliyotukuka Mkuru!” wakimaanisha wanakubaliana na hayo mawazo na utekelezaji uanze mara moja. Mwenyekiti akaendelea kusema, “Sawa, mawazo nayapitisha na yaanze kufanyiwa kazi kuanzia sasa. Pia dumisheni tabia ya kutembelea familia mbalimbali zikiwemo za majirani zenu huku mkipima imani ya wanakaya hao kwa Mungu wao kama ni thabiti ama siyo thabiti. Fanyeni hivyo mkiwa kwenye hali ya ubinadamu. Hata kama kaya haina mtoto ama watoto, jengeni mazoea na wakubwa wa hizo kaya ili iwe vyepesi kuwatupia mikosi ili kwa kila wanachokifanya chenye kuleta maendeleo yao kikwame na kisifanikiwe kabisa. Nisisitize tena hapo hapo, msisahau kuwa mnawauliza historia zao ikiwemo majina yao hasa ya ukoo na chimbuko lao ikiwemo idadi ya ndugu zao, mahali walipo na wanafanya nini. Hii si mnafahamu huwa inaturahisishia tunapomhitaji mtu kwa kazi zetu za kuzimu iwe nyepesi kumchukua. Huwa kila siku tunaambiana na leo narudia tena kuwa ni sisi tu wenye nguvu za

kuzimu wenye maisha mazuri kwani huku tulipo tunapata tunachokitaka na kwa muda wowote tunaotaka. Tofauti na ajali wanazotusababishia hawa washenzi wanaojidai huko duniani kupitia Mungu wao, umewahi kusikia sisi tunakufa hovyo! Mrungu wetu ni mkubwa sana na anatulinda muda wote ndiyo maana tunapotaka kuwaua wao kwa ajili ya nyama na damu inatuchukua dakika chache tu bila kujali njia gani utaitumia. Pia hapa mlipo kila mtu ana usafiri wake (ungo ama fisi), unaweza kwenda sehemu yeyote ile bila bughudha yoyote yule. Barabara yetu ni anga ambapo hakuna mabonde wala milima wala askari wa barabarani na vikwazo vingine vyovyote vile."

Baada ya mazungumzo mwenyekiti alisoma ajenda nyingine ambayo ni upandishwaji wa vyeo kwa wale waliofanya matukio magumu na makubwa yenye kutisha kwenye ulimwengu wa kawaida ikiwemo ajali kubwa za majini na nchi kavu, kuvuruga na kuua familia, utengenezaji wa magonjwa makubwa makubwa ya kisasa mfano ukimwi, kisukari, shinikizo la damu, n.k. Shughuli hiyo ya kupandishwa vyeo iliendeshwa na mgeni rasmi ambaye ni mchawi mkuu kitengo cha

kuvuruga maisha ya watu hususan wenye mali na ndoa.

Gagula, mgeni rasmi, mchawi mkuu maarufu kutoka ughaibuni, ni mwanamke mwenye umbo la kuvutia. Aliongoza ukanda mzima wa Kaskazini, Kaskazini Mashariki, Mashariki, Kusini Mashariki na Kusini. Mara nyingi alipata mialiko maalum iliyo na matukio na mipango mizito ya kichawi. Alipanda vyeo hatua kwa hatua na kufikia uongozi huo mkubwa wa ukanda huo. Ni mwanamke mwembamba mrefu, mwenye shingo ndefu kama ya twiga, anayetembea kwa mikogo. Vidole vyake viwili vya kati vya mikono yote miwili vilikuwa na pete kubwa katika kila kidole cha kati cha kila mkono. Kidole chake cha kushoto cha pete kilipambwa na pete ya angavu. Wasifu wake wa nje haukusadifu kabisa wasifu wake wa ndani. Alikuwa mwanamke katili sana, aliyepanda vyeo kwa kuua idadi kubwa ya watu kwa njia mbalimbali. Hata wale waliokuwa wameshindikana kuwatoa uhai. Gagula alikuwa na uwezo mkubwa sana wa kuleta madhara kwa aina mbalimbali. Alihusika sana pia kuangamiza karibu nusu ya familia yao akianza na wazazi wake wote wawili na ndugu zake ili kujiimarisha kichawi. Huyo ndio mwenyekiti wa wachawi wa ukanda wote huo.

Mgeni rasmi alianza kwa kusema, "Ahsante sana mwenyekiti kwa kuendelea kupanda vyeo hasa

kwa kila kitengo. Wajumbe, kabla sijaanza zoezi la kugawa vyeti niseme haya machache kuhusu mwenyekiti. Mwenyekiti wenu Kuchi ana umri mkubwa sana, wakati huo hana hata mtoto mmoja. Lakini mnamwona anapanda vyeo kila mwaka sababu ya kutoa sadaka kuzimu kwa kutuletea ndugu zake wa damu ama watoto wa ndugu zake wa damu. Nanyi igeni mfano huo ili mpande vyeo, kupanda vyeo kuna heshima na raha yake. Nadhani mmenielewa vizuri. Hongera sana mwenyekiti. Sasa nianze kuwapandisha vyeo wanaostahili akiwemo mwenyekiti wenu."

Ilipofika usiku wa manane, zoezi la upandishwaji vyeo na kugawa vyeti vya kichawi lilikamilika na mwenyekiti akafungua sherehe ya kula nyama za watu na kunywa damu za watu. Ilipofika saa tisa usiku, wajumbe walianza kutawanyika na shughuli ya kuwarudisha binadamu waliotumiwa kama viti ilianza. Ilipofika saa kumi usiku kila kitu kilikuwa kimemalizika na kila mchawi akiwemo mwenyekiti walielekea kwenye kaya zao. Lakini muda wote huo, mwenyekiti alikuwa akimuwazia sana Ipanga kuwa ana nini hadi anashindwa kufanikisha mipango ya kichawi dhidi yake. Akawa anawaza mwenyewe

moyoni mwake, “Mimi na wadogo zangu ninaoishi nao pamoja na wenzetu wote tumefanikisha kumteketeza kila mmoja ndani ya ukoo wetu aliyeibuka akiwa na nyota inayong’aa ama aliyejifanya ameanza kuinuka kiuchumi ama mwenye akili ya kimaisha ikiwemo kufanya vizuri katika masomo yake shuleni ama chuoni, wote hao waliishia kuzimu. Sasa huyu kijana anataka kutufanya kama tunavyohangaika na baba yake! Wakati kaka na dada zake hawakutuhangaisha kiasi hiki, tulifanikisha kuwapeleka kuzimu tena kwa kutumia magonjwa mepesi mepesi tu! Lakini huyu kijana hadi tumetumia majeshi yetu ya ziada na tukamtengenezea ugonjwa wa kutokewa upele mwili mzima uliomsababishia vidonda ndugu ambavyo angeishi navyo kwa muda wa miaka miwili. Hii ni kutokana na mitambo yetu tulivyokuwa tumeiseti ili baba yake atumie pesa zake zote ikiwa ni pamoja na kuuza mali zake zote, yaani afilisike kwa sababu ya kutumia gharama kubwa za matibabu ya huyu anayejifanya mwanae kipenzi. Lakini kilichonishangaza ghafla tu akawa amepona na huku mtambo wetu ukionesha giza totoro. Yaani mimi kabisa mimi (huku aking’ata vidole vyake), nitahakikisha ninamteketeza Ipanga hata kwa gharama na nguvu yoyote ile. Leo hii

inabidi tukae kikao na wenzangu tena cha mchana kweupe tuone nini tukifanye kwani hii sasa ni dharau na fedheha kubwa sana kwangu."

Kulipopambazuka, Ipanga alijiandaa na kwenda shule kama kawaida lakini ndugu wa baba yake waliarifiana wakutane mchana kujadili jinsi ya kumshughulikia Ipanga pamoja na baba yake. Ilipofika mchana wakakutana na kuanza kujadili kwa kina mikakati yao. Kuchi akasema, "Jamani, mmehakikisha mmetawanya dawa uwanja mzima ili yeyote atakayekuja apumbazike akili na aghairi kubisha hodi hadi tutakapomaliza kikao chetu?" Gufa akajibu, "Ndiyo, nimechanganya na ile dawa ya kujikwaa na kuanguka." Kuchi akasema, "Huyu kijana na baba yake wamekuwa gumzo kwetu, tufanyeje jamani?" Nzile akasema, "Mimi wazo langu tuendelee na dawa za kumlisha, kumnywesha na nyingine alalie kwa muda wa miezi sita hivi tuone maendeleo yakoje. Tukienda haraka sana itakuwa mapema sana na jamii itatushtukia kuona mabadiliko ya haraka haraka kwa kijana wakati ni mgeni. Lazima tumpambe kwa watu wanaotuzunguka kuwa ni kijana mzuri, mwenye akili na ndiye jicho pekee la kaka yetu na sisi pia kwani tunampenda sana." Kuchi akashauri,

“Lakini tukiwa tunafanya hivyo lazima mmoja kati yetu aende huko kijijini ili kumvuruga kichwa baba yake ili tutakapo kuwa tunamtengenezea mwanae hoja mbaya na za kumusingizia akubaliane nasi!.”

Nzile akaongezea, “Siyo kumvuruga kichwa tu, inatakiwa alishwe dawa hata za kumchukia mke wake na kumwona kama taka taka kwani anajifanya kama kafika. Kwa ufupi tu ndoa yake ivunjike kabisa.” Kuchi akampongeza, “Safi sana mdogo wangu, kumbe una akili kiasi hiki! Ndiyo maana huwa ninawapenda sana. Sasa nani aende huko kijijini?” Nzile akapendekeza, “Acha huyu mdogo wetu aende na mimi nibaki nikimwongezea nguvu pale atakapokwama.” Kuchi akauliza, “Unasemaje mdogo wetu?” Gufa akajibu, “Hakuna shaka kabisa, hakikisheni mnaniandalia makombora mazito na ya kutosha.” Wote wakacheka kisha Kuchi akahitimisha, “Hilo usiwe na shaka kwasababu awamu hii hatutaki mzaha. Unatarajia kuondoka lini?” Gufa akajibu, “Kesho kutwa, leo usiku nitamalizia kazi ya kumtia ukichaa kijana wa mama Makanyaga anayejifanya anapenda sana elimu na eti msomi wa chuo kikuu anayetaka kumkwamua mama yake huyo mjane kimaisha wakati mimi ninataka awe mtu wa dhiki

tu kila kukicha, hee! Hee! Heee!. Kesho nitamtazamia kama kichaa kimeanza kumpanda halafu kesho kutwa ndipo nitaondoka." Kuchi akasema kwa furaha, "Safi sana. Sasa nisikilize kwa makini sana, ukifika huko hakikisha unaonesha upendo wa kinafiki wa hali ya juu sana hususan kwa mke wake. Hakikisha unakuwa naye bega kwa bega hasa jikoni katika kuandaa vyakula ili upate nafasi nzuri ya kuweka dawa kwa kila chakula kinacho andaliwa. Mengine tutakuwa tunafahamishana jinsi hali halisi ilivyo tutakapokuwa tukikutana kwenye vikao vyetu. Sisi hatuna neno na siku zote nguvu zetu za kuzimu ni kali, kupitia Mrungu wetu tunayemuabudu na kumtukuza tutashinda."

Walimaliza mipango yao kisha wakatawanyika na kila mmoja akaendelea na majukumu yake. Kesho yake kijana wa mama Makanyaga akaanza kuwa anaongea mambo mengi na ya ajabu ajabu huku akitaja vitu ambavyo havieleweki, wakati huo akizunguka zunguka tu mtaani hapo. Mama yake Makanyaga ni mwanamke mrefu akiwa na umbo imara kama la kiume. Anapotembea, utaona hana yale madaha waliyonayo wanawake wengi. Anakakamaa tu muda wote. Makanyaga ni kijana

mpole na mwungwana, hakuwa tofauti na rika la akina Ipanga na Masha.

Watu wengi walianza kumshangaa akiwemo mama yake na baadaye wakagundua kuwa siyo hali ya kawaida kwake ambapo walilazimika kumkamata, kumfunga kamba miguu na mikono kwani alikuwa na nguvu nyingi sana, na hatimaye kumkimbiza hospitalini. Alipofikishwa hospitalini, madaktari walimpima na kugundua kuwa ana malaria kali na imepanda kichwani hivyo wakamchoma dawa za usingizi huku wakimpatia matibabu mengine. Hapo Gufa akawa amekamilisha zoezi lake na kesho yake akasafiri kwenda kijijini kwa mzee Utulivu. Alifika salama kijijini na kupokelewa na baadhi ya wanajamii waliomfahamu kuwa ni ndugu yake mzee Utulivu.

Walimsindikiza nyumbani kwa mzee Utulivu, walipofika tu nyumbani, alijikwaa na kudondoka chini kama mzigo wa kuni. Alinyanyuka pole pole na kujifuta mchanga wakati huo waliomsindikiza pamoja na wazazi wa Ipanga wakimpa pole sana na kumwuliza kama kuna mahali amepata jeraha. Mama Ipanga akasema kwa huruma, “Pole sana wifi, umeumia sehemu yoyote ile ili tuone utaratibu wa dawa?” Wifi yake akajibu, “Hapana wifi,

najisikia nipo salama tu, hakuna sehemu niliyopata jeraha." Mzee Utulivu akasema, "Pole sana dada yangu! Pole pia kwa uchovu wa safari ndefu." Dada yake akajibu, "Ahsante sana kaka. Habari ya huku kwenu?" Wifi yake akajibu, "Huku ni nzuri kabisa. Wifi zangu wengine hawajambo pamoja na kijana wetu?" Wifi yake akajibu, "Hawajambo na wanawasalimia sana." Mzee Utulivu akauliza, "Kijana anaendeleaje na masomo yake?" Dada yake akajibu, "Kijana anaendelea vizuri kabisa, kila mmoja anamsifia kwa jinsi alivyo na akili na anavyopenda shule. Hongereni sana kwa malezi mema." Wifi yake akajibu, "Ahsante wifi ila sisi sote ni Mungu pekee ndiye aliye mlezi wetu mkuu." Mama Ipanga alipojibu hivyo, wifi yake tayari akapata picha kuwa familia ya kaka yake ina imani thabiti kwa Mungu wao na pia kitendo cha yeye kujikwaa na kudondoka chini wakati akiwa amebeba dawa za kichawi kilimthibitishia hilo. Wakati huo wote mbwa wake Ipanga alikuwa pembeni akimtazama na kumtathmini kwa makini sana mgeni huyo aliyezuru hapo nyumbani.

Ilipofika kesho yake asubuhi, mama Ipanga alikwenda shambani kuchimba mihogo kwa ajili ya kunywea uji. Pia mzee Utulivu alikwenda mwaloni

kuchukua kitoweo kutoka kwa wavuvi wake wa samaki. Walimwacha mgeni nyumbani peke yake. Wakati huo wote mgeni wao alikuwa akijiuliza maswali mengi sana juu ya kilichomzuia usiku kutoka kwenda kufanya shughuli zake za kichawi. Kwa hasira alinyanyuka kitandani na kwenda kunyunyuzia dawa ya kuwapumbaza akili kwenye mtungi wa maji ya kunywa uliowekwa sebuleni. Kipindi anaelekea kufanya tukio hilo, mbwa wa Ipanga alibweka sana kwa nje na hakuwa na jinsi ya kuingia sebuleni sababu mlango mkubwa ulikuwa umefungwa. Baada ya kunyunyuzia dawa kwenye maji ya kunywa, alinyunyuzia tena dawa nyingine mlangoni kisha akarudi kukaa kwenye chumba alichoandaliwa. Baada ya muda, mama Ipanga akarudi na kuanza kuandaa uji na kuchemsha mihogo.

Lakini muda wote huo mbwa aliendelea kubweka huku akiutazama mlango mkubwa wa sebuleni kama vile anataka kuingia ndani ingawa ulikuwa bado umefungwa. Mama ipanga aliona ni kelele tu za huyo mbwa akaamua kumkamata kisha akampeleka nyuma ya nyumba akamfunga kwa mnyororo chini ya mti ambapo huwa anafungwa. Muda wote huo mbwa aliendelea kubweka bila

kukoma ingawa mgeni ndani alijua ni hali tu ya kawaida mbwa kubweka, hakujua anabweka kwa kile alichokifanya yeye. Mama Ipanga alirudi jikoni kuendelea kuandaa chakula cha asubuhi. Alipomaliza alitoka jikoni (jiko lililojengewa kwa nje) na kwenda nyumba kubwa. Alipofungua mlango wa sebuleni tu kuingia ndani, alihisi miguu inapata ubaridi. Hiyo hali haikumpa wasiwasi sana kwa kudhani ametoka jikoni kwenye joto, ndiyo maana alihisi hivyo. Aligonga kwenye mlango alipokuwa kalala wifi yake kisha wakasalimiana ingawa muda huo wifi yake alijifanya kama ndio kashtuka kutoka usingizini.

Baada ya kumaliza kusalimiana na wifi yake, aliingia chumbani mwake kuanza kufanya usafi. Kipindi akiendelea kufanya usafi alihisi miguu inakufa ganzi, jambo ambalo lilimshangaza. Ilibidi akae kwanza kitandani huku akijaribu kuikanda kanda kwa kutumia mikono. Wakati anaikanda miguu yake, mzee Utulivu naye akafika, alielekea moja kwa moja jikoni kuweka kitoweo kisha akaingia ndani na kumkuta mke wake anajikanda miguu, akamwuliza, “Mke wangu, umekuwaje miguu? Mbona unajikanda?” Mke wake akamjibu, “Mimi mwenyewe ninashangaa, nimeanza kuhisi

baridi tu ila sasa nahisi tena kama inakufa ganzi." Mzee Utulivu akauliza, "Hali hii imekuanza muda gani?" Mke wake akamjibu, " Siyo muda mrefu, kipindi ninaingia humu ndani."

Mzee Utulivu alishika miguu ya mkewe na kuanza kumsaidia kuikanda. Baada ya muda miguu ikapoa wote wakanyanyuka. Mzee Utulivu akauliza, "Mgeni umesalimiana naye?" Mke wake akajibu, "Ndiyo, nadhani nimemwamsha mimi kipindi namsalimia. Ila amekwisha amka." Mzee Utulivu akasema, "Sawa, ngoja nikamwangalie huyu mbwa, sijui kapatwa na nini anavyobweka hivyo!" Mke wake akasema, "Hata mimi nimemkuta hapo mlangoni anabweka hivyo hivyo ikabidi nikamfunge huko nyuma kwasababu anapoamua kutusumbua na kelele zake za kubweka hadi inakuwa kero. Mzee Utulivu akasema, "Kumbe ni wewe ndiye uliyemfunga, basi tumwache atatulia tu." Mke wake akasema, "Sawa mme wangu, mimi najisikia nafuu, ngoja niendelee na usafi humu ndani." Mzee Utulivu akasema, "Sawa mke wangu, ngoja niwafungulie hawa kuku, naona muda umekwenda sana." Mke wake akaitikia, "Sawa mume wangu." Mzee Utulivu alitoka nje kwenda kufungua banda la kuku lakini

wakati huo wote naye alihisi ubaridi kwenye miguu yake ingawa haukuchukua muda mrefu kisha ukawa umekwisha. Baada ya muda mfupi, dada yake naye akatoka nje kisha wakasalimiana.

Walipomaliza kusalimiana, dada yake akauliza alipo wifi yake. Mzee utulivu akamjibu kuwa yuko ndani chumbani. Alipojibiwa hivyo alitembea kuelekea nje kwenye chanja ya kuanikia vyombo kuchukua kikombe kisha akaelekea jikoni. Alipoingia jikoni, akarudishia mlango wa jiko kisha akanyunyuzia dawa kwenye uji na mihogo viliyokuwa vinachemka mafigani kisha akachota maji kwenye kikombe akatoka nje kwenda kupiga mswaki na kunawa uso. Mama Ipanga aliendelea na usafi hadi mlagoni sebuleni, aliona chenga chenga za dawa iliyonyunyuziwa na wifi yake lakini hakuziwazia na kuzitilia maanani kama ni dawa. Alifikiria ni upepo uliokuwa ukivuma ndio umesababisha hizo chenga chenga za vumbi na kuamua kuzifagia kwa kuzirushia nje. Baada ya kumaliza usafi alielekea jikoni na kukuta chakula tayari kimeiva na kuanza kukiandaa tayari kwa kutengwa. Baada ya muda mfupi, alitenga chakula subuleni na wote wakaanza kula.

Walipomaliza kula, mzee Utulivu na mkewe wakanywa pia maji ya kunywa kama kawaida yao kwani kila wakimaliza kula chakula hunywa maji ya kunywa. Wakati huo wote, dada yake mzee Utulivu alifurahia sana moyoni mwake kwani hatua ya kwanza ya shughuli yake ilikuwa imefanikiwa. Yeye binafsi dawa hizo zisingeweza kumdhuru kwa sababu zilikuwa zimenuiwa kwa mzee Utulivu na mkewe tu. Muda ulivyokuwa ukizidi kwenda ndipo dawa ilizidi kufanya kazi na kuanza kubomoa ngome ya imani ya maombi ndani ya familia ya mzee Utulivu. Madhumuni ya dada yake mzee Utulivu kuhusiana na dawa hiyo ya kwanza ni kufunga ufahamu wa wana familia hiyo na tayari alikuwa amefanikiwa. Ilipofika mchana mzee Utulivu alikwenda kumfungulia mbwa ili ale chakula sehemu ambayo huwa anatengewa. Alimkuta mbwa akiwa kimya sana na amejilaza. Akamfungua kamba kisha taratibu sana mbwa akanyanyuka na kuanza kutembea kuelekea ile sehemu ambapo huwa anatengewa chakula. Alipofika alikinusa tu kile chakula kisha akakiacha na kurudi ile sehemu alipokuwa amefungwa kisha akalala tena.

Muda huo wote Mzee Utulivu hakumfuatilia tena mbwa akidhani kuwa alikuwa anaendelea kula chakula. Mbwa aliendelea kuishiwa nguvu kwani utendaji wake wa kazi za kuilinda ile familia kwenye mambo ya kichawi na ushirikina ulitegemea sana maombi ya wanafamilia hiyo hususan mama Ipanga. Ilipofika usiku, mama Ipanga alikwenda tena kumwekea mbwa chakula cha usiku ila cha kushangaza akakikuta kile chakula alichowekewa mchana bado hakijaliwa na kiko vile vile. Aliamua kukimwaga na kumwekea cha muda ule kisha akaelekea sehemu ambapo huwa anafungiwa na kumkuta mbwa wao kajilaza na katulia wakati huo hajafungwa kamba. Alipomwita akasimama kisha akaongozana naye hadi sehemu yake ya kulia chakula , alipofika alikinusa tena na kukiacha. Kitendo hicho kwa mara ya pili kilimshangaza sana mama Ipanga ikabidi amwite mmewe. Mama Ipanga akasema, “mume wangu, nakuomba kidogo huku nyuma ya jiko.” Mzee Utulivu akajibu, “Sawa ninakuja mke wangu.” Wakati huo dada yake mzee Utulivu naye akadakia kwani alishtuka kuona kama kuna kitu wamehisi juu ya hila zake, “Wifi, kuna nini? Ngoja na mimi nije!” Mama Ipanga akajibu, “Hapana wifi, wewe kaa tu usije. Ni kuhusu mbwa wetu tu.” Wifi

yake akauliza, “Kwani amekuwaje wifi?” Mama Ipanga akajibu, “Wifi wala usijali, hakuna shida yoyote ile.” Wifi yake akasema, “Sawa wifi.”

Mzee Utulivu alipofika, mke wake akaanza kumwelezea. Mama Ipanga akaanza, “Leo sijui Mbwa amekuwaje, nimekuta hata chakula cha mchana hajakila. Sasa nimemwekea hiki na chenyewe kakinusa tu akakiacha wakati chakula chenye mchuzi wa nyama huwa anakipenda na hula sana.” Mzee Utulivu akasema, “Atakuwa labda anaumwa kwani anaonekana kanyong’onyea na hata habweki kama alivyokuwa akibweka asabuhi. Tusubiri kufikia kesho tumwone, na ikibidi nitakwenda kumchukulia samaki kwa wavuvi wetu umchemshie tuone pia kama ataweza kula.” Mama Ipanga akajibu, “Sawa mme wangu, itabidi ufanye hivyo sababu huyu mbwa ni kipenzi cha kijana wetu. Akisikia amekufa, atakosa raha huko aliko.” Mzee Utulivu akajibu, “Sawa mke wangu, nimekuelewa vizuri.” Ulipofika muda wa kula chakula cha usiku, mama Ipanga alitenga chakula wote wakala kisha wakaelekea kulala. Mama Ipanga akasema, “Kapumzike wifi, maana naona kama unaanza kusinzia.” Wifi yake

akakubali kwa kusema, “Haya wifi, niwatakie usiku mwema.”

Mzee Utulivu na mkewe walimtakia mgeni usiku mwema kisha wakaelekea chumbani mwao kulala. Kipindi wanataka kulala, mama Ipanga alianza kusali na kumwomba Mungu wake lakini akili yake haikuwa sawa na hata mpangilio wa sala na maombi yake ukawa unavurugikavurugika na kukosea tofauti na siku zote. Alijaribu pia kusali na kuomba kwa kufumba macho lakini hakuweza kwani alikuwa akiona maluweluwe na wakati mwingine kuchanganya sala ama maombi na hayafiki mwisho. Akajiuliza sana muda huo bila kupata majibu. Akakumbuka siku hiyo toka asubuhi hata sala na maombi yake ya kimoyo moyo yamekuwa yakijichanganya changanya tu kila alipokuwa akisali na kuomba, hatimaye aliamua kulala tu ingawa mumewe alikuwa amekwishapitiwa na usingizi mzito sana. Muda wote huo wa usiku, mgeni wao alikuwa akihangaika sana ili aweze kuondoka kichawi kwenda kwenye shughuli zake lakini hakufanikiwa. Hasira zilizidi kumpanda huku akijiuliza chanzo kinachomzuia kupaa kichawi ni nini. Alivyokuwa akijitahidi kutaka kupaa ndivyo

alivyozidi kubanwa na hatimaye kusababababisha kubanwa na kifua huku akipumua kwa shida. Kipindi hicho chote, dada zake pia walikuwa wakijaribu kumtazama kwenye darubini zao za kichawi bila mafanikio na badala yake waliona moshi mweusi na mzito sana. Walipokuwa wakijaribu kumwongezea nguvu za kichawi, walijikuta wanabanwa misuli miguuni mwao na kuamua kuacha kabisa.

Kesho yake asubuhi, mzee Utulivu na mkewe waliamka mapema na kuendelea na ratiba ya hapo nyumbani kama kawaida. Baada ya muda, mama Ipanga alimuaga mumewe kwenda shambani kuona palizi limefikia wapi kwani kuna mtu alikuwa kalipwa pesa kwa ajili ya kupalilia shamba la mihogo. Lakini alimfahamisha mumewe kuwa atarudi mapema. Kipindi mama Ipanga anamuaga mumewe, wifi yake alisikia mazungumzo yote na alipoondoka tu naye akaamka na kutoka ndani. Alipofika nje alimsalimia kaka yake na kujiulizisha, “Kaka, wifi kaenda wapi?” Kaka yake akajibu, “Katoka kidogo ila atarudi muda si mrefu. Ameona asikuamshe mapema, akadai atakusalimia atakaporudi.” Dada yake akajibu, “Sawa kaka, ila mimi leo nitaondoka. Nilikuja kuwajulia hali tu.”

Kaka yake akauliza kwa mshangao, “Mbona haraka na ghafla hivyo! Subiri utaondoka kesho.” Dada yake akajibu, “Hapana kaka, nitaondoka leo. Ngoja nimsaidie wifi kuandaa uji na mihogo kwani akitoka huko atakuwa kachoka sana.” Kaka yake akasema, “Hapana dada, anakuja muda si mrefu na akifika ataandaa mwenyewe.” Dada yake akasema, “Kaka nawe, kwani kuna kazi gani wakati ni muda mfupi tu chakula kitakuwa kimeiva. Hebu ngoja tena nifanye haraka.”

Ilibidi kaka yake amwache aendelee na shughuli za hapo nyumbani. Alifungua banda la kuku kisha akamchukua mbwa nyuma ya nyumba ambapo huwa anafungwa akamfunga. Mbwa alionyesha kuchangamka kidogo lakini alikuwa habweki kama ilivyozoeleka. Baada ya kumaliza kumfunga mbwa, alielekea mwaloni kwa wavuvi wake kuchukua kitoweo kwa ajili ya nyumbani kwake na nyingine kwa ajili ya dada yake anayesafiri. Baada ya mzee Utulivu kuondoka, dada yake alifurahi sana na kuanza kujinafasi muda huo, alichukua dawa nyingi akazichanganya kwenye uji ikiwemo dawa ya kumfanya kaka yake kumchukia mkewe pamoja na mwanaye,na nyingine dawa ya kumfanya awasikilize na awakubalie dada zake kwa kila kitu watakachomweleza ama kumwamuru akifanye.

Baada ya muda mama Ipanga alirudi na kumkuta wifi yake akiwa jikoni. Mama Ipanga akamwuliza, “Wifi, mbona unajihangaisha hivyo kupika! Ona na moshi unavyokusumbua machoni. Ungeacha tu kwani nimewahi kwa kujua nakuja kuandaa chakula.” Wifi yake akajibu, “wifi nawe, mbona kawaida tu kwani haya ndiyo maisha tuliyokulia ya kupikia kuni. Tena wifi, leo naondoka. Nilikuja kuwasalimia mara moja tu.” Mama Ipanga akashituka kidogo kisha akamweleza, “Wifi, acha maskhara basi! Mbona imekuwa ghafla hivyo?” Wifi yake akasisitiza, “Hapana wifi na wala siyo maskhara, ninaondoka leo. Nimekwisha mwambia hata kaka kuwa ninaondoka leo.” Mama Ipanga akasema, “Sawa wifi kama umeamua hivyo. Basi ngoja nikakuchimbie mihogo ya kwenda nayo kwa ajili ya chai.” Wifi yake akajibu, “Sawa wifi, tutashukuru sana kwani vitafunwa vinatusumbua sana huko.” Mama Ipanga aliweka jembe lake begani kisha akaelekea shambani kumchimbia wifi yake mihogo mitamu pamoja na viazi vitamu. Punde si punde mzee Utulivu akarudi huku amebeba samaki wa kitoweo aina ya sato na kupokelewa na dada yake kisha akawaweka jikoni.

Baada ya dakika chache, mama Ipanga naye akarudi akiwa amebeba kichwani mihogo mitamu pamoja na viazi vitamu. Alipofika alielekea moja kwa moja jikoni na kuanza kuviandaa kwa ajili ya safari ya mgeni. Mgeni alimaliza kujiandaa, wakala chakula kisha wakamwandalia mizigo yake na kumsindikiza kwenda sehemu ya usafiri. Baada ya muda mchache alianza safari kuelekea mjini. Waliporudi nyumbani, mama Ipanga alimpakulia mbwa wao chakula hasa samaki na kukila vizuri bila shida yoyote. Wala mzee Utulivu na mkewe hawakuweza kufikiria zaidi kwa nini mbwa wao alikataa kula chakula wakati mgeni akiwepo, wao walidhani alikuwa anaumwa ndiyo maana alikataa kula chakula siku zile.

Mgeni alifika mjini alikotokea na kuwakuta dada zake wakihangaika usiku na mchana kujua nini kinaendelea huko aliko. Alipofika tu walimkaribisha huku wakiwa na wasi wasi sana na bila kufanya chochote kile walimwingiza kwenye chumba chao na kuanza kumwuliza. Kuchi, “Nini kilitokea huko na mbona ulikuwa hata huhudhurii kwenye vikao vyetu?” Gufa akajibu, “Kwanza nipeni pole sana!Mji ule mimi ulinishinda kabisa, kila nilipokuwa nikitaka kupaa nije kwenye vikao

nilishindwa kabisa na nilipolazimisha nilibanwa na kifua hadi nikashindwa kupumua vizuri na ndio sababu iliyonifanya nitoke huko mapema." Nzile akasema kwa huzuni, "Pole sana mdogo wetu. Hata sisi tumeshangaa kukuona umerudi mapema hivi! Imekuwa vizuri umetoka huko haraka kabla madhara makubwa hayajakupata."

Wakati huo wote dada mkubwa alikuwa akimsikiliza mdogo wake kwa makini sana na huku akilinganisha anavyopata ugumu pia kwa Ipanga kwa muda anapomhitaji kumfanyisha kazi za kichawi. Gufa akazidi kuelezea, "Yaani kwa jinsi nilivyokuwa nimejipanga na utaalamu wangu wote wa kutoka kuzimu, hamuwezi amini nilipofika kwenye mji wa huyo mshenzi nilianguka ghafla kama gunia la mahindi, nilipo nyanyuka tu niliona moto mkali sana unaizunguka hiyo nyumba. Nilichoshukuru, nilipoanza safari ya kuelekea hapo nyumbani, nilikutana na wanao nifahamu wakanipeleka hadi pale nyumbani. Hivyo niliponyanyuka baada ya kuanguka, nilitembea kufuata uelekeo wa walionisindikiza hadi nikajikuta nimefika kwenye kiti nikakaa. Baada ya muda mchache ndipo akili ikawa imekaa sawa na ule moto ukapotea. Kwakweli hadi leo hii nimetoka

hapo, sijui ni nini kilichopo kwenye mji huo hadi kunifanya niwe hivyo. Lakini mambo mengine nimeyakamilisha ipasavyo." Baada ya maelezo hayo, wote kwa pamoja walianza kumwomba mungu wao wa kuzimu ili kazi iliyofanyika kwenye familia ya mzee Utulivu ifanikiwe vizuri na kwamba wangeandaa sadaka ya damu za watu kwa ajili ya kutoa shukrani.

Baada ya mwaka mmoja, hali ya familia ya mzee Utulivu ikabadilika sana. Mzee Utulivu akaanza kumwona mkewe kama kinyesi cha binadamu. Akawa ni mtu wa kumkaripia na kumfokea mara kwa mara. Mama Ipanga akaanza kupaona nyumbani kwake pachungu sana huku akikaa mwenyewe kwa huzuni na kujililia mara kwa mara. Ipanga naye hali yake ikaanza kuwa mbaya sana kwani mara kwa mara akawa analalamika kusumbuliwa na tumbo. Pia shuleni kwake mambo yakamgeuka akawa ni mtu wa kusoma haelewi na hatimaye kushindwa kufanya vizuri mitihani yake. Pia kila siku za kufanya mitihani zinapokaribia ilikuwa lazima aumwe sana tumbo linalompelekea kuhara na vichomi hadi kushindwa kukaa vizuri kwenye chumba cha mitihani. Kila aliposoma ama kujisomea na rafiki zake kwa ajili ya mitihani

ilimchukua dakika chache tu kupoteza kumbukumbu ya kila alichosoma. Hali hiyo ilimyong'onyesha sana na kumfanya aishi bila amani na taratibu akaanza kupoteza mwelekeo wake kielimu. Rafiki zake na walimu wake waliendelea kumtia moyo na kumwandalia ratiba mbalimbali zitakazo msaidia katika kusoma kwake kwani waliufahamu uwezo wake kielimu kutokana na ufaulu wake ulivyokuwa mzuri katika kujiunga na sekondari. Pia uwezo wake ulivyokuwa mkubwa darasani kipindi anaanza kidato cha kwanza. Ingawa Ipanga aliyazingatia hayo yote kutoka kwa wanafunzi wenzake na walimu wake lakini hayakufua dafu na kila kukicha aliendelea kushuka zaidi kielimu. Nyumbani alipofikia napo hali ikazidi kuwa mbaya kwani hao ndugu wa damu wa baba yake walimpatia kila aina ya sifa chafu ikiwemo uvutaji wa bangi, sigara, wizi n.k.

Siku moja mzee Utulivu alikwenda mjini kuwasalimia dada zake, alipofika tu dada zake wakaanza kummwagia sifa mbaya za kijana wake ambazo wamemtengenezea. Kuchi akasema, "Bora kaka yetu umekuja, yaani ni hatari sana. Kijana tuliyekuwa tunamtengemea ameanza kujiunga na makundi ya ajabu." Mzee Utulivu akauliza kwa

mshangao, “Kijana gani huyo dada?” Kuchi akajibu, “Huyu mwanetu Ipanga. Siku hizi anaaga anakwenda shule lakini hafiki, anakwenda milimani na rafiki zake kuvuta bangi. Ukimwona, hata huwezi kumtamani kwani hayo mabangi anayoyavuta amekwisha yafanya kama chakula na yamemkondesha sana. Tumejaribu kumsihi ayaache lakini naona tunampigia mbuzi gitaa tu” Mzee Utulivu hakuamini,akauliza kwa mshangao, “eeh! eeeh! eeeeh!. Huyu Ipanga ninayemjua mimi leo kafikia hatua hiyo ya kuvuta bangi?” Nzile akajibu, “Kaka, hata sisi kitendo hicho kinatushangaza sana. Kajaa kiburi tu, sijui ni hayo mabangi anayoyavuta ndiyo yanamfanya hivyo!” Kuchi akadakia, “Bora angevuta mabangi akaishia hapo! Na wizi sasa ndio umeshamiri, yaani siku hizi tumekuwa wa kuficha vitu hasa pesa! Ukiiacha tu kweupe lazima aibe!” Nzile akasisitiza, “Ndio hivyo! Ili apate pesa za kununulia hayo bangi anayovuta.”

Kuchi akaanza kulia huku akifuta machozi na kusema, “Yaani mwanangu huyu niliyekuwa ninamtegemea aje awe mrithi wa mali zangu, Mungu alininyima mtoto lakini nikajua ninaye mtoto wa kaka yangu ambaye pia ni mtoto wangu.

Ninahangaika huku na kule nikijua yupo mwanangu ambaye atakuwa mshauri wangu mkuu na mrithi wa mali zangu! Sasa ndio huyo kaangukia kwenye kuvuta bangi na kuiba. Ninaumia mimi jamani! Huyu Mungu tumemkosea nini jamani?" Mzee Utulivu akasema, "Ngoja, leo ataniona. Nilikuwa na mpango wa kurudi kijijini leo lakini ngoja nimsubiri atanitambua." Kuchi akasema, "yaani hizi labda ni tabia za kwao na mama yake huko. Sisi kwetu hatuna tabia za kijinga hivi. Ndio maana wewe kaka yetu hadi leo unatupenda, lakini tungekuwa na hizi tabia tusingekuwa hivi tulivyo. Hatuwezi kukusema vibaya kaka yetu ila huyo mke wako ametuletea tabia za ajabu ajabu tu. Koo nyingine siyo za kuoa mwanamke kabisa." Akainama kama anasikitika kidogo, kisha akaendelea, "Huko jikoni, fanyeni haraka ili kaka ale, msisahau pia kumchemshia mayai." Mzee Utulivu akasema, "Hapana dada, hata hamu ya kula imeniishia ninamsubiri tu huyu mtoto aje anione. Yaani huko mama yake ananichanganya na yeye tena anichanganye!" Kuchi akauliza, "Huko kwako?" Mzee Utulivu akasema, "Mama yake naye kajaa kiburi tu, anapika chakula kama vile anampikia mbwa. Yaani ninashindwa hata jinsi ya kuelezea." Kuchi akadakia, "kama nilivyotoka

kusema! Kwa kweli huyu mke wako, mh! Anajiona, anadharau, wala hatupendi, sijui kwa vile yuko kwenye nyumba nzuri ya bati! Tunapenda sana kuja kukutembelea kaka yetu wa pekee ila tunapomfikiria huyo mke wako tunakata tamaa. Bora tukae tu hapa utakuwa unatukuta." Mzee Utulivu akasema, "Anikosanishe na ninyi dada zangu haiwezekani! Nilikwishamwambia akitaka anaweza kwenda kwao, mimi sina shida yoyote." Gufa akamtega kwa kusema "utaishije bila mke kaka, mwache tu usimfukuze." Mzee Utulivu akauliza, "Kwani hapa siwezi kuishi na ninyi dada zangu." Kuchi akasema, "Mbona mwanzo tuliishi pamoja kipindi unatulea. Tena asikutese kabisa! Hapa ni kwako na tutazidi kukulea tu kaka yetu." Muda wote huo dada zake walikuwa wakifurahi sana mioyoni mwao kwa kuwa dawa walizozifanya zinaleta matokeo mazuri kwao.

Ilipofika jioni, Ipanga alirudi kutoka shule huku akiwa amechoka sana na anahisi njaa kwani pesa iliyoachwa awe anapewa kwa ajili ya kununua chakula awapo shuleni alikuwa hapewi na hivyo kuufanya mwili wake kudhoofu. Alipofika alimkuta baba yake kaketi nje ya nyumba. Ipanga alifurahi sana kumwona baba yake. Ipanga

akamsalimia, “Shikamoo baba!” Mzee Utulivu akajibu, “Marhaba, twende chumbani kwako nina shida na wewe!” Ipanga alishituka kidogo kwani siyo kawaida ya baba yake kutomchangamkia ukiachilia muda ambao wamekaa bila kuonana. Ipanga akajibu, “Sawa baba!” Kisha akaelekea chumbani kwake akiongozana na baba yake. Walipofika chumbani, baba yake akafunga mlango na kuanza kumwuliza Ipanga, “Hebu niambie!, nilikuleta huku kuja kusoma ama kuvuta bangi na kuwaibia hapa nyumbani?” Swali hilo lilikuwa gumu sana kwa Ipanga kulijibu, ikabidi amtazame tu baba yake kwa mshangao! Kwani alichoulizwa ni kitu kigeni kwake. Baba yake akamwuliza tena huku akimsogelea Ipanga, “Ninataka uniambie, nilikuleta huku kuja kusoma ama kuvuta bangi na kuwaibia pesa pamoja na kudokoa mboga hapa nyumbani?” Ipanga akajibu kwa upole, “Baba mimi sielewi unachoniuliza!” Mzee Utulivu akafoka “Kwa hiyo mimi ni mwehu eti? Mimi ni mwehu!”

Mzee Utulivu alitoa mkanda wake wa suruali na kuanza kumchapa mwanaye. Hakuishia hapo, alimpiga makofi na mateke pia. Ipanga alilia kwa huzuni sana kutokana na maumivu ya hicho kipigo aliyokuwa anayapata. Baba yake alipotosheka

kumpiga akamweleza kuwa hatampatia huduma yoyote ile inayohusiana na shule ikiwemo kumlipia ada. Hayo maneno yaliendelea kumwumiza sana Ipanga kwani alipenda sana elimu yake na pia mama yake alimweleza kuwa ni elimu tu ndicho kitu pekee kitakacho msaidia maishani mwake.

Siku iliyofuata, mzee Utulivu akarudi kijijini kwake huku akiwa amejawa na hasira za kijana wake kubadilika na kuwa na tabia mbaya kiasi hicho. Alipofika nyumbani kwake alimkuta mkewe yuko jikoni lakini hakumsemesha bali alikwenda moja kwa moja ndani na kuelekea chumbani kitendo hicho kiliendelea kumshangaza sana mke wake. Ilibidi anyanyuke na kumfuata mumewe ndani kujua nini kimemsibu. Mkewe akamwuliza, “mume wangu, una tatizo gani mbona umenipita hapo jikoni nakusemesha hata hunijibu?” Mzee Utulivu akamjibu, “Niache tu, yaani kila sehemu taabu tu!” Mkewe akamwuliza, “Kipi kimetokea huko mjini hadi kikakupelekea usirudi?” Mzee Utulivu akajibu, “Si huyo mwanao!” Mkewe akauliza tena“Amekuwa mwanangu peke yangu? Haya amepatwa na nini?” Mzee Utulivu akajibu, “Bora angekuwa amepata tatizo tungeona nini cha kumsaidia kuliko hayo anayojitakia mwenyewe.”

Mkewe akauliza kwa mshangao, “Kuna nini mume wangu! Hebu niweke wazi!” Mzee Utulivu akaendelea kuzungumza, “Sisi tumempeleka huko kwa kazi moja tu ya kusoma. Sasa yeye kaanzisha kazi nyingine ya udokozi wa pesa hapo nyumbani, udokozi wa mboga, na kibaya zaidi haendi shule anashinda milimani anavuta bangi hadi zimempelekea kakonda kama mchi.”

Baada ya kusikia hayo, Mama Ipanga ambaye alikuwa amesimama ilibidi akae chini huku akimwazia mwanae. Mzee Utulivu akaendelea, “Dada zangu wanampenda na wanampa kila kitu lakini anawaletea kiburi kwa ajili ya hizo bangi zake anazovuta.” Pole pole machozi yalianza kumbubujika Mama Ipanga akiwazia mwanae wa pekee ndio kampoteza hivyo kwa kujiunga na makundi maovu. Baada ya muda kidogo alimwomba mume wake ruhusa ili mwisho wa wiki hiyo hiyo aende mjini kumwona mwanae. Mzee Utulivu akamruhusu lakini akamwambia aende na kurudi siku hiyo hiyo. Mama Ipanga alishukuru kupata ruhusa hiyo kwani alikuwa akihitaji pia msaada kutoka kwa wifi zake ili wamsaidie kumshauri kuhusu mumewe kwani alikuwa amebadilika sana kitabia, amekuwa akimgombeza

mara kwa mara bila sababu zozote za msingi. Wakati huo wote dada zake mzee Utulivu walianza kusambaza maneno machafu na ya uongo kumhusu Ipanga kwa kila jirani ama wageni wanaozuru hapo nyumbani bila kujali ni wa kiume ama kike.

Ilipofika mwishoni mwa wiki, mama yake Ipanga aliamka asubuhi sana na kuanza kujiandaa kwa ajili ya safari kuelekea mjini. Pia aliandaa samaki pamoja na viazi vitamu kwa ajili ya kuwapelekea wifi zake. Hatimaye muda ulifika akaanza safari. Alifika mjini na kuwakuta wifi zake wameketi nje wakibadilishana mawazo ya hapa na pale. Walipomwona walifurahi kinafiki, wakampokea mizigo kisha wakamkaribisha aketi ndani. Wifi yao alionesha furaha kwa nje lakini asilimia kubwa alikuwa akimuwazia mwanae Ipanga kutokana na hali ya tabia mbaya aliyoelezwa na mumewe. Walifurahi wote kwa pamoja na muda mfupi tu wakamtengea chai. Kuchi akasema, “Wifi karibu kwanza chai.” Mama Ipanga akajibu, “Ahsante wifi.” Mama Ipanga alianza kunywa chai taratibu sana huku mawazo yake yote yakiwa hayapo hapo kwenye chai. Huku akiendelea kunywa chai, wifi yake mdogo akaita

kwa sauti, “Ipanga! Ipanga! Njoo ndani umsalimie mama, kaja.” Ipanga aliitika na kuanza kutembea kuja akitokea kwenye banda la bata alilokuwa akilifanyia usafi.

Wakati huo wote hakujua moyoni mwa mama pakoje. Aliingia ndani na kumkuta mama yake kaketi anakunywa chai kwa vitumbua kisha akamsalimia. Ipanga akamsalimia “Shikamoo mama!” Mama yake akajibu, “Marhaba mwanangu! Hujambo!” Ipanga, “Mimi sijambo mama.” Ipanga alipojibiwa hivyo na mama yake sura ya huzuni ilimtawala sana, machozi yakamlengalenga ingawa ilibidi ajitahidi sana kujizuia ili Kuchi na wadogo zake wasigundue. Mama yake pia na alipigwa butwaa sana kumwona mwanae alivyokonda huku akionekana siyo mtu wa furaha kabisa. Baadaye Kuchi akamwambia Ipanga, “Haya kamalizie kufanya usafi wa nguo zako za shule ndipo uje umsalimie vizuri mama yako.” Ipanga akatoka ndani huku akijiuliza akilini mwake, “Ninaambiwa nikafanye usafi wa nguo zangu kabla sijamaliza kusafisha banda! Nikiliacha likiwa hivyo ninaweza kugombezwa. Ngoja nimalizie kwanza usafi wa banda.”

Ilibidi Ipanga akaendelee na usafi wa banda la bata. Mama Ipanga alipomaliza kunywa chai akaanza kuongea na wifi zake kuhusu mumewe, “Wifi ninawaombeni mnisaidie hata kwa ushauri tu. Mimi na mume wangu hatuko vizuri kwani kila kunapokucha ndivyo mume wangu anazidi kuwa mkali. Ninafokewa, ninatukanwa, ninasemwa vibaya, siku hizi hata ninapopika chakula na kumtengea ananisonya tu na kama akila atakula kidogo tu. Anadai nina dharau, kiburi na kibaya zaidi imefikia hatua ananiambia kama nimeshindwa kuishi nae niondoke tu niende kwetu ama popote pale ninapotaka. Ninaombeni msaada wenu wifi zangu kwani hali ya ndoa yangu siyo nzuri kabisa.” Kuchi akasema, “Mmmhh! pole sana wifi yetu. Mimi ninadhani huwa humjui vizuri huyo mume wako! Huwa kama anaumwa kichaa. Kinapoamka, huwa kinaamka kweli kweli. Yaani huyo! tuuu!” Nzile akasema, “Dada, unakumbuka hata kipindi kile tunaishi nae kijijini kwetu. Wehu wake ulikuwa ukimpanda anagomba ovyo kweli, yaani hatukai kwa raha na hatimaye tukaamua kumwachia mji.” Kuchi akadakia “Kweli kabisa. Wifi, mimi nakushauri ukiona yamezidi nenda tu kwanza nyumbani kwenu umwachie mji ili ajifunze.” Gufa akaunga mkono, “Kweli kabisa

dada, hata mimi nakuunga mkono. Bora umwache tu kwanza ajifunze." Mama Ipanga akaitikia, "Sawa wifi zangu, nimewasikia na nimewaelewa vizuri. Kijana wetu anaendeleaje na masomo?" Kuchi akajibu "Anaendelea vizuri sana, tena hadi shuleni kwake wanamsifia alivyo na nidhamu nzuri." Nzile akaongezea, "Kwa kweli kijana ana nidhamu nzuri sana, yaani hata wageni wanapokuja hapa wanamsifia kweli kwa jinsi alivyotulia." Mama Ipanga akawaambia, "Baba yake alikuja huko akadai ameanza kujiunga na makundi mabaya." Kuchi akadakia, "Wifi, huyo tumekwisha kukuambia, yawezekana kichaa chake kimepanda. Sisi tulimwambia kwamba kijana ajichunge tu asiingie kwenye makundi ya uvutaji bangi. Sasa nadhani yeye akalichukulia hilo kuwa anavuta bangi. Yaani huyu kaka, siyo tu ukichaa nadhani na akili zimeanza kumruka."

Maelezo hayo ya wifi zake yalimshangaza sana mama Ipanga na kuendelea kuvuruga akili yake. Kwa vile muda nao ulikuwa ukienda mbio, ilibidi awafahamishe kuwa muda sio mrefu ataanza safari ya kurudi kijijini. Walimwita tena Ipanga na kumwambia aje hapo walipoketi na mama yake. Ipanga alipofika hapo ikabidi aketi na mama yake

akaanza kumwuliza maendeleo ya shuleni huku Ipanga akiitikia kila kitu kuwa ni kizuri. Alijibu hivyo kwa kuhofia Kuchi na wadogo zake wanaweza kumfokea kama atasema ukweli wa maisha yake kwa sasa kuanzia shuleni hadi hapo nyumbani. Pia hayo majibu ya Ipanga hayakumridhisha sana mama yake kwani aliona uso wake umejaa huzuni. Ingawa walikuwa na siku chache za kufunga shule, mama yake alimsisitiza pindi atakapofunga shule aende kijijini kwa ajili ya likizo yake.

Mama Ipanga alinyanyuka na kuaga ili aanze safari yake ya kurudi kijijini. Kipindi ananyanyuka kuanza safari, wifi zake wote nao walinyanyuka ili kumsindikiza huku Kuchi akisema, “Kwa kweli mwanao anajitahidi sana kusoma. Na sisi tunamsisitiza mara kwa mara asome ili hatimaye atusaidie.” Maneno hayo yalimkasirisha sana Ipanga ingawa hakuwa na jinsi ya kufanya. Walimsindikiza hatimaye wakamuaga na kurudi nyumbani. Mama yake Ipanga alipokuwa safarini kuelekea nyumbani kwake kijijini alijiuliza maswali mengi sana juu ya mumewe kutokana na maneno aliyoambiwa na wifi zake. Akawa akiwaza, “Mume wangu huwa anapandwa na kichaa! Toka lini!

Nimemfahamu na kuishi nae takribani mwaka wa arobaini sasa na sijawahi kuona wala kusikia haya niliyoambiwa leo. Lakini ukichaa ama wehu huendana na kufokewa hivi ninavyofokewa kwa sasa? Mbona huu ukichaa unakuwa kwangu tu lakini wanapokuja rafiki zake ama watu wengine huzungumza nao vizuri na kupanga mambo yao vizuri tu! Mbona kwa wafanyakazi wake huzungumza nao vizuri na kupeana pesa kama kawaida! Pia wanasema Ipanga anaendelea vizuri na masomo wakati huo hao hao walimwambia mume wangu kuwa Ipanga amejiunga na makundi ya wavuta bangi na pia amekuwa mdokozi. Mbona hii hali inanichanganya sana!"

Mama Ipanga aliendelea kujihoji maswali mengi sana lakini asipate majibu. Wakati huo wifi zake waliendelea kufurahi sana kwa sababu malengo yao yalikuwa yanaendelea kutimia. Kuchi akasema, "Hongera sana mdogo wetu umepambana huko kijijini na tunaanza kuona matunda." Gufa akajibu, "Na bado, hadi afunge virago vyake arudi kwao kwani hatutaki hata kumsikia. Eti anajisemesha kuomba ushauri yaani kesi ya ngedere upeleke kwa nyani!" Kuchi akaongeza, "Huyu tumpe mwaka mmoja tu tuone, akiwa bado yupo basi naye ni

mwanamke wa shoka na atakuwa amekwishatukanwa na ukoo wake mzima. Lakini hakikisheni kila siku mnamchomea na kupuliza hizo dawa ili azidi kumchukia mkewe." Nzile akasema, "Dada nawe, kusahau kuifanya hiyo kazi kila siku ni sawa na kwenda kujisaidia haja kubwa bila kujisafisha." Alivyosema hilo neno wote wakacheka.

Baada ya siku chache Ipanga alianza kufanya mtihani ya nusu mhula kabla ya kufunga shule. Lakini muda huo wote alikuwa akiumwa tumbo ambalo lilisababisha kutokufanya mitihani yake kwa utulivu. Pia, ingawa alitumia nguvu kubwa sana katika kujisomea kwa ajili ya maandalizi ya mitihani yake, kila alipoingia chumba cha mitihani alijikuta amekwishasahau kila kitu kuambulia maluweluwe tu kichwani. Aliendelea kufanya mitihani hivyo hivyo kwa kubahatisha na mwisho akamaliza. Siku ya kufunga walitangaziwa kuwa wawajulishe wazazi tarehe ya kufuata matokeo. Alipofika nyumbani aliwafahamisha ndugu wa baba yake yake tarehe ya kufuata matokeo wakadai watayafuata wao wala asisumbuke kumfahamisha baba yake. Siku iliyofuata Ipanga akasafiri kuelekea kijijini kwao. Alipofika kijijini aliwakuta wazazi

wake akawasalimia, wakaitikia ingawa baba yake alionekana kama ni mtu mwenye hasira. Pia alionesha kumpuuzia mwanae Ipanga. Ipanga aliingia ndani na kutunza begi lake kisha akatoka nje na kuanza kufunga mabanda ya kuku kwani giza lilikuwa linaanza kutanda. Ilipofika usiku mama yake alitenga chakula, wote wakaanza kula lakini muda wote huo baba yake akawa anasonya mara kwa mara. Kitendo hicho kilimfanya Ipanga akae si tu kimya bali hata mbali nae kwa kuhofia anaweza kumpiga mara nyingine. Walipomaliza kula, Ipanga aliondoa vyombo akavipeleka jikoni, akafuta meza kisha akawatakia usiku mwema na kuelekea chumbani kwake kulala. Kipindi ananyanyuka mama yake akamweleza, "Ipanga, kesho asubuhi tutaelekea shambani kwenye palizi." Ipanga akajibu, "Sawa mama." Muda wote huo baba yake alikuwa kimya tu ambapo si kawaida yake kwani mara nyingi anapokuwa na familia yake, hupenda kuzungumza habari mbalimbali ikiwemo shughuli zake za uvuvi.

Ilipofika kesho yake asubuhi, Ipanga aliamshwa na mama yake kisha wakaelekea shambani. Kipindi wanaelekea shambani, Ipanga alimwuliza mama yake, "Mama mbwa wangu toka jana nilipofika

sijamwona. Siku hizi amekuwa mzururaji kiasi hicho?" Mama yake akajibu, "Hapana mwanangu, sisi mbwa wako alitushangaza. Alitoweka tu ghafla akiwa kafungwa kwenye mnyororo. Nilipokwenda kumfungulia ale chakula cha mchana, nilikuta mnyororo umejifunga kama ambavyo huwa tunamfunga shingoni lakini mbwa hayupo." Hilo jibu lilimshangaza sana Ipanga na kumfanya aduwae kwa huzuni huku akijiuliza mahali mbwa wake alipo. Muda wote huo, mama yake alikuwa hayajali masuala ya mbwa bali alitaka kujua maisha halisi ya Ipanga shuleni na hapo nyumbani alipofikia. Walifika shambani na kuanza palizi huku mama yake akimwuliza, "Mwanangu unaendeleaje na masomo?" Ipanga akajibu, "Mama, hali ya masomo si nzuri sana." Mama Ipanga akasimama huku kashikilia jembe lake mkononi. Akamwuliza mwanae, "Kwa nini unasema hali si nzuri mwanangu?"Ikabidi Ipanga amweleze mama yake mwanzo hadi mwisho huku akibubujikwa na machozi.

Mama yake akapata uchungu sana hali iliyosababisha akae juu ya tuta. Ipanga akaongezea "Yaani kwa sasa sifa zote mbaya ni za kwangu ikiwemo kuvuta bangi, kuiba pesa, kudokoa mboga

na mengine mengi tu. Kibaya zaidi kila mtu anayekuja hapo nyumbani wakiwemo wageni wa kutoka mbali wanaambiwa wachukue tahadhari ili nisije nikawaibia. Siku moja mvua ilinyesha sana na baada ya kukatika ndugu yake baba mkubwa akaniita tusaidiane kupanga mawe kwenye mlango wa banda la bata ili kuzuia maji ya mvua yasiingie ndani ya banda. Tuliweka jiwe la wastani kwenye gunia tukashika huku na kule, kipindi tunaelekea kwenye banda mguu wake mmoja ukateleza kwenye tope akaanguka na jiwe likamuangukia mguuni na kumkata. Lakini cha kushangaza kila aliyekuja kumsalimia baada ya kutoka hospitali alimweleza kuwa mimi ndiye niliyemponda na jiwe mguuni nikiwa na lengo la kumvunja mguu. Hali hiyo pia iliniumiza sana mama. Kingine mama, kipindi baba kaja huko, ndugu zake walimwambia mambo mengi ya uongo kunihusu. Jioni nimetoka shule nikamkuta baba kachukia sana na akasema anataka twende nae chumbani mwangu. Tulivyoingia tu akaniuliza kuwa alinileta huku kuvuta bangi ama kusoma. Nilishangaa sana na sikuwa na jibu kisha akaanza kunichapa kwa kutumia mkanda wake wa suruali, makofi na mateke.” Mama yake alikuwa akimsikiliza mwanae huku amejiinamia.

Baada ya maelezo ya kijana wake, akamwuliza kwa sauti ya chini sana, “Mwanangu unasali kila mara lakini?” Ipanga akajibu, “Mama, ninashindwa kujua kwa sasa nimepatwa na nini, kila ninaposali sala na maombi yangu navurugikiwa tu na kama ni usiku nikilazimisha sana ninapitiwa na usingizi hadi nashtuka usiku wa manane. Kila siku hali iko hivyo mama.” Hayo maneno yalimshangaza sana mama yake kwani naye kila anapotaka kusali hiyo hali humkuta pia. Alimwambia tena mwanae kwa kumtia moyo, “Endelea kuomba hivyo hivyo wala usiache kabisa. Hiyo ni hali tu itapita, sawa mwanangu?” Ipanga akajibu, “Ndiyo mama, nimekuelewa na nitajitahidi.” Baada ya kumaliza mazungumzo hayo, Ipanga alimwuliza mama yake, “Mama, Masha amekwisha kuja nyumbani kuniulizia ama hajaja likizo?”

Mama yake alishindwa namna ya kumjibu kwa muda kutokana na matatizo aliyoyapata rafiki yake Masha. Mwishowe akamweleza, “Mwanangu, sikubahatika kukueleza juu ya matatizo aliyoyapata rafiki yako Masha.” Ipanga akamwuliza, “Alipatwa na matatizo gani ama aliugua tena?” Mama yake akajibu, “Hapana alifiwa na wazazi wake.” Ipanga akauliza, “Wote baba na mama?” Mama yake

akamjibu, “Ndiyo walitofautiana miezi miwili tu.” Ipanga akauliza tena, “Walipatwa na nini?” Mama yake akaendelea kumjibu, “Alianza kufariki baba yake kwa kutapika damu. Baadaye alifuata mama yake, aliamka kichwa kinamwuma sana na ilipofika jioni akawa amefariki.” Hiyo taarifa ilimhuzunisha sana Ipanga kisha kwa upole akauliza, “Masha alikuwepo misibani?.” Mama yake akajibu, “Ndiyo walimfuata kuja kumzika baba yake. Aliongozana na mwalimu wake na walikaa siku tano wakarudi shuleni. Ulivyotokea msiba wa mama yake pia wakamfuata, akaongozana na mwalimu mwingine. Hapo pia alikaa siku tano akarudi shuleni. Lakini likizo hii atakuja. Kipindi cha msiba wa mama yake, mwalimu mkuu alimwombea kwa baba yako kuwa atakapokuwa anakuja afikie hapo nyumbani kutokana na ndugu zake kuwa walevi wa pombe na hawana makazi maalumu. Pia asije akaathirika kielimu. Baba yako alikubali na pia kuahidi kuwa atamsaidia kielimu pale atakapokwama.” Ipanga akasema, “Sawa mama, nimekuelewa lakini naogopa hata kwenda kwao. Yupo nani kwa sasa?” Mama yake akajibu, “Kuna aliyekuja msibani hapo anadai ni dada yake, mtoto wa baba yake mkubwa.” Ipanga akasema, “Itabidi nimsubiri yeye akija ndipo nitakwenda nae hapo kwao.” Mama

Ipanga akasema, “Sawa mwanangu.” Baada ya mazungumzo hayo wote waliishiwa nguvu ya kuendelea na palizi, ikabidi wajiandae tu kurudi nyumbani huku mama Ipanga akiwa na mawazo zaidi juu ya mazingira anayoishi mwanae huko mjini na jinsi mwanae anavyoshuka kielimu na kibaya zaidi kwa jinsi anavyougua tumbo mara kwa mara hasa mitihani inapokaribia.

Tarehe ya kufuata matokeo ya Ipanga ilifika, Kuchi akawaambia wadogo zake kuwa yeye ndiye atakayeyafuata matokeo shuleni. Alikwenda shuleni na kukuta walimu wamekaa makundi makundi wakigawa matokeo kwa kuzingatia kidato. Mwalimu mmoja akamkaribisha kisha akamwuliza, “Karibu mzazi, umekuja kuchukua matokeo?” Akajibu, “ndiyo, ila pia ninahitaji kuonana na mkuu wa shule. Sijui nimemkuta?” Mwalimu akajibu, “Ndiyo umemkuta, ila kwanza ungechukua matokeo. Mwanao yuko kidato gani?” Kuchi akajibu, “Yaani hata sijui, na kwa vile huwa ni mtoro mtoro?” Mwalimu akamwuliza tena, “Kwani anaitwa nani?” Kuchi akajibu, “Anaitwa Ipanga Utulivu.” Alipotaja hilo jina mwalimu akashangaa sana kwani takribani walimu wote wanajua vizuri tabia na nidhamu ya Ipanga kuwa

ni njema. Akamweleza, “Sawa mzazi. Nenda kwa yule mwalimu aliyevaa shati jeupe, atakupatia matokeo ya kijana wako.” Kuchi akajibu, “Sawa mwalimu.” Alipofika hapo alipoelekezwa akakaribishwa na huyo mwalimu, “Karibu mzazi. Mwanao anaitwa nani?” Kuchi akajibu, “Ipanga Utulivu.” Mwalimu akasema, “Sawa, wewe ndiye unaishi na Ipanga?” Kuchi akajibu, “Ndiyo mwalimu.” Mwalimu akamwuliza, “Ni mtoto wako?” Kuchi akajibu, “Hapana, ni mtoto wa kaka yangu.” Mwalimu akasema, “Mtoto wenu matokeo yake siyo mazuri na anazidi kushuka ufaulu wake kila kukicha. Jitahidini kumsaidia kijana wenu.” Kuchi akaguna kisha akasema, “Mmmmh!, mwalimu we acha tu, yaani huyu kijana.”

Kwa vile huyo mwalimu alikuwa akiendelea kuwagawia wazazi wengine ripoti za matokea ilibidi aachane na ndugu wa Ipanga na kuendelea kuwasikiliza wazazi wengine kwa kuwa tayari alikuwa amempatia matokea yake. Lakini Kuchi alimwuliza, “Mwalimu, kwa mkuu wa shule ni wapi?” Ikabidi mwalimu asitishe kwanza kuwahudumia wazazi wengine na kumjibu, “Nenda kwenye ule mlango unaoutazama, kuna mama utamkuta ndani kisha atakuonesha ofisi ya

mkuu wa shule." Kuchi akatembea kuelekea kwenye mlango aliooneshwa. Alipoingia ndani alimkuta mama mtu mzima na kumwuliza kama mkuu wa shule yupo maana ana shida nae. Yule mama akamwambia asuburi kidogo kwani kuna mgeni mwingine. Kipindi anamalizia kumweleza, yule mgeni akatoka naye akaruhusiwa kuingia akamwone. Mkuu wa shule, mwanamme wa rika la kati, maji ya kunde, macho madogo na pua ndefu, alikuwa amekalia kiti cha kujizungusha. Alikuwa amevaa surulia ya rangi ya bluu bahari na shati jeupe, na tai ya rangi ya kijani. Koti lake la rangi ya zambarau ikiashiria mtu anayejipenda na kujali sana usafi. Miwani yake midogo ilimpa haiba ya pekee. Ni mtu ambaye hajizuii anapoona mtu hatumii busara katika maamuzi. Ni mwepesi wa kukemea mwenendo au ushauri na mazungumzo yanayokusudia kubomoa badala ya kujenga.

Kuchi aliingia ofisini kwa mkuu wa shule na kumkuta ameketi kisha akamwambia, "Karibu mzazi, shikamoo!" Kuchi akajibu, "Marhaba mwanangu, habari ya kazi?" Mkuu wa shule akajibu, "Nzuri tu. Karibu uketi kwenye kiti." Kuchi akasema, "Ahsante sana." Mkuu wa shule akamwuliza, "Nikusaidie nini mzazi?" Kuchi

akasema, “Mkuu mimi nimekuja nina shida tena kubwa sana.” Mkuu akamwuliza, “Shida gani hiyo mzazi?” Kuchi akajibu, “Inamhusu kijana ambaye ni mwanafunzi wenu hapa anaitwa Ipanga, kwa kweli mkuu naomba msaada wako. Huyu kijana ni mtoto wa kaka yangu tumbo moja na yuko kijijini anafanya shughuli kazi zake za kuhangaika hapa na pale. Sasa niliona nimchukue huyu kijana ili nimsaidie apate elimu yake ili kesho na kesho kutwa ajitegemee na kusaidia wazazi wake. Sasa kijana amekuwa na kiburi, dharau, kuvuta bangi na makundi aliyojiunga nayo ndiyo usiseme. Amekuwa mdokozi wa hela hapo nyumbani na hata mboga jikoni. Yaani mkuu ni taabu tupu. Sasa naombeni msaada wenu. Yaani hata mkimfukuza tu shule kwani amekwisha kutuchosha kabisa hapo nyumbani. Tunakaa na kulala roho juu juu tukihofia anaweza kutuletea wezi wenzake wakatuvamia usiku.”

Mkuu wa shule akaanza kujihoji kwa jinsi anavyomfahamu Ipanga na sifa anazoambiwa. Ikabidi apate wazo la kumwita makamu wake washauriane vizuri na isitoshe yeye ndiye anayewaelewa wanafunzi vizuri zaidi yake. Akamweleza mlezi wake, “Sawa mzazi,

nimekusikia. Ngoja wakamwite msaidizi wangu kwasababu yeye ndiye anayewaelewa vizuri hawa wanafunzi." Kuchi akajibu, "Sawa mwalimu." Makamu mkuu wa shule aliitwa na baada ya muda mfupi akawa amefika. Mkuu wa shule akamweleza, "Makamu, huyu ni mlezi wa mwanafunzi aitwaye Ipanga. Hebu msikilize ana tatizo na kijana huyo." Makamu akasema, "Karibu mlezi na ninaomba nikusikilize." Kuchi alirudia maelezo hayo hayo aliyomwambia mkuu wa shule ingawa aliendelea kusisitiza afukuzwe shule. Makamu akamwambia, "Sawa, tumekuelewa. Kipindi Ipanga anakuja kuripoti aliletwa na mzee mmoja hivi akadai ni baba yake mzazi, kweli ni baba yake mzazi?" Kuchi akajibu, "Ndiyo ni baba yake ila huwa anaishi huko kijijini." Mkuu wa shule nae akauliza, "Ni nani ambaye huwa anamlipia ada na mahitaji mengine ya shule?" Kuchi akajibu, "Huwa anamlipia baba yake." Mkuu akamweleza, "Kama anamlipia baba yake, basi tunamwomba huyo huyo baba yake aje hapa shuleni. Mwambie aje tutakapofungua shule, sawa mzazi?" Kuchi akajibu, "Sawa mwalimu nitamueleza aje." Makamu akasema, "Tunashukuru kwa taarifa hizi." Kuchi akasema, "Ahsanteni na kwa herini."

Kuchi alinyanyuka kisha akaondoka zake kuelekea nyumbani. Muda huo mkuu wa shule na makamu wakaendelea kumjadili na roho mbaya aliyonayo juu ya kijana huyu kwani wanamfahamu vizuri na tabia njema aliyonayo kwa walimu, wanafunzi wenzake na hata wafanyakazi wengine hapo shuleni. Mkuu wa shule akamweleza makamu wake, "Huyu mlezi anaonekana ni mwongo pia. Mwanzoni alinieleza kuwa yeye ndiye anayemsaidia Ipanga mahitaji yake yote kwasababu baba yake yuko kijijini na hana uwezo. Sasa hivi tena anasema anayemlipia ada ni baba yake." Makamu akaongeza, "Mkuu, kwa mlezi anayejitambua na mwenye nia njema na kijana wa ndugu yake, huwezi kutoa ushauri kuwa kijana afukuzwe shule hata kama ni mtukutu kiasi gani. Tumeona wazazi na walezi wengi hapa ambao vijana wao wemekutwa na kesi mbalimbali lakini wanapambana ili vijana wasifukuzwe shule." Hivyo waliona ni vema wazungumze na baba yake juu ya maendeleo ya kijana wake kielimu kwani anazidi kushuka kila kukicha.

Ilipobaki wiki moja kufungua shule, Masha alikwenda kijijini kuwasalimia na pia alikuwa amemkumbuka sana rafiki yake Ipanga. Alipofika

kijijini, alifikia kwa mzee Utulivu na kumkuta Ipanga rafiki yake akiwa anafungia banda la kuku, alipomwona tu akamkimbilia kisha wakakumbatiana kwa furaha. Baada ya salamu, Ipanga alilichukua begi la rafiki yake na kuliingiza ndani wakati huo rafiki yake akaelekea kwa wazazi wa Ipanga kuwasalimia ambao walifurahi pia kumwona. Kesho yake asubuhi Ipanga alimsindikiza Masha kuona hali ya mazingira ya kwao ilivyo. Walipofika walimkuta dada aliye achiwa mji kisha wakamsalimia. Alifurahi sana kumwona Masha akiwa na hali nzuri kiafya. Akasema "Karibu sana Masha." Masha akaitikia, "Ahsante dada. Huyu ni rafiki yangu anaitwa Ipanga. Mtoto wa mzee Utulivu." Dada yake akasema, "Sawa, ninamfahamu baba yake na mara nyingi hupita hapa kunijulia hali anapokwenda kutazama mifugo yake. Karibu Ipanga." Ipanga akajibu, "Ahsante dada." Wakati huo wote nyuso zao zilikuwa zimejaa huzuni hasa wanapotazama makaburi mawili yaliyojipanga pembeni kidogo ya nyumba. Masha alipomaliza kuongea na dada yake pamoja na kutazama mazingira ya hapo nyumbani, alimwambia rafiki yake waondoke na kurudi nyumbani.

Baada ya siku mbili, Ipanga na Masha walianza kupeana habari za masomo na kubadilishana maongezi mbalimbali. Masha alianza kwa kusema, “Ipanga, ninaamini huko shuleni utakuwa unawaongoza sana kimasomo kwa sababu ninakufahamu ulivyo na wewe ndiye umenisaidia sana hadi nami nimefika sekondari! Ipanga aliinamisha kichwa chini kisha akakinyanyua na kusema, “Ndugu yangu, mambo yananiendea kombo sana, sijui nimepatwa na nini. Ninajitahidi sana kusoma, nasaidiwa sana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu lakini kwa muda mfupi tu, ninasahau kile nilichokisoma ama nilichofundishwa yaani kwa ufupi ninakuwa sina ninachokikumbuka. Pia mazingira ninayoishi huko ni magumu sana.”

Masha akamwuliza, “Lakini uliniambia pale unaishi na ndugu wa damu wa baba yako?” Ipanga akajibu, “Ni kweli kabisa! Ila siamini kama kweli ni ndugu zake wa damu na wanatoka tumbo moja kutokana na mambo wanayonifanyia. Yaani nikiwa shuleni unapofika muda wa kwenda nyumbani huwa nawaza sana.” Masha akamwuliza, “Umekwishamweleza baba hali hiyo hapo nyumbani?” Ipanga akajibu, “Ninashindwa hata nianzie wapi kumweleza baba kwasababu kuna

siku alikuja huko, ndugu zake hao wakamwambia mambo mengi sana ya uongo kunihusu akaanza kunipiga bila hata ya kunisikiliza. Pia baba siku hizi namwona kubadilika sana, muda wote anakuwa amekasirika tu." Masha akamwunga mkono, "Kweli kabisa, ninamuona amekuwa ni mtu wa kufokafoka tu bila hata sababu za msingi." Ipanga akasema, "Ndio hivyo Masha, ni ngumu sana kuweza kumwambia kitu akiwa katika hali hiyo." Masha akamwuliza, "Mama je, umekwishamweleza?" Ipanga akajibu, "Ndiyo, mama nilimweleza kila kitu isipokuwa hana maamuzi zaidi katika hilo. Alinisisitiza tu niendelee kusali na kuomba kwa Mungu wetu aliye juu na yote yataisha." Masha akasema, "Kweli kabisa Ipanga, kama ulivyowahi kuniambia kipindi kile ninaumwa kuwa tusali na kumwomba Mungu muda wote. Mimi huko niliko ninasali sana." Ipanga akauliza, "Tumefunga shule muda, ulikuwa wapi siku zote hizo?" Masha akajibu, "Kuna mwalimu aliyenisindikiza kwenye msiba wa mama, aliyaona mazingira ya huku kijijini pamoja na hali ya ulevi wa ndugu zangu akaniambia kama nitapenda, likizo zangu zote niwe naishi kwake. Sasa muda wote huo nilikuwa naishi kwake na kumsaidia shughuli zake za hapa na pale." Ipanga

akapongeza, “Hongera sana Masha. Mazingira ya kwake ni mazuri?” Masha akajibu, “Kwa kweli ninamshukuru sana Mungu wetu aliye juu kwani hapo ninaishi kama niko nyumbani. Hakuna shida yoyote ile.” Ipanga akasema, “Ninatamani sana kutoka hapo nilipofikia ila mama hana ndugu huko.” Masha akasema, “Nikwambie kitu Ipanga, Mungu atatusaidia na tutafaulu vizuri tu.” Ipanga akaitikia kwa unyonge, “Sawa Masha, Ahsante sana na Mungu wetu ni mwema sana.”

Hatimaye muda wa likizo ulikwisha, Ipanga na Masha wakaanza kujiandaa kurudi shuleni. Masha alitangulia kuondoka kwani alihitaji kukaa siku moja pale nyumbani kwa mwalimu wake kabla ya kuanza masomo lakini Ipanga alihitaji afike nyumbani na kesho yake aanze kwenda shule. Kipindi Masha anawaaga wazazi wa Ipanga ili arudi shule, mzee Utulivu alimwita, “Masha njoo hapa kwanza.” Masha akamsogelea mzee Utulivu. Mzee Utulivu akaendelea, “Hizi hapa pesa za ada kwa miaka yote iliyobaki. Pia chukua hii pesa nyingine ya matumizi kwa huo muda wote utakapokuwa shuleni. Uzitunze vizuri, hiyo ya matumizi utumie vizuri.” Masha akasema, “Sawa baba, ahsante, ninashukuru sana.” Mzee Utulivu

akamwuliza, “ulisema unahitaji pesa ya nini tena?” Masha akajibu, “Pesa ya mitihani pamoja na viatu vya shule, vimeniishia.” Mzee Utulivu alihesabu pesa nyingine kisha akampatia na kumtakia safari njema. Muda wote huo Ipanga na mama yake walikuwa wakitazama Masha anavyokabidhiwa pesa. Mama Ipanga naye alimpatia mihogo ya kwenda kuchemsha kwa ajili ya kunywea chai, ingawa jana yake alimpatia kiasi cha pesa kwa ajili ya matumizi yake safarini. Pia alimtakia safari njema na kusisitiza atunze vizuri pesa hizo kisha Ipanga akamsindikiza hadi kwenye kituo cha basi. Ipanga akamuaga rafiki yake, “Masha, mimi nikutakie safari njema, tutawasiliana kupitia barua kwa anuani za shuleni.” Masha akasema, “Sawa Ipanga, nawe ukajiandae kwa ajili ya kuja mjini kesho. Halafu sijakuuliza. Hivi mbwa wako alikwenda wapi?” Ipanga akajibu, “Hata mimi sijui! Nilipokuja sikumkuta, niliambiwa alipotea ghafla tu pale chini ya mti ambapo tulikuwa tunamfunga.” Masha akasema, “Sawa Ipanga, tutawasiliana. Nakutakia masomo mema.” Ipanga akasema, “Ahsante Masha, nawe pia nikutakie safari njema.”

Baada ya kuagana, Ipanga alirudi nyumbani na kufanya maandalizi ya kwenda shule kesho yake.

Akiwa kwenye maandalizi, mama yake alimwita na kumweleza, “Ipanga mwanangu, kama nilivyokwambia, kumbuka kusali na kuomba kwa Mungu aishie juu. Jitahidi sana usiache kwani hayo yote yatapita tu. Sawa mwanangu?” Ipanga akajibu, “Ndiyo mama. Sasa hivi kidogo nina nafuu na sala na maombi yangu kwa Mungu wetu aliye juu naanza kuzifikisha mwisho. Pia hata yale mawenge niliyokuwa nikiyapata kipindi nasali na kuomba yamepungua.” Mama yake akasisitiza, “Mwanangu, endelea kuomba na kusali hivyo hivyo bila kukoma. Mungu wetu aliye juu atakusimamia kwa kila jambo.” Ipanga akamshukuru mama yake akasema, “Ahsante sana mama.” Mama yake akasema, “chukua hiki hapa kiasi cha pesa, kitakusaidia shuleni walau uwe unapata hata chai ya bila kitafunwa ili uchemshe tumbo.” Ipanga akasema, “Ahsante sana mama.”

Baada ya muda, Ipanga aliendelea na maandalizi yake huku mama yake naye akielekea jikoni kuanza maandalizi ya chakula cha usiku. Ilipofika usiku baada ya kumaliza kula, Ipanga aliwafahamisha wazazi wake kwa mara nyingine kuwa anatarajia kuondoka kesho yake. Mama yake akasisitiza ajitahidi kusoma zaidi wakati baba yake akiwa

kimya bila hata kuongeza neno lolote. Baada ya hapo, Ipanga aliingia chumbani kwake kisha akalala na baada ya muda wazazi wake nao waliingia chumbani mwao wakalala. Kesho yake asubuhi, mzee Utulivu alimwita mwanae sebuleni, mwanae alipofika akamwuliza pesa inayo hitajika shuleni. Ipanga akamtajia kiasi cha pesa kinachohitajika ikiwemo pesa ya viatu ingawa alikwisha mfahamisha kabla. Baba yake akazihesabu pesa kisha akazidondosha chini kwenye sakafu na kumwambia mwanae, "Najua hizo pesa napoteza tu." Kisha akatoka nje. Ipanga alijiuliza maswali mengi sana kutokana na hicho kitendo cha baba yake kumdondoshea pesa chini.

Hakuwa na jinsi, ilibidi aziokote kisha akaingia ndani na kuzitunza kwenye begi lake. Pia akafikiri ni jinsi gani amweleze mama hali hiyo lakini ilimwia vigumu hivyo akaamua kukaa kimya. Muda ulipowadia Ipanga aliwaaga wazazi wake kisha akaanza safari kuelekea mjini. Ipanga alipofika mjini, alielekea moja kwa moja hadi nyumbani na kuwakuta ndugu wa baba yake wamekaa nje ya nyumba huku wakijadiliana mambo mbalimbali. Aliwasalimia kisha akaingia chumbani kwake ingawa walimwitikia salamu yake kwa shingo upande.

Sura ya Nne

Kesho yake asubuhi na mapema, Ipanga alijiandaa na kuanza safari ya kwenda shule kwani ndiyo ilikuwa siku ya kufungua shule. Alipofika shuleni alikutana na makamu mkuu wa shule akamwuliza. “Ipanga, mzazi wako yuko wapi?” Ipanga alishangaa na kumjibu mwalimu wake, “Nilimwacha nyumbani kijijini. Mwalimu, kwani ulikuwa unamhitaji?” Mwalimu wake akajibu, “Ndiyo, kwani hakupata ujumbe wa wito?” Ipanga akajibu, “Hapana ,labda hakupata kwani angekwisha kuja ama kuniambia chochote juu ya wito huo.” Mwalimu akamwuliza, “Kuna mama mmoja mrefu hivi mweusi, alikuja shuleni, ni nani yako?” Ipanga akashtuka kisha akamjibu mwalimu kuwa ni dada wa baba yake.

Mwalimu akamwuliza tena, “huyo ni ndugu yako kweli?” Ipanga akajibu, “Ndiyo, ni tumbo moja na baba yangu.” Mwalimu alishindwa kujizuia na kusema, “Inaonekana ana roho mbaya sana. Alikuja hapa akapendekeza ufukuzwe shule kisa una tabia mbaya nyumbani na pia una makundi yanayojihushisha na uvutaji bangi. Lakini tulimwambia atuitie baba yako mzazi, huyo ndiye tunaweza kuongea nae ili akusaidie mazingira

mazuri ya kujisomea kwani tulijadili na kuona hapo unapoishi ni hatari sana. Sasa cha kufanya wewe ukifika nyumbani mwambie kuwa hutakiwi kuja shule bila baba yako. Umenielewa vizuri?" Ipanga akajibu, "Sawa mwalimu nimekuelewa."

Ipanga aliendelea kuwaza na kuwazua kuhusu hayo matendo maovu anayofanyiwa na ndugu wa baba yake hasa Kuchi bila kupata suluhisho. Jioni ilipofika, alirudi nyumbani huku akiwa amenyong'onyea sana. Aliwasalimia ndugu wa baba yake kisha alipakua chakula na kuanza kula. Baada ya kumaliza kula na kuosha vyombo, alimfahamisha Kuchi kwa kumwambia, "nimeambiwa nisiende shule hadi nitakapokwenda na baba kutokana na ujumbe uliopewa." Kuchi akadakia, "Eeh! kweli nilikuwa nimekwishasahau. Mwanangu, utu uzima nao una matatizo ya kusahausahau. Siku nimekwenda kuchukua matokeo yako, waliniita ofisini na kuniambia kuwa baba yako anahitajika kwa mkuu wa shule. Sijui ni mambo ya ada ama michango mingine! Mimi hata sielewi. Sasa itabidi uandike kabarua kadogo ukapeleke kwenye usafiri wa kwenda kijijini ili kesho kutwa aje." Ipanga akajibu, "Sawa, nitaipeleka kesho kwa sasa muda umekwenda na

hakuna usafiri wowote wa kwenda kijijini kwa huu muda." Kuchi akamwunga mkono, akisema "Kweli kabisa mwanangu. Leo nimekukaangia mayai, nenda kachukue kwenye sahani iliyofunikwa na kawa huko jikoni."

Ipanga alielekea jikoni kuchukua yai alilokaangiwa na kulila ili kumridhisha tu. Siku hiyo hata chakula hakula vizuri kwa sababu ya kuwafikiria kwa yale wanayomfanyia hasa huyo Kuchi. Kesho yake alipeleka barua ya kumtaka baba yake afike shule mara moja na siku iliyofuata baba yake akaja na kupitiliza hadi shuleni kwani Ipanga alikwishatangulia mapema. Mzee Utulivu alipofika shuleni, Ipanga alimpokea na akamsalimia kisha akampeleka moja kwa moja katika ofisi ya mkuu wa shule. Alipomfikisha, mkuu akamwambia Ipanga amwite makamu wa shule kisha yeye aingie darasani kuendelea na masomo.

Makamu alifika kwa mkuu wa shule na kumkuta baba yake Ipanga ameketi kisha akamsalimia. Mkuu akamtambulisha mzee Utulivu kwa makamu kuwa ndiye baba yake mzazi Ipanga. Makamu akajibu kuwa anamkumbuka maana alimwona siku ile alipomleta Ipanga kuripoti shuleni. Makamu akasema, "Karibu mzee!" Mzee

Utulivu akaitikia, “Ahsante mwalimu.” Makamu akaanza kuzungumza, akasema, “Mzee tumekuita hapa kwa jambo moja tu. Kuna mama mmoja hivi wa makamo alikuja hapa shuleni kipindi cha kuchukua matokeo ya wanafunzi. Akatujulisha kuwa yeye ndiye anayemlea mwanao kwa sababu wewe uko kijijini. Ila kilichotushangaza, akadai mwanao afukuzwe shule kwa sababu anavuta bangi, na ana kiburi sana hapo nyumbani, anaiba pesa na wakati mwingine hudokoa mboga jikoni. Hiyo habari wewe unayo?” Mzee Utulivu akajibu, “Ndiyo, nilikuja siku moja ndugu zangu wakanieleza habari hiyo na nilikasirika sana ikabidi siku hiyo nimpige sana kijana. Tumemleta mjini kusoma na sio kujiunga na hayo makundi na hatimaye kuvuta bangi.”

Mkuu wa shule aliendelea kumwuliza, “Kipindi anasoma shule ya msingi umeishi nae muda wote huo hadi kumaliza darasa la saba?” Mzee Utulivu akajibu “Ndiyo, nimeishi nae na alikuwa na tabia nzuri sana. Haya amekuja kuyafanyia huku alipokuja sekondari.” Mkuu akamwuliza, “Wakati wa likizo alikwenda sehemu gani ama alikuwa hapa hapa mjini kwa ndugu zako?” Mzee Utulivu akajibu, “Hapana, wakati wa likizo alikuja kijijini.”

Mkuu akauliza tena, “Hata alipokuwa huko kuna makundi ya wavuta bangi hapo kijijini aliyokuwa anashirikiana nayo ama hata kuonana na vijana wa hayo makundi?” Mzee Utulivu akajibu “Hapana, sikuwahi kumwona maana muda mwingi alikuwa nyumbani ama alikwenda shambani na mama yake.” Makamu nae akauliza, “Kutokana na hayo mashitaka ya ndugu zako, wewe binafsi uliwahi kukaa nae na kumwuliza juu ya hizo tuhuma?” Mzee Utulivu akajibu, “Hapana, sijawahi kukaa nae nikamwuliza.” Mkuu akasema, “Mzee, kwa asilimia kubwa wewe ndiye utakayechangia kuharibikiwa kwa mwanao. Ili kujua ukweli juu ya tuhuma zote hizo alizoeleza dada yako dhidi ya mwanao siku hiyo, tumetuma wapelelezi wetu wakiwemo rafiki zake lakini imethibitika kuwa hayo yote anasingiziwa. Labda la kuiba mboga ingawa tunavyo mfahamu sidhani sababu hapa pia tuna somo la upishi na yeye ndiye msimamizi mkuu huko jikoni kwa upande wa wanafunzi. Lakini hatujawahi kupata taarifa yoyote ile kutoka kwa mwalimu wake anayeshughulikia mambo ya jikoni kuwa mwanao ni mwizi wa vyakula. Tunakueleza hivi si kwa lengo la kumfichia mwanao maovu, bali tunamfahamu vizuri kijana wako kwa tabia nzuri aliyonayo kwetu sisi kama

walimu na kwa wanafunzi wenzake pia. Mara nyingi tumekuwa tukiwashauri wanafunzi wenzake wajifunze tabia njema kutoka kwa mwanao."

Makamu mkuu wa shule nae akaongeza, "Mzee, ninaweza kusema ulifanya kosa kubwa sana la kumwadhibu mwanao tena kwa kumchapa kwa maneno ya kuambiwa na bila hata kumpa muda ukamsikiliza. Kwanza unamfanya kijana si tu akuogope, bali hata kukuchukia." Mkuu akamwuliza mzazi, "Mzee, tangu kijana amekuja likizo amekueleza nini juu ya hali hapo anapoishi?" Mzee Utulivu akajibu, "Wala hata hajaongea na mimi!" Mkuu akauliza tena, "Tangu umeishi nae hali hiyo ya kutokuongea na wewe ndio hali yake?" Mzee Utulivu akajibu, "Hapana mwalimu, kijana amekuwa akinishirikisha mambo mengi, ila nimemwona kabadilika wakati huu aliokuja likizo." Mkuu akasema, "Mzee, siyo kuwa amebadilika! Wewe ndiye umembadilisha sababu umetengeneza uzio kati yake na yako. Usipokuwa makini, utampoteza kabisa. Siku zote huwa ninasema kuwa hebu ninyi wazazi tusaidiane kuwalea vema hawa watoto na kuwatengenezea mazingira mazuri ya kujisomea wawapo nyumbani. Pata muda

zungumza na mwanao, mwulize kama ana changamoto yoyote ile. Pia tukushauri tu mzee wetu, huyu mwanao ungemtafutia sehemu nyingine akaishi ili asome vizuri kwani hapo inavyoonyesha siyo salama kwake. Sijui unatuelewa mzee?"

Mzee Utulivu aliendelea kujibu huku ameinamisha kichwa, "Nawaelewa vizuri walimu." Makamu akasema, "Sisi tulikuita ili tukushauri uangalie namna ya kumsaidia mwanao sababu amekuja hapa akiwa anafanya vizuri sana katika masomo yake ila kadri siku zinavyozidi kwenda ndivyo anavyozidi kushuka. Mwishowe atakuchukia bure kwa hiyo usimwonee mtoto sana, ana akili za kuweza kubaini tatizo lilipo. Sawa mzazi?" Mzee Utulivu akajibu, "Sawa nimewaelewa, hata hivyo huo ni mji wangu na sina sehemu nyingine anaweza kuishi. Ninawaza sijui nifanyeje na hapa kwenu ni shule ya kutwa." Makamu akatoa maoni, "Kama itashindikana sana, sisi tunaweza kumwombea akae na rafiki yake aliyepanga chumba hapa jirani na shule, isipokuwa wewe umtafutie pesa ya chakula. Unasema umempatia chumba, chumba hicho akitumie kubadilisha nguo tu ila mara nyingi awe na rafiki

zake ambao wanajitahidi sana kusoma na wanafanya vizuri." Mzee Utulivu akakubali kwa kusema, "Sawa walimu, itabidi nifanye hivyo kwa sababu sina namna kabisa." Makamu akasema, "Sawa mzee, tunashukuru kwa ushirikiano wako huo. Chochote kile kitakachokwenda tofauti kuhusu kijana wako, tutakuita tujadiliane zaidi." Mzee Utulivu akajibu, "Sawa, ahsante sana." Mkuu akasema, "Sawa mzee, karibu tena."

Mzee Utulivu aliaga na kutoka nje ya ofisi ya mkuu wa shule akisindikizwa na makamu. Alimwomba makamu amwite kijana wake Ipanga kwani ana shida nae kidogo. Makamu alimuaga mzee Utulivu kisha akaenda darasani kumwita Ipanga. Ipanga alifika na kumsindikiza baba yake huku wakizungumza. Mzee Utulivu akamwuliza, "Hebu niambie, huwa unapewa pesa ya kunywa chai shuleni?" Ipanga akajibu, "Hapana baba, Tangu nianze shule nilipewa mara mbili tu ile mwanzoni kisha nikaambiwa pesa imekwisha." Mzee Utulivu akamwuliza swali lingine, "Nyumbani je!, huwa unakunywa chai?" Ipanga akajibu, "Chai huwa inachemshwa lakini huwa sijui muda inaonyweka. Mara nyingi mimi kunywa chai labda aje mgeni ninywe nae ama ninywe na wewe

unapokuja." Mzee Utulivu akamwuliza, "Mafuta na sabuni huwa unapewa lakini?" Ipanga akajibu, "Hapana, mafuta huwa sipewi. Yanapoisha mama akiwa hajaja, huwa napewa na yule mama jirani ingawa nayo mara nyingi huwa ninakuta yamechotwa." Mzee Utulivu akauliza, "Ni nani ambaye huwa anachota mafuta yako?" Ipanga akajibu, "Sijui, kwa sababu huwa niko shule na mlango huwa uko wazi tu." Mzee Utulivu akamwuliza tena, "Sabuni huwa unapewa lakini?" Ipanga akajibu, "Hapana, mara nyingi sabuni huwa ninapewa na wapangaji hapo nyumbani."

Baada ya maelezo hayo yote, mzee Utulivu alihisi kuishiwa nguvu kwani kila anapokuja lazima awaachie dada zake hasa Kuchi pesa nyingi tu kwa ajili ya matumizi ya kijana wake. Hakufikiria sana kuhusu tuhuma alizopewa juu ya Ipanga kwa sababu dawa alizopewa zilikuwa zinaendelea kumfunga ufahamu. Alimpatia pesa ya matumizi mwanae kisha akamweleza kuwa kuanzia wiki itakayofuata, atahamia chumba cha nje ambacho kina komeo. Pia akamweleza kuwa mambo mengine ataongea na makamu wake. Ipanga alipokea kiasi hicho cha pesa kisha akamkubalia kuhusu kuhamia chumba cha nje. Baada ya hapo, baba yake alimuaga na kuondoka.

Ipanga alirudi shule na kuingia darasani lakini baada ya muda mfupi, makamu akaenda kumwita na kuanza kuongea nae. Makamu akaanza kwa kusema, “Ipanga sikiliza, tumeongea na baba yako amekubali tukuombee kwa rafiki yako ili uwe unakwenda kujisomea huko. Pia mambo mengine ikiwemo chakula, utaona mwenyewe jinsi ya kufanya, kama utashirikiana nae kuhusu chakula ama utakuwa unakula gengeni.” Ipanga akamshukuru sana makamu mkuu wa shule kwa msaada aliompatia. Baada ya kusema hayo, makamu akamwita rafiki yake Ipanga aliyepangishiwa chumba na wazazi wake. Alipofika makamu akamweleza, “Tizi, kama nilivyokueleza siku ile jinsi ya kumsaidia rafiki yako katika mazingira ya kusoma. Bahati nzuri tumeongea na baba yake pia na amekubali awe anakwenda kusoma kwa rafiki zake. Sasa ninaomba umpokee na kumsaidia zaidi katika kusoma na kujisomea.” Tizi akaafiki kwa kusema, “Sawa mwalimu, hakuna shida yoyote. Hadi sasa huwa ninajitahidi sana kumsaidia ila imekuwa vizuri amepata muda mwingi.” Makamu akasema, “Sawa, mambo mengine yote mtapangiana ninyi wenyewe huko, kikubwa sisi tunataka mwendelee kuwa na nidhamu nzuri pia na matokeo mazuri.” Tizi

akaahidi, “Sawa mwalimu, tutajitahidi.” Makamu akawaruhusu waende darasani nae akelekea kwenye ofisi yake kuendelea na majukumu.

Mzee Utulivu alifika kwa ndugu zake kisha wakasalimiana. Walipomaliza kusalimiana tu Kuchi akamwuliza, “Kaka utatumia chai ya mchai mchai ama uji wa ulezi?” Mzee Utulivu akajibu, “Hapana nimekunywa nilipofika tu mjini.” Kuchi akauliza, “Ndiyo kusema umekwishafika hadi shuleni kwa kijana wetu?” Mzee Utulivu akajibu, “Ndiyo na ndipo ninatoka muda huu.” Kuchi akasema, “Hawa walimu wasumbufu tu, nadhani hata hawakuwa na jambo la maana walilokuitia. Mimi kuna mmoja nilionana naye wiki mbili hivi zilizopita nikiwa barabarani naelekea sokoni, akadai tumhimize kijana wetu ajisomee kipindi hiki cha likizo. Nikamwambia sawa. Mnaendeleaje huko nyumbani lakini? “Mzee Utulivu akajibu, “Tunaendelea vizuri. Huyu kijana nae amedai apewe chumba cha nje kwa ajili ya kujisomea zaidi.” Kuchi akadakia, “Tena chumba hicho hapo.” Mzee Utulivu akasema, “Mimi nilidhani kina mpangaji!” Gufa akasema, “Hapana alikuja ila hajakilipia. Atakikubali hicho cha ndani alipo Ipanga kwa sasa sababu yeye ni mtu wa kusafiri safiri sana kwa jinsi

alivyotwambia." Mzee Utulivu akasema, "Basi sawa, utamweleza ahamishie vitu vyake kwenye chumba hicho." Kuchi akasema, "Sawa, leo akitoka shule nitamwambia." Mzee Utulivu akaaga, "Mimi ninaondoka sasa, kuna mambo ninataka nikafanye kwanza mjini na baadaye ndipo nielekee kijijini." Kuchi akasema, "Basi usubiri kidogo chakula, wanamalizia kuandaa." Mzee Utulivu akasema, "Hapana dada, usijali kwani nina haraka sana leo." Kuchi akaendelea kusisitiza, "Jamani kaka! Basi ngoja nikukaangie yai la bata haraka haraka." Mzee Utulivu aliendelea kukataa kisha akanyanyuka, akaaga na kuondoka.

Ipanga aliporudi kutoka shule alikabidhiwa chumba akakifanyia usafi kisha akahamisha vitu vyake na kuviweka kwenye chumba hicho kipya. Alikabidhiwa ufunguo mmoja ila baada ya wiki moja akaweka kitasa kipya hivyo funguo zote akawa nazo yeye. Alipomaliza alimfuata Kuchi na kumweleza, "Sengi, kwa sasa nitakuwa ninakwenda kujisomea kwa rafiki yangu tunayesoma nae shuleni. Ni yule Tizi ambaye huwa anakuja hapa nyumbani kunisalimia. Pia msiwe mnaniachia chakula kwani ninapotoka shuleni, ninapitilizia huko huko kwa rafiki yangu

kujisomea.” Kuchi alipigwa na butwaa kwani ni taarifa ya ghafla sana kwake na wakati huo kuna dozi ya kuendelea kumpumbaza akili Ipanga iliyokuwa ikiendelea kupitia chakula alichokuwa anatunziwa pindi anapokuwa shule. Kuchi akamwuliza Ipanga, “Baba yako analijua suala hili la kwenda kujisomea kwa rafiki yako na kula huko huko?” Ipanga akajibu, “Nilimwelezea kidogo kuwa nitakuwa ninakwenda kujisomea huko kwa rafiki yangu kwani nae anamfahamu, akakubali. Pia, kwao kuna umbali kidogo, hivyo sitaweza kuwa narudi nyumbani kula.” Kuchi akamwuliza tena, “Kwa hiyo,lini utaanza kwenda huko?” Ipanga akajibu, “Nitaanza leo na nitakwenda muda si mrefu.” Kuchi akawaita wadogo zake na kuwapatia hiyo taarifa ya Ipanga.

Baada ya muda mfupi, Ipanga aliwaaga kisha akaondoka. Kitendo hicho cha kutokula chakula chao kiliwakera sana hao ndugu wa baba yake hasa yule Kuchi. Kisha akawaambia wenzake kuwa usiku wa siku hiyo atatumia muda mwingi sana kwenye darubini yao ya kichawi kumchunguza Ipanga pamoja na baba yake kujua kama wamekwisha ugundua mchezo wao wa kichawi. Usiku ulipofika walikutana kwenye kikao chao cha

kichawi kama kawaida yao inavyokuwa kila siku ili kupeana majukumu ya siku hiyo. Kuchi ambae ni mwenyekiti wao akaanza kwa kusema, “Leo sitakuwa na mambo mengi na wala sitagawa majukumu mapya. Ninataka kila mmoja aendelee na kazi nilizogawa jana, na kama umemaliza basi fanya mambo yako binafsi. Upande wa darubini, nitakuwepo mimi mwenyewe kwa hiyo ninaomba nisisumbuliwe kabisa. Anayehitaji kutumia darubini, tumieni hizi ndogo ndogo. Kila mmoja tawanyika.” Wote waliinama na kusema maneno ya kumkubalia mwenyekiti wao kisha wakatawanyika kila mmoja kwenda kwenye kazi yake.

Mweyekiti alikwenda kwenye darubini kuu ya kichawi akaanza kumtafuta Ipanga lakini alikuwa hamkamati vizuri kwani ilionekana kama vile taswira yake ipo kwenye maji ambayo yana mawimbi. Kipindi anaendelea kumtafuta ili amvute vizuri huko napo Ipanga alikuwa anasali na kuomba kwa Mungu wake aliye juu. Hivyo hivyo mama yake naye muda huo huo alikuwa akisali na kuomba kwa Mungu wake aliye juu. Mwenyekiti aliendelea kumvuta huku akiomba miungu na miungu wake wa kuzimu bila mafanikio na hatimaye mkono ulitoka kwenye hiyo darubini

yake ambayo ni ungo mkubwa uliofunikwa na sanda nyeusi huku umezungushiwa viganja vya mikono ya watoto wachanga iliyokaushwa ukampiga usoni kwa nguvu sana. Alishituka sana na kujizuia asipige kelele kwa maumivu aliyoyapata usoni.

Baada ya hiyo hali, darubini ikaonesha giza. Ilibidi aahirishe hilo zoezi na kupaa kuelekea nyumbani anapoishi huku akijihisi kizungu zungu kikali sana. Kesho yake asubuhi aliamka uso umemvimba na haoni vizuri. Wachawi wenzake wakiwa katika hali ya kiubinadamu walikwenda kumpa pole na kumpelekea dawa ya kumkanda kwani usiku huo huo walipata taarifa kuwa mwenyekiti wao kapata shida. Siku iliyofuata, hali ya mwenyekiti ilizidi kuwa mbaya na ikabidi waitishe kikao cha dharura kichawi kujadili hali yake. Wakiwa katika kikao hicho, mjumbe mmoja akasema, “Jamani, mwenyekiti wetu anaweza asione tena kutokana na shida aliyoipata. Sasa tunafanyaje?” Mjumbe mwingine ambaye ni mganga mchawi akajibu, “Nimemtazama kwenye ramli yangu hali yake siyo nzuri. Mimi pia sina uwezo wa kumtibu zaidi kutokana na hali hiyo. Dawa nilizozileta jana, ni za kutuliza maumivu tu

lakini sio kumtibu kabisa. Hapa cha kufanya kuna mwenzetu ambaye ni mganga mchawi kavuka miiko kumi ya kichawi na ndiye mwenye uwezo wa kumtibu. Nilipita kwake kumweleza na ndio maana nimechelewa kidogo kwenye kikao hiki. Nilipofika kwake, alimtazama mwenyekiti kwenye ramli yake tukaona anaweza kumtibu. Kama atakuwa na nguvu kidogo, tumpeleke kwa usafiri wa fisi lakini kama hatakuwa na nguvu itabidi huyo mganga aje amtibie huku ingawa atakuwa anakuja kila siku usiku wa manane kumtibu. Ila kuna tatizo moja, kuna baadhi ya dawa hazitakiwi kupandishwa kwenye ungo wala fisi. Kwa vile ni mwenzetu, amesema gharama ya kumtibu ina thamani ya ng'ombe dume kumi na wawili. Sijui ninyi mnasemaje?"

Mjumbe mmoja akasema, "Itabidi aje tu kwasababu hata jana alitakiwa akaoge maji ya ziwani, lakini nilipompandisha kwenye fisi akashindwa kukaa na nilipomkalisha kwenye ungo akakaa ila hakuwa na nguvu kabisa. Ilibidi nimshushe nikamlaza kwani niliona kwa kasi ile anaweza kudondoka." Mjumbe mwingine akahoji, "Jamani tutatumia njia gani kuwapumbaza hao binadamu ili wasigundue kinachoendelea kama

tutaamua atibiwe hapo hapo nyumbani?" Mganga mchawi akajibu, "Itabidi kumpeleka hospitali kesho ili wamuandikie dawa ila tukatae asichomwe sindano wala kulazwa. Kesho kutwa atakapokuja mganga wetu atafikia hapo kwangu na atakuwa anaendelea kumtibu. Hivyo watu wenyewe kwa akili zao watakuwa wanajua ni hizo dawa za hospitali na pia wote kwa pamoja tutakuwa tunamshukuru huyo dokta atakayemwndikia dawa." Mwingine naye akauliza, "Pesa ya kumpa huyo mwenzetu kwa ajili ya tiba tutaipata wapi?" Mwingine tena akajibu, "Tutamwuliza mwenyekiti pesa aliyonayo kisha itakayo baki tutatafuta pa kumkopea."

Basi baada ya mazungumzo hayo kila mmoja wao akatawanyika kuendelea na shughuli zao za kichawi za kila siku. Kesho yake asubuhi walimpa mwenyekiti wao mrejesho wa kikao chao cha dharura akasema, "Sawa, fanyeni hivyo haraka kwani nakufa najiona." Nina pesa ya ng'ombe tisa, nyingine itakayobaki nitaimalizia kuilipa baada ya miezi miwili, wapangaji wangu watakuwa wamekwisha kunilipa kodi." Alikuwa anazungumza hivyo huku akitetemeka mwili mzima na kuhemea juu juu. Gufa akamweleza,

“Dada, jiandae sasa twende kwanza hospitali kwani tulikubaliana hivyo ili watu wanaokuja kukusalimia wajue ni ugonjwa wa kawaida ambao ni mzio ndio umekusababishia hali hiyo.” Kuchi akasema, “Sawa, jamani uwii!, Nakufa!, Nakufa!, Fanyeni haraka mtaalamu huyo aje.” Mmoja wao akamjibu, “Atafika leo jioni badala ya kesho. Hadi sasa yupo safarini anakuja.” Mwenyekiti akasema, “Jamani nilidhani anakuja na usafiri wetu wa haraka kumbe tena anapanda basi! Nakufa mie!” Nzile akamwambia, “Dada, si utulie basi! Kuna baadhi ya dawa na masharti yake ndio maana anakuja kwa usafiri wa basi. Wewe pia unalijua hilo! Mwishowe unataka wageni watakaokuja kukujulia hali wagundue mipango yetu sasa.” Kuchi akajibu, “Sawa! Sawa! Ninanyamaza kabisa.”

Muda sio mrefu, Ipanga alifika nyumbani akitoka anaposomea na kumkuta Gufa kasimama nje. Alimsalimia akaitikia ingawa hakumwambia kuwa Kuchi yumo ndani anaumwa. Alifungua kwenye chumba chake na baada ya muda akaenda nyumba kubwa kuwasalimia sengi zake wengine. Alipofika mlangoni akukuta viatu vingi mlangoni, akashtuka kuwa chumbani kwa Kuchi kuna nini. Alisogea kisha akabisha hodi na kuingia ndani.

Aliwasalimia wengine waliokuwemo ndani wakamwitikia. Alipofika kwa Kuchi aliyekuwa amekaa kwenye kiti tayari kwa maandalizi ya kupelekwa hospatali alimsalimia ila hakuitikia. Akamsalimia mara ya pili vivyo hivyo hakumwitikia. Hatimaye mmoja wa waliokuwemo humo ndani akamjibu Ipanga kuwa amwache kwanza apumzike hata hajisikii kuongea. Ipanga alikubaliana na maelezo hayo ingawa yalimpatia mashaka sana kwani kabla hajabisha hodi alisikia sauti ya huyo Kuchi akiongea. Ipanga alisimama kwa dakika chache tu kisha akatoka nje na kurudi chumbani kwake.

Baada ya muda walileta usafiri na kumpeleka hospitali akaandikiwa dawa kisha akarudishwa nyumbani. Ilipofika jioni, huyo mtaalamu ambaye ni mganga mchawi alifika na kuanza kumtibu kwa kificho huku wengine wote wakijua anatibiwa kwa dawa za hosptalini. Mganga wao alimtibu kwa muda wa mwezi mmoja na hatimaye akawa amepona kabisa. Baada ya kupona, Kuchi alimwuliza mganga huyo chanzo hasa cha nguvu ya Ipanga hadi kumshindwa kiasi hicho kwa kila dawa anayoitumia kichawi. Mganga alimjibu kuwa yeye katumia tu uzoefu wa kumtibu kama

anavyotibu wagonjwa wengine wenye tatizo kama hilo. Lakini nguvu halisi za huyo kijana huyo hakuziona.

Muda ulivyozidi kusonga mbele, maisha ya Ipanga kielimu yakaanza kubadilika na kuwa mazuri kwani ufaulu wake ulianza kupanda. Hali hiyo ilimfurahisha sana Ipanga, rafiki zake, walimu wake pamoja na mama yake kwani baba yake hakutaka kabisa kusikia kuhusu elimu ya mwanae. Pia hali hiyo ilimfurahisha sana rafiki yake Masha ambaye walikuwa wakiwasiliana pamoja kupitia barua kwa anwani za shule. Ipanga na mamaye hawakuacha kusali na kumwomba Mungu wao aliye juu kila mara usiku na mchana. Maisha yaliendelea hivyo hivyo hatimaye Ipanga na Masha wakahitimu kidato cha nne. Baada ya miezi kadhaa, matokeo ya kidato cha nne yalitoka na Ipanga akawa amefaulu kwa ushindi wa daraja la pili na Masha akawa amefaulu kwa ushindi wa daraja la nne. Ipanga alichaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule iliyopo hapo hapo mjini na Masha hakuweza kupangiwa shule yoyote ili kutokana na ushindi hafifu alioupata. Lakini muda wote huo Ipanga na Masha walipotezana katika mawasiliano baada ya kuhitimu kidato cha nne kwani Masha

hakurudi tena kijijini kwa sababu alianza kujishughulisha na kazi ya kibarua cha kukata nyasi kwa ajili ya ng'ombe wa watu pamoja na kufanya usafi wa mazingira ya nje ya nyumba za watu huko alikokuwa.

Sura ya Tano

Ipanga aliendelea na masomo ya kidato cha tano katika mchepuo wa sayansi. Aliishi katika mazingira ya kutokula kwa ndugu wa baba yake kwa muda wote huo wa masomo yake. Ndugu wa baba yake na wajumbe wengine waliendelea kuumiza vichwa vyao jinsi ya kumlisha Ipanga chakula chenye dawa walizoziandaa. Siku moja wakiwa kwenye kikao chao cha kichawi, mmoja wa wajumbe akamwambia Kuchi. "Mwenyekiti, nimepata wazo, kwa nini tusiangalie kama tuna wajumbe wetu walioko sokoni kwenye migahawa anapokula huyu mtoto anayetuumiza kichwa ili tumtumie yeye kuendeleza dawa ya kumpumbaza kupitia chakula?" Mwenyekiti akajibu, "Hili pia ni jambo jema. Wajumbe mnaonaje juu ya wazo hili?" Mjumbe mmoja akajibu, "Mwenyekiti, hili wazo ni zuri na inawezekana kabisa. Kikubwa tujue anakula kwenye mgahawa gani." Mwenyekiti akasema, "Ninawapa hilo zoezi la kufuatilia anakula kwenye mgahawa upi ili tupange taratibu zetu. Inatakiwa asifaulu mitihani yake ya kidato cha sita. Hivyo, kesho nahitaji kupata majibu juu ya hilo." Wote kwa pamoja wakaahidi kulifanyia kazi zoezi hilo na

kisha wakatawanyika kwenda kuendelea na shughuli zao za usiku wa hiyo siku.

Kesho yake walileta majibu kwa mwenyekiti ingawa hayakuwa mazuri kama alivyoyatarajia. Mjumbe mmoja akasema, “Mwenyekiti, mgahawa ambao huwa anapendelea kula chakula tumeupata na karibu kila siku jioni huenda kula. Hata jioni ya leo tumemwona akiingia ndani kula. Lakini changamoto kubwa ni kwamba, wenye mgahawa huo sio wenzetu na tumejaribu kuongea na mwenzetu ambaye pia ana mgahawa jirani na mgahawa anapokula Ipanga akadai zoezi halitawezekana. Kwa sababu hata yeye alikwisha jaribu kuwaingizia wazo wakakataa tena kwa kumwambia asije akajaribu tena kuwapelekea wazo la namna hiyo. Nilijaribu kuwabembeleza kwa kuwapatia pesa nyingi sana lakini walinijibu bora waendelee kubaki na umasikini walio nao kuliko kufanya hicho kitendo cha kuwawekea ama kumwekea mteja wao dawa za kichawi kwenye chakula. Hivyo alichukizana nao na hadi sasa huwa hawaelewani vizuri.” Mwenyekiti akasema, “Mbona zoezi linataka kuwa gumu sana! Kwa nini anakuwa mgumu hivi hata kumfanya awe kichaa!

Siamini kama huyu nae anataka kutushinda kama baba yake!"

Kipindi mwenyekiti kajiinamia anawaza nini cha kufanya, mjumbe mmoja aliingiza hoja na kusema, "Mwenyekiti, mimi nina wazo. Kwa vile kwa sasa inakuwa vigumu kumlisha dawa hata kichawi, kwanini tusitumie mjumbe mwenzetu wa kijijini kwao kwa muda anaokwenda likizo?" Mwenyekiti akajibu, "Huu ni mtihani, lazima tukubali. Tuna mwenzetu huko aitwaye Kikavu. Huwa hacheleweshi mambo ila kwa familia ya mzee Utulivu mwenyewe anaonekana kushindwa kwani mnakumbuka hata kile kipindi, tulimwongezea nguvu za kichawi lakini mambo yakashindikana. Kumbuka kila tulipokuwa tukimwongezea nguvu ndipo alizidi kubanwa na kuumia kifua. Siku alipoamua kwenda mwenyewe kichawi kuichunguza zaidi hiyo familia ya mzee Utulivu, aliishiwa nguvu na kujikuta anadondoka chini. Kipindi anagalagala hapo chini asijue cha kufanya, ghafla aliishiwa nguvu za kichawi na kujikuta wa kawaida huku akihojiwa maswali na jitu kubwa sana mfano wa mwamba. Baada ya kumaliza kuhojiwa aliruhusiwa kuondoka huku akiwa mtupu kama alivyozaliwa na alipofika nyumbani

kwake alipooza miguu na mikono hadi leo hii tunavyoongea bado kapooza. Pia vifaa na dawa zinazotumika kumwongezea nguvu ni ghali sana. Lakini mnaona kwa wazazi wa Masha alitumia nguvu kidogo sana na sasa tunao huku kuzimu wanatufanyia shughuli zetu. Mimi ninaona, tumpige mikosi mzee Utulivu kwenye biashara yake afilisike na mwisho Ipanga na mama yake wao tuwatengenezee chuki kubwa sana kwenye jamii zao ili kila mmoja awachukie na kuonekana kinyesi."

Mjumbe mwenzao akaongeza, "Tena kweli mwenyekiti. Pia tuna wanachama wenzetu ambao ni mabinti warembo wazuri tu, inabidi tufanye juu chini Ipanga na Masha wawatongoze ili wawe wapenzi wao na ikiwezekana wawaoe. Hapo tutakuwa tumewamaliza kabisa kwani watalishwa hadi ile dawa inayovundikwa sehemu za siri kwa siku saba na kuchanganywa kwenye chakula. Hapo hawatawaza lolote lile zaidi ya sisi kuwafanya tunavyotaka." Mjumbe mwingine akadakia, "Mwenyekiti huko shuleni wanaposomea tuna wajumbe wenzetu ambao ni wanafunzi na wengine walimu, wamejaribu kwa kila namna kuwaweka karibu wawe wapenzi wao lakini wamejikuta

wakipewa majibu magumu na kuambiwa hawataki mazoea. Hilo tunalifanyaje?"

Ingawa mwenyekiti alikuwa anaiona hali ya kuwachawia Ipanga na Masha jinsi ilivyo ngumu, ilibidi awape maneno ya kuwatia moyo, "Pole pole tutawanasa tu kwani hata miji mikubwa katika mataifa mbalimbali haikujengwa kwa siku moja. Hivyo, kuwafanikisha hawa watu hususan Ipanga ni hatua za hapa na pale bila kukata tamaa. Ikishindikana zaidi, tutatumia wajumbe wenzetu wanaume ili wawashawishi na kuwatengenezea mazingira ili mabinti zetu wawapate kiurahisi." Baada ya maneno hayo, wajumbe wote katika hicho kikao wakaelewa na kumkubalia mwenyekiti wao. Mwenyekiti akaongeza, "Tena hakuna kucheleweshe mambo hapa, siwaoni mabinti zetu wengine hapa, wako wapi?" Mjumbe mmoja akajibu, "Wengine wapo njiani wanakuja na wengine wapo na waume za watu kwa ajili ya kuvuruga ndoa zao." Mwenyekiti akaamuru, "Piga mbiu waje mara moja niwape maelekezo kisha wakaendelee na shughuli zao."

Baada ya mwenyekiti kusema hivyo ilipigwa mbiu ya kichawi na dakika moja tu wote wakawa wamefika. Mwenyekiti akawauliza mmoja mmoja

wale waliokuwa na waume za watu wakizini, “Wewe umemwacha anazini na nini?” Akajibu, “Mkuru nimemwacha anaendelea kuzini na fisi.” Mwenyekiti akamwuliza wa pili, “Wewe umemwacha na nini?” Naye akajibu, “Mkuru nimemwacha anazini na gogo la mgomba.” Akamwuliza wa tatu, “Wewe umemwacha anazini na nini?” Akajibu, “Mkuru, nimemwacha anazini na msukule. Nina kazi ya kumyonya ufahamu wake asiwazie tena mke na watoto wake. Niliamua kwenda na msukule ili yeye akiwa anaendelea kuzini naye huku mimi nikicheza na kichwa chake kumwondolea ufahamu.” Mwenyekiti akatoa pongezi, “Kazi nzuri sana, endeleeni kufanya hivyo na pia mkumbuke tunauhitaji sana wa pesa hivyo mnavyowateka akili ni vyepesi kuwa mnapewa hata bila ya kuwaomba. Pia kumbukeni tunahitaji pesa nyingi kwa ajili ya kuwatibisha wanachama wetu wazee, kujitibisha sisi wenyewe pamoja na kuwalisha hawa mitunge tulionao huku kuzimu. Mnanielewa vizuri ninyi mabinti?”

Wote kwa pamoja wakaitikia, ndiyo mkuru. Mwenyekiti akaendelea, “Nimewaiteni hapa kwa suala moja tu ili mrudi kuendelea na kazi zenu. Ipanga na Masha wanataka kutuchanganya akili.

Sasa inatakiwa mkafanye nao mapenzi, sio mkafanye nao mapenzi usiku wakiwa usingizini kama mnavyofanya mkiwa na hamu zenu!, Hapana! Inatakiwa mzini nao wakiwa na fahamu zao za kiubinadamu ingawa haidhuru ikiwa mchana ama usiku. Kuna dawa mpya tumepata ambayo inatakiwa iwekwe sehemu za siri ndipo mkutane nao kimwili. Ila hakikisheni hamtumii kinga mnapojamiiana. Ni bora mkawaaminisha kwa kushawishi mkapime kwanza ili mkutane nao kimwili ili dawa ifanye kazi sawa sawa. Mfanye kwanza taratibu zote mzijuavyo na mziwezavyo, ila siku mtakapopeana ahadi ya kukutana kwa ajili ya hilo tendo mtufahamishe ili mpewe hiyo dawa mweke ndipo muanze safari kwenda kukutana kimwili. Watakaofanikisha hilo tendo sawa sawa watapewa zawadi nono ikiwemo kupandishwa cheo na safari za hapa na pale ndani na nje ya nchi. Mimi nimemaliza, haya tawanyikeni."

Walipomaliza kupewa maelekezo hayo, wakatawanyika na kila mmoja akarudi alipokuwa kuendelea na kazi yake. Mwenyekiti akaendelea na kikao, "Tayari mabinti wameondoka, nilikuona kama unawaza. Ulitaka kusema nini!" Mjumbe huyo akasema, "Mkuru, mimi nina wazo kuhusu

Ipanga. Tunaye mwanachama mwenzetu ambaye sasa ni zamu yake kutoa sadaka ya mtoto ampendaye huku kuzimu na ana ukaribu na urafiki wa familia ya akina Ipanga. Kwa nini tusitumie nafasi hiyo kumtengenezea Ipanga kitu kibaya kwenye jamii?" Mwenyekiti akaunga mkono, "Wazo zuri sana, huyo mjumbe ambaye sasa ni zamu yake kumtoa mwanaye sadaka yuko hapa kwenye kikao?" Mjumbe akajibu, "Ndiyo mkuru, niko hapa na ni kweli muda wa kumtoa sadaka mwanagu kipenzi umefika." Mwenyekiti akamwuliza, "Tofauti na urafiki wetu mimi na wewe, kuna wengine katika familia hiyo una urafiki nao wa karibu?" Akajibu, "Hapana mkuru, ni wewe tu. Labda na wale madada wadogo zako na watu wengine ambao huwa unanitambulisha kwao." Mwenyekiti akasema, "Hapo hakijaharibika kitu. Haya leteni mbinu tutakayotumia ili kifo chake kimuangukie Ipanga." Mjumbe mmoja akasema, "Kwanza, kwa vile kijana huyo naye amehamia hapa kimasomo, tumshawishi awe anakwenda kwa Ipanga kujisomea na itafikia hatua ataanza kulala kwenye hicho chumba chake. Hapo tutafanya yetu ili kijana huyo afie humo ndani ambapo tayari serikali itamkamata Ipanga na sisi

tutaanza kusema kuwa yeye ndiye amehusika na kifo chake."

Mwenyekiti aliendelea, "Sawa, ni wazo zuri isipokuwa sijaona chanzo cha tatizo kati ya huyo kijana na Ipanga ili tupate nguvu ya kusema kuwa Ipanga ndiye kahusika. Nadhani mnafahamu vizuri kabisa kuwa hizi mbinu za vifo huwa tunatengeneza mgogoro ama sababu ambayo huwa tunaichukulia kuwa ndicho chanzo cha yeye kumwua mtu. Ili hata utakapokuwa unawajengea hoja watu, waelewe kuwa kweli hiyo ndiyo sababu. Nadhani wote kwa pamoja mnanielewa vizuri?" Wajumbe wote wakajibu, "Ndiyo mkuru, tunakuelewa vizuri." Mwenyekiti akaendelea, "Ndio hivyo, kwenye jamii kuna watu wanauelewa tofauti tofauti sana, kwa hiyo lazima kutumia akili nyingi sana katika kila jambo zito ili wasitutilie mashaka yoyote yale." Mjumbe mwingine akasema, Mkuru, mimi naona baada ya kuwa wanalala chumba kimoja, tumtengenezee chuki na kiburi huyo kijana kwa Ipanga ili Ipanga amgombeze ndipo tuanzie hapo." Mwenyekiti akasema, "Ninavyomfahamu, Ipanga ni mkali na mkorofi ingawa siyo msemaji sana. Hivyo anaweza kuamua kumfungia tu mlango na kumwambia huyo kijana

arudi kwao. Hivyo tutakuwa hatujatimiza malengo yetu."

Wakati huo wote mwenyekiti alikuwa akiwajibu hoja zao huku akifikiria nini cha kufanya na baadaye akapata wazo. Mwenyekiti akasema, "Nimepata wazo. Ipanga kwa sasa anamiliki simu aliyonunuliwa na baba yake. Tuichukue hiyo simu kichawi ikiwa chumbani mwao na kisha lazima tu watavurugana kwa vile wanaishi wawili tu humo ndani. Kama ambavyo huwa tunafanya kuleta migororo katika familia nyingi ama kwa wana ndoa kwa kuchukua pesa na vitu kichawi kisha wakaanza kuvurugana wao kwa wao na kupoteza imani miongoni mwao." Mjumbe mwingine akasema, "Mkuru, tena kweli! Hiyo ndiyo njia nzuri na salama kwetu, nasi baada ya kuichukua simu hiyo tutaanza kusema na kuwaambia watu kuwa Ipanga alisema aliyeiba simu yake atakufa." Mwenyekiti akapinga hoja hiyo ya mjumbe, "Hapana, tusiseme kuwa atakufa. Sisi tuseme kuwa Ipanga alisema aliyeiba simu yake ataona. Kwa vile hatua ya kwanza kabla ya kumleta kuzimu huyo kijana ni kumtia wehu, hivyo wataamini kwamba Ipanga ndiye aliyemtengenezea dawa ama ndiye aliyemfanya kuwa mwehu kwa sababu ameiba

simu yake. Halafu hatua ya kumwua itakuwa nyingine ambapo tutakuwa tunaongea kwa wanajamii kwa kujifanya tunawaibia siri kuwa wawaogope sana Ipanga na mama yake kwani ni wachawi hatari sana. Tukishatengeneza hilo tukio hadi huyo kijana kumleta kuzimu, kisha tukaanza kuwaambia watu kuwa hao ni wachawi watatuamini bila shaka yoyote." Wajumbe wote walikubaliana na mbinu za mwenyekiti na kuzibariki tayari kwa utekelezaji. Maisha ya Ipanga na shule yaliendelea kuwa mazuri ya wastani yaliyomfanya kufaulu mitihani yake ya kidato cha tano na kujiunga na kidato cha sita kwani utaratibu wa shule hiyo mwanafunzi haruhusiwi kujiunga na kidato cha sita mpaka afaulu mitihani ya kidato cha tano. Wakati wote huo vitimbi vya hapa na pale vilikuwa vikimkumba sana Ipanga ila kwa ajili ya kusali na kuomba kwake na mama yake alivivuka. Wakati huo wote mabinti warembo ambao ni wachawi waliendelea kumzongazonga ili awatongoze.

Siku moja Jumamosi akiwa anaelekea nyumbani akitokea shuleni kujisomea, alikutana na binti mmoja barabarani huku binti huyo kajiinamia anakanda tumbo lake na akionekana kuhitaji

msaada. Ipanga alimsogelea kisha akamsalimia ingawa moyo wake ulilipuka na kuanza kumwenda mbio lakini hakujali kwani hakujua nini maana ya ishara hiyo. Alimwuliza, “Samahani dada una shida yoyote ile?” Yule binti akamjibu, “Ndiyo kaka, ninaumwa sana tumbo.” Ipanga akamhurumia kisha akamwuliza tena, “Pole sana! Tatizo hili huwa linakutokea mara kwa mara?” Yule dada akajibu, “Hapana, hii hali imenitokea muda huu tu, ninashindwa hata kujua shida ni nini hasa!” Muda huo wote, yule binti alikuwa akiongea huku akidondosha machozi kuonesha kwamba ana hali mbaya. Ilibidi Ipanga amshike mkono na kumsaidia kutembea akamkalisha ukingoni wa barabara. Akamwambia amsubiri hapo kwa muda wa dakika chache ili akamchukulie maji madogo ya kunywa dukani ili ajaribu kunywa aone kama ataweza kuwa sawa. Ipanga alikwenda kumnunulia maji madogo kisha akampatia akanywa.

Baada ya kunywa yale maji, alionekana amepata nafuu kidogo, akamshukuru Ipanga. Ipanga aliomba amsindikize hadi anapoelekea ili ahakikishe amefika salama. Yule binti alikataa na kusema, “Hapana kaka, usijali nitafika tu salama. Pia nikushukuru tena kwa msaada wako.” Ipanga

akamjibu, “Usijali dada, lengo langu ni kuhakikisha unafika salama huko uendako. Labda unaweza kuwa na namba ya simu ili baadaye nikujulie hali?” Yule binti akajibu, “Hapana, nina laini tu kwani simu yangu ni mbovu. Ninaomba wewe ndio unipe namba yako niiandike na nitakapo fika nyumbani nitaazima simu niiweke laini yangu kisha nikupigie kukufahamisha.” Ipanga akamtajia namba yake ya simu akaiandika kiganjani kwake. Ipanga alikaa hapo kwa muda mfupi kisha akumuaga binti akaondoka kuendelea na ratiba zake. Siku moja Ipanga akiwa chumbani kwake kapumzika, aliamua kwenda kuwasalimia ndugu wa wa kike wa baba yake. Alipomaliza kuwasalimia, Kuchi akamwambia, “Ipanga, tena bora umekuja kwani nina shida na wewe.” Ipanga akasema, “Sawa sengi, unaweza kuniambia.” Ipanga alikaa kwa makini sana kumsikiliza sengi yake anamwambia kitu gani. Kuchi akamweleza hivi, “Ipanga, kuna kijana mwenzako anataka awe anakuja kujisomea na wewe hasa usiku unaporudi.” Ipanga akamwuliza, “Ni kijana gani huyo sengi?” Kuchi akamjibu, “Ni yule mtoto wa mama Yaya ambaye ni Yaya mwenyewe.Tangu walipohamia hapa jirani, hana mtu wa kujisomea nae ndio maana mama yake alikuja kuomba uwe unajisomea nae.

Atakuwa anakuja kujisomea hasa usiku." Ipanga akajibu "Hakuna shida sengi, yeye aje tu." Kuchi akasema, "Ngoja nikamwambie mama yake aje nae kwani ni hapa nyumba ya nyuma tu." Ipanga akasema, "Sawa sengi."

Kuchi alinyanyuka na kwenda kumwita mama Yaya wakaja na Yaya mwenyewe. Yaya akakutanishwa na Ipanga kisha Ipanga akampa Yaya ratiba yake ya kujisomea. Yaya alifurahi sana kuwa sasa atakuwa anasaidiwa kimasomo sababu Ipanga yupo kidato cha sita na yeye yupo kidato cha tatu. Baada ya mazungumzo hayo, Yaya akamwomba Ipanga kuwa ataanza kuja kujisomea kesho yake na Ipanga akamjibu hakuna shaka na anakaribishwa sana. Kesho yake Yaya akaja usiku baada ya kumaliza kula akamkuta Ipanga tayari kwani siku hiyo Ipanga aliwahi kurudi kwa kujua ana mgeni. Yaya alibisha hodi kwa Ipanga, "Hodi kaka!" Ipanga akajibu, "Karibu, ingia ndani."

Yaya aliingia ndani kisha akamsalimia, "Shikamoo kaka!" Ipanga akaitikia, Marhaba, karibu uketi. Yaya akajibu, "Ahsante sana." Baada ya hapo, Ipanga alimwuliza Yaya kuwa ni masomo gani hasa angependa kusaidiwa. Yaya alijibu kuwa angependa kusaidiwa sana masomo ya sayansi

kwani ndio mchepuo wake. Ipanga akamwuliza tena, “Sawa, hivyo leo ungependelea tuanze na somo gani?” Yaya akajibu, “Kaka napenda tuanze na somo la hisabati.” Ipanga akamwuliza tena, “Sawa, tuanze na mada gani?” Yaya akajibu, “Kama tukianzia na mada ya kwanza ni sawa tu kaka.” Ipanga akasema, “Basi hakuna shaka. Ninaomba uwe unajisomea kwa muda mfupi nimalizie kufanya kazi hii, inahitajika kukusanywa kesho asubuhi, ndipo nianze kukufundisha.” Yaya akasema, “Hakuna shaka kaka.”

Ipanga alimaliza kazi aliyokuwa akifanya kisha akaanza kumfundisha kijana huyu. Kipindi anaendelea kumfundisha huku akimpatia maswali na kuyafanya vizuri, akajikuta anatamani zaidi kumsaidia kwani alimwona ni kijana mwenye uelewa na anapenda kujibiidisha kwenye masomo yake. Baadaye kijana alichoka na akapumzika wakati huo Ipanga akaanza kujisomea na baada ya saa kadhaa akamaliza kujisomea, akaomba na kusali kisha nae akalala. Ilipofika alfajili wote waliamka na kujisomea kidogo kisha kijana akamuaga Ipanga na kuelekea kwao kwa ajili ya kujiandaa kwenda shule. Ipanga nae akaanza kujiandaa tayari kwa kwenda shule. Ipanga

aliendelea kumsaidia kijana huyo kwa muda wa miezi sita hivi na tayari akawa amemwamini hadi kufikia hatua akamkabidhi ufunguo mmoja wa chumbani kwake ili muda wowote kijana atakapojisikia kusoma awe huru kufanya hivyo. Siku moja saa nne usiku, Ipanga alikuwa akijisomea na tayari akawa amekwisha funga mlango kwa sababu kijana alimtaarifu kuwa hatakuja kutokana na uchovu aliokuwa nao. Siku hiyo alijikuta anapitiwa na usingizi mzito sana uliopelekea kujiona yuko sehemu huku kazungukwa na umati wa watu. Alikuwa anaongoza huo umati uliomzunguka kwa kuomba. Aliomba sana kwa muda mrefu bila kupumzika kisha akamaliza kuomba. Alishtuka kutoka usingizini muda wa saa tisa usiku na kujikuta ameloa jasho mwili mzima. Hiyo hali ilimshangaza sana kwani amezoea kusali na kuomba kwa hali ya kawaida akijitambua lakini sio kupitia ndotoni. Ilibidi asipande kitandani kulala kwani muda huo alikuwa kwenye maandalizi ya kujisomea hatua ya mwisho kwani mitihani yake ya kuhitimu kidato cha sita ilikuwa inakaribia.

Baada ya muda alianza mitihani yake ya kumaliza kidato cha sita huku ile hali ya kubanwa

tumbo na kuhara kila anapoanza mtihani ikiendelea kupungua. Siku ya kuanza mtihani wa kwanza akiwa kwenye chumba cha mtihani asubuhi alipatwa na kizungu zungu kikali sana. Alipoinama chini na kuanza kusali, hiyo hali ya kizunguzungu ikapungua na baada ya muda kidogo ikapotea kabisa na kumfanya aanze kufanya mtihani. Kipindi chote cha kuanza mitihani yake hadi kumaliza alikuwa akiishi kwa rafiki zake. Alipomaliza mitihani akarejea kwenye chumba chake.

Ndugu wa damu wa baba yake pamoja na washirika wao wa mambo ya kuzimu walizidisha chuki kwa Ipanga ingawa hawakutaka kumwonesha moja kwa moja. Waliendelea na mikakati yao ya kumpatia sifa chafu katika jamii. Siku moja Gufa alimwita,akasema “Ipanga, kuna jambo nataka nikuambie mwanangu ila unifichie siri.” Ipanga akamjibu, “Hakuna shaka sengi.” Gufa akaongeza, “Nitatafuta muda mzuri tujifiche huko nyuma ya nyumba nikueleze.” Ipanga akajibu, “Sawa sengi.” Baada ya siku mbili akamwita, “Ipanga mwanangu, leo baadaye tutakuwa na muda mzuri wa kuongea kwani hawa ndugu zangu wengine hawatakuwepo, na mimi sitaki watuone.”

Ipanga akakubali kwa kusema, “Sawa sengi.” Kweli baada ya muda Gufa akamwita wakazunguka nyuma ya nyumba na kuketi juu ya matofali yaliyokuwa yamepangwa chini. Akaanza kumweleza, “Ipanga mwanangu, ninakupenda sana na ninaumia sana kuona wenzangu wanavyokuchukia. Kwani wangejua, wewe ilitakiwa wakupende kwa nguvu zao zote kwa sababu hadi hapa tulipo ni kwa sababu ya upendo wa dhati wa baba yako. Yaani kama Kuchi ananikera anavyokuwa anakusema sema vibaya kwa watu. Sema tu sina uwezo ila ningeondoka hapa nikaenda kuishi hata huko kusikojulikana ili mradi tu nisisikie maneno machafu anayokusema kwa watu mbalimbali ikiwemo ndugu zetu wa karibu. Ona hata sisi anavyotunyanyasa kisa yeye ni mkubwa, wapangaji wote hapa kodi ya nyumba huwa anachukua yeye. Huwa unaona wanampatia yeye, siyo?”

Ipanga akajibu, “Ndiyo, huwa naona.” Gufa akaendelea kueleza, “Sasa sisi wakati mwingine hata sabuni ya kufulia huwa anatunyima hadi tunasaidiwa na wapangaji. Lakini tabia hii kazaliwa nayo kwani amekuwa hivi hivi tangu akiwa mdogo kwa jinsi alivyokuwa akitusimulia mama

yetu. Mpaka nimesikia kwa watu akidai kuwa huwa unaiba pesa na kumpelekea mama yako kijijini. Yaani huyu, ninavyopendana na wifi yangu, akiyasikia maneno hayo si itakuwa aibu kwangu pia. Hata majuzi nilitoka huko kwenda kumsalimia wifi yangu kipenzi. Si uliona mwanangu?" Ipanga akajibu, "Ndiyo, niliona." Gufa akaongeza, "Yaani huyu ndugu yetu anatuweka katika wakati mgumu sana hata kwa kaka kwani akiyasikia haya maneno hatajisikia vizuri. Nakuibia siri hii mwanangu, kwanza huyo Kuchi, siyo ndugu yetu wa damu. Mama yetu alitembea na mwanaume mmoja hapo kijijini na ndiye aliyempatia ujauzito. Baba yetu alilea ujauzito tu hadi kupata mtoto ambaye ndio huyo dada yetu. Hii ni siri nimekuibia, kwani ni mimi tu ndiye ninayejua haya mambo na nimekwambia wewe kwasababu nakupenda mwanangu. Jambo jingine analoniudhi huyu dada yetu, eti ulipoacha kuwa unakula hapa nyumbani alianza kusema kwa watu umeacha kula kwa sababu chakula cha hapa labda hakiungwi vizuri kikawa kitamu. Mimi nimekuwa nikimkatalia sana na kumwambia kuwa wewe ni mwanafunzi kwa hiyo una muda wako maalum wa kula na si chakula cha hapa cha kuliwa mara saa nne usiku mara saa tano usiku. Chai yenyewe inapikwa

anapojisikia yeye kwa kuamua ipikwe ama isipikwe. Kwani huwa unakula wapi mwanangu?"

Ipanga akajibu, "Huwa ninakula kwa rafiki zangu huko ninakosomea." Gufa akahitimisha kwa kusema, "Kumbe, mimi yangu ni hayo na ningekuwa na uwezo na nina nyumba yangu, ningekuchukua tukaenda kuishi pamoja. Humo mwako una nguo ambazo zimeisha hazivai? Nataka nimpatie mtoto wa rafiki yangu hana kabisa nguo." Gufa akauliza. Ipanga akajibu, "Hapana sengi, sina kwa sasa." Gufa akasema, "Sawa, ninaomba karatasi ambazo ulikuwa unazitumia kuandika ulipokuwa unajisomea ili niwe nawashia mkaa sababu hiki kimvua kinanipa shida kweli hadi mkaa kuja kuwaka." Ipanga akasema, "Sawa sengi, nitakukusanyia nikupatie." Gufa akasema, "Nitashukuru sana mwanangu. Haya, nikuache uendelee na kazi zako." Ipanga akaitikia, "Sawa sengi."

Wote walinyanyuka kisha kila mmoja akaendelea na mambo yake. Lakini kipindi Ipanga anamsikiliza sengi yake alijiuliza maswali mengi sana ikiwemo uhakika wa wa maneno aliyokuwa akimwambia hasa yaliyokuwa yanamuhusu Kuchi. Mojawapo ni kuhusu chakula kuwa hakiungwi

vizuri ambapo neno hilo alilisikia kwa masikio yake mwenyewe huyo huyo Gufa akimwambia mgeni aliye zuru hapo nyumbani na kusisitiza kuwa anamaliza pesa za baba yake kununulia chakula wakati hana uwezo wa kufaulu masomo yake. Ilibidi asiyajali sana maneno ya huyo sengi wake.

Baada ya siku kadhaa, Ipanga alifanya usafi wa chumba chake na kuzikusanyia karatasi zote nje ili azichome moto. Alizitenganisha na magazeti mbalimbali yaliyokuwa yamejaladia madaftari yake. Alijikuta anawasha moto zile karatasi alizokuwa akizitumia kuandika kumbukumbu zake kipindi anajisomea na karatasi zote zikaungua. Alibakisha magazeti na majarida mbalimbali ndipo akakumbuka kuwa aliombwa karatasi za kuwashia moto. Ilibidi ampelekee hayo ingawa Gufa aliyapokea kwa shingo upande kwani lengo lake alihitaji karatasi zilizoandikwa kwa mkono wake kwa ajili ya kazi zake maalum za kichawi walizokuwa wakiendelea nazo juu ya Ipanga. Wakati huo wote, kijana aliendelea kuja kufundishwa na Ipanga na kumfanya ufaulu wake kupanda kila kukicha.

Sura ya Sita

Baada ya siku kadhaa, Ipanga alipata kazi ya kujitolea kwenye kiwanda cha kutengeneza biskuti na kuanza kufanya kazi. Kiwanda hicho kimechukua eneo kubwa sana. Kiwanda kimejaa majengo na karakana nyingi. Baadhi ya wafanyakazi wanaishi ndani ye eneo la kiwanda ili kufanya kazi kwa ufanisi na kuwahi kazini. Hakutaka kurudi kijijini kwani tayari alikwishawapa taarifa wazazi wake kuwa atakapohitimu kidato cha sita atabaki mjini kutafuta kibarua cha kufanya huku akingoja matokeo yake. Kitendo cha Ipanga kupata kibarua kiliwaumiza sana ndugu hao wa baba yake ingawa walijipa moyo kuwa hatafanya kazi muda mrefu. Atafukuzwa na pia mtihani aliyoifanya ya kidato cha sita hatafaulu hivyo atakuwa ni mtu wa kutanga tanga tu bila mwelekeo wowote wa maisha. Walijipa moyo kutokana na mitego yao ya kichawi waliyokuwa wamemtega. Ipanga aliendelea na kazi yake ya kujitolea kwa muda wa miezi michache huku akipatiwa pesa ya nauli na chakula tu. Baadaye uongozi wa kampuni ulifurahishwa sana na utendaji wake wa kazi hivyo

wakakubaliana na kuamua kuanza kumlipa mshahara.

Siku moja asubuhi baada ya Ipanga kuripoti kazini, aliitwa ofisini kwa mkurugenzi. Hali hiyo ilimwogopesha sana kwani kwa asilimia kubwa ukiitwa kwenye ofisi hiyo, basi kunakuwa na tatizo kubwa. Aliitikia wito na kuelekea kwenye ofisi ya mkurugenzi. Mkurugenzi wa kiwanda cha biskuti ni mzee wa makamo, mnene, mweupe na kitambi cha wastani. Anapenda kuvaa suti mara kwa mara. Ofisi yake ni kubwa yenye shelfu kubwa moja ikionesha mafaili mengi na kabati ambalo muda wote limefungwa na kufuli. Meza yake ilikuwa na mafaili machache kwenye makasha mawili yaliyoandikwa ingia na ondoa. Pembeni kulikuwa na jokofu, na meza nyingine ndogo ilikuwa na glasi, maji ya chupa na paketi mbili za biskuti. Alitumia miwani yake kusomea, hivyo wakati akimwangalia mtu, alishusha miwani na kumwangalia mtu kwa macho ya kawaida bila miwani.

Ipanga ofisini na kuambiwa aketi kwenye kiti. Aliketi huku akijihisi kutetemeka na kuwaza kuna kosa gani alilifanya hapo kiwandani kwa siku chache zilizopita wala asilione. Alipofika, mkuregenzi msaidizi akamweleza, “Ipanga,

kwanza pole kwa kukukatisha majukumu yako kwa muda. Tumekuita hapa kwa kuwa mkurugenzi mkuu anahitaji kuongea na wewe maneno machache tu kisha ukaendelee na majukumu yako." Ipanga baada ya kusikia, kisha akaendelee na majukumu yake moyo wake ukaanza kutulia halafu akasema, "Sawa boss." Mkurugenzi mkuu akaanza kuzungumza, "Ipanga, kwanza hongera kwa kazi nzuri. Kazi zako zinaonekana na tunaomba uongeze bidii zaidi na zaidi. Kutokana na utendaji kazi wako tumeona kuanzia mwezi huu, tutaanza kukulipa mshahara, tutakupa pesa ya kulipia chumba na pesa ya usafiri."

Ipanga akasema huku akitikisa kichwa kwa ishara ya kukubali, "Ahsanteni sana." Mkurugenzi mkuu akaendelea, "utasaini mkataba wa mwaka mmoja kwa afisa utumishi na atakupatia taratibu zote." Ipanga akaitikia, "Ahsanteni sana boss." Afisa utumishi akasema, "Ipanga, baada ya muda wa kazi utakuja ofisini kwangu kwa taratibu zote." Ipanga akasema, "Sawa ahsante." Baada ya maelezo hayo walimruhusu Ipanga kwenda kuendelea na shughuli zake. Ipanga alitoka ndani ya hiyo ofisi akiwa amejawa na furaha kubwa. Baada ya muda wa kazi kwisha, alikwenda akamwona afisa

utumishi na kusaini mkataba ili kukamilisha kila kitu na kuanza kulipwa mshahara.

Baada ya siku chache matokeo yao ya kidato cha sita yakatoka na Ipanga akawa amefaulu na kupata sifa za kujiunga na chuo kikuu cha Poda kilichopo jijini Mwazi. Ipanga na wazazi wake hasa mama walifurahi sana. Kitendo hicho kiliwaudhi sana dada zake mzee Utulivu na kupelekea wao kwa wao kugombezana kuwa wanapopeana kazi za kufanya kuzimu juu ya Ipanga kuna wanaoleta uzembe na kusababisha kushindwa kuzaa matunda. Walipanga asihitimu kidato cha nne kahitimu, wakapanga asihitimu kidato cha sita kahitimu, wakapanga apate matokeo mabaya yasimwezeshe kujiunga na chuo kikuu kapata matokeo mazuri ya kumfanya kujiunga na chuo kikuu. Wakapanga afukuzwe kwenye hicho kibarua chake ndani ya muda mfupi lakini hadi sasa yupo kazini na maisha yake yameanza kuwa mazuri hadi ananunua vitu vya thamani chumbani kwake.

Ugomvi huo uliwachukua takribani wiki nzima na walikuwa hawasemeshani wakiwa kuzimu kwenye kazi zao za kichawi na hata walipokuwa katika hali ya ubinadamu hadi ikamlazimu mchawi mkuu wa kanda ya magharibi kuja kuwasuluhisha

na kuwaambia, “Nimekuja haraka haraka baada ya kuona utendaji kazi wenu huku una mashaka kwa wiki sasa na nimeambiwa chanzo ni ugomvi wenu ninyi kwa ninyi. Ninataka hali hiyo muiache mara moja kwani inaweza kusababisha mkapewa adhabu kali ikiwemo kushushwa vyeo vyenu hivyo mlivyonavyo. Pia ninadhani taarifa mnayo kuwa mkitaka kumleta binadamu kuzimu ikashindikana, msimng’ang’anie kwani mnaweza kufa wenyewe. Mungu wao wa kweli wa hao binadamu ana nguvu sana na ninadhani kila mmoja analijua hilo, anaweza kumlinda na kumsimamia binadamu ambaye huwa anamwomba mara kwa mara sehemu yoyote ile iwe kwenye maisha yake, familia yake, kazini kwake, kwenye nyumba yake ya ibada, shuleni na hata sehemu yoyote ile. Hebu nipeni majina pamoja na kipande cha nguo ya ndani ya huyo kijana anayewaumiza kichwa.”

Ndani ya sekunde ishirini kipande cha nguo ya Ipanga ya ndani kikawa kimeletwa. Akawauliza tena, “Huyu kijana wamekwisha mpiga chapa yetu ya kichawi kwenye paji lake la uso ili kila mwenzetu atakayemwona ajue siku yoyote atahitajika kuzimu?” Mwenyekiti akajibu, “Ndiyo mkuru Mgatu, lakini kila tukimpiga chapa

haikamati inafutika." Akaendelea kumchunguza Ipanga kwa darubini ya kichawi aliyokuja nayo. Baada ya dakika moja akawajibu, "mtahangaika na kijana huyu. Anasali na kuomba sana hivyo atakayepambana nae ataanguka. Na kila anaposali (swali) na kuomba hivyo, kuna nguvu nyingine za ziada zinakuja ingawa hizi nguvu sio za Mungu wake wala malaika wake, sijui zinatoka wapi kwani kila nikijaribu kuzifuatilia nakutana na moto mkali sana ambao unaweza kunidhuru. Hivyo nawashauri endeleeni kumchafua tu lakini hayo mambo mengine yaacheni kabisa kwani mtapoteza gharama kubwa sana na bado hamtafanikiwa. Naona hapa kuna kombora kubwa sana linaelea tumboni mwake ambalo mmetumia vichembe vingi sana kulipata na sifa ya hili kombora kwa binadamu wa kawaida miezi kumi na mbili ni mingi ilitakiwa awe amekwishakufa, lakini naliona hadi limeshaota ukungu inamaanisha lina miaka mingi sana ila halijazaa matunda yeyote yale. Nadhani mmenielewa."

Wajumbe wote wakakubali kwa ishara yao ya kichawi kuwa wamemwelewa. Akawaambia tena, "Naona mna mpango wa kumchafua kwenye jamii yake. Naweza kuwasaidia?" Wote kwa pamoja

wakakubali tena kwa ishara yao ya kichawi. Akawaomba jina la kijana anayetolewa sadaka na mama yake kuzimu wakamtaja pamoja na baadhi ya vitu kutoka kwenye mwili wa huyo kijana vilivyofungwa pamoja kwenye kitambaa. Walipo mpatia akatulia ndani ya dakika tatu huku akiomba miungu yake. Alipomaliza aliwaeleza kuwa kazi imekamilika na watapata majibu ndani ya siku tatu. Lakini hali hiyo ya ugonjwa kwa huyo kijana itakapoanza kujitokeza tu, waanze kusema chanzo ni huyo Ipanga.

Baada ya mazungumzo hayo aliwaaga kisha akaenda zake. Mwenyekiti na wajumbe wenzake wakapeana ishara ya kuwa sasa wako pamoja na kuanza kushughulika kumchafua Ipanga katika jamii. Siku moja jioni Ipanga akiwa amekaa chumbani mwake akiwaza mambo ya hapa na pale, alisikia mlango wake ukikongwa. Alinyanyuka na kufungua akakuta kijana anayemfundisha ndiye anagonga. Kijana akamwamkia, “Shikamoo kaka!” Ipanga akajibu, “Marhaba, karibu ndani.” Kijana akaitikia, “Ahsante, nimeleta hivi vitabu uwe unavitazama,nitakuja usiku nikimaliza kula.” Ipanga akasema, “Sawa, ngoja niwe ninavitazama.”

Ipanga alivichukua hivyo vitabu kisha akarudi ndani kuketi huku akiwa anasikiliza radio kupitia simu yake ya mkononi. Kijana alipomaliza kula alikuja hadi ndani kwa Ipanga kufundishwa na kujisomea kama kawaida yake. Alipoingia ndani tu, Ipanga nae akakumbuka hajakwenda kula chakula cha usiku, akamwambia kijana, "Ngoja nami nikale kwani nimejisahau sana leo na muda umekwenda sana." Kijana akasema, "Sawa kaka,nitakuwa nikijisomea huku ninakusubiri. Tena kuna maswali ya fizikia yamenishinda, utanisaidia pia." Ipanga akasema, "Hakuna shaka, sitachelewa." Ipanga alinyanyuka, akaiweka simu yake kwenye umeme ili ipate moto, kisha akaondoka. Kipindi anakula, alikumbuka kuna mfanyakazi mwenzake alihitaji kumwuliza kitu kinachohusu masuala ya kazi ili akiandae usiku huo. Baada ya kumaliza kula, alipita dukani kununua vocha kisha akaelekea nyumbani.

Alipofika chumbani mwake hakumkuta kijana. Alitazama sehemu alipoweka simu ili aiwashe aweke vocha azungumze na mfanyakazi mwenzake, hakuiona simu badala yake kulikuwa na chaja tu. Alitulia akidhani ni kijana ndiye aliyoichukua kwani kuna wakati huwa anamwomba kuwasiliana na wanafunzi wenzake.

Baada ya muda mfupi kijana akaingia ndani, Ipanga akamwuliza kuhusu simu. Kijana akasema, “Kaka, nina dakika chache tu nimeingia uwani kujisaidia haja ndogo, tangu ulipoondoka simu ilikuwa hapo. Nilipokwenda uwani nimeiacha hapo hapo na hata mlango niliubana.” Ipanga akasema, “Kweli nimekuta mlango umebanwa. Sasa simu imeenda wapi? Na huo mda mchache tu umetoka, nani kaingia humu ndani? Maana hatuna mazoea ya watu kuingia ndani mara kwa mara.”

Wakati huo wote wakishangaa na kusikitika, kijana alikuwa akipekua chumba kizima akitafuta simu. Ipanga alitoka nje na kuwauliza baadhi ya wapangaji kama kuna mtu wamemwona hapo nyumbani ambaye siyo mwenyeji wa hapo. Wapangaji wote wakasema hakuna mtu waliyemwona. Muda kidogo tu Kuchi alifika huku akijifanya kushangaa na kumwita Ipanga, “Ipanga mwanangu, usihangaike kabisa, mwizi wako ni huyo kijana unayelala nae humo ndani. Tena ameiba na kumpa rafiki yake yule anaeishi nyumba ya nne ili waiuze. Hata mimi nilishangaa kwa nini leo huyo rafiki yake amekuja mara kwa mara hapa nyumbani! Kumbe ndio ulikuwa mpango wao huo. Tena ungemfuata muda huu kabla hawajakwenda

kuiuza.” Ipanga ambaye alionesha kuhamaki, alimfuata kijana ndani aliyekuwa akihangaika bado kutafuta simu huku na kule bila mafanikio na kumwuliza, “Gosha, rafiki yako amekuja muda gani leo huku?” Kijana akajibu leo ni siku ya pili kaka sijaonana na rafiki yangu.” Ipanga akauliza, “lakini tunaweza mpata kwao?” Kijana akajibu, “Ndiyo nadhani atakuwepo tu.”

Ipanga na Gosha wakatoka nje kisha wakamwomba mtoto wa jirani akamwite Nungu. Nungu alikuja kisha Ipanga akamwambia, “Ninaomba simu uliyoichukua humo ndani muda si mrefu.” Nungu alipigwa na bumbuwazi kuambiwa hivyo na Ipanga. Alimweleza kuwa hajui chochote kuhusu simu na hapo nyumbani ana siku ya pili hajafika. Hali hiyo iliendelea kumchanganya Ipanga ambaye baada ya muda alimruhusu Nungu kuondoka. Aliondoka lakini aliwaza na kujisikia vibaya sana Ipanga kumwita yeye mwizi. Baadaye watu wote waliingia ndani kulala, Ipanga na Gosha pia waliingia ndani ingawa kijana alipofika ndani hakukaa, aliendelea kutafuta simu huku na kule hata hivyo Ipanga alimzuia akisema, “Hapana, usisumbuke hivyo. Simu imekwisha potea na kama itakuwemo humu ndani

tutaipata tu." Kijana akakubali kwa kusema, "Sawa kaka." Kijana aliacha kisha wakalala kwani muda huo ilikuwa inaelekea saa sita usiku. Kesho yake alfajiri kijana akaamka akiwa mnyonge sana akamsalimia Ipanga kisha akamuaga aende kujiandaa kwa ajili ya shule kama ambavyo huwa anafanya. Ipanga nae alimsalimia na kumtakia masomo mema kisha naye akaamka na kuanza kujiandaa ili aende kazini.

Jioni aliporudi kutoka kazini kwake akakutana na Gufa wakasalimiana kisha akamweleza "Mwanangu Ipanga, aliyeiba simu yako ni Gosha ili akaiuze. Leo hii huyo Nungu amempelekea hiyo simu mama Pezi, yule wa mtaa wa tatu kwenye nyumba yenye miti ya machungwa ili ainunue. Sijajua kama mama Pezi aliinunua ama hakuinuua. Lakini ujue hivyo kuwa mwizi wako ni huyo Gosha na kampatia Nungu ili amsaidie kuiuza." Ipanga akasema, "Sawa sengi, nimekuelewa." Waliachana, Ipanga akaelekea moja kwa moja hadi chumbani mwake na kumkuta kijana amevuruga vitu ndani mpaka amechoka, kujilaza kitandani akiwa tayari amepitiwa na usingizi. Alimwamsha, kijana akashtuka na kuamka kisha akamsalimia Ipanga.

Walipomaliza kusalimiana, Ipanga akamwuliza, “Una tatizo gani mbona huna raha?” Kijana akajibu, “Nafikiria simu yako tu kaka.” Ipanga akasema, “Tangu jana nilikwambia kuwa hiyo tayari imekwisha potea, na kama imo humu ndani tutaipata tu. Naomba uwe na amani pia kwani vitu hivi ni vya kupita.” Baada ya kijana kuelezwa hivyo na Ipanga akapata amani kidogo moyoni mwake. Ipanga aliendelea kuwaza kuhusu mazingira ya upotevu wa simu yake. Hakuwa na wazo kabisa kuwa simu yake imeibiwa na kijana anayeishi nae humo ndani kwani kwa muda aliokaa nae alikuwa anamjua vizuri tabia yake. Hofu yake kubwa ilikuwa kwa yule rafiki yake kuwa huenda yeye ndiye alikuja akaingia humo ndani na kuchukua simu kwani ni mara chache sana hupenda kuingia humo ndani. Ilibidi aende kwa mama Pezi akamwulize kama hiyo simu ameiona kwani wanafahamiana.

Alipofika kwa mama Pezi, alimkuta kaketi nje anamnyonyesha mtoto wake. Ipanga akamwamkia, “Shikamoo mama Pezi!” Mama Pezi akitikia, “Marhaba Ipanga, leo umeonekana huku, mvua itanyesha.” Ipanga akasema, “Hapana, mambo ndio mengi tu.” Mama Pezi akasema, “Sawa Ipanga,

karibu tupo." Ipanga akaitikia, "Ahsante sana. Mama Pezi, ninatafuta simu ya kununua ya bei ndogo. Niliambiwa kuna kijana alikuwa anauza simu amekuletea wewe uione sasa kama hukuinunua, nataka niinunue." Mama pezi akamjibu, "Mdogo wangu Ipanga, mimi nina simu yangu tena bado mpya, hii hapa. Huyo kijana uliyeambiwa kanilitea mimi simu ninunue sijamwona na wala simfahamu. Tena kizuri zaidi, leo nimeshinda hapa nyumbani wala sijatoka. Huyo aliyekupatia hizo taarifa kakuongopea." Ipanga akasema, "Nimeambiwa umeletewa simu hiyo na rafiki yake Gosha anayeitwa Nungu." Mama Pezi akamwambia Ipanga, "Huyo kijana ninamfahamu ila nina kama mwezi mmoja hivi sijamwona.

Baada ya Ipanga kupewa maelezo hayo ikabidi waanze kuzungumza hoja zingine tu. Muda ulipokwenda sana Ipanga akaaga na kuondoka. Kwa vile muda wa kula ulikuwa unakaribia ilibidi aende moja kwa moja gengeni ambapo huwa anakula chakula. Akiwa njiani kuelekea kwenye chakula, aliwaza mambo mengi juu ya mazingira ya kupotea kwa hiyo simu bila majibu. Akawaza taarifa aliyopewa na Gufa isivyokuwa ya kweli kwani mhusika amekataa na asingeweza kuficha

chochote kwani wanaheshimiana sana. Baada ya kuwaza hivyo aliamua jambo moja tu kuwa simu imepotea, kinachotakiwa arudishe laini yake na anunue simu nyingine kwani aliona anajiumiza kichwa bure tu.

Alipomaliza kula alirejea nyumbani na kwenda moja kwa moja chumbani kwake. Alipoingia ndani alimkuta kijana kajiinamia huku analia. Ipanga alishtuka sana na kumwuliza, “Mbona unalia, kuna nini?” Kijana, kwa huzuri sana akajibu, “Sengi anasema kwa watu kuwa mimi ndiye niliyeiba simu yako.” Ipanga akamwuliza, “Simu iliyoibwa ni ya kwangu ama ya kwao?” Kijana akajibu, “Ni ya kwako.” Ipanga akamwambia, “Sasa nakuomba, usiwaze wala kusikiliza maneno yao kabisa. Nimekueleza kuwa tuachane na mambo ya simu kwani imekwishapotea na kama ipo tutaipata tu. Unanielewa vizuri?” Kijana akajibu, “Ndiyo kaka, nakuelewa.” Baada ya hayo maneno ya Ipanga, kijana akatulia na akapata nafuu sana moyoni mwake kwani alidhani mtazamo walio nao hao wanaomweleza ndiyo mtazamo alionao Ipanga. Kuanzia siku hiyo usiku, Ipanga akaendelea kumfundisha kama kawaida.

Baada ya wiki moja, Ipanga alitoka kazini na kuambiwa kuwa kijana alikuwepo hapo nyumbani ila katoka muda sio mrefu lakini cha kushangaza, anaongea maneno ambayo hayaelewiki. Ipanga alishangaa sana kusikia maelezo hayo. Akajiuliza mwenyewe akilini mwake, "Usiku kipindi namfundisha mbona alikuwa sawa tu, hadi nilimpatia maswali akayafanya na nilipoyasahihisha aliyapata yote!. Leo pia asubuhi nimeondoka nikamwacha ndani nae akijiandaa ili aondoke akisema kuwa kachelewa kwa kuwa alitakiwa kufika shuleni saa tatu. Hivyo hakuwa na ratiba ya kuwahi mapema kama siku zote anavyowahi. Sasa hii ya kuongea maneno ambayo hayaelewiki imetoka wapi!" Ipanga aliendelea kujihoji bila kupata majibu. Kila mmoja wao hapo alikuwa amehamaki kutokana na hali ya kijana huyo kisha akawauliza mahali kijana alipo. Mmoja wa wapangaji akamjibu kuwa amekodi teksi na kwamba anaelekea kwenda kutangaza kwenye redio. Hiyo hali ikazidi kumchanganya Ipanga. Huku akiwaza, akasikia tena kijana mmoja anasema kuwa yupo hapo kwao anaendelea kuongea ovyo ovyo. Ipanga na baadhi wa wapangaji wakaelekea hapo kwao na kumkuta Gosha akiongea mambo mengi sana ikiwemo kujitangaza kuwa anataka

kwenda bungeni muda huo sababu kesho yake asubuhi atapewa nafasi na spika wa bunge azungumze juu ya matatizo ya wananchi wa huo mtaa anapoishi. Baada ya kusikia maneno hayo, Ipanga alijisikia vibaya sana na kuamini kuwa ni kweli anaumwa.

Wakashaurina hapo wakiwemo wazazi wa kijana huyo kuwa wamkamate kisha wampeleke hospitali. Walimkamata kisha wakamkimbiza hospitali. Walipofika hospitalini, aliongea maneno mengi sana mengine ya kufurahisha na kuchekesha hadi mwuguzi akashindwa kutambua ni nani mgonjwa miongoni mwao. Mwuguzi alipouliza ni nani mgonjwa, kijana akamtaja dereva teksi kuwa ndiye anayeumwa tumbo kwa sababu huyo dereva taksi alikuwa na kiribatumbo. Baaada ya kijana kujibu hivyo, wote walicheka na kumweleza mwuguzi kuwa huyo huyo kijana ndiye anayeumwa. Kijana aliendelea kusisitiza mwuguzi awatazame wote hapo vizuri atabaini kuwa mgonjwa ni huyo huyo dereva teksi. Mwuguzi akamweleza kuwa sawa amekwishamgundua ila anaomba ampime yeye kwanza kisha ndipo ampime na huyo dereva teksi. Kijana alichukuliwa vipimo kisha akapelekwa wodini na kuchomwa

sindano ya usingizi kwani alianza kuwabishia kwa kila alichokuwa akielekezwa. Baada ya kuchomwa sindano hiyo alisinzia na matibabu mengine yakaendelea. Baada ya muda waliambiwa waondoke na abaki baba yake tu kwa ajili ya kumuuguza usiku huo. Ipanga na baadhi ya wapangaji wa kwao pamoja na ndugu wa kijana waliondoka kurejea nyumbani huku kila mmoja akijadili juu ya kuugua kwa kijana huyo.

Kesho yake asubuhi Ipanga alikwenda kazini ila akiwa kazini akampigia simu baba yake huyo kijana kumjulia hali kwa kutumia simu nyingine aliyoinunua siku tatu zilizopita baada ya kuibiwa ile ya mwanzo. Baba yake akamjibu kuwa hali yake bado kwani hakuna mabadiliko yoyote toka jana yake. Ipanga akamwambia atakwenda jioni kumwona akitoka kazini kwake. Ilipofika muda wa saa kumi, Ipanga akaomba ruhusa kazini kwake ili awahi hospitali akamsalimie kijana. Kazini kwake walimruhusu akaelekea hospitali. Alipofika hospitalini alimkuta kijana amefungwa kamba miguu na mikono huku akilalamika afunguliwe kamba na kwamba anataka kuondoka kwenda kuishi mbali kwani mtaa huo anaoishi kuna wachawi. Ile hali ya kufungwa kamba ilimfanya

Ipanga kudondokwa na machozi ambayo aliyafuta haraka sana kwa kitambaa chake cha mkononi na hakuna aliyegundua miongoni mwao wote waliokuwepo pale.

Kijana yule alipomwona Ipanga akamweleza "Kaka, naomba unitoe humu unipeleke nikaishi uzunguni kwani mtaa huu una wachawi wengi sana. Hata wewe kaka nakuomba utoke kwenye mtaa huu, si salama kwako kutokana na wachawi hao. Tena wachawi wakubwa ni shaaa…..!" Alipotaka kuwataja akapaliwa na mate, akaanza kukohoa na baada ya dakika chache akatulia na kuanza kuzungumzia habari ya kwenda bungeni. Baada ya muda mfupi tena, kijana akaanza kujishika kooni kama vile kuna kitu kinambana. Akasema, "Jamani simu inanibana! Waiteni madaktari wanitolee hii simu inayonibana kooni!" Wote waliokuwapo hawakushangaa sana kwa kujua ni maneno anayoropoka tu kama anavyoropoka. Ipanga alipokuwa anaambiwa hayo mambo ya uchawi mara simu inamkaba kooni hayakumwingia akilini. Kwanza hakujua vizuri maana ya uchawi ila kilichokuwa kinamhuzunisha ni kijana kufungwa kamba wakati ni mtu aliyekuwa nae mara kwa mara usiku akimfundisha

na yuko vizuri tu mwenye akili zake nzuri. Ipanga aliendelea kupigwa bumbuwazi hadi muda wa kuona wagonjwa ukaisha na kutakiwa kurudi nyumbani. Aliongozana tena na watu wengine waliokuja kumsalimia kijana. Alipofika nyumbani, mpangaji mmoja akamwita, “Ipanga, njoo, nina shida na wewe.” Ipanga akaenda kumwona mpangaji huyo kisha mpangaji akamwuliza Ipanga, “Una habari gani yoyote inayokuhusu?” Ipanga akajibu, “Hapana, sina habari yoyote.” Mpangaji akamwambia, “Sasa ni hivi, kila mgeni anayekuja hapa nikiwemo mimi mwenyewe anaambiwa na Kuchi kuwa Ipanga aliapa, atakayeiba simu yake ataona. Sasa kijana ameona sababu ya kuiba simu yako.” Baada ya kuambiwa hivyo, Ipanga alihisi kuishiwa pumzi na mwili wake wote kama umemwagiwa maji ya barafu. Alikaa kwenye ngazi kwa dakika kadhaa hivi kisha mpangaji akaendelea “Amekwishawaambia watu wengi, kawaulize hata watoto wa hapo jirani watakwambia. Pia hata kama ukienda kumwuliza mwenyewe nipo radhi kuja kulithibitisha hili mbele yake.”

Ipanga alinyanyuka taratibu akamshukuru mpangaji kwa taarifa kisha akatembea kuelekea nyumba ya jirani. Aliwakuta watoto wa jirani

wakicheza. Alimfuata mtoto mkubwa kuliko wote, akamwuliza iwapo leo bibi yake alimuagiza sehemu yoyote kwa maana hupenda kumuagiza dukani. Mtoto akajibu, “Ndiyo, alikuwa na wageni akaniagiza skonzi.” Ipanga akamwuliza, “Kipindi anaongea na wageni, ulisikia amenitaja mimi?” Mtoto akajibu, “Ndiyo, alisema wewe una roho ya uuaji. Umemfanya hivyo kijana wa watu kwa sababu tu amekuibia simu.” Ipanga akamshukuru, “Ahsante kwa kunieleza.” Ipanga alitoka akaelekea chumbani mwake na kuanza kulia wakati huo kila kiungo cha mwili wake kikionesha hakina ushirikiano na kingine.

Ulipofika muda wa kwenda kula chakula cha usiku hakwenda, kwa sababu kwanza hakuwa anahisi njaa na pili hakuwa na nguvu za kufika huko. Alianza kukumbuka vizuri kuwa hospitalini, kijana alilalamika kuwa simu inamkaba kooni na huku Kuchi anasema yeye ndiye kamfaya hivyo kijana kutokana na kumwibia simu yake. Na kibaya zaidi anawaambia watu mbalimbali wakiwemo wageni wanaokuja hapo nyumbani kutoka sehemu mbalimbali. Alijiuliza pia, “Watu watanionaje na kunichukuliaje mimi kuanzia hapa nyumbani na nitakapo pita!” Mwisho aliamua akamwulize Kuchi

kwa nini anamsema hivyo kwa watu. Alinyanyuka akiwa amejawa na hasira hadi kwa huyo Kuchi aliyekuwa ameketi sebuleni na kumwambia, “Sengi kwa nini unawaambia watu kuwa mimi ndiye nimemfanya hivyo kijana wa watu ukidai kuwa ni kwa sababu ameiba simu yangu? Nimewahi kuja kwako kukueleza kuwa yeye ndiye aliyeiba simu yangu?” Kuchi,akamjibu kwa mshangao “Tobaa! Wewe Ipanga, toka lini mimi nikasema maneno hayo? Mh! Jamani. Hapana kabisa, mimi sitaki kuyasikia maneno hayo, kabisa. Unataka kunikosanisha na wazazi wako. Mimi siko tayari kabisa kukosana na wazazi wako.” Ipanga akamwambia, “Ngoja nikawaite waliokusikia ukiyaongea.” Kuchi akasema kwa mshtuko, “Hapana! Hapana kabisa, mimi sitaki maneno.” Mwisho Kuchi akajifanya kuangua kilio. Ipanga akaamua kuondoka kurudi chumbani kwake huku akimwacha akijiliza.

Baada ya muda Ipanga alipanda kitandani kulala lakini usiku kucha hakupata usingizi akiwaza hali iliyomtokea. Kulipokucha akajiandaa na kuelekea kazini kwake huku akiwaza ni nani wa kumshirikisha suala hilo linalomtesa akilini mwake japo apewe ushauri tu. Alifika kazini na kuanza

shughuli zake huku akiwaza kuwa labda kila aliyekutana nae njiani anayemfahamu tayari amekwisha ambiwa kuwa yeye ndiye aliyesababisha kijana kuugua kisa simu. Muda ulipokaribia wa kutoka kazini akaanza kuwaza kuwa apite hospitalini akamwone kijana ama aende moja kwa moja nyumbani. Akawaza tena, "Labda hata wazazi wa kijana wamekwishapewa habari hizi ili wanichukie au wanipige ama wanikamate na kunipeleka polisi. Pia, labda nikienda nyumbani pasipo hospitalini watasema ni kweli na ndio maana sikwenda kumwona!"

Maswali hayo yasiyo na majibu yalimchanganya sana Ipanga. Kuna mfanyakazi mwenzake mtu mzima alimwona Ipanga kama vile hayuko sawa kwani hata kipindi wapo pamoja mezani wanakula aliona hata ulaji wake sio wa kawaida kama vile ni mtu mwenye mawazo sana. Alijaribu kumwuliza Ipanga iwapo ana tatizo lolote. Ipanga akamwambia, hakuwa na tatizo kabisa. Lakini, baada ya muda mfupi, Ipanga akaamua kumshirikisha huyo mfanyakazi mwenzake kwani alikosa kabisa mwafaka moyoni mwake kuwa apite hospitalini ama asipite. Ilibidi amwelezee hali halisi kuanzia kuibiwa simu hadi kufikia ugonjwa wa

kijana na maneno yanayosemwa, tena na ndugu zake wa damu. Kwanza mfanyakazi mwenzake alimpa pole na pili akakiri kweli yupo kwenye wakati mgumu. Alimshauri apite akamwone mgonjwa na pia akamwambia kuwa atamsindikiza hadi hospitali ili kama kuna chochote kitatokea amsaidie. Ipanga alishukuru sana na akajihisi moyo wake umepata ahueni.

Baada ya saa za kazi kwisha, Ipanga na mfanyakazi mwenzake waliongozana hadi hosipitalini kwa mgonjwa. Waliwakuta watu wengi wamekuja kumwona mgonjwa wakiwemo ndugu wa mgonjwa, wapangaji wa hapo nyumbani kwa baba yake pamoja na wanafunzi wenzake. Walipofika walimkuta mgonjwa akiongea vilevile huku akilalamika anakabwa kooni na simu iliyogota kwenye koo. Baada ya kusikia maelezo hayo kutoka kwa mgonjwa mfanyakazi mwenzake na Ipanga alizidi kubaini kuwa ni kweli Ipanga yupo kwenye wakati mgumu na wa hatari sana. Alimwomba Ipanga amwoneshe baba wa huyo mgonjwa naye Ipanga akamuonesha. Baada ya muda alimsogelea baba yake kijana huyo wakasalimiana, kisha akamwambia, “Samahani, mimi ni mfanyakazi mwenzake na Ipanga. Poleni

kwa kuuguza." Baba yake kijana yule akasema, "Ahsante sana. Tupo tu, hali ndio bado iko kama unavyomwona."

Mfanyakazi mwenzake Ipanga akauliza, "Nini zaidi kilimtokea na mbona analalamika sana kuwa simu inamkaba kooni?" Baba yake kijana yule akajibu, "Daktari wake anasema malaria imepanda kichwani, ndio maana anaongea maneno tofauti tofauti. Kwa mfano simu imegota kooni,inamkaba, mara kuna mtu anamkaba kooni, mara anakabwa na kitu kingine tu!" Mfanyakazi mwenzake Ipanga akasema, "Poleni sana. Mungu atamsaidia tu atapona. Ipanga alinifahamisha kuwa kuna kijana huwa anasaidia kumfundisha anaumwa, amelazwa, nikamwambia nitamsindikiza kuja kumjulia hali." Baba wa kijana akasema, "Tunashukuru sana. Tupo na Ipanga pamoja, kweli amekuwa akimsaidia kijana na kupandisha ufaulu wake shuleni vizuri tu. Pia amesaidia sana kwani mwanangu alipoanza kuugua alikodi teksi ambayo alizunguka nayo siku nzima lakini Ipanga alilipia gharama ya teksi na baadhi ya gharama hapa hospitalini. Hivyo hatuwezi kumsema vibaya kijana wa watu."

Mfanyakazi mwenzake Ipanga akasema, “Ni vizuri kama anasaidia hivyo na kila mmoja wetu hapo kazini amekuwa akimwuliza mara kwa mara kinachomsibu kutokana na huzuni aliyo nayo kwa sasa. Kibaya zaidi, nasikia aliibiwa simu ila mgonjwa anadai simu inamkaba kooni. Hicho ndicho kinazidi kumpa huzuni zaidi, hata hali chakula vizuri.” Baba wa kijana akashtuka kidogo, “Kumbe!, hebu mwite tuzungumze nae kidogo.” Ipanga aliitwa wakasogea pembeni kisha wakaanza kuzungumza. Baba wa kijana akaanza kwa kusema, “Ipanga, ondoa hofu kabisa juu ya kijana kutamka maneno mengi ikiwemo kukabwa na simu kooni. Hataji simu tu, bali hutaja vitu vingi vinavyomkaba koo. Kwa hiyo ondoa hofu kabisa kijana wangu na ninaomba uwe na amani. Unanielewa vizuri lakini?” Ipanga akajibu, “Ndiyo baba Gosha, nimekuelewa.”

Baada ya mazungumzo hayo walirudi kwa mgonjwa ambaye tayari alikwisha anza kupata vidonda miguuni na mikononi kutokana na kufungwa kamba. Ipanga alimhurumia sana kijana, hata hivyo hakuwa na chochote cha kufanya kuweza kumwokoa. Baada ya muda waliaga na kuondoka. Wakiwa njiani, Ipanga alimshukuru

sana mfanyakazi mwenzake kwa kumsaidia, nae akaendelea kumsihi atulie kabisa na asisikilize maneno yoyote yatakayokuwa yakisemwa juu yake. Pia akamsihi kwamba chochote kile atakachoona kinamtatiza, asisite kumfahamisha hata kwa simu kwani yuko pamoja naye. Walizungumza mambo mengi kisha wakaachana, kila mmoja akaelekea kwake.

Siku hiyo usiku ulipowadia, mwenyekiti aliitisha kikao cha kichawi kama kawaida yao, kukutana kila siku. Siku hiyo wakapongezana kidogo kwa hatua kubwa waliyoifikia ya kumleta kijana Gosha kuzimu na kuendelea kumchafua Ipanga. Mwenyekiti akamsihi mtoa sadaka hiyo ya kijana kuja kuzimu ambaye ni mama yake mzazi kijana kuwa, “hakikisha unaendelea kumbana huyo mumeo na ndugu zake wote wanaokuja ili wasisali na kuomba kwa imani ya Mungu wao aliye juu. Wataharibu kila kitu, kwa maana hayo makombora yamekwishaiva, yakikutana na hiyo nguvu yataturudia sisi na yakiturudia tu, kujitibisha ni gharama ya ng’ombe ishirini kila mmoja ama kifo. Ni vizuri inapotokea hali hiyo ya kutaka kusali na kumwombea kijana, hakikisha watu wenye imani haba ama wajumbe wenzetu huku kuzimu ndiyo

wawe wanamwombea. Nasisitiza tena, lifanyie kazi hili suala kwa umakini sana kama nilivyokuelekeza. Hata kama wakimtoa hospitali ili akatibiwe kienyeji, hakikisha unalazimisha apelekwe kwa mganga ambaye ni mwanachama wetu huku kuzimu na kama siyo mwanachama wetu, hakikisha anapelekwa kwa mganga ambaye tunaweza kumhonga pesa ama vitu vya thamani akamwachilia tukamchukua kichawi. Nadhani umenielewa vizuri." Mama wa Gosha akasema, "Ndiyo mkuru. Kwanza nikutoe hofu tu kuwa mume wangu nilikwishammaliza kiufahamu siku nyingi. Huwa ninafanya nitakavyo na kumpeleka vyovyote vile ninavyoamua. Ndiyo maana vikao vyote muhimu vya huku kuzimu huwa ninamtumia kama kiti changu. Nilimwachia ufahamu wa kuvaa nguo ili asivae amegeuza pamoja na ufahamu wa kusalimiana na watu. Hivyo kuhusu huyo, usihofu kabisa mkuru. Nimekwishatengeneza mazingira kichawi, hivyo hoja zote ninazipanga na kuziamua mimi ila mume wangu ni msemaji kwa kile nitakachomweleza. Angekuwa nae anajifanya mgumu, mbona kitambo tu angekuwa amekwishakuja huku kuzimu." Mwenyekiti akampongeza kwa kusema, "Safi sana na hongera kwani tunaona unavyopambana.

Tuandaeni mazingira ya sherehe kwani sadaka yako siku chache tu itatufikia huku kuzimu." Wote kwa pamoja wakafurahi kusikia kauli hiyo ya mwenyekiti wao.

Mwenyekiti akaendelea, "Mkumbuke sheria zote kuwa hatutamchukua moja kwa moja. Wale waandaaji mazingira, mmekwishaandaa mazingira ya kumhifadhia ili wanapokwenda makabulini kuzika nasi iwe vyepesi kumchukua bila bughudha yoyote ile?" Mwakilishi wa waandaaji akajibu, "Ndiyo mkuru, kila kitu kipo tayari. Tutamhifadhi nyuma ya mlango wa sebuleni kwao." Mwenyekiti akasema, "Sawa, hiyo inahitaji umakini wa hali ya juu sana kwa sababu akitokea mjuaji yeyote ama mtu wa Mungu wao wa kweli tutaanza kunyang'anyana. Hapo mnajua huwa kuna vita kali sana. Kitu kingine kabla sijasahau, atakayewekwa kwenye kitanda hapo hospitalini kabla ya kumchukua huyo kijana ni yule msukule mzee kama tulivyo kuwa tumepanga awali ama mmekwisha badilisha?" Mjumbe mmoja akajibu, "Mkuru, tuwawekee huyo huyo msukule mzee ndiye washugulike naye hapo hospitalini kwa siku chache kabla hatujamwua kwani hawezi kazi yoyote ile kwa sasa na hahitajiki kabisa."

Mwenyekiti akasema, “Sawa, nilitaka kusahau, hivyo unamaanisha kijana tumchukulie hapo hapo hosptalini?” Nilikuwa ninawaza tumtoroshe hadi pembeni ya mji kisha tumning’inize aonekane amejinyonga kwa kutumia kamba za magome ya miti?” Mjumbe mwingine akasema, “Mkuru hapo hapo hospitalini tu. Tumpeleka huko tutakuwa tunaingiza gharama ambazo hazina msingi wowote.” Mwenyekiti akaagiza, “Kazi hii tuifanye alfajiri na mapema kama ambavyo huwa tunafanya tukishirikiana na wenzetu ambao ni wauguzi hapo hospitalini. Alfajiri hiyo tumchukue kijana na tumwue huyo msukule tuwaachie wahangaike nae hadi kumzika.”

Mwenyekiti akaendelea, “Sawa nimekuelewa. Mjumbe mtoa sadaka nakuagiza, hakikisha anazikwa hapa hapa kwani mipango yote tumekwisha ikamikilisha. Akienda kuzikwa kwingine mipango yote itaharibika na itabidi tupange tena upya na kupanga kwa dharura kuna kufanikiwa ama kushindwa kwani hatujui huko tuendako watu watakuwa na nguvu kiasi gani ya imani kwa Mungu wao.” Mama kijana akasema, “Sawa mkuru, hilo halina shaka kabisa.” Mwenyekiti akamaliza huku akicheka, “Sasa Ipanga

anaendelea kukipata cha mtema kuni, watu wengi tayari wanajua simu ndiyo inayomtesa kijana. Hongereni kwa kumchafua na pia tuendelee hivyo hivyo hata kwenye msiba wa kijana. Tena nitaongeza utaalamu mpya zaidi, yaani ile siku tunajiandaa kwenda makaburini kuzika. Mzee tuliowapa akitolewa tu nje akiwa ndani ya jeneza, naamini umati wote watakuwa karibu kulitazama hilo jeneza wakiamini ni kijana aliyelala ndani ya jeneza huku wapo kimya. Nitakachokifanya hapo, nitaachilia mlio wa kuitia wa simu yake iliyoibiwa. Ili kila mmoja aliyeko pale asikie, na baada ya dakika chache tu, nitaachilia tena mlio wa ujumbe mfupi uliokuwa kwenye hiyo hiyo simu iliyoibiwa. Milio yote hiyo nitaiachilia ikitokea pale pale kwenye jeneza. Hapo ndipo tutammaliza kabisa Ipanga kwani atapatwa na msongo wa mawazo kwa kufikiria hilo tukio bila majibu." Baada ya maneno hayo wenzake walifurahi sana na kisha mwenyekiti akawaruhusu kila mmoja kuendelea na majukumu yake. Wakati huo wote Ipanga na mama yake waliendelea kuwa wanasali na kuomba kwa Mungu wao aliye juu mbinguni.

Baada ya wiki mbili Ipanga akiwa kazini kwake muda wa mchana, alipata ujumbe mfupi kwenye simu yake ukitokea kwa mpangaji wao.

Alipofungua na kusoma akakuta ni taarifa kuwa kijana amefariki muda sio mrefu. Ipanga aliishiwa nguvu, alitembea taratibu hadi kwa yule mfanyakazi mwenzake mtu mzima kidogo akamfahamisha. Ulipofika muda wa kutoka kazini, Ipanga aliongozana na huyo mfanyakazi mwenzake hadi msibani. Watu walianza kupeana taarifa na ilipofika jioni, kukawa na watu wengi wakiwemo ndugu jamaa na marafiki wa wazazi wake marehemu. Wengi wao walipokuwa wakija walikuwa wakijadili kilichomwua kijana ni simu ndiyo ilikuwa imegota kooni mara kwa mara. Mfanyakazi mwenzake Ipanga akaendelea kumsihi Ipanga aendelee kuwa mtulivu kwamba ni muda tu anaupitia nao utaisha. Kesho yake jioni kikao cha kuratibu taratibu za mazishi kilifanyika kikishirikisha ndugu wa baba yake marehemu pamoja na baba wa marehemu, ndugu jamaa na marafiki wa familia hiyo. Waliazimia kuwa kijana anatakiwa akazikwe kijijini upande wa baba. Wakamweleza baba wa marehemu ili amfikishie ujumbe wa hayo maazimio ya kikao mkewe. Baba wa marehemu alimwita mkewe na kumpa taarifa hiyo kuwa wana shamba kijijini kwao walilolitenga kwa ajili ya makaburi, hivyo kikao kimeazimia kijana akazikwe huko shambani.

Mama wa marehemu alipoambiwa habari hizo, akakataa na kusema kijana wao lazima azikwe hapo mjini na akamfahamisha akawataarifu ndugu zake hilo na hakuna mjadala. Pia akamwambia kwa nini ameshirikishwa kwenye kikao hicho bila ya kumtaarifu ili ampe msimamo wake. Mumewe akamwomba msamaha kisha akarudi kwa ndugu zake pamoja na marafiki wa karibu wa familia hiyo kuwajulisha kuwa, yeye na mkewe hawaafiki kijana wao kwenda kuzikwa kijijini. Atazikwa hapo hapo mjini. Waliendelea na mvutano huo hadi usiku wa manane. Mwisho wake mama wa marehemu aliingilia kikao akawafahamisha ndugu wa mume wake kuwa kama watakwenda kuzika kijijini, waende wakazike wao ila yeye hatakwenda. Mume wake naye baada ya kusikia hiyo kauli ya mkewe, akawaambia ndugu zake kuwa kama mke wake hatakwenda naye pia hatakwenda hivyo wataenda kuzika wao pekee yao. Ndugu wa mwanaume wakaitana tena kujadili ila wakafikia mwafaka kuwa wakubaliane nao kama wahusika wamekataa. Lakini pia wakatoa msimamo wao kuwa, wakimaliza kuzika wataondoka.

Kesho yake asubuhi wakaandaa utaratibu wa mazishi na ilipotimu saa sita mchana mwili wa marehemu ukaletwa kutoka hospitalini. Walifanya

taratibu zote za kiimani za dini yao na ilipotimu saa nane mchana, mwili wa marehemu ukaandaliwa tayari kutoa heshima za mwisho kabla ya kwenda makaburini. Siku hiyo, Ipanga hakwenda kazini ili aweze kumsindikiza rafiki yake. Alikuwa pia na yule mfanyakazi mwenzake aliyekuwa akimfariji. Kipindi mwili wa marehemu tayari umetolewa nje, msemaji wa familia alianza kutoa utaratibu jinsi ya kuaga kwa watu waliohudhuria hapo msibani kwani walikuwa wengi sana. Alipokuwa akiendelea kutoa utaratibu na wakati huo watu wote wapo kimya wakimsikiliza, alinyamaza kidogo kumeza mate. Kipindi amenyamaza, mara ghafla sauti ya mlio wa kupokelea simu ya Ipanga iliyopotea ukaita kwa sauti kubwa kutokea kwenye jeneza. Dakika chache tena msemaji wa familia alipokuwa akihitimisha kutoa utaratibu, mara tena sauti ya mlio wa ujumbe mfupi wa simu hiyo hiyo ya Ipanga iliyopotea ukalia kwa sauti kubwa ukitokea hapo hapo kwenye jeneza.

Ipanga aliposikia hiyo milio ya simu yake iliyopotea akahisi kutetemeka kwani watu wengi hapo msibani walikuwa wanasimuliana kuwa chanzo cha kifo cha huyo kijana ni simu na kusikika kwa milio hiyo ikitokea kwenye jeneza. Alimwuliza mfanyakazi mwenzake aliyekuwa naye

karibu kama amesikia mlio wowote wa simu. Mfanyakazi mwenzake alimjibu kuwa hajasikia chochote. Taratibu za kuaga zilifanyika na kumalizika kisha wote wakaelekea makaburini kuzika. Walipokamilisha mazishi na kurudi tena nyumbani, Ipanga aliendelea kuwauliza watu mbalimbali kama wamesikia chochote juu ya hiyo milio iliyosikika ikitokea kwenye jeneza lakini wote kwa muda tofauti tofauti walimjibu kuwa hawakusikia chochote. Ipanga aliendelea kusononeka moyoni mwake bila kupata jibu kamili juu ya milio ya simu yake iliyopotea kusikika tena kwa sauti kubwa ikitokea kwenye jeneza.

Kuchi na wadogo zake pamoja na wajumbe wenzao wa kuzimu walishangazwa sana na kitendo cha wao na watu wengine kutosikia mlio wa simu ukitoka kwenye jeneza. Walijaribu kupeleleza huku na kule kuona kama watu wengine wamesikia huo mlio lakini kila aliyeulizwa alisema hajasikia chochote. Ilipofika usiku wa manane wakaitana kufanya kikao chao kama kawaida kisha wakamfanyia sherehe na kumpandisha vyeo mama mzazi wa kijana kwa kuwa mchawi mwema, pia wakamkaribisha kijana kuzimu na kumtengenezea dawa za kichawi za kumbadilisha akili pamoja na kumharibia ulimi. Lakini kwa vile kijana alikuwa

na imani kiasi na kuwakaba makoo wachawi waliokuwa wakimfanyia hizo dawa za kumpoteza ili asionekane kwa macho ya wanadamu wa kawaida lakini dawa hazikufua dafu. Baadhi ya watu wakawa wanamwona mtaani na wakati mwingine maeneo ya nyumbani kwao. Baada ya mwezi mmoja, mwenyekiti wao akawaeleza kwenye kikao chao, “Huyo kijana sasa anatuletea balaa kubwa hapa mtaani, anashindwa kutulia kwa sababu dawa zote anazipiga na kuzimwaga, hii inapelekea watu wamwone ingawa tunajitahidi sana kumficha. Tumejaribu kumnyima chakula ili adhoofu lakini akila kidogo tu anapata nguvu anarudia yale yale. Sasa mnaamuaje, tumwue ama tukamtupe mkoa mwingine ambako hawamjui?” Mjumbe mmoja akapendekeza, “Mkuru, tukamtupe katika mkoa ambako hafahamiki, watu watakuwa wanamchukulia kama mwehu tu kwani atakuwa ni mtu wa kula na kulala jalalani.” Mwenyekiti akaunga mkono, “Sawa sawa. Itabidi mtoa sadaka hii ambaye ni mama yake mzazi atwambie haraka ni mkoa gani hawana ndugu ili tukamtupilie mbali kesho usiku maana wasumbufu wa namna hii ni kuwafanya hivyo tena haraka.”

Muda huo, mama yake alikuwa naye kuzimu akimpatia dawa kwa kumlazimisha ili

kumpumbaza. Mjumbe mmoja aliagizwa haraka haraka kwa mtoa sadaka akamtajia mkoa kisha akarudi kwenye kikao na kumfahamisha mwenyekiti. Waliandaa utaratibu wote na kumtupa mkoa wa tano toka mkoa walipo ambako hakuna hata mtu mmoja anayemfahamu kisha wakarudi. Kijana alianza kuonekana mtaani huku akila na kulala jalalani na watu wa mkoa huo wakawa wanamshangaa huku wakijiuliza huyo mwehu katokea wapi.

Sura ya Saba

Baada ya siku kadhaa, matokeo ya akina Ipanga yakawa yametoka na Ipanga akawa ni mmoja wapo kati ya wanafunzi waliofaulu katika shule yake pamoja na kusoma kwa taabu na misukosuko ya ndugu zake. Baada ya miezi michache akapata nafasi ya kujiunga na chuo kikuu. Yeye na wazazi wake walifurahi hasa mama kwa kuchaguliwa kujiunga na chuo kikuu cha hapo jijini Mwazi. Ilibidi pia amfahamishe bosi wake pale kazini kwake, bosi wake naye alifurahi sana kisha akamwambia muda wa kwenda chuo ukifika amfahamishe. Ulipofika muda wa kwenda chuoni, Ipanga alimfahamisha bosi wake.

Baada ya kumfahamisha, bosi wake akampatia kiasi cha pesa cha kujikimu chuoni kwa muda wa miezi mitatu kisha akamwambia, “Ipanga, umekuwa mfanyakazi na mchapa kazi hodari kwenye kampuni yetu. Tunasikitika sana kuwa unaondoka. Tumekaa na uongozi mzima wa kampuni. Tumekubaliana tukupatie kiasi cha pesa kwa ajili ya kujikimu hapo chuoni kwa miezi mitatu mbele, pia tutaomba utuletee fomu yako ya malipo hapo chuoni tuone nini tunaweza kukuchangia zaidi. Mwisho kama hutajali, tunaomba kipindi cha

mafunzo kwa vitendo, uwe unakuja hapa hapa kiwandani kwetu." Ipanga akajibu, "Nashukuru sana kwa hayo bosi. Hakika nitakuwa nakuja kufanya kazi hata kama ni muda wa likizo endapo mtaniruhusu pia." Bosi wake akasema, "Kwa hilo ondoa hofu kabisa, muda wowote upatapo likizo unakaribishwa. Tena ninakupatia namba yangu ya simu ya mkononi, kwa chochote usisite kunifahamisha." Ipanga akasema, "Nashukuru sana bosi."

Bosi akamtajia namba yake ya simu, Ipanga akaijaza kwenye simu yake ila kwa kiwewe akawa amekosea namba moja. Bosi akamwambia ampigie ili naye aiweke namba yake kwenye simu yake. Ipanga alipopiga akaambiwa kuwa namba anayopiga haipo. Ipanga akamwambia tena bosi, "Samahani bosi, nimekosea namba moja nimeiruka." Bosi wake akamtajia tena kwa mara ya pili kisha Ipanga akampigia ikaita. Bosi naye akawa ameiweka namba ya Ipanga kwenye simu yake. Baada ya hapo bosi akamuaga Ipanga kisha akamwambia kesho aende kwa mhasibu akachukue pesa zake na pia atakapopata fomu ya gharama za malipo ya chuo, atamtumia ujumbe mfupi ili amletee fomu yeye mwenyewe. Baada ya kutoka ofisini kwa bosi, Ipanga akaenda kumalizia kazi kisha aanze

kukabidhi baadhi ya vitu alivyokuwa kakabidhiwa hapo kiwandani. Alionana pia na mfanyakazi mwenzake, akamwambia Ipanga, "Rafiki yangu, wewe una bahati sana. Jana kulikuwa na kikao cha bosi na baadhi ya viongozi, wakawa wanajadili kuwa walitaka kwenda kukusomesha chuo kimoja hivi. Kipo mpakani mwa nchi ya magharibi ila sasa wakasema umewapa taarifa kuwa umepata chuo hapa hapa jijini, wameahidi wataendelea kuwa karibu nawe hata kwenye chuo hicho utakachokwenda. Huyu bosi hadi kukukubali hivi, basi amekupenda sana, nadhani unafahamu na unaona vile anavyoogopwa. Endelea kuwa mchapakazi hivyo hivyo na tabia njema, utafika naye sehemu nzuri sana kwani anapompenda mtu huwa anajitolea sana kumsaidia." Ipanga akasema, "Ahsante sana rafiki yangu. Pia kama nilivyokwisha kukufahamisha, kesho ndiyo itakuwa siku ya mwisho kuja hapa kazini. Ninataka niende kijijini kuwasalimia wazazi kisha nifunge safari ya kwenda chuoni." Mfanyakazi mwenzake akasema, "Sawa Ipanga, nikutakie safari njema katika masomo yako na tutazidi kuwasiliana."

Baada ya mazungumzo hayo, waliagana kisha Ipanga akaelekea nyumbani. Kesho yake aliwahi kazini ingawa siku hiyo hakufanya kazi kwani kazi

kubwa ilikuwa ni kushughulikia malipo yake kwa mhasibu na kuwaaga wafanyakazi wenzake. Alilipwa pesa zote alizoahidiwa kisha akaanza safari kurudi nyumbani na siku hiyo hiyo akasafiri kuelekea kijijini kwao. Muda wote huo hali ya baba yake kiuchumi ilianza kuyumba na akawa ni mtu wa kufanya uvuvi wa hasara tu kila kukicha. Alipofika alipokelewa vizuri na wazazi wake hasa mama ingawa baba hakuonekana kuwa mtu wa furaha sana. Ilipofika usiku Ipanga aliwaelezea azma yake ya kwenda chuo ingawa taarifa ya awali alikuwa amekwishawapatia. Aliwaambia kuwa baada ya wiki moja ataelekea chuoni. Alimfahamisha baba yake kiasi alichonacho kwa muda huo na pia kiasi anachotakiwa kuongezewa kwenda nacho chuoni. Baada ya kumweleza hivyo baba yake, alianza kuzungumza kwa kulalamika kuwa hana pesa. Ipanga hakutilia maanani sana kwa sababu alimwona mzee wake akibadilika sana kadri siku zinavyozidi kwenda. Pia alijua kuna fomu inayoainisha gharama zote ambayo anatakiwa aichukue chuoni na aipeleke kwa bosi alipokuwa anafanyia kazi kwani aliahidi kumsaidia. Baadaye Ipanga aliwaaga wazazi wake kisha akaelekea chumbani kwake kulala.

Usiku wa manane akiwa usingizini alisikia mlio wa mbwa wake akibweka, alishtuka toka usingini kisha akasikia sauti nyingine ikimwambia, “Ipanga, kesho asubuhi njoo kandokando ya ziwa jirani na shambani kwenu nina mazungumzo marefu sana na wewe.” Ipanga haraka akili ikamtuma kuwa ni yule Mamba. Sauti ile ilisikika ikimwambia hivyo tu kisha ikapotea. Ipanga hakupata tena usingizi hadi kulipokucha. Ilipofika asubuhi alifanya kazi za hapo nyumbani haraka haraka kisha akamuaga mama yake kuwa anaelekea kuangalia shamba la huko kandokando ya ziwa kisha akaondoka. Alikwenda mbio sana hadi kando kando ya ziwa. Muda mchache tu alipofika aliona maji yakihangaika huku na kule mithili ya mawimbi yasiyokuwa na mwelekeo maalum kwani hali ya hewa ilikuwa shwari na hakukuwa na upepo wowote ule.

Alipokuwa akiyatazama hayo mawimbi ghafla Mamba alijitokeza na kumwambia, “Usiogope Ipanga, mimi Amani. Naomba ukae hapo chini ya kivuli cha huo mti na mimi nitasogea hapo jirani tuzungumze vizuri.” Ipanga alisogea kwa woga kwani mara ya kwanza alipokuwa akiongea naye alikuwa mbali naye lakini siku hiyo alimsogelea sana ingawa alikua miguu yake kaiweka ndani ya maji. Mamba akaendelea, “Kwanza pole na

misukosuko yote uliyoipitia na pia hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na chuo kikuu." Ipanga akasema, "Ahsante huku akihamaki sana kuona anajua kila kitu kumhusu. Pia baada ya kusikia hivyo mapigo yake ya moyo yakaanza kutulia taratibu ili amsikilize zaidi. Mamba akaendelea, "Ipanga, wewe si mtoto sasa bali ni mtu mzima na inabidi uelewe vitu vinavyokusibu. Nilikwambia siku ile kuwa ninaitwa Amani, jina langu linaendana na sifa zangu kwani ninapenda amani sana hasa kwa familia ama mtu anayemcha Mungu aishiye juu mbinguni kutoka moyoni mwake. Ndiyo maana mara nyingi nimekuwa nikisisitiza wewe na mama yako msali na kuomba sana wakati wote bila kuchoka. Niliwaambia hivyo kwa sababu mna vita kubwa sana na kibaya zaidi vita yenu ni ya ndani. Adui wa ndani huwa ni hatari sana kuliko adui wa nje. Kibaya zaidi awe ni adui wa ndani na hujamfahamu, atakuangamiza na kukuteketeza kabisa."

Ipanga alishangaa kusikia maelezo hayo kisha akauliza, "Siku ile uliniambia uchawi na leo unaniambia maadui! Unaweza kunielimisha vizuri?" Mamba akajibu, "Ninashukuru una kumbukumbu kidogo, adui wa mtu ama familia inayomcha Mungu aliye juu ni mchawi ingawa

Mungu hana uadui na mchawi." Ipanga akauliza, "Huyu mchawi ni wa namna gani hadi anakuwa adui wa mtu ama familia inayomcha Mungu?" Mamba akasema, "Ipanga, mchawi ni mtu yeyote yule anayejifunza ama kufundishwa mambo ya kishirikina na makazi yao makuu ni kuzimu. Mchawi ana sifa kuu moja tu, hataki kuona amani ama furaha ama maendeleo ya mtu mwingine, haidhuru ni ndugu yake wa damu, ndugu yake asiye wa damu, rafiki yake au hata jirani yake. Unapokosa maendeleo, unakosa pia furaha na unapokosa furaha unakosa pia amani. Motokeo ya kukosa furaha na amani ni umaskini, vifo vya aina mbalimbali, ndoa kuvunjika, na mengine mengi tu. Nadhani kwa hilo umenielewa vizuri." Ipanga akasema, "Ndiyo nimekuelewa."

Mamba akaendelea, "Nimehangaika na wewe sana Ipanga, toka unaumwa hadi kupelekwa hospitali na sasa unakwenda chuo kikuu." Ipanga aliposikia hivyo akashangaa sana na kumwuliza huyo Mamba, "Umehangaika na mimi, mbona huwa tunaonana hapa tu, huko kwingine kote sijawahi kukuona?" Yule Mamba akacheka kidogo, kisha akasema, "Ipanga, hapa pia bado hujaniona na kamwe huwezi kuniona kwani mimi ni mzimu. Ninawachukia sana watu wenye roho mbaya kwa

wenzao hususan wachawi, kwa sababu nami nilikuwa binadamu kama wewe lakini kwa sababu ya roho mbaya waliyo nayo walinipatia ugonjwa wa kichaa na kufanikisha kunipeleka kuzimu kichawi. Nilipofikishwa huko niliwashinda na kuvuruga baaadhi ya mambo yao kwa nguvu za Kimungu nilizokuwa nazo na kuamua kuniacha huru. Baada ya kuachwa sikuweza tena kurudi duniani kwa umbo la ubinadamu kama wewe hapo ulivyo. Nikijitokeza kwako kama nilivyo unaweza kupoteza uhai kwani nina nguvu za ajabu sana. Mara nyingi ninakuja kwako kupitia wanyama. Nikuulize swali kidogo tu?" Ipanga akajibu, "Ndiyo niulize." Mamba akamwuliza, "Yule mbwa wako ulijua alitokea wapi?"

Ipanga alishtuka kidogo kisha akajibu, "Wala hata sikujua, nilijikuta yupo tu hapo nyumbani." Mamba akasema, "Basi yule hakuwa kama mbwa wengine, nilikuwa mimi nikaamua kukutibu kabisa ugonjwa uliokuwa nao. Huo ugonjwa haukuwa wa hospitali, ulipewa ugonjwa huo kichawi na pia walikuwa na lengo la kumfilisi kabisa baba yako kutokana na gharama za matibabu yako na baada ya kufilisika na wewe ungekufa." Ipanga akainamisha kichwa chini kidogo huku akitafakari kisha akamwuliza, "Mbona uliondoka?" Mamba

akamjibu, “Nguvu zangu za kupambana na wachawi hutegemea sana maombi yenu hasa wewe na mama yako. Nimekueleza adui wa ndani ni hatari sana. Kuna mgeni alitokea mjini, alipofika hapo akaweka dawa za kuwafunga ufahamu wazazi wako na kuwafanya kusali na kuomba bila mwelekeo maalum na kunifanya mimi pia nguvu za kuwasaidia zikapungua na nikaamua kuondoka. Hata wewe ulikuwa hivyo hivyo unasali na kuomba bila mwelekeo maalum ila tangu upewe chumba cha nje na kuacha kula chakula cha hapo ulipopelekwa kusomea umepata nafuu. Kipindi kabla haijawa hivyo, ulikuwa unakula dawa za kichawi kupitia chakula, unakunywa dawa hizo kupitia maji na kulala pia katika kitanda kilichowekewa dawa za kichawi. Ndiyo maana ulikuwa na hali mbaya sana, ilipelekea hadi ukawa na wazo la kutoroka ukaishi mbali kwa kuona baba yako mzazi hakuelewi na anazidi kukupa adhabu ambazo hukuzistahili kuzipata. Tambua kwamba baba yako naye sio yeye halisi kwani unajua maisha mliyoishi awali. Dawa za kichawi alizolishwa na kunyweshwa ndizo zinamfanya hivyo alivyo sasa. Unaona hadi sasa biashara yake inayumba. Anaelekea kufilisika na atafilisika tu.”

Ipanga akauliza, “Kwa nini tusimsaidie baba yangu kama nilivyomsaidia rafiki yangu Masha?” Mamba akajibu, “Nguvu yake ya kusali na kuomba kwa Mungu aliye juu ni hafifu sana, angekuwa amekwishakufa lakini maombi kidogo ya mama yako ndio yanayomfanya aishi hadi leo.” Ipanga akauliza, “Kwa hiyo unamaanisha wanaofanya hivyo ni ndugu zake?” Mamba akajibu, “Hilo liko wazi kabisa, siyo kwake tu, anafanyiwa mama yako na wewe pia. Lakini ninyi mnaokolewa na kusali na kuomba.” Ipanga akauliza“ Kwa nini wanafanya hivi sasa wakati hata huko mjini wanaishi kwenye nyumba ya baba na huwa anawapa kila kitu ikiwemo pesa za matumizi?” Mamba akajibu, “Ili kumridhisha mchawi unapaswa ujiunge naye katika mambo ya kishirikana, vinginevyo hata iwe miaka mingapi atakuumiza tu endapo ukiwa hujamgundua ama kuwagundua washirika wake ambao anaweza kuwatumia endapo atahisi umemfahamu. Hii ni sawa na mfano huu. Kuna mtu mmoja alikuwa akifuga nyoka wengi kwenye shimo refu kidogo kwenda chini na lenye upana mkubwa. Aliwalisha wale nyoka wakastawi vema na kupelekea kuwafanya kama sehemu ya vivutio kwani watu walitoka sehemu mbalimabli kuja kuwatazama wale nyoka. Ilifikia hatua ni bora

akose yeye chakula na kushinda ama kulala bila kula lakini nyoka wake wapate chakula. Kwa muda aliowahudumia hao nyoka ilifikia hatua ni kama walimfahamu na kumzoea kwani alipokuwa akifika walianza kujinyoosha vichwa vyao huku wakimtazama ila kwa watu wengine waliofika hapo wala nyoka hawakuhangaika na chochote zaidi ya kulala tu. Siku moja jamaa huyo alipokuwa anawapa chakula hao nyoka wake aliteleza na kudondoka kwenye shimo hilo. Bila kujali nyoka walianza kumshambulia kwa kumgonga na akalazimika kupiga kelele ambapo watu walikuja kumwokoa na kumkimbiza hospitali kwa matibabu. Alipopona, hakutaka hata kuiona picha ya nyoka iliyochorwa kwenye karatasi kwani aliwachukia sana."

Ipanga akasikitika sana. Mamba akaendelea, "Hivyo basi, akili ya mtu mchawi ni kama ya nyoka, hata umtendee mema na mazuri kiasi gani ipo siku atakudhuru tu ama kukuharibia maisha yako ama kukuua kwani hiyo ndio furaha yake . Wakati huo wote Ipanga alikuwa makini sana kusikiliza, kisha Mamba akaendelea, "Nina mambo matatu ya msingi yaliyonifanya nikuite nikueleze kwani yawezekana tusionane wala kunisikia tena." Ipanga aliposikia hivyo akashtuka kidogo.

Mamba akaendelea, “Usishtuke Ipanga, nimejitoa na ninafanya hivi kwa ajili yako pamoja na familia yako, mnatendewa mambo ambayo hamkustahili kutendewa kabisa na wala hamna kosa lolote lile, hasa wewe. Sikutaka kukwambia mapema kwa sababu ulikuwa hujakua na kukomaa vizuri. Mengine ni mambo ya kutisha kidogo lakini naomba univumilie tu uyajue. Hivyo ninaomba unisikilize kwa makini sana.” Ipanga alikaa kwa makini na kuanza kumsikiliza huyo mamba. Wakati huo wote woga wa kumwogopa huyo mamba uliisha akawa ni mtu wa kutafakari vema kwa yote anayoambiwa.

Mamba akaendelea, “Jambo la kwanza ni kuhusu wewe mwenyewe pamoja na maisha yako, jambo la pili ni kuhusu rafiki yako Masha na jambo la tatu ni kuhusu wazazi wako. Naanza jambo la kwanza, Mungu amempatia kila mwanadamu karama yake ya maisha na ninyi mnaziita nyota. Kuna waliopewa ama aliyepewa nyota inayong’aa sana, kuna waliopewa ama aliyepewa nyota inayong’aa wastani na kuna waliopewa ama aliyepewa nyoya yenye mng’ao hafifu ila wote ni wake. Tunapozungumzia nyota ni mafanikio ama tunu ama baraka ya familia ama mtu kwa kila anachokifanya bila kujali umri wake, umbo lake

wala elimu yake. Sasa mchawi ama wachawi huziona nyota hizi mapema sana wakati mwenye nyota akiwa bado tumboni mwa mama yake ama mchanga mara tu anapozaliwa. Wanachokifanya, huanza kupambana kuiiba hiyo nyota ili iwasaidie katika shughuli zao za kichawi ama kwenye shughuli zao za kibiashara. Inaposhindikana kuichukua nyota hiyo, hapo ndipo vita inapoanza ikiwemo kuuliwa kwa huyo mwenye nyota ili hiyo nyota ichukuliwe kwa nguvu. Hizi shughuli za kunyang'anywa nyota kichawi haziwezi kufanikiwa hadi awepo mtu ama watu wa karibu sana yaani ndugu wa anayetaka kunyang'anywa ambao nao ni wachawi. Hata katika familia, unaweza kukuta mmojawapo kati ya mama au baba ni mchawi anahangaika kuchukua nyota ya mwenzake ambaye lazima ashirikiane na ndugu zake ili kuichukua."

Mamba aliendelea, "Sio hivyo tu, miongoni mwa watoto wa tumbo moja, unakuta yumo ama wamo wenye nyota zinazong'aa vizuri lakini wenzake ama mwenzake ni mchawi hivyo anachukua nyota ya mwenzake kichawi. Sasa kwa wazazi wako, wewe ni mmojawapo wa watu wenye nyota inayong'aa, ndio maana tangu utotoni unasumbuliwa na wachawi ambao ni ndugu zenu.

Ungekuwa umekwisha kufa kama kilichowatokea wenzako, lakini niliamua kukupigania na ndio maana hadi sasa nakusisitizia kusali na kuomba kila mara kwa Mungu wa juu Mbinguni ili niendelee kupata nguvu za kukupambania na kuipambania familia yako pia. Huwezi kuwa na kumbukumbu vizuri, ila utotoni mwako ulipoanza kutambaa, uliugua sana na kuchelewa kutembea. Ulitibiwa hospitali kubwa na ndogo lakini hukupona. Ulipakwa dawa na dawa za mitishamba bila mafanikio. Baada ya hivyo vyote kushindikana, ulipona taratibu bila dawa yoyote ile ambapo iliwashangaza wote kwa jinsi ulivyopona na ulikuwa ni mjadala kwa hao ndugu zako wachawi waliotaka kukuua kupitia ugonjwa huo. Ninakueleza matukio makubwa makubwa tu, ukiachilia mbali hayo madogo. Ugonjwa mwingine ni ule wa kutokwa na upele mwili mzima, huo wenyewe ulikuwa unajitambua vizuri na uliona taabu na adhabu uliyokuwa unaipata huku ukizungushwa hospitali za huku na kule ikiwemo hospitali kubwa ya kitaifa ya rufaa bila mafanikio." Ipanga akamjibu, "Ndiyo! Kabisa! Nilikuwa ninapata maumivu makali sana hususan wakati wa usiku." Mamba akaendelea, "Sio maumivu tu, hata moyo ulikuwa kama unataka kuchomoka." Ipanga

akakubaliana naye, “Kweli kabisa, wakati mwingine nilikuwa ninamwambia mama awe ananikandakanda sehemu ya moyo ili nipoe.” Mamba akasisitiza, “Ndio hivyo, nilipambana sana kukupigania na washirika wao wote kwenye hospitali ulizokuwa ukipelekwa hawakuweza kukusogelea.” Ipanga akauliza, “Washirika wao hospitali?” Mamba akajibu, “Hawa watu wapo kila mahali, yaani shuleni, hosptalini, kwenye nyumba za ibada, na sehemu nyingine nyingi tu.”

Ipanga akashangaa sana na kuuliza tena, “Kwenye nyumba za ibada ni mahali pa Mungu, wao wanaingiaje sasa?” Mamba akajibu, “Ni kweli Ipanga, hiyo ni sehemu ya kukusanyika kwa ajili ya kumwomba Mungu aliye juu, lakini unapokuwa humo, imani yako thabiti kwa Mungu ndio inayokufanya uwasiliane na Mungu lakini wachawi huamini miungu yao, hivyo sehemu za Ibada ama nyumba za ibada kwao ni sehemu ya kujifichia uovu wao na ndio maana wakati mwingine huwa mstari wa mbele kujifanya wanazitii, kuzilinda na kuziheshimu amri za Mungu. Hufanya hivyo kwa mwonekano wa nje tu, ili kuwapumbaza watu wasifikirie uovu wao. Unanielewa vizuri Ipanga?” Ipanga akajibu, “Ndiyo ninakuelewa vizuri kabisa.” Mamba akaendelea, “Huko kote hospitalini

ulikopelekwa ilishindikana kwani kila siku saa kumi na moja alfajiri nilikuwa ninaimarisha ulinzi sana kwako ili wachawi wasikuchukue." Ipanga akauliza kwa mshangao, "Wachawi wasinichukue saa kumi na moja alfajiri?" Mamba, "Ndiyo, asilimia kubwa ya wachawi huchukua watu wao saa kumi na moja alfajiri. Vifo vya wagonjwa wanaochukuliwa kichawi na kupelekwa kuzimu huwa vinatokea saa kumi na moja alfajiri. Lakini unakumbuka ulipona ukiwa nyumbani na kupitia mbwa wako ambaye ni mimi. Hivi unajua ni kwanini hadi leo hujamsimulia mtu yeyote ikiwemo wazazi wako ingawa ulitaka kufanya hivyo?" Ipanga akajibu, "Hapana sijui." Mamba akasema, "Kila ulipotaka kuwasimulia ulivyopona ulikumbwa na usingizi mzito sana, mimi ndiye nilikuwa ninakupa usingizi huo kwa sababu sikutaka wengine wajue ikiwemo hao ndugu zako wachawi kwani sio kila kitu kinachotendeka hapa chini ya jua watu wanapaswa kukijua, vingine hubaki siri ya mhusika na Mungu wake tu. Unakumbuka tukio la kifo cha rafiki yako aliyekuwa anakuja chumbani mwako unamsaidia kujifunza masomo?" Ipanga akajibu, "Ndiyo, ninakumbuka vizuri, tena kuna vitu nilitaka kukuuliza kwani hadi sasa sielewi kabisa." Mamba

akasema, “Kweli ninajua huelewi kabisa ila usiwe na hofu kwani hilo limekwisha pita. Lengo kubwa lilikuwa kukuchafua wewe mbele ya umati wa watu pale msibani, ila nilichokifanya, nilizimisha ile milio ya simu na ninadhani ndio inakupa mawazo sana. Niliizimisha, isipokuwa nikaruhusu uisikie wewe tu ili siku nitakapokuja kuongea na wewe ujue ni nini kilichokuwa kikitendeka. Ukiachilia mbali na hayo, tumboni kwako kuna kitu kinakuhangaisha sana hasa upande wa kushoto wa tumbo.”

Ipanga akadakia, “Ni kweli kabisa, ninapata maumivu makali sana na wakati mwingine ninashindwa kukaa vizuri.” Mamba akaendelea, “Maumivu hayo yanakuwa makali sana kipindi unapokuwa unajiandaa kufanya mitihani hasa mitihani ya kitaifa.” Ipanga akakiri, “Yaani ni sahihi kabisa, huwa ni hivyo.” Mamba akasema, “Unakumbuka vizuri tatizo hili lilianza lini?” Ipanga akajibu, “Ninakumbuka lilianza nilipokuja kusomea mjini.” Mamba akasema kwa msisitizo, “Hakika kabisa, kuna kitu cha kichawi ulilishwa, hicho kitu kina kazi kuu mbili, moja ni kuozesha vitu vilivyoko tumboni mwako ikiwemo maini, mapafu, utumbo na hatimaye tumbo kuvimba na

kupelekea kutapika damu ambapo ingekuwa mwisho wa maisha yako. Kazi ya pili ni kukupotezea kumbukumbu hasa unapokuwa unasoma. Nadhani unakumbuka mwanzoni ulikuwa unasoma sana lakini kila ulichosoma hakikukaa kichwani, dakika tano tu unasahau kila kitu ulichosoma." Ipanga akaitikia, "Aisee, ni kweli kabisa, lakini kwa sasa hii hali imepungua kwa kiasi fulani." Mamba akasema, "Siyo imepungua kwa kiasi fulani, mwanzoni ulibanwa sana fikra kupitia dawa ulizokuwa unapewa kwenye chakula, maji ya kunywa na hata kuwekewa kitandani unapolala. Ulipoacha kula, kunywa na kuhama chumba ndipo ukaanza kupata ufahamu wa kuomba na kusali kwa Mungu aliye juu na hapo ndipo nami nikaanza kupata nguvu za kukusaidia."

Muda wote huo, Ipanga hakuona tena yupo na Mamba ambaye ni mnyama tena wa hatari sana bali alijiona kama yupo na binadamu wa kawaida tena ambaye ni msaada mkubwa sana katika maisha yake. Mamba aliendelea, "Hadi sasa bado kuna shida tumboni mwako, ila usishtuke na wala usiogope kwani itakwisha kabisa. Ili uwe safi na salama kabisa, inatakiwa hicho kilichomo tumboni kitolewe na kukitoa anahitajika mtu wako wa

karibu sana na mwenye imani thabiti ya Mungu ndiye akutolee. Je, unaweza kumpata?" Huku Ipanga akiendelea kuwaza kwa mtazamo wa kibinadamu kuwa ni nani amsaidie, Mamba akasema, "Hebu usiwaze, hii shughuli atakusaidia rafiki yako Masha."

Ipanga akashangaa sana kusikia jina la Masha kwani wamepotezana muda mrefu sana na hata hajui mahali alipo wala anafanya nini. Akamwambia Mamba, "Nina muda mrefu sana sijamwona na hadi sasa sijui yuko wapi." Mamba akajibu, "Masha yupo na atakuja hivi karibuni kwani naye aliangukia kubaya sana. Hayo mambo ya Masha tutaongea baadaye. Mambo yanayokuhusu nimemaliza, labda kama una swali lolote lile!" Ipanga aliendelea kupoa kama mtu aliyenyeshewa na mvua huku akiwazia hicho kilicho tumboni mwake. Mamba akamwambia tena, "Kijana, kama una swali uliza kwani leo ndio siku ya mwisho kuniona hivi unavyoniona." Baada ya kusikia hivyo Ipanga alishtuka kama mtu aliyekuwa usingizini kisha akauliza, "Hiki kilichoko tumboni kitatoka lini?" Mamba akajibu, "Utakapokwenda chuoni. Masha atakutafuta siku si nyingi utakapokuwa chuoni. Ukishaonana naye

atakuomba kesho yake mwende sehemu yenye utulivu ambapo ni mlimani akakusimulie changamoto ya maisha yake, mkubalie mwende naye. Mtakapofika huko na kuketi kwenye mwamba, pembeni yako kutakuwa na mafuta ya mgando machache sana yaliyomwagika juu ya huo mwamba mlioketi. Yakombe yote uyapake tumboni hasa sehemu ambapo tumbo huuma sana. Ukisha yapaka, hiyo sehemu ya tumbo itavuta sana na utasikia maumivu kiasi. Baada ya muda hiyo sehemu itavimba mfano wa jipu, ikiwa hivyo, muombe Masha aikamue kwa nguvu kama linavyokamuliwa jipu lililoiva. Atakamua kisha kuna kitu kitatoka, kikitoka hicho kitu, komba tena mafuta kidogo yaliyobaki ukipake na baada ya hapo kitupe. Baada ya zoezi hilo usimwambie Masha kitu chochote kwani yeye atakuwa anawaza vitu vingine kichwani mwake na baada ya kumaliza, hatajua nini kimetokea. Baada ya hapo endeleeni na mazungumzo yenu na tayari utakuwa umepona kabisa."

Ipanga akaitikia, "Sawa, nimekuelewa vizuri." Mamba akasema, "Nasisitiza tena, usiache kusali na kuomba kila mara kwani hawa wachawi ni wengi sana na kibaya zaidi wana mtandao mkubwa sana." Ipanga akasema, "Nina dhani ni hao ndugu wa

baba tu!" Mamba akasema, "Karibia kila ukoo kuna mchawi ama wachawi." Ipanga akauliza, "Kwani wanajifunzia wapi huo uchawi na kwanini Mungu hawapi adhabu kali kwa kutesa watu hivi?" Mamba akasema, "Katika kila ukoo kuna mzimu wa kichawi na unapomshika mtu ndio anakuwa mchawi bila kujali rangi wala kabila. Zamani, wazee wenu waliishi wakiwa wamejifungia kwenye magunia yaani hawaoni mambo ya nje yanavyokwenda, lakini ninyi sasa mnaishi ndani ya matenga yaani mnaona kila kitu kilichopo nje. Mungu kawapa hiyo neema kupitia kutembea na kuchangamana na makabila ya ndani na nje ya nchi yenye mila na desturi tofauti tofauti kupitia kuhamahama kimakazi, kibiashara ama kielimu. Hii imepelekea kuweza kubaini mambo yaliyo mema na mabaya na jinsi ya kuyafuata yaliyo mema ama kujiepuesha na yaliyo mabaya. Hiyo tu haitoshi, bado mmejikuta mnaishi katika maisha ya ukuaji wa sayansi na teknolojia ambapo dunia sasa imekuwa kijiji kwani mnapata habari na matukio mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kwa muda mfupi sana. Binadamu wote ni wa Mungu ingawa wapo wanaokwenda kinyume na matakwa ya Mungu. Mlipewa akili lakini kizuri zaidi mkapewa ufahamu tofauti na wanyama wengine. Ufahamu

huo unakuwezesha kutambua mema na mabaya na ndio maana mnaweza kubaini jambo jema na baya."

Ipanga aliendelea kusikiliza kwa makini huku akijaribu kufikiria siku hiyo ya kutolewa hicho kilichoko tumboni mwake. Akijiuliza itakuwaje, huku akiwazia zaidi maumivu kwani aliambiwa atakamuliwa kama linavyokamuliwa jipu. Mamba akaendelea, "Ninataka kuhama upande wako, ninadhani huna tena swali!" Ipanga akadakia, "Nina swali la mwisho." Mamba akasema, "Haya, uliza." Ipanga akauliza "Yule kijana alipoanza kuugua hicho kichaa, alipatwa na nguvu nyingi sana ikalazimu afungwe kamba kipindi alipokuwa amelazwa hospitalini. Alitoa wapi nguvu zote hizo?" Mamba akamjibu, "Hakuwa yeye." Ipanga akapigwa na butwaa kusikia hivyo. Ikabidi Mamba amfafanulie vizuri, "Usishangae, nakwambia hakuwa yeye huyo kijana. Kijana alikuwa tayari amechukuliwa kichawi ingawa ninyi mlikuwa mnamwona kama ni yeye. Nimekwishakwambia wachawi wana sayansi ya hali ya juu sana wanapofanya mambo yao." Ipanga akauliza tena kwa udadisi zaidi, "Yule alikuwa nani na yeye alipelekwa wapi?" Mamba akajibu, "Muda ule

anaanza kuugua ndipo walipomchukua kichawi na kumficha sehemu alipokuwa anaishi. Yule aliyekuwa hospitalini hadi anafariki ni mtu wao aliyekuwa kuzimu anaumwa na alikuwa ni mzee ingawa ninyi mlikuwa mnamwona kama ni kijana. Kijana mwenyewe alichukuliwa rasmi kipindi ninyi mnaelekea makaburini kuzika na muda wote huo alikuwa kafichwa nyuma ya mlango mkubwa wa sebuleni hapo kwao akiwa ameshikiliwa na baadhi ya wachawi. Uliona kulikuwa na mvutano mkubwa sana walipotaka kusafirisha maiti." Ipanga akakubaliana naye, "Ndiyo nakumbuka." Mamba akasema, "Ndio hivyo, tuyaache hayo. Sasa kuhusu wazazi wako, sitaongea sana ila nashukuru kwa sasa mama yako anavyojitahidi kusali na kuomba kila mara kwani hiyo hali hunipatia nguvu sana ya kuendelea kuwapigania dhidi ya mambo hayo ya kichawi."

Ipanga akauliza, "Ni kwa nini baba yeye huwa haombi na kusali mara kwa mara?" Mamba akajibu, "Tangu alipozaliwa hakuwahi kuishi wala kufikiria kumfanyia mtu hila yoyote ile. Hivyo basi anafikiria maisha aliyoishi na anayoishi yeye ya upendo ndio kila mmoja anayaishi na ndiyo maana humwamini na kumthamini kila mmoja. Hivyo kwa sehemu kubwa ndugu zake aliowatendea wema

ndio hao hao waliokuwa wanamwangamiza hadi leo.Ninyi mna misemo yenu kuwa shukrani ya punda ni mateke na kikulacho ki nguoni mwako. Walianza kumchawia toka kitambo sana ikiwemo kumfunga ufahamu. Ndio maana hivi juzi amekuja mmoja wao kumfanyia dawa kali zaidi na ndio maana unaona kwa sasa shughuli zake zinaporomoka kwa kasi. Mali ambazo umekua unamwona nazo ni mara mbili ya ambazo angekuwa nazo kama sio kusumbuliwa katika mambo hayo ya kishirikina. Kwa ufupi tu walimfanyia dawa ya kumfunga ufahamu wa kusali na kuomba. Lakini yote haya yataisha kwani kwa sasa maombi yanapitia kwa mama yako na wewe pia. Nadhani umenielewa vizuri." Ipanga akajibu, "Ndiyo, nimekuelewa ila sijajua kama mali zake zitarudi kama ilivyokuwa mwanzo." Mamba akasema, "Hapana, hazitarudi kama mwanzo na hii ni kwa sababu ya huruma yake kwa watu pamoja na nguvu za kufanya kazi kwani amezeeka sasa. Hao ndugu zake wachawi hupenda kuomba pesa na anapowapatia huenda kumtengeneza ili aishiwe pesa na miradi yake ifilisike kabisa. Kumbuka Ipanga, watu waovu hutembea na mambo makuu mawili vichwani mwao. Wasipokujadili kuhusiana

na vitu unavyomiliki basi watakujadili kuhusu mwonekano wako ulivyo."

Ipanga akahoji, "Kwa nini asiache kuwapa pesa?" Mamba akajibu, "Kutoa ni moyo na yeye hajaumbiwa moyo wa uchoyo. Anapoelezwa tatizo lolote lile kwa yeyote yule huwiwa kusaidia hata wewe umekuwa shahidi ambavyo huwa anawasaidia watu hapo kijijini kwenu." Ipanga akasema, "Nimekuelewa vizuri. Je, mimi ninaweza kumsaidia baba kutoka kwenye hiyo hali?" Mamba akasema, "huna jinsi ya kuweza kumsaidia baba yako tofauti na kuendelea kumwombea. Una swali lolote kuhusu baba yako?" Ipanga akasema, "Hapana, sina swali lolote." Mamba akasema, "Sawa! Kama nilivyokueleza awali kuwa mengine anayoyafanya baba yako kwa sasa msamehe bure kwani siyo yeye. Ni dawa alizopewa toka kitambo zinazompelekea kuendeshwa kama kifaa ninyi mnakiita roboti inayoendeshwa na rimoti. Rimoti hiyo ipo kwa ndugu zake wa damu, kikubwa endeleeni kumwombea tu. Tukiachana na hayo, tuje jambo la mwisho linalomhusu rafiki yako Masha. Kwa sasa ana hali, naweza kusema ni mbaya sana ingawa mengi atakueleza yeye mwenyewe."

Ipanga akashtuka kisha akauliza, “Kwani amerudia tena kuumwa kama awali?” Mamba akasema, “Hapana, alijikuta yupo kwenye mtego wa kumpenda binti na kuzaa naye ambaye yupo kwenye mtandao wa kichawi na ndugu zake.” Ipanga akauliza, “Mbona ndugu zake huwa wanasema hawajui alipo kwa sasa?” Mamba akajibu, “Wanajua vizuri sana lakini hawawezi kusema kwani njia wanazozitumia kujua alipo ni tofauti na uhalisia wa kibinadamu. Hivyo, walimtumia binti ambaye yupo huko anapoishi ili ampende na hatimaye wawe wapenzi na ndivyo ilivyotokea hadi wakapata mtoto wa kike.” Ipanga akazungumza kwa mshangao, “Kumbe Masha ana mtoto sasa!” Mamba akasema, “Ndiyo, tena kwa sasa ni mkubwa tu.” Ipanga akasema, “Ni muda mrefu sana sijaonana naye wala kuwasiliana naye.” Mamba akasema, “Ndiyo na nisikilize kwa makini kwa sababu mwishoni kuna maagizo nitakupatia ili umwambie huyo rafiki yako Masha.” Ipanga akasema , “Hata sijui nitampata wapi.” Mamba akaendelea, “Nimekwambia utakapokwenda chuoni atakuja na akifika mtafanya nilivyokueleza awali kisha ndipo utampatia maelekezo nitakayokuelekeza mwishoni. Unanielewa vizuri?” Ipanga akajibu, “ndiyo, nimekuelewa.”

Wakiwa kwenye mazungumzo hayo, ghafla alitokea mtu kwa mbali akitembea akija uelekeo wao walipokuwa akifuata njia iliyokuwa inapita pembeni yao. Ipanga akaonesha kuduwaa kwa hofu kuwa itakuwa picha gani katika jamii endapo huyo mtu anayekuja atamfahamu na kumwona ameketi na Mamba. Mamba akawa ameitambua hofu ya Ipanga kisha akamwambia "Usiogope wala usibabaike Ipanga, huyo mtu anayekuja hataweza kutuona wala kutusikia." Baada ya maelezo hayo kutoka kwa Mamba hofu ya Ipanga ikapungua kidogo na kweli yule mtu akapita karibu yao kisha akaenda zake. Mamba akaendelea, "Nitakueleza mambo machache tu kuhusu rafiki yako Masha. Baada ya kuwa na huyu binti waliishi wote kama mume na mke kwa miaka kadhaa hivi. Kwa vile yule binti alikuwa ni mchawi na kwa maelekezo ya watu wa karibu yake walipambana kumwingiza Masha kwenye uchawi wakashindwa hivyo wakaamua kumtesa kiuchawi ili hatimaye wampeleke akaishi na kuwafanyia kazi zao kuzimu."

Ipanga akahoji kidogo, "Umesema ndugu zake Masha ndio wanaoshirikiana na huyu binti, je ndugu zake wa karibu ni akina nani?" Mamba akajibu, "Ndugu zake wa karibu na huyo binti ambao ni mama yake mzazi huyo binti, bibi yake

kizaa mama na baadhi ya dada na kaka zake ambao ni washirika kwenye chama kimoja cha kichawi." Ipanga akauliza, "Vipi kuhusu baba yake?" Mamba akajibu, "Mama binti yule anaishi kwao baada ya kuachika kwa mumewe wa kwanza. Alipoachika akawanga'ang'ania watoto wote aishi nao kwao kwa lengo la kuwafanya watoto hao kitega uchumi ingawa kubwa zaidi ni kuwafundisha uchawi. Huyo binti aliyezaa na Masha ni mtoto wa mwisho wa huyo mama ingawa yeye ana baba yake mwingine. Binti aliishi na Masha kwa muda mfupi kisha akaachana naye." Ipanga akauliza, "Kwa nini huyo binti hakwenda kuishi na baba yake?" Mamba akajibu, "Baba yake alitamani sana kuishi na mwanae lakini huyo mama yake aling'ang'ania kwa nguvu zote ili akae nae kwa lengo la kumfundisha uchawi na akafanikisha. Vivyo hivyo huyo binti aliyezaa na Masha alitumia mfumo aliotumia mama yake wa kumng'ang'ania mtoto wakati hana uwezo wa kumtunza kama rafiki yako Masha alivyotaka lakini kwa lengo moja tu kumfundisha uchawi na ukizingatia ndiye mjukuu pekee wa kike katika familia ile. Ila kupitia imani aliyokuwa nayo Masha kwa Mungu kupitia kusali na kuomba kwake aliokoka na kufanikiwa kuachana na yule binti kwani siyo rahisi kiasi hicho

kuchomoka kwenye mikono ya mchawi. Lakini walivyoachana aling'ang'ania sana mtoto kwa nguvu na vitisho na uongo wa aina mbalimbali ili abaki na mtoto kama alivyofanyiwa yeye na mama yake. Lengo kubwa la binti huyo ni kumng'ang'ania mtoto ili aendelee kumfundisha mambo ya kichawi. Masha alijaribu kupambana sana ikiwemo kutumia taratibu zote za kifamilia na kisheria, lakini binti kwa kujiamini akishirikiana na familia yake walikuja juu wakidai mtoto huku wakitoa sababu mbalimbali za uongo ikiwemo mtoto wao hawezi kulelewa na mama wa kambo. Sababu hizo walizokuwa wakizitoa, vitisho hivyo walivyokuwa wakivisema, uongo wote waliokuwa wakiusema, na kila kitu walichokuwa wakikifanya kilikuwa na lengo moja tu kumng'ang'ania huyo mtoto ili waendelee kumrithisha uchawi."

Ipanga akaeleza, "Mbona hii ni kama mfanyakazi mwenzagu pale nilipokuwa nafanyia kazi kijana alimsomesha binti kwa gharama kubwa sana na kumtafutia kazi, lakini mwanamke akamfanyia vituko wakaachana. Ingawa kijana alipambana sana amchukue mtoto ili amsomeshe kwenye shule nzuri lakini yule mzazi mwenzake pamoja na familia yake akiongozwa na mama wa mwanamke wakaja juu pia kumng'ang'ania mtoto

wakati hawana uwezo wa kumsomesha." Mamba akasema, "Nilikwisha kukwambia kuwa sifa na furaha kuu ya mchawi ni kuharibu hasa penye mafanikio ama maendeleo. Unaweza kumtendea mchawi ama familia ya kichawi mambo mazuri ikiwemo kuwapa heshima kubwa, lakini unapofika sehemu ya kutaka kuvuruga mipango yao ya kichawi, wote huja juu tena kwa nguvu zote. Ninyi katika hali ya kibindamu mtashangaa sana kuona kama ni kitu kidogo na mbeleni kinaweza kuwa na faida kubwa kwao. Nikuulize kitu katika hali ya kawaida mzazi gani asiyependa maendeleo ya kwake binafsi pamoja naya mwanaye ama wanawe?" Ipanga akasema, "Hayupo, wote huhangaika ili mwanaye ama wanawe waendelee."

Mamba akafafanua, "Basi elewa kwamba, kwa mtu mchawi yeyote yule, kitu kama kitakuwa na maslahi ya kichawi, hata kama umemfanyia kitu kizuri kiasi gani ama umemfanyia mambo mazuri kiasi gani, atasimamia hayo maslahi hasa ya kuingiza mwanachama mpya kwa namna yoyote ile ili afanikiwe. Hicho ndicho kilichomtokea rafiki yako Masha na mpaka leo hii ni miaka imepita hajafanikiwa kumchukua mtoto." Ipanga akauliza tena, "Lakini kuna wakati ataweza kufanikiwa?" Mamba akasema, "Kufanikiwa atafanikiwa ila kwa

kusali na kuomba sana kwa sababu mama yake mzazi ndiye anayehusika kumwingiza mwanaye kwenye uchawi. Lakini hata Masha asipofanikiwa, wao wakifanikiwa na mtoto kuwa mchawi kamili, wataanza kumsukuma aende kwa baba yake kwa lengo la kumtumia mtoto ili kumroga Masha. Ila hadi sasa wamekwishajaribu kwa asilimia kubwa lakini wanamchosha tu kwani mtoto mwenyewe hataki uchawi. Kikubwa kabisa utamwambia Masha aachane na ushauri wa watu, utampeleka pabaya, kikubwa asali na kumwombea mtoto wake ili Mungu atende miujiza kwa mtoto asiushike uchawi." Ipanga akasema, "Ningependa kujua, kwanini huyo mzazi mwenzake na Masha anamfanyia hivyo mtoto wake wakati anaona hakuna faida yoyote ile. Swali jingine, hao wanaomshauri Masha mpaka kuona kuwa anapelekwa kubaya ni akina nani?"

Mamba akajibu, "Faida kubwa ya mchawi hususan mwanamke awapo kuzimu hupambana na kutoa kafara mbalimbali ili awe mtawala ama apande cheo. Hiyo hali hupelekea hata anapokuwa katika hali ya kawaida ya kiubinadamu atataka kuwa mtawala ama msemaji mkuu wa familia haidhuru yuko kwake, ameolewa ama hajaolewa.

Akiwa ameolewa, kwa kawaida kitu kimoja hutokea kati ya vitu vitatu kwenye familia yake kama mmewe siyo mchawi. Kwanza humtengenezea dawa mumewe ili amtawale kwa kila idara. Hii humfanya kuwa huru na kutenda kila anachokitaka kutokana na hulka yake. Mfano, kama ana hulka ya kunywa pombe, atakunywa muda wowote na kurudi nyumbani muda wowote anaotaka bila kubughudhiwa na mumewe ambaye mara nyingi hufanywa kama mtafutaji wa pesa za matumizi na mlinzi wa nyumbani tu. Hujitahidi kumsema vibaya na kumdhalilisha mumewe kwenye jamii inayomzunguka ili watu wamwone hafai kabisa. Kama mwanamke ana hulka ya kutoka nje ya ndoa, humtengenezea mumewe dawa za kumkosesha nguvu za kiume, kupitia hilo atajifanya kumgombeza mumewe na kumtengenezea hofu na mfadhaiko moyoni mwake kuwa hana hamu naye kwenye tendo la ndoa. Hivyo huamua kutembea na wanaume wengine na hata kama mumewe akijua hatakuwa na nguvu za kushitaki kwa watu kutokana na dawa alizopewa za kupumbazwa na pia hofu aliyojengewa kuwa yeye ana matatizo ya nguvu za kiume. Pili, hutengenezewa dawa ya kumfanya aichukie nyumba na familia yake kwa ujumla. Hii hutokea

pindi mwanaume anaamua kuikimbia na kuitelekeza familia na yeye kwenda kuanzisha maisha mapya sehemu nyingine kabisa. Tatu, humtengenezea dawa mumewe ya kumfanya kuugua na hatimaye kupoteza maisha katika hali ya ubinadamu. Umenielewa vizuri?" Ipanga akajibu, "Ndiyo ninakuelewa vizuri sana."

Mamba akaendelea, "Uliuliza ni akina nani wanamshauri vibaya. Kwa sababu ya muda sitakueleza yote, hata hivyo yeye pia atakusimulia. Lakini baada ya kuachana na mzazi mwenzake, amepitia mambo mengi na changamoto nyingi ikiwemo kutupiwa jini." Ipanga aliposikia jini alishtuka na kushangaa sana, kisha akamwuliza Mamba, "Alitupiwa jini wakati huwa nasikia jini ni upepo tu?" Mamba akamjibu, "Yote haya atakueleza yeye mwenyewe. Nadhani umenielewa." Ipanga akasema, "Ndiyo, nimekuelewa vizuri." Mamba akahitimisha, "Sina neno zaidi labda kama una swali lolote unalotaka kuuliza." Ipanga akauliza, "Umesema sitakuona tena, endapo nikihitaji msaada wako zaidi nitafanyaje?" Mamba akajibu, "Utasali na kuomba kisha utapata ufumbuzi wa shida yako. Ni kwa nadra sana kujitokeza na kuzungumza hivi

tunavyozungumza, hivyo una bahati sana mimi kujitokeza hivi kwako." Ipanga akasema, "Ninashukuru sana kwa kunipigania mimi na familia yangu. Ninaomba uendelee kutupigania hivyo hivyo pamoja na watu wote wenye mapenzi mema." Mamba akasema, "Usinishukuru mimi, mshukuru sana Mungu na pia endelea kusali na kumwomba muda wote, naye atakufanikishia mambo yako zaidi na zaidi vile impendezavyo."

Ipanga akasema, "Sawa, nitaendelea kufanya hivyo." Mamba akamuaga Ipanga, "Kwa heri na uwe na maisha mema." Ipanga akapata wazo lingine, "Ninaweza kukuliza kitu kabla hujaondoka?" Mamba akamjibu, "Kuwa huru sana, karibu uulize." Ipanga akauliza, "Watu wengi huamini kuwa mzimu ni kitu kibaya mfano wa shetani, lakini mbona wewe umekuwa mwema hivi kwangu?" Mamba akacheka kisha akasema, "Hahahahahaaa! Ipanga, ni bora umeniuliza hili swali kwani toka awali niliona jinsi lilivyokuwa likikutesa moyoni mwako. Kwanza kabisa, asili ya mzimu ni mwanadamu na kumbuka kuna mwanadamu mwenye roho mbaya na mwingine mwenye roho nzuri ambaye anauishi uungu ndani yake. Lakini neno mzimu hupingwa sana sehemu

mbalimbali ikiwemo kwenye nyumba zenu za ibada pasipo kujua vema asili ya neno mzimu. Ninasema hivyo kwa sababu tatizo la wanadamu walio wengi wanaamini sana kusikia na kuweka akilini pasipo kuchukua muda kutafakari vema wanachoambiwa. Mfano, hapa ulipo wewe unaitwa Ipanga, si ndiyo?" Ipanga akajibu, "Ndiyo, ninaitwa Ipanga."

Mamba akasema, "Neno Ipanga linakuwakilisha umbo lako tu la nje lakini asili yako ni roho yako ambayo itaishi hata pale utakapofariki dunia. Hivyo uhalisia wa roho yako ndio matokeo ya hivyo ulivyo kitabia na matendo, ndio maana wengi huenda mbali zaidi na kusema fulani ana roho nzuri ama ana roho mbaya. Hiyo roho nzuri ama mbaya inawasilishwa na jinsi unavyoishi na unavyotenda. Pia kumbuka, hapa duniani hakushushwa kutoka mbinguni. Ulizaliwa na wazazi wako wawili ambao ni baba yako na mama yako. Yaani ninamaanisha una vinasaba vya wazazi wako ambavyo ndivyo vimekufanya wewe ufanane ama na baba yako, mama yako ama ndugu yako yeyote yule kutoka upande wa baba ama mama kwa sababu kupitia vinasaba hivyo ndio wazazi wako walipatikana. Unaweza kufanana na mmoja

kati yao kwa kupitia matendo, tabia ama mwonekano. Kufanana huko, ina maana una roho mojawapo kutoka kwenye huo mlolongo upande wa baba ama mama ama wote kwa pamoja. Wewe unaweza kuwa unawafahamu babu na bibi kizaa baba yako na mama yako, je unawafahamu babu na bibi wa hao babu zako na bibi zako?" Ipanga akajibu, "Hapana, hata siwafahamu."

Mamba akasema, "kwa hiyo, hizo zote ni roho ambazo kila mwanadamu anazo kutokana na uzao wake hadi kule kwa wazazi wetu wa kwanza ambao ni Adam na Eva ama wengine humwita Hawa." Ipanga akauliza kwa mshangao, "Kwa hiyo unamaanisha kuwa sisi asili ama chimbuko letu linatoka kwa Adam na Eva ama Hawa?" Mamba akajibu, "Ndiyo, Mungu baada ya uumbaji wa mbingu na dunia pamoja na viumbe vyote, alimuumba mwanadamu kwa mfano wake ambaye ni Adam na Eva ama Hawa alimuumba kutoka ubavuni wa Adam. Hapo ndipo kizazi kilipoanzia hadi kukufikia wewe hapo pamoja na wengine uwafahamuo." Ipanga akauliza, "Kwani mzimu ndiyo pepo?" Mamba akajibu, "nimekwambia kuwa mzimu ni roho ambayo imewahi kuishi katika ulimwengu wa nyama yaani mwanadamu

lakini mapepo ni roho ambazo hazijawahi kuishi duniani kama wanadamu. Tambua kuwa kila binadamu ana harufu yake ya mwili hivyo mzimu unapomtokea ndugu, jamaa ama rafiki yake humtambua kwa harufu yake ya mwili ukiachilia vitu vingine. Lakini mapepo hutambulika kwa marashi yao. Hapo sasa umenielewa vizuri!" Ipanga akasema, "Hakika kabisa, nimeelewa vizuri sana." Mamba akaaga, "Mimi nakwenda sababu hata muda wenyewe sio rafiki sana kwangu." Ipanga akamshukuru "Ahsante sana." Mamba akajivuta hadi majini kisha akazama na kutokomea. Ipanga alinyanyuka akajifuta mchanga kisha akaanza safari ya kurudi nyumbani kwao sababu muda ulikuwa umekwenda sana.

Sura ya Nane

Chuo kilipofunguliwa, Ipanga aliwaaga wazazi wake kisha akaelekea mjini kwa maandalizi ya kwenda chuoni. Kabla ya kwenda chuo, alikwenda sehemu alipokuwa akifanyia kazi kuwaaga na siku iliyofuata alielekea chuoni. Baada ya miezi miwili akiwa chuoni alipigiwa simu na namba ngeni alipoipokea kumbe alikuwa ni rafiki yake Masha. Alimwahidi wikendi inayofuata atamtembelea hapo chuoni. Ipanga alifurahi sana kupokea simu ya rafiki yake kwani alikuwa na shauku sana ya kuonana naye. Ilipofika siku ya Jumamosi asubuhi, Masha alimpigia simu tena kuwa tayari amefika hapo chuoni. Ipanga alikwenda kumpokea wakaelekea kwenye mgahawa wa chuo kunywa chai. Huku wakiwa wanakunywa chai, Masha alimwomba waende sehemu tulivu wazungumze kwani ni kitambo sana hawajaonana.

Ipanga alimkubalia kisha akamwuliza waelekee sehemu gani ya utulivu anayoipenda yeye, Masha akamjibu waende kwenye mlima ambao upo jirani kidogo na chuo hicho. Ipanga akamkubalia na baada ya kumaliza kunywa chai, alinunua chupa mbili ndogo za maji ya kunywa kisha wakaanza safari kuelekea kwenye mlima huo. Walifika

mlimani, Masha akamwambia rafiki yake wapumzike kwenye mwamba uliokuwa katika mlima huo.

Walipumzika kwa kujilaza kwenye mwamba huo. Kabla hawajaanza mazungumzo yoyote yale, ghafla Ipanga akaona mafuta ya mgando pembeni yake. Akayachota taratibu na kujipaka tumboni sehemu ya kushoto alipokuwa akipata maumivu ya tumbo. Alifanya hivyo kwani alikuwa anakumbuka maelezo na maelekezo yote aliyopewa na yule mamba. Dakika chache baada ya kujipaka mafuta, tumbo lilianza kujivuta na hatimaye kujitengeneza kama jipu upande wa kushoto. Muda wote huo Masha alikuwa kajipumzisha kwa kujilaza chali ili kuutuliza mwili uliokuwa unatokwa na jasho kutokana na kupandisha mlima huo. Ipanga alimwita Masha na kusema, “Masha, ninaomba unisaidie kunitumbua hiki kijipu.” Masha alimkubalia kisha Ipanga akavua shati lake naye Masha akaanza kumtumbua jipu. Alilikamua kwa nguvu, hatimaye likapasuka na kutoa usaha ulioambatana na sindano mbili zilizo kaa mithili ya alama ya kujumlisha huku zimezungushiwa uzi mweusi pande zote. Ipanga alishangaa sana kuona hizo sindano, alizishika na kukomba tena kiasi

kidogo cha mafuta kilichobaki akazipaka kisha akazitupa chini ya huo mwamba.

Baada ya hilo zoezi kukamilika, Ipanga alivaa tena shati lake na kumsemesha Masha ambaye alionekana kama alikuwa kwenye usingizi mzito sana. Masha aliitikia na baadaye akaanza kumwelezea mkasa wote alioupitia. Ipanga alimpa pole sana rafiki yake kisha akamwuliza, "Huyo mtu alikushauri nini na ulifanya nini?" Masha akajibu, "Baada ya kuachana na binti huyo huku akiendelea kumng'ang'ania mtoto wangu, jamaa yangu alinishauri anipeleke kwa mganga na bila kufikiria sana nikafanya hivyo. Siku hiyo hiyo tulifunga safari kwenda kwa mganga na tulipofika alitukaribisha na kutupeleka moja kwa moja kilingeni anakoagulia. Mganga alianza kuzungumza lugha ambayo mimi sikuielewa na baada ya muda mfupi akaanza kuitafsiri. Aliniambia kuwa nimshukuru sana Mungu wangu kwa kuendelea kuwa hai vinginevyo ningekuwa nilishafariki muda mrefu sana kutokana na jinsi nilivyokuwa nimelogwa. Nilishtuka sana kusikia hayo maneno kutoka kwa mganga ingawa yeye aliendelea kuzungumza lugha ambayo hatukuielewa huku akitikisa kichwa na kusonya mara kwa mara.

Alipomaliza alianza kuzungumza na wakati mwingine akituuliza maswali huku akitutazama usoni. Mganga akasema, “Binadamu tumebadilika sana, tumekuwa na mioyo ya kikatili kuwazidi hata wanyama. Mwenzako kakukosea nini hadi umwumize kiasi cha kutaka kumuua!! Kijana! Hebu tuyaache hayo ila kikubwa unatakiwa kutibiwa tena mapema sana iwezekanavyo vinginevyo kuna dalili ambazo naziona sio nzuri kabisa.” Baada ya kusikia hayo maneno, woga ulianza kwisha, nikaanza kumwuliza maswali mganga huyo. Mganga akasema, “Kijana, haitapendeza kujua yote hayo unayoyauliza ila cha msingi inatakiwa uanze tiba mapema iwezekanavyo. Hapo ulipo takribani kila siku usiku huwa unalishwa kichawi nyama za maiti, mijusi, n.k ingawa wewe huwa unajichukulia kuwa ni ndoto tu. Lakini huwa hujiulizi kwa nini unapoamka asubuhi unazisikia nyingine zimekwama kwenye koo na unapokunywa maji mengi ndipo hushuka tumboni! Hapo ulipo kila siku usiku huwa unafanya tendo la ndoa na misukule. Hali hiyo huwa inakushangaza sana, kukutana kimwili na mtu ambaye humwoni mwili wake wala sura yake. Hapo ulipo huwa unapotelewa na pesa unapozitunza kwenye mfuko wako wa suruali, ndani au chumbani unapolala

hata kama ufiche sehemu gani ya siri. Mambo ni mengi sana ila ninaomba niishie hapo lakini jitahidi sana upate tiba mapema hata kama si hapa kwangu."

Yaani rafiki yangu Ipanga, yale yote aliyokuwa akiyaongea huyo mganga, yalikuwa ya kweli, nikawa nashangaa ameyajuaje. Niliendelea kumsumbua aniambie chanzo cha hayo yote ni nini kabla hajaanza tiba kwani nilimwambia anitibu tu. Mwanzo alisita, lakini niliendelea kumhakikishia huku tukisaidiana na jamaa aliyenipeleka hapo kuwa hatutasema kwa mhusika ama wahusika na lengo kubwa ni kujikinga na kuchukua tahadhari nao. Alikubali na kuanza kutuelezea, "Wewe kijana kuna binti umezaa naye na uliishi naye kwa muda ingawa kwa sasa huishi naye. Huyu binti ni mchawi tena mchawi hatari sana. Uliachana naye lakini alikuwa tayari kakutegea bomu ambalo lingelipuka muda wowote. Huo uchawi upo kwenye familia yake kutoka kwa bibi yake kizaa mama, mama yake mwenyewe na hata dada na baadhi ya kaka zake. Ndio maana unaona dada zake wanaolewa na kuachika kwa ajili ya tabia zao za kichawi. Vivyo hivyo mama yao aliachika kwa mume wake kwa ajili ya tabia hizo hizo za kichawi.

Ninakuona unajaribu sana kuhangaika kumchukua huyo mtoto wako na ninamwona ni wa kike. Ni bora ukaachana naye. Umewahi kujiuliza kwa nini kila unapojaribu kumchukua mtoto huyo familia yao nzima inakuja juu! Ni kwa sababu mtoto wako huyo ndiye mjukuu pekee wa kike katika familia hiyo na ndiye kipenzi chao sio tu kibinadamu, bali hata kwenye mambo yao ya kichawi. Kwa taarifa tu fupi, mwanao tayari ameanza kufundishwa mambo ya kichawi na mwalimu wake mkuu ni mama yake ambaye wewe ni mzazi mwenzako. Hivyo huyo mwanao kujinasua na uchawi ni neema ya Mungu tu kwa sababu wako naye huko na kamwe hawawezi kumwacha aje kwako hadi wawe wamekamilisha na kumfanya mchawi kamili. Akishakuwa mchawi kamili ndipo watamruhusu aje kwako hata kwa kumlazimisha ili lengo kuu wamtumie kichawi huyo mtoto wako kukumaliza wewe na familia utakayokuwa nayo. Hujawahi kujiuliza kwa nini huyo mzazi mwenzako anajiamini sana hasa mnapotofautiana na kujibizana! Anajiamini kwa sababu ya ujasiri wake kichawi na vile alivyojiaminisha kuwa amekumaliza kwa kukutengenezea dawa za kichawi. Ninyi vijana, jaribuni sana kuangalia familia za kwenda kuoa ama kuolewa vinginevyo

mnakutana na madhara kama haya. Jaribuni kuzingatia taratibu za kufanya kabla ya kuoa ama kuolewa ama kuzaa kwa lengo la kuja kuishi pamoja baadaye. Mfano mimi, kupitia wazee wangu, walichunguza mji ninaotaka kwenda kuoa kuona kama kuna magonjwa ya kurithi, uchawi, uchoyo, tabia mbaya, n.k. Ona sasa, huna kosa lolote lile, na ninaona hapa jinsi ulivyomhangaikia kwa moyo mwema huyo mzazi mwenzio ikiwemo kumsomesha na kumtafutia kazi nzuri lakini haya ndiyo malipo yake kwako. Lakini kaa ukijua kuwa mchawi fadhila yake ni kukuvuruga akili ama kukuua, ndio maana pamoja na kumsaidia na kuisaidia familia yake kadri ulivyoweza lakini shukrani yake kwako na hata familia yake kwa ujumla ni kukuua. Ninaomba niishie hapo kwani kuna wagonjwa wengine wananisubiri hapo nje. Pia ukumbuke kuwa huwezi kuendelea maishani mwako kwa kuwa kila pesa unayoipata inapitiliza tu bila kufanya jambo lolote la msingi na kukupelekea kuishi kwa madeni kila kukicha."

Ipanga, yote aliyokuwa akiniambia huyo mganga yalikuwa ya kweli kabisa hivyo nikamwambia afanye vyovyote anavyoweza ili nipone. Aliniambia gharama, nikalipa na kuanza

tiba ambayo ilichukua takribani mwezi nikawa nimepona kabisa. Niliamua kukaa mbali sana na huyo mzazi mwenzangu, mtoto wangu pamoja na familia yake kwa ujumla ili kuokoa maisha yangu. Siku moja nikiwa mtaani, nilisikia watu wazima wakiwa wanazungumzia mambo hayo hayo ya kichawi. Mmoja kati yao akawa anadai kuwa kuna kitu kinaitwa jini ambacho ni mlinzi mkuu wa binadamu dhidi ya wachawi. Nilishawishika sana kujua zaidi na ikabidi nisogee karibu ili nisikie zaidi bila wao kujua kuwa nafuatilia mazungumzo yao. Huyo mtu alisifia sana kuhusu ulinzi wa jini akisema kuwa hutolewa kwa mganga. Haraka haraka nikawaza kichwani nipange ratiba ya kuonana na mganga aliyenitibu ili anipe na mimi jini linilinde dhidi ya wachawi. Siku iliyofuata nilikwenda kwa mganga na nikamweleza habari ya ulinzi wa jini dhidi ya wachawi. Mganga akanipa taratibu zote na masharti yake kisha akaniuliza kama ninaridhia. Nilimwambia naridhia kisha akaniambia gharama na nikalipa tayari kwa kukabidhiwa ulinzi wa jini.

Mganga aliniambia nitoke nje ya kilinge kwa muda mchache ili aandae mambo yake. Nilikaa nje kwa muda mchache tu kisha akaniita, niliingia

ndani ya kilinge na kumkuta kashikilia kichupa kidogo kilichozibwa sehemu zote. Alinikabidhi kichupa hicho kisha akaanza kuongea lugha ambayo mimi sikuifahamu. Baada ya kumaliza, aliniuliza ninapoishi iwapo nimepanga ama ni mji wangu. Nikamwambia nimepanga. Akanipa maelekezo kuwa nikatafute sehemu yoyote yenye mti mkubwa, nikifika nikichimbie hicho kichupa chini pembeni ya mti huo. Haraka haraka nilifikiria nikawa nimepata sehemu ya kuupata huo mti kisha nikaondoka kwa utaratibu alionielekeza kwenda kukifukia hicho kichupa. Nilirudi kwangu na kuendelea na shughuli zangu kama kawaida.

Ilipofika usiku, nilisikia sauti ya binti ikitokea pembeni kidogo na nilipokuwa nimejilaza ikiniita jina langu na kunisihi nisiogope kwani amepewa jukumu la kunilinda, baada ya kuniambia hivyo sauti hiyo ikapotea. Niliogopa kidogo ingawa mwanzo mganga aliniambia nitakachokiona wala kukisikia nisiogope. Siku ya pili usiku, muda ule ule nilisikia vyombo vikigongana na harufu ya nyama na wali vilivyoungwa vizuri. Niliamka na kuwasha taa lakini sikuona kitu. Vyombo vyangu vya kupikia vilikuwa kwenye beseni kwa mpangilio ule ule nilivyovipanga. Niliwaza sana,

harufu hiyo inatokea wapi, na hivyo vyombo mbona vyombo vinavyogongana, sivioni. Ghafla ilisikika sauti ya huyo binti ikiniambia kuwa nisiogope kwani anapika chakula chake. Sikuwa na cha kusema, nilikaa kimya huku nikipiga moyo konde na woga wa hapa na pale. Siku iliyofuata tena usiku, nilisikia mazungumzo ya watu zaidi ya wawili. Huku nikiendelea kuduwaa, sauti ikasikika tena ikiniambia nisiogope kwani yupo na wageni wake wamemtembelea. Niliendelea kujipa uvumilivu ili nione hatima yangu juu ya ulinzi nilioutarajia kuupata.

Ile hali ya mazungumzo ya watu wawili ama zaidi pamoja na vyombo kugongana ikiwemo harufu ya vyakula vya aina mbalimbali vilivyopikwa kwa mapishi tofauti tofauti viliendelea kusikikaa kwa siku kadhaa. Baada ya hapo, hiyo hiyo sauti ya binti ikasikika muda ule ule wa usiku ikisema kuwa anataka kujitokeza nimwone ingawa aliendelea kusisitiza nisiogope kwani yeye ni wa kawaida tu. Nilimkubalia kwa shingo upande kisha akajitokeza na kuniambia kuwa atakuwa nami muda wote huku akinilinda. Akaongeza kuwa chochote kile nitakachokitaka nisisite kumweleza lakini siyo suala la

mapenzi.Alisisitiza tena kuwa nisimwambie mtu yeyote yule juu yake kwani nitaharibu kila kitu. Niliendelea kumkubalia huku nikiwa ninajihisi kama nipo ndotoni kwa kile ninachokisikia na kukiona. Niliendelea kuishi maisha hayo mageni kwangu pasipo kujua hatima yangu, kibaya zaidi siku moja nilikuwa nikiwaza mambo yangu wakati wa mchana, binti huyo alijitokeza na kunizuia nisiwaze hayo mambo na nilipomwambia kwa ishara kuwa aondoke watu watamwona, alinijibu kuwa hakuna mtu mwingine wa kumwona isipokuwa yeye mwenyewe!

Tuliendelea na maisha hayo kwa muda mrefu sana akiwa ananiita kaka na mimi nikimwita dada. Alinifahamisha kuwa siku moja atanitoa usiku wa manane twende matembezini ili akanishangaze japo alinitahadharisha nisiogope kwa kila nitakachokiona. Alisisitiza nitazame tu bila kuongea chochote na nitaongea na kuuliza maswali pindi atakaponiruhusu kufanya hivyo. Niliogopa kidogo kuwa anataka kunipeleka wapi usiku huo na kunionesha ama kunifanyia nini hicho ambacho sistahili kuongea wala kuuliza maswali kwa muda huo. Siku hiyo ikafika, akaniambia nijiandae nami nikamjibu kwa woga kuwa nipo tayari kwa safari

ingawa siku hiyo sikula kabisa chakula cha usiku nikiiwazia safari hiyo ya kunishangaza na aina ya mtu ninayekwenda naye. Muda ulipofika akaniambia, "Sasa twende." Nilidhani angefungua mlango tupite twende zetu lakini haikuwa hivyo. Tulipita ukutani na mara tukajikuta tupo nje. Ila kabla hatujatoka nje, nilijiona kama nimejivua kutoka kwenye mwili wangu halisi ambao nilikuwa nautazama kitandani kwangu nilipokuwa nimelala.

Tulianza safari ambayo ilikuwa fupi sana kwani tulipokuwa tunapiga hatua moja tulienda umbali wa kama hatua milioni moja hivi. Njiani humo niliona vitu vingi sana ikiwemo wenzake na huyo binti, wengine alisalimiana nao na wengine tuliwapita tu bila kuwasalimia. Lakini mitaa yote tuliyokuwa tunapita nilikuwa ninaitambua vizuri. Tulikwenda hadi kwenye mtaa anapoishi mwanamke niliyezaa naye mtoto. Tulipofika akaniuliza kama huo mtaa ninaufahamu, nilimjibu kuwa ninaufahamu na ndipo kwao na mzazi mwenzangu na nikamwonyesha nyumba yao. Nilipomwonyesha nyumba akaniambia kwamba nisijali kwani tunaelekea hapo hapo kwenye huo mji ingawa alizidi kusisitiza kuwa nitakayoyaona nikae kimya. Tulifika tukajibanza pembeni kidogo

ya nyumba yao. Kwa macho yangu, nilimwona huyo mzazi mwenzangu pamoja na watu wengine akiwemo mama yake mzazi, baadhi ya dada, kaka na ndugu zake wakiwa uchi nje ya uwanja wa nyumba yao wanafanya mambo yao ya kichawi ikiwemo kunywa damu. Nilishtuka sana kuona hivyo ingawa huyo dada aliendelea kunionyesha ishara kuwa nikae kimya. Baada ya muda mfupi, walikuja fisi kwa kasi ya upepo na kila mmoja wao akapanda fisi wake na kuondoka. Nilipoona hivyo, niliwaza sana kuwa kumbe binti niliyezaa naye mtoto ni mchawi pamoja na familia yake hasa mama yake ambaye huwa ninamwona ni mkarimu na mwenye kushika dini sawa sawa!

Baada ya wao kuondoka nasi tulianza safari ya kurudi nyumbani. Tukiwa njiani tunarudi, tulipita kwenye nyumba moja ya ibada, yule dada akaniambia nimsubiri asali (swali) kwa dakika chache ndipo tuendelee na safari. Nilimsubiri kwa nje, aliingia kusali ingawa hakuwa peke yake kwani wengi kama yeye waliingia na kutoka kwa ajili ya kusali. Baada ya muda kidogo alimaliza kusali kisha tukaendelea na safari kurudi nyumbani. Tukiwa njiani tunarudi aliendelea kunieleza mambo mbalimbali yahusuyu ulimwengu wa

kichawi na jinsi baadhi ya ndugu, marafiki, wafanyakazi na majirani zangu wanavyoshirikiana na mzazi mwenzangu katika mambo ya kichawi. Wamefikia hatua ya kupanga taratibu za kutaka kunipeleka kuzimu ingawa katika hali ya kibinadamu nionekane nimefariki. Kibaya zaidi, huyo mzazi mwenzangu alikuwa akimfundisha mwanangu mambo ya kichawi na mara nyingi alikuwa akimtanguliza mbele kila wanapokwenda kuwanga ama kwenye vikao vyao vya kichawi.

Kadiri siku zilivyokuwa zikienda, nilianza kumzoea dada huyo. Naye alianza kunizoea na ikafikia hatua akaniambia nitafute shughuli yoyote ya kujipatia kipato nifanye kwani muda wote huo alikuwa akinipatia pesa ya matumizi na mahitaji yote niliyokuwa nikihitaji. Aliponiambia hivyo, niliamua kuanzisha kibanda cha kuuza bidhaa ndogo ndogo za matumizi ya nyumbani. Alinipatia pesa nikatengeneza kibanda hicho eneo nilipopanga chumba na baada ya siku chache kilikamilika tayari kwa kupanga bidhaa. Tulipanga siku ya kwenda kununua bidhaa za kibandani na ilipofika tuliongozana naye wakati huo mkononi sikuwa na pesa yoyote ile tofauti na nauli. Nilijiuliza maswali mengi sana jinsi atakavyonipatia pesa ya kulipia

hizo bidhaa za kibandani kwani siku zote pesa huwa ananipatia kupitia kuziweka kwenye kawa iliyopo ndani.

Baada ya kushuka kwenye daladala, alinitangulia mbele hadi kwenye duka mojawapo linaouza bidhaa za jumla na kuniambia niagize bidhaa zote ninazohitaji. Nilitoa karatasi yangu niliyokuwa nimeorodhesha bidhaa kisha nikaanza kuagiza huku sijiamini kwani huyo dada haonekani kwa watu wengine ila mimi tu, atawezaje kutoa pesa ya kulipia bidhaa hizo! Bidhaa zote nilizoziorodhesha mimi zilikamilika akawa ananionyesha nyingine kwa ishara kuwa niziongezee kwenye manunuzi na nikafanya hivyo. Mwuza duka alizifunga bidhaa zetu vizuri kisha akatuitia kijana wa toroli akavipakia kwenye toroli tayari kwa kuanza safari. Wakati tunajiandaa kuanza safari, mwuza duka aliniita na kunipatia risiti ya manunuzi ya bidhaa zote. Muda wote huo, yule dada alikuwa ndani ya duka jirani na alipo mwuza duka huyu kisha akatoka nje na kuniambia kwa ishara kuwa tuondoke. Tuliondoka na mtu wa toroli aliyekuwa amepakia bidhaa zetu hadi nyumbani kwenye kibanda. Tulifika, tukashusha bidhaa kisha dada akaniambia nikachukue pesa

kwenye kawa nimpatie mwenye toroli. Niliichukua pesa ile nilipompatia aliiweka mfukoni kwake bila hata ya kuihesabu kisha akaenda zake. Tulipanga vitu vyote kwenye kibanda na siku iliyofuata nikaanza kuuza.

Siku moja huyo dada aliniambia kuwa angenipeleka kwao nipaone. Nilimwuliza, kwao ni sehemu gani. Alinijibu kuwa ni mbali lakini kuna uwezekano wa kwenda na kurudi siku hiyo hiyo. Nilimwambia kuwa hakuna shaka isipokuwa atanijulisha siku tutakayokwenda. Alinijibu kuwa tutakwenda baada ya siku mbili. Kweli baada ya siku mbili, aliniambia nijiandae tuanze safari ingawa hakunifahamisha muda kamili ambao tulitakiwa kuanza safari. Nilijiandaa kuanzia asubuhi kuwa nitasafiri bila kujali naelekea wapi na kuna mazingira gani huko niendako.

Muda ulizidi kwenda mpaka saa tano usiku hivi ndipo akaniambia nijibadilishe. Yaani mwili niuache kitandani ili tuanze safari kwani huko tuendapo hautakiwi mwili wa kawaida. Nilifanya hivyo kisha tukaanza safari kuelekea kwao. Njiani alinionesha miji na majiji mengi sana makubwa na madogo ndani na nje ya nchi. Mengine nimezoea kuyasikia kwenye vyombo vya habari na mengine

kuyasoma kwenye maandiko mbalimbali. Pia alinionesha majengo makubwa ya hoteli na ofisi mbalimbali ambazo nimezoea kuziona kwenye picha na runinga. Hata hivyo sikuwa na furaha sana moyoni kwa ajili ya kuwaza huko kwao kukoje. Tulifika ufukweni mwa bahari ya Hondu, akaniambia tutapunguza mwendo kidogo tukiwa tunapita juu ya bahari. Nilimwuliza kwa nini tupunguze mwendo. Alinijibu kuwa chini ya bahari kuna makazi ya watu wakubwa. Nilimwuliza tena kuwa watu wakubwa kivipi!. Alinijibu kuwa ni watu wenye vyeo mbalimbali katika jamii yake. Kutokana na mvutano wa nguvu walizonazo tukitembea haraka tutaishiwa nguvu na tutadondoka. Tulianza kutembea taratibu juu ya bahari huku sehemu nyingine akinielekeza nisipite. Tulitembea kidogo tu kisha tukaanza kushuka chini ya bahari mithili ya mtu anavyozama baharini ama ziwani ama mtoni na kupotelea kwenye maji.

Tulipofika chini ya bahari nilianza kushangaa vitu na mambo niliyoyaona kama vile miji mizuri sana na ya kisasa yenye taa za barabarani nzuri zilizopangiliwa vizuri. Tulipita kwenye mitaa ya miji hiyo huku tukielekea nyumbani kwao. Muda wote huo dada alikuwa amejawa na furaha sana

huku akinieleza mambo mbalimbali juu ya huo mji wao ingawa nilikuwa na mawazo sana juu ya hiyo safari. Pia aliniambia kuwa familia yake itafurahi sana kumwona amewaletea mgeni ambaye ni binadamu wa kawaida kwani huwa ni nadra sana binadamu kukubali kwenda huko. Tulifika nyumbani kwao, tukakaribishwa, kisha tukaingia ndani. Tulipofika ndani, tulikaa chini kwani wao hawana viti wala chochote kile sebuleni kwao tofauti na mazulia ya kukalia tu. Nilianza kutambulishwa kwa ndugu, jamaa na marafiki mbalimbali. Baada ya utambulisho huo, niliendelea kushangaa mambo ya huko ikiwemo nyumba yao iliyojengwa kwa dhahabu tupu kuanzia msingi hadi kuezekwa, pamoja na vyombo kama vile sahani na glasi. Kililetwa chakula aina ya pilau nyama ya kuku chenye harufu na ladha nzuri sana. TulileteWa pia juisi nzuri iliyotengenezwa kwa matunda mbalimbali, tukaanza kula na kunywa. Tulipomaliza kula tulikaa kidogo kisha tukaaga na kuanza safari kurudi duniani. Kipindi tunarudi hatukuchukua muda mrefu tukawa tumefika nyumbani kwa sababu tulirudi moja kwa moja tofauti na ilivyokuwa wakati tunakwenda kwao. Alinipitisha maeneo mbalimbali ya mji niyaone. Tulipofika nyumbani tuliingia ndani na

nilipotazama kitandani niliuona mwili wangu umelala vile vile nilivyouacha. Nilijivisha mwili wangu na kurudi katika hali ya kibinadamu.

Kesho yake tukiwa kibandani, nilimwuliza huyo dada maswali mengi sana yakiwemo kuhusu maisha yao huko na chakula chao kikuu. Alinijibu chakula chao kikuu ni damu ya binadamu. Niliogopa sana kusikia hiyo kauli na nikamtaka anifafanulie zaidi. Aliniambia nisiogope kusikia hivyo na ndio uhalisia wenyewe huo. Akasema kuwa kuna kipindi binadamu anaweza kuwa kakaa halafu ghafla akahisi joto ambalo si kali sana, muda huo kuna mwenzetu anakuwa kajibanza jirani yake anamnyonya damu ingawa mwanadamu anakuwa hamwoni. Nilimwuliza ikiwa hii ndio huwa inapelekea sisi kuishiwa damu na kupelekwa hospitalini kuongezewa damu nyingine. Alinijibu kuwa hapana, anayemnyonya damu binadamu hadi kupelekea kuongezewa damu ni mwenzetu ama wenzetu wenye roho mbaya na wakatili na wakati mwingine huwa wanatumiwa na binadamu kwa ajili ya kumpeleka kuzimu ingawa ninyi hujua kama amefariki. Lakini sisi wenye tabia zisizo za kikatili humnyonya binadamu damu kidogo tu kisha huenda kwa mwingine na hatimaye

unatosheka. Ninyi binadamu mwilini mwenu kuna vitu vinavyotengeneza damu na hata kama ikipungua kidogo hujitengenezea tena na kurudi kwenye kiwango chake. Ukimnyonya damu yote itaisha na atakufa, hivyo siku nyingine hutapata tena mtu wa kumnyonya damu kwa ajili ya chakula kwani wote watakufa.

Nilimwuliza tena kama kuna uhusiano kati ya ajali zinazotokea hasa barabarani pamoja na uhitaji wao wa damu. Alinijibu tena kuwa kama alivyoeleza awali kuna wenzao pia wenye roho mbaya kama za binadamu. Kuna walio wazinzi, kuna wakatili n.k Wale wenye roho mbaya ndio mara nyingi hutengeneza ajali ili kupata damu nyingi za watu na wakati mwingine huenda kuzitumia kwa mambo yao ikiwemo kafara za binadamu walio na mrengo huo. Nilimwuliza tena juu ya kafara za binadamu kwamba zikoje na zina uhusiano gani nao. Alinijibu kuwa binadamu walio wengi huwatumia hao wenye roho mbaya kwa ajili ya kufanikisha mambo yao zaidi kiuchumi na kisiasa. Ukiona ajali ambayo imetengenezwa na hao wenzetu, ujue kuna tukio la kumpatia binadamu kitu.Ukubwa wa kitu huendana na wingi wa damu ambapo wingi wa damu ndio ukubwa wa tukio la ajali.

Nilimwuliza tena huyo dada iwapo wanamnyonya damu kila binadamu.Akanijibu, hapana, sio kila binadamu huwa tunamnyonya damu. Kuna binadamu wengine ni watu wenye imani thabiti kwa Mungu ingawa wanaweza kuwa wahudhuriaji wazuri kwenye nyumba za ibada ama la. Huwezi kuthubutu kuwasogelea kwani unaweza kuishiwa nguvu ama kuungua moto." Muda wote huo Ipanga alikuwa yuko kimya akimsikiliza rafiki yake huku mwili wake ukitetemeka na kwa mbali uwoga ukimjia kuhusiana na hilo tukio lililomkuta rafiki yake Masha. Masha aliendelea kumsimulia Ipanga, "usishangae Ipanga, nimepitia mambo mengi sana hadi sasa. Ilifikia hatua nikajiona mimi ni kama jitu tu, utu ukawa umenitoka. Baadaye yule dada alianza kunishawishi sana niwe mpenzi wake. Hilo suala liliniogopesha sana nami nikamwambia siwezi kwani natamani kuoa mwanamke mwenye umbo la binadamu kama mimi. Nilipomweleza hivyo nilidhani atanikasirikia, lakini hakunikasirikia wala kuonesha dalili zozote zile za kukasirika na akawa amenielewa vizuri. Uzuri wa huyo dada alikuwa hanilazimishi kitu kwani kila alichotaka kunifanyia ama mimi nikifanye ni lazima aliniuliza ili niamue mwenyewe.

Kuna siku aliniambia tena twende tukatembee na nilimkubalia ingawa siku hiyo ilikuwa ni muda wa mchana. Tukiwa njiani nilimwona mwanadada mmoja ameumbika sana na nikawa ninamtazama. Huyo dada akaniuliza kuwa mbona nimemtazama sana huyo mwanadada ama nimempenda! Nilimjibu kuwa hata kama nimempenda, sina uwezo wa kumpata. Baada ya kumjibu hivyo alitabasamu kisha akaniuliza tena niseme kama nimempenda ili anikutanishe naye kimwili. Huku nikiwa nashangaa jinsi atakavyonikutanisha naye kimwili wakati hatujui hata anaishi wapi, alichukua mkono wake akaupitisha usoni mwangu kama vile ananipangusa. Akaniambia nimtazame huyo mwanadada, nilipomtazama nikaona umbo lake lote kama alivyozaliwa. Akaniambia tena kuwa amefanya hivyo kwa sababu tayari nimekwishampenda huyo mwanadada na kwamba nijiandae kwani usiku nitakwenda kukutana naye kimwili. Kwa ujinga wangu nilikubali ingawa moyoni nilikuwa na hofu sana. Muda wote huo nilikuwa nazungumza naye lakini tunapopishana na watu ninanyamaza kwani mimi ndiye nilikuwa ninamwona ninayezungumza naye. Baada ya muda nilimwuliza kuwa huyo mwanadada nitakutana naye kimwili tukiwa wapi. Akasema kuwa nisiwe

na wasiwasi wowote ule kwani atanipeleka anapoishi.

Niliendelea kumwuliza kuwa itawezekanaje ilhali kwao hatupajui na wala hatujui kama yuko pekee yake ama kaolewa. Alinijibu kuwa hilo suala nimwachie yeye isipokuwa nijiandae kiakili kuwa usiku nitakwenda kukutana na huyo mwanadada. Baada ya mizunguko yote, jioni tulirudi nyumbani. Niliandaa chakula changu cha usiku nikala na nilipomaliza kula aliniambia nipumzike ila ataniamsha usiku wa manane anipeleke kama alivyo niahidi. Kweli nililala na ilipofika usiku wa manane aliniamsha na kuniambia nijiandae twende. Niliuacha mwili kitandani na kuanza safari nikiwa na mwili mwingine kama ambavyo huwa ninafanya. Tulitembea mpaka kwa huyo dada, tuliingia ndani hadi chumbani kwake. Tulimkuta huyo dada kalala fofofo, dada akaniambia niondoe blanketi, nimvue nguo kisha niendelee na ya kwangu yeye ananisubiri nje. Nilifanya hivyo kisha nikaanza kumchezea chezea na alipoonesha ushirikiano nami kukidhi haja yangu nilitoka nje na kumkuta dada akinisubiri kisha tukaondoka. Tulipofika nyumbani niliuvaa mwili wangu wa kawaida kisha dada akaniambia ni lazima nioge,

nikaenda kuoga kisha nikalala usingizi hadi asubuhi. Baada ya tukio hilo, nikajikuta nimekuwa na tabia ya kutembea na wanawake mbalimbali kwani kila niliyekuwa nikimwona mzuri kwangu basi usiku ilikuwa ni lazima nitembee naye wakati mwingine bila hata kumwambia dada ingawa alikuwa akijua na kukaa kimya.

Siku moja nilimwona mwanamke nikamtamani na nikajiandaa nitembee naye usiku ule. Ilipofika usiku niliondoka bila hata kumfahamisha dada kama nilivyozoea. Nilifika kwao na huyo dada, niliingia ndani kama kawaida ingawa ghafla nilianza kuhisi mwili wangu hauko sawa. Nilijilazimisha nifanye vile ambavyo huwa nafanya, nilishindwa na kuanza kuishiwa nguvu. Punde si punde nilimwona dada na wengine wa aina yake ambao sikuwafahamu wakinishika na kunivuta tutoke nje, tulitoka nje na kukuta hali ya hewa imechafuka sana kwa upepo wenye hewa nzito. Tulifanikiwa kujipenyeza kwenye hilo gharika hadi tukafika nyumbani huku tukiwa tumechoka sana. Dada akaniambia nilale na kwamba tutaongea vizuri kesho yake asubuhi nami nilifanya hivyo huku nikiwa na mawazo lukuki. Ilipofika kesho yake asubuhi, dada aliniambia kuwa familia ama

mtu yeyote yule ambaye ni mcha Mungu ni hatari sana. Ukilazimisha unaweza kuishiwa nguvu ama kuungua na moto. Ndio maana hata wao hawawezi kabisa kumsogelea mtu mcha Mungu ama familia ya wacha Mungu ama majumba yao ya ibada yenye uwepo wa Mungu wa kweli.

Baada ya kunieleza hayo, hatimaye akanishauri kuwa siyo vizuri kuwa mzinifu kiasi hicho na kama sijiwezi kabisa nitafute mwanamke, nioe. Nilimkubalia kisha nikamwuliza iwapo wao pia hujamiiana na binadamu wa kawaida. Alinijibu ndiyo na siyo tu kujamiana bali hata kuoa na kuolewa na kuzaa watoto. Aliponiambia hivyo nikamwuliza tena jinsi wanavyozaliana, aliniambia kuwa huwa pia wanazaa na binadamu wa kawaida lakini wakati fulani ukifika ni lazima waende kuishi kuzimu. Lakini kuna wengine huwa wanakataa kwenda kuishi kuzimu baada ya kufurahishwa na maisha ya hapa ulimwenguni na ndio ambao husikia ama huona mwanamke mzuri lakini ana miguu ya kwato. Nilishangaa sana aliponiambia hivyo na nikamwuliza tena kuwa ni kwa nini naye asiolewe na wenzake. Alinijibu kuwa kuolewa ama kutoolewa ni mapenzi ya mtu binafsi na nafsi yake, wengi wanaogopwa na binadamu wa kawaida kwa

ajili ya mionekano yao pia na masharti wengi wao wanayoyatoa.

Nilimwuliza juu ya masharti wanayoyatoa. Alinijibu kuwa ni usafi wa mwili, mavazi na nyumba ama chumba anapoishi. Pili, hawapendi msongamano wa watu, mfano kama ni chumba hakitakiwi kuingiliwa ama kulala watu tofauti tofauti. Tatu hawependi uongo, kila unapoamka hadi unapolala hufuatilia ratiba yako hasa maongezi na matendo. Mwisho ni masharti ya kawaida mfano vyakula, mavazi, marashi n.k. Maisha yangu na dada huyo yaliendelea kwa muda mrefu sana lakini hatimaye nikaona sina maisha yoyote ninayotarajia kuyaishi huko mbele niendako tofauti na kuwa karibu naye tu. Hivyo nilianza kupanga wazo la kuja kumwambia ili aniache niendelee na maisha yangu.

Siku moja nilipanga nimwambie uhalisia kuwa ninahitaji kuwa huru. Baada ya siku chache, nilimwomba kuwa ningekuwa na mazungumzo naye usiku. Alinijibu kwamba nisijali na hicho nilichotaka kumweleza tayari anakifahamu. Aliongeza kuwa anatarajia kurudi kwao hivi karibuni kwani alikuja kuishi duniani kwa ajili yangu, baada ya kuitwa na yule mganga ili aje

anipe ulinzi. Nilimweleza kuwa ni kweli kabisa kwani ninatakiwa niwe huru. Siku moja usiku nikiwa najiandaa kulala, huyo dada alikuja akakaa kitandani kwangu ambapo haijapata kutokea hata siku moja. Aliniambia kuwa anataka kuondoka na hatutaonana tena kwani anarudi kwao aliponipeleka kipindi kile. Nilimwuliza kwa nini hatutaonana tena wakati huwa mnakuja ulimwenguni na pia wenzake huwa tunaonana nao mara kwa mara. Alinijibu kuwa huko hutoki hivi hivi mpaka upewe ruhusa. Akasema hao niliokuwa ninawaona wapo makundi mawili. Kundi la kwanza ni wale walioitwa kufanya kazi mbalimbali hapa ulimwenguni mfano mmoja wapo ni kazi aliyokuwa anaifanya kwangu ya kunilinda na wachawi.

Kundi la pili ni waliotoroka huko ama walioagizwa kufanya kazi hapa duniani wakalowea kwa kutaka kuwa huru ama kufurahishwa na maisha ya hapa duniani. Hao wanakuwa tayari wametengwa kabisa na hawawezi kurudi huko tena. Aliniambia kuwa kuna nguvu aliniwekea kwa kuwa anapaswa kuzitoa ili niwe binadamu wa kawaida. Alinishika kichwani akawa amezitoa nguvu hizo na baada ya dakika chache tu nikajihisi

mchovu sana mwili mzima. Baada ya kuziondoa nguvu hizo mwilini mwangu alipotea machoni mwangu nikabaki nasikia sauti tu. Mwishoni kabisa aliniambia kwa heri na kwamba uhai wangu sasa upo mikononi mwa Mungu kisha sauti ikapotea.

Baada ya hapo, niliishi maisha ya hofu sana huku nikijiona nipo tofauti sana na binadamu wenzangu na kibaya zaidi nikikumbuka matukio ya kinyama niliyokuwa nikiyafanya. Nilishindwa kulielezea tukio hilo kwa watu kwani nilihofia wangenichukuliaje. Wewe ni mtu pekee ambaye nimekueleza hadi saa. Mwanzoni nilikuwa napata maluweluwe juu ya matendo niliyokuwa nikiyafanya hasa usiku ninapokuwa nimelala lakini kwa sasa yanakwenda yanapungua hasa nilipozidisha nguvu ya maombi." Ipanga akasema, "Pole sana rafiki yangu kwa yaliyokukuta." Masha akajibu, "Ahsante sana rafiki yangu. Yote hayo yalisababishwa na dada niliyezaa naye na nitamchukia na kumlaani mpaka mwisho wa maisha yangu. Nilishauriwa kwenda kwa mganga nikijua kuwa ninakwenda kutibu tatizo kumbe bila kufahamu ndio niliongeza tatizo." Ipanga akamtia moyo, "Usijali kwani hakuna lenye mwanzo likakosa kuwa na mwisho. Tukazane tu

kumwomba Mungu kwani ninadhani hiyo ndio tiba sahihi." Masha akamuunga mkono, "Kweli kabisa Ipanga." Ipanga akamwuliza Masha, "Unajishughulisha na nini ama unatarajia kufanya shughuli gani?" Masha akajibu, "Nilikuwa na kile kibanda cha bidhaa ndogo ndogo za nyumbani lakini alipoondoka yule dada mambo yote yakaharibika ikiwemo kukosa wateja. Hivyo kwa sasa ninafanya kibarua cha kulima ili nipate mtaji wa biashara. Niliamua kuanza maisha upya kabisa."

Baada ya kusikia neno hilo la kibarua cha kulima Ipanga alijiinamia huku ameshika kichwa chake hadi machozi yakamdondoka. Aliwaza jinsi alivyomfahamu vizuri rafiki yake na jinsi alivyokuwa na uwezo mkubwa wa kiakili darasani. Hivi sasa ameharibikiwa kimaisha kiasi cha kuwa kama mtoto wa mtaani na kibaya zaidi kufanya vibarua, na hasa kibarua cha kulima anachokifanya sasa!! Baada ya dakika kadhaa, Ipanga alifuta machozi kisha akamwuliza Masha, "Ni kiasi gani cha pesa unahitaji kama mtaji na ni biashara gani unatarajia kufanya?" Masha akajibu, "Ninahitaji elfu hamsini ingawa kwa sasa kupitia vibarua nilivyokwishafanya nimetunza elfu tano. Kazi

ninayotarajia kufanya ni kilimo cha mboga mboga na pilipili. Nilikwenda kuuliza bei ya mbegu nikaambiwa jumla ni shilingi elfu hamsini." Ipanga akasema, "Basi usijali rafiki yangu, nitakupatia kiasi hicho cha pesa kilichobaki ili uanzishe kilimo chako mwenyewe uachane na kazi za kulipwa kwa kutwa." Masha akasema, "Ninashukuru sana rafiki yangu, isipokuwa ninaomba nikamalizie kuandaa shamba la tajiri mmoja. Tulikuwa tumekwishaelewana nimlimie kwa elfu moja na kesho kutwa nitamalizia." Ipanga akasema, "Sawa nimekuelewa, hakuna shaka kabisa ila ungekuwa hujalianza ungesitisha. Sehemu gani unatarajia sasa kuanzisha hilo shamba la mboga mboga na pilipili?" Masha akajibu, "Kuna mzee mmoja nilipokuwa ninasomea, alinipatia shamba na kuniambia nilitumie niwezavyo ila nisipande mazao ya kudumu. Huyu mzee nilikuwa nawasaidia watoto wake kimasomo na wote walifaulu na sasa wanasoma elimu ya juu." Ipanga akasema, "Sawa Masha, nimekuelewa." Masha akauliza, "Umepata wapi pesa kiasi kwamba unataka kunisaidia? Ama mzee amekupatia pesa nyingi ya ziada baada ya kujiunga na chuo?" Ipanga akajibu, "Hapana Masha. Siku hizi baba hayuko kama tulivyokuwa awali. Amekuwa ni mtu

wa kunifokea tu kila mara na imefikia hatua hata ninashindwa kumwambia mambo yangu ama matatizo yangu. Pesa hizi nilizipata kwa kufanya kazi katika kiwanda cha soda baada ya kuhitimu elimu ya sekondari. Nilitunza mshahara wangu na nyingine nilipewa kama zawadi kwa jinsi nilivyofanya nao kazi vizuri." Masha akampongeza, "Hongera sana Ipanga na Mungu aendelee kukusimamia." Baada ya mazungumzo marefu, Masha na Ipanga walirudi chuoni na walipofika chuoni, Masha aliaga na kuondoka kwani majira ya jioni yalikuwa yamekaribia. Ipanga alimruhusu Masha kuondoka ila akamwambia wakutane mjini baada ya siku tatu ili akampatie kile kiasi cha pesa alichoahidi kumpatia. Waliagana kisha Masha akaondoka.

Baada ya siku tatu, Ipanga na Masha walikutana mjini kisha wakaingia ndani ya benki ambapo Ipanga alitoa pesa kiasi cha shilingi elfu hamsini na kumpatia Masha. Masha akasema, "Kwa sasa ninahitaji elfu arobaini na nne tu." Ipanga akamwambia, "Hapana Masha, hizo elfu sita ulizonazo zitakusaidia kwa matumizi mengine." Masha akasema, "Basi sawa, ninashukuru sana Ipanga." Ipanga akasema, "Wala usijali rafiki

yangu, Mungu akutangulie na ipo siku nitakuja kukutembelea na kukusaidia pia kwani mara nyingine siku za mwisho wa juma huwa sina vipindi chuoni." Masha akasema, "Karibu sana Ipanga na nitafurahi kukuona huko." Walitoka ndani ya benki kisha wakaagana na kila mmoja akaenda zake.

Baada ya siku chache, Masha alianza shughuli yake ya kilimo cha mboga mboga na pilipili. Alipambana kulitunza shamba na baada ya wiki kadhaa vikastawi vizuri tayari kwa kuvunwa. Alianza kutafuta wateja sehemu mbalimbali akisaidiwa na mzee aliyempatia shamba pamoja na Ipanga. Walifanikiwa kupata wateja wengi kutoka sehemu mbalimbali za miji na vijiji na kuuza mboga mboga na pilipili kwa jumla na reja reja. Masha alipata kiasi kikubwa sana cha pesa kupitia kilimo hicho. Ipanga alipofika mwaka wa pili chuoni, pesa ya kuendelea na masomo chuoni ilikosekana kwani ilifikia hatua baba yake akasitisha kumpatia pesa kutokana na biashara yake ya uvuvi kufilisika. Kitendo hicho kilimsononesha sana Ipanga. Siku moja akiwa anamsaidia rafiki yake Masha kuvuna pilipili, alijikuta anadondokwa na machozi. Masha alishtuka kisha akamwuliza, "Ipanga, una tatizo

gani? Nimekuona unafuta machozi kwa mkono." Ipanga akajibu, "Ni kuhusu mambo ya chuoni." Masha akauliza, "Chuoni kumetokea nini?" Ipanga akajibu, "Kesho kutwa tunaanza mitihani ya kumaliza muhula huu wa pili. Tumetangaziwa kuwa ambao hatujamaliza kulipa ada hatutaruhusiwa kufanya mtihani na kesho ndio mwisho wa kulipa na hadi sasa sina uhakika wa kupata pesa. Jana nimepokea ujumbe kutoka kijijini kwa wazazi kuwa wamekosa kabisa pesa." Masha akamkatiza, "Kabla hujaendelea zaidi kunieleza, ni kiasi gani cha pesa kinachohitajika na mbona hukunijulisha suala hilo?" Ipanga akajibu, "Wewe pia bado unapambana na maisha ili yakae sawa. Siyo vizuri kukuingizia habari zinazohusu pesa na hasa kama hii ya ada." Masha akasisitiza, "Hapana Ipanga, niambie ni kiasi gani!" Ipanga akajibu, "Kwa sasa ninadaiwa laki nne, ndio iliyobaki." Masha akasema, "Twende kwanza nyumbani nikakupatie kiasi hicho cha pesa ukalipe kisha urudi." Ipanga akamshukuru kwa kusema, "Sawa, ninakushukuru sana Masha." Wote walinawa mikono na kuelekea alipopanga Masha ingawa hapakuwa mbali sana kutoka shambani kwake.

Walipofika waliingia ndani kisha Masha akachukua hicho kiasi cha pesa na kumpatia Ipanga. Ipanga alipoaga, Masha akamwongezea kiasi kingine cha pesa kwa ajili ya nauli ya kwenda na kurudi. Ipanga alipanda gari akaelekea benki kulipa ada kisha akaelekea chuoni kupeleka risiti ya malipo. Alipokamilisha alirudi tena kwa Masha na kumkuta akiwa shambani na wateja wakinunua bamia. Ipanga alimsaidia Masha kuvuna pilipili kwa ajili ya wateja na ilipofika jioni akaondoka kurudi chuoni. Ipanga aliendelea kumsaidia rafiki yake Masha katika shughuli za kilimo kila mara apatapo wasaa hasa kipindi cha mwisho wa juma ama kipindi cha mapumziko. Pia aliendelea kumtafutia masoko mbalimbali ya mboga mboga na pilipili.

Sura ya Tisa

Masha aliendelea kumlipia ada rafiki yake Ipanga hadi alipohitimu chuo. Baada ya Ipanga kuhitimu chuo alianza jitihada za kutafuta kazi ya kuajiriwa huku akiendelea kumsaidia rafiki yake Masha shughuli za shambani. Alitafuta kazi kwa muda mrefu sana huku akitembelea ofisi mbalimbali bila mafanikio. Siku moja jioni baada ya kumaliza shughuli zao za shamba, Masha alimwambia rafiki yake, "Ipanga, ni muda sasa unatafuta kazi! Pia ulinieleza kuwa ile kazi uliyokuwa ukifanya kiwandani na kuahidiwa kuwa watakuajiri baada ya kuhitimu chuo, kumetokea changamoto. Uliniambia kwamba yule bosi alihamishwa ghafla na sasa uongozi wa bosi aliyepo ambaye ni mwenyeji amejaa ukabila katika utumishi. Hajali utendaji kazi wa mtu na ndio maana ameshindwa kukuajiri kwani wewe si wa kabila lake. Lakini ninafahamu maana ya kazi kuwa ni shughuli yoyote ile iliyo halali kwa mujibu wa katiba yetu ya nchi inayoweza kukuingizia kipato. Kwa muda ambao umeanza kutafuta kazi hadi sasa, unaona ni kiasi gani cha pesa tumekwishapata. Fikiria kuhusu muda huo unaotoka ama kusafiri kwenda kutafuta kazi. Tungekuwa pamoja hapa shambani ni kiasi

gani cha pesa tungekiongezea! Sisemi unafanya vibaya kutafuta kazi ila namaanisha uwezo wa kipato kwa kazi yetu hii, ni ule ule ama hata zaidi ya hiyo kazi ambayo ungeipata."

Ipanga alimtazama Masha usoni kwa makini kisha akajiinamia kwa sekunde kadhaa huku akiwaza maisha yake yote zikiwemo safari anazozifanya kwenda kutafuta kazi. Masha amekuwa akimpa pesa ya nauli pamoja na matumizi yote ikiwemo malazi ambapo hiyo pesa inatokana na kuuza mboga mboga pamoja na pilipili hapo shambani. Masha aliendelea kumweleza, "Ni vema sasa tukashirikiana katika shughuli hizi za shamba na ikiwezekana tuongeze mashamba pamoja na vitendea kazi. Ipanga akasema, "Nimekuelewa Masha na ninakubaliana nawe kwa hilo wazo lako na kuanzia sasa tutashirikiana katika shughuli hii ya kilimo." Kuanzia hapo, Masha na Ipanga walishirikiana katika shughuli zao za kilimo. Walifanya kazi kwa ushirikiano mzuri hadi kufikia hatua ya kuongeza mashamba na aina mbalimbali za mboga mboga pamoja na pilipili na hatimaye kujipatia pesa nyingi sana. Hii ilitokana na kuuza mazao yao sehemu mbalimbali ikiwemo maofisini, mashuleni hasa

shule za bweni, masokoni, mahotelini na kwa wateja binafsi.

Baada ya maisha ya Ipanga na Masha kiuchumi kuzidi kuimarika, siku moja Ipanga alimwambia rafiki yake, “Masha, kwa sasa tunazidi kukusanya pesa nyingi sana. Unaonaje tukitafuta kiwanja mjini tukakinunua ili tuweze kujenga duka kubwa sana la kuuza bidhaa zetu tu. Badala ya wateja wetu kuja kutufuata huku pembeni ya mji, waje moja kwa moja kwenye duka letu. Pia tuanzishe ufugaji wa kuku wa kienyeji, tuwe tunauza nyama ya kuku na mayai pia. Baada ya hapo, tuanze mpango wa kupaki bidhaa zetu na kuziuza nje ya nchi.” Masha akamwunga mkono, “Ipanga, hayo ni mawazo mazuri kweli, itawezekana kweli kuuza nje ya nchi?” Ipanga akamjibu, “Niamini Masha. Hakuna kinachoshindikana mbele ya Mungu wetu aishiye juu mbinguni. Tutazitangaza bidhaa zetu kwenye mitandao mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Mungu atatusaidia na tutapata wateja kila mahali. Pia tutatengeneza fursa ya ajira kwa vijana ambao hawana ajira na tutakuwa tunapata thawabu kwa Mungu pia.” Masha akasema, “Nimekuelewa vema Ipanga, ninakuomba ushughulike tupate kwanza kiwanja mjini ili tuanzishe ujenzi.” Ipanga akasema,

“Hakuna shaka Masha, nitaanza hili zoezi kesho jioni baada ya kazi.” Kesho yake jioni Ipanga alikwenda mjini kutafuta kiwanja ingawa hakufanikiwa kukipata.

Alijiandaa kurudi nyumbani kwao, lakini kabla hajaanza safari ya kurudi, alionana na mtu anayefahamiana naye. Akamshirikisha azma yake ya kupata kiwanja kikubwa mjini. Mtu huyo alimwahidi kuwa atamfanyia kazi hiyo na kwamba ampe siku mbili. Akamtaka arudi tena mjini siku ya tatu kujua alipofikia. Siku ya tatu Ipanga alirudi tena mjini kama alivyokuwa ameahidiana na yule jamaa. Alipofika mjini alimkuta huyo jamaa ambaye alimjulisha kuwa bado hajapata kiwanja cha bei nzuri kwani alichopata kilikuwa na bei ya juu sana hivyo hataweza kukimudu. Jamaa alimjibu hivyo kwa kuwa mwanzoni Ipanga kumwambia anajishughulisha na kilimo cha mboga mboga. Ipanga akamwuliza, “Kwani hicho ulichokipata kiko sehemu gani?” Jamaa akajibu, “Kipo katikati kabisa ya mji, lakini hicho kinawafaa matajiri. Ndio wenye uwezo wa kukinunua. Wewe hutakiweza rafiki yangu.” Ipanga akamwuliza tena, “Tunaweza kwenda ili nikione?” Jamaa aliona kama anamsumbua lakini hakutaka kumwonesha Ipanga

kuwa anamsumbua kwani alijua hataweza kumudu bei ya hicho kiwanja. Akajibu kwa shingo upande, “Sawa, twende ukakione.”

Huyo jamaa na Ipanga waliongozana kuelekea kwenye kiwanja ingawa jamaa alikuwa hajamtamjia Ipanga bei ya kiwanja hicho. Walipofika Ipanga akawa amekipenda sana kwani kipo barabara kuu na pia pande zake zote tatu kuna nyumba za ghorofa likiwemo jengo la benki. Ipanga akamwuliza huyo jamaa, “Kiwanja hiki kinauzwa bei gani?” Jamaa akajibu, “Mwenye eneo alitamka milioni mia moja.” Ipanga akauliza, “Unaweza kufahamu kwa nini anakiuza kiwanja hiki?” Jamaa akajibu, “Mmiliki wa kiwanja ni mzee fulani. Anakiuza ili arudi kwao kwani sio mwenyeji wa taifa hili.” Ipanga, “Kwa sasa anaishi wapi ili kama kuna uwezekano twende nionane naye kabisa ili nijue bei ya mwisho?” Baada ya kusikia kauli hiyo kutoka kwa Ipanga, jamaa akashangaa na kuamua kumpatia ushirikiano wa kutosha. Jamaa akajibu, “Anaishi hapo mtaa wa saba tu, tunaweza kwenda ili ukaonane naye.” Ipanga akakubali, “Sawa, twende tukaonane naye.” Walitembea kuelekea mtaa wa saba kuonana na mzee huyo.

Walipofika walimkuta mzee huyo amepumzika nje kibarazani, wakamsalimia. Mzee aliwakaribisha vizuri kwani alimfahamu yule jamaa. Hawakutaka kupoteza muda, yule jamaa akamwambia mzee madhumuni ya kufika kwake, na kwamba mhitaji wa kiwanja hicho ni huyo waliyekuja naye, yaani, Ipanga. Mzee akasema, "Karibu sana kijana na ninadhani huyu mheshimiwa amekwisha kukutajia gharama halisi." Ipanga akajibu, "Ndiyo mzee, ninajua hiyo ni gharama ya mwanzo kabla ya mazungumzo. Sasa ninaomba uniambie punguzo lako hasa, ni shilingi ngapi!" Muda wote huo jamaa alizidi kumshangaa Ipanga na kilimo chake cha mboga mboga kutaka kununua hicho kiwanja. Hakuamini kuwa kilimo hicho tu ndicho kinachoweza kumfanya Ipanga kuwa na pesa nyingi kiasi hicho. Aliamini, anaweza kuwa anafanya kazi migodini kwenye pesa nyingi na kwamba habari ya kilimo cha mboga mboga ilikuwa si ya kweli. Mzee akasema, "Kijana, mimi nimekwambia bei yangu, labda nikusikilize wewe." Ipanga akasema, "Mzee wangu, naona muda umekwenda sana na giza linakaribia. Pesa niliyo nayo ni milioni hamsini tu."

Mzee alitabasamu kidogo kisha akamwambia, “Kijana, ningekuwa ninakiuza kwa pesa hiyo usingekikuta. Bei ya mwisho ni milioni tisini na tano, chini ya hapo labda uangalie sehemu nyingine.” Ipanga akamjibu, “Sawa mzee nimekuelewa vizuri, ninaomba kesho nije na mwenzangu tujadiliane zaidi ingawa naamini bado unaweza kutupunguzia tena kidogo sisi wanao na ukizingatia ndio tunaanza maisha hivyo.” Mzee alitabasamu tena kisha akasema, “Ninyi njooni tu hiyo kesho tutaona nini cha kufanya.” Ipanga na jamaa waliaga kisha wakaondoka. Wakiwa njiani, Ipanga akamwambia jamaa, “Ninaomba tuonane tena kesho jioni ili twende kwa huyo mzee kwa mara nyingine. Nitakuja na mwenzangu na ninaomba tukupitie hapo hapo nilipokukuta leo. Sawa?” Jamaa akajibu “Hakuna shaka Ipanga, mtanikuta nikiwasubiri.”

Sura ya Kumi

Ipanga aliporudi alimweleza Masha jinsi kilivyo pamoja na maelezo kutoka kwa mzee mwenye kiwanja. Masha akasema, “Kusema kweli mazingira ni mazuri sana kwani kiwanja kipo mjini kabisa na mbele yake imepita barabara kubwa ya lami. Upande wake wa kushoto kuna jengo la benki na tayari benki hiyo inafanya kazi. Unashauri nini ndugu yangu juu ya kukilipia?” Ipanga akasema, “Mimi ninashauri tukinunue, lakini kabla ya kufikia mwafaka kwamba tukinunue inabidi kesho twende kwanza nawe ili ukakione.” Masha akasema, “Hakuna shaka, kesho asubuhi twende mara moja tukakione wote kisha tukubaliane nini cha kufanya.” Ipanga akaitikia, “Hakuna shaka kabisa.” Kesho yake asubuhi walikwenda mjini kukiona kiwanja huku wakiongozana na jamaa aliyempeleka Ipanga. Walipokiona kwa pamoja wakakubaliana kukinunua. Walikamilisha taratibu zote za manunuzi kwa gharama ya shilingi milioni tisini. Baada ya siku chache walianza ujenzi wa duka kubwa la kuuza mazao yao ikiwemo mbogamboga. Walipata mafanikio makubwa sana yaliyowapelekea kusaidia watu mbalimbali wenye uhitaji ikiwemo wazazi wao, ndugu, jamaa na

marafiki zao. Pia waliajiri wafanyakazi wengi hasa vijana wasio na ajira ili kuwasaidia kazi za shambani na dukani maana walianza kuzidiwa na kazi.

Siku moja Kuchi akiwa mjini na aliamua kupita dukani kwa akina Ipanga na Masha ili kuona jinsi ofisi yao inavyofanya kazi kukiwa na wateja wengi sana. Aliporudi nyumbani ilibidi awashirikishe ndugu zake juu ya alichokiona kwenye ofisi hiyo. Kuchi akaanza kwa kusema, "Yaani leo nina hasira sana mpaka ninatamani kupasuka kwa ajili ya huyo mshenzi. Siku zote nilikuwa nikiambiwa lakini leo nimejionea kwa macho yangu mwenyewe." Gufa akauliza, "Ni nani huyo dada?" Kuchi akajibu, "Huyu Ipanga! Leo, kipindi ninatoka safari ikabidi nipite mjini kwenye duka lake. Niliyoyaona! Nimeshikwa na hasira ambayo toka nizaliwe sijawahi! Jengo la kifahari lenye duka kubwa sana la mboga mboga ndani pamoja na nafaka mbalimbali."

Nzile akasema, "Dada nawe huwa ni msahaulifu tu. Ninakumbuka siku moja kuna kijana wa jirani yetu nilionana naye akatwambia kwamba ameona duka la Ipanga likitangazwa kwenye runinga ya wananchi kuwa wanauza mboga mboga, nafaka na

matunda ya aina zote. Pia akatwambia kuwa ni duka zuri sana na lenye ofisi nzuri ndani yake. Kibaya zaidi hizo mboga mboga, nafaka na matunda anaviuza ndani na nje ya nchi yetu. Licha ya hayo, gari analotembelea Ipanga ni yale magari ya kifahari." Gufa akaongeza, "Nyumba anayoishi yeye ni nyumba kama zile za wafalme. Kijijini kwa wazazi wake penyewe kapatengeneza kama uzunguni na kibaya zaidi anasaidia sana watu mbalimbali wenye uhitaji ikiwemo kuwasomesha watoto kutoka katika familia zisizojimudu kiuchumi." Kuchi akasema, "Hayo yote mnayoyasema nilikuwa nikiyasikia ila sikuweza kufikiria kuwa amefanya mambo makubwa kiasi hicho. Maana pamoja na kila aina ya dawa na mikosi tuliyomtupia leo ndiyo nimeamini na ndio maana ninawaambieni nina hasira ambayo sijawahi kuwa nayo tangu nizaliwe."

Gufa akaendelea, "Kwa kweli tumetumia dawa zenye kugharimu pesa nyingi sana kwa huyu manaharamu na wazazi wake hasa mama yake. Lakini matokeo yake tunaambulia kufedheheka sana kwetu sisi na jamii nzima inayotuzunguka. Yaani hali hii inakatisha tamaa sana kwa sababu hizo gharama tulizokwisha tumia kama

tungejengea nyumba tu, labda tungekuwa na nyumba zaidi ya mbili lakini matokeo yake tunaambulia aibu na kuendelea kuwa maskini." Kuchi akadakia, "Hebu ninyi tulieni. Huu sio wakati wa kuendelea kujilaumu. Sasa ninaweza kusema hivi ,hiyo kazi ya huyo mshenzi, ninyi pumzikeni. Niachieni mimi. Nitahakikisha inajulikana mbichi na mbivu. Nimekuja na toleo jipya la dawa ya radi, ninaahidi kumkausha kabisa kwa kutumia radi kwani naona nguvu nyingine zimeshindikana." Nzile akaingilia mazungumzo na kusema, "Bora umejiongeza dada yetu. Tumechoka kusikia hilo jina la huyo mshenzi na sifa kede kede anazopewa kutoka kwa watu mbalimbali." Gufa akaongeza, "Mimi ndio nimemchoka kabisaa, nasubiri kwenda kuona tu maiti yake kwa jinsi ilivyoharibika kwa umeme wa radi."

Kuchi akasema, "Mimi naona hata kunisemesha hapa mnanicheleweshea muda wangu wa kuitengeneza hii radi. Niacheni niingie chumbani nishughulike na hili kwanza." Kuchi aliingia chumbani kwao ambapo kumehifadhiwa vifaa vya kichawi na madawa mbalimbali akaanza kutengeneza radi kwa ajili ya kumpiga Ipanga siku ya kesho yake. Kuchi alikamilisha kutengeneza radi

na akasubiri ili kesho yake aitume kwenda kumwua Ipanga. Kesho yake muda ukafika wa kwenda kuituma. Ingawa hali ya hewa ya siku hiyo ilikuwa ni jua kali, lakini ghafla wingu dogo lilitanda na mvua kiasi ikaanza kunyesha. Dakika chache tu zilipopita toka mvua ianze kunyesha, Kuchi akiwa kwenye chumba chao chenye vitu vya kichawi zikiwemo dawa aliachilia radi. Radi ilisafiri kwenda kwa Ipanga na sekunde chache ikarudi na kupiga nyumbani kwa akina Kuchi. Iliua mifugo yote wakiwemo mbuzi, paka, bata, kuku na mayai yote kwenye mabanda yalipasukapasuka. Kuchi alijiuliza mambo mengi sana ikabidi awashirikishe wadogo zake ambao pia walishangaa tukio hilo kwani lilikuwa geni kwao. Iliwachukua siku kadhaa wakitafakari hilo tukio na huku wakizidi kushikwa hasira kwa nini radi haikumpiga mtu waliemlenga.

Baada ya tafakari yao, waliamua kuwa wote kwa pamoja watamfuata Ipanga kichawi usiku ili wamwue kabisa. Waliandaa dawa zao zote za kichawi ambazo ni kali sana kisha wakapanga siku ya kwenda kumywesha kichawi ili baada ya siku chache tu atapike damu na kupoteza maisha. Siku ilipowadia walifunga safari usiku wa manane huku

wakiongozwa na mkubwa wao Kuchi hadi kwenye nyumba ya Ipanga. Walianza taratibu zao za kichawi ili waingie ndani kwenye nyumba ya Ipanga ila ghafla waliishiwa nguvu na kupoteza mwelekeo baada ya mwanga mkali kutoka juu kuwamulika. Punde si punde, walijikuta wapo chini ya miti wakigalagala. Wachawi wenzao walifika kuwapa msaada wa kuwafikisha nyumbani kwao. Hali hiyo iliwapelekea kuugua maradhi mbalimbali kwa muda mrefu bila pasipo kupata nafuu. Kadri siku zilivyozidi kusonga ndivyo hali ya Kuchi na ndugu zake ilivyozidi kuwa mbaya wakawa ni watu wa kulala kitandani tu muda wote.

Siku moja, Kuchi alimwambia jirani yake aliyekuwa akipita mara kwa mara kuwajulia hali, “Jirani, simu yangu ina muda mrefu sijaichaji. Ninaomba ukanichajie uniletee kuna mtu ninahitaji kuzungumza naye.” Jirani akasema, “Jirani nawe, sasa hilo jicho moja linaloona ndilo linakupa hamasa ya kuongea na simu?” Kuchi akasema, “Yaani, nalo naona linakaribia kutoona kwani kuna muda linapoteza nguvu ya kuona.” Jirani akamtia moyo, “Usijali mwaya jirani yangu, utapona tu hayo macho.” Kuchi akasema, “Tunashukuru sana.

Haya, wewe nisikucheleweshe. Kanichajie dakika chache tu uniletee." Jirani akaitikia, "Sawa jirani, hakuna shaka." Jirani alitoka na kuelekea kwake kuchaji simu ya Kuchi kisha baada ya dakika chache akawa amemletea simu. Jirani akasema, "Haya jirani, hii hapa simu." Kuchi akamwambia, "Nitafutie jina la Ipanga kisha uipige niongee naye." Jirani alilitafuta jina kisha akapiga simu . Ilipoanza kuita akampatia Kuchi.

Ipanga akiwa ofisini kwake aliona simu ikiita kwa namba ngeni akaipokea. Alipoipokea, ikasikika sauti ya mwanamke mtu mzima ikisema, "Ipanga mwanangu, samahani, ninaomba nikuone kwani nina shida sana na wewe." Ipanga aliitambua sauti kuwa ni ndugu wa baba yake aitwae Kuchi kisha akaamua kumjibu, "Hakuna shaka, mimi mwenyewe nitakuja na nitakufahamisha siku ya kuja." Kuchi akamsihi, "Ipanga mwanangu, ni dharura, hivyo ninaomba usichukue siku nyingi kuja." Ipanga akajibu, "Sawa, nitakufahamisha." Kuchi akasema, "Ahsante sana mwanangu. Hiyo ni namba yangu, utaiweka kwenye simu yako." Ipanga akaitikia kwa kusema, sawa kisha akakata simu. Baada ya kukata simu, alijiuliza sana maovu aliyofanyiwa na Kuchi pamoja na wadogo zake na

kujikuta ghafla anapata hasira. Hasira zake hazikuishia hapo, ilibidi aende kwenye ofisi ya Masha iliyomo humo humo ndani ya duka lao na kuanza kumsimulia Masha. Masha ,naye baada ya kuelezwa hivyo alishangaa sana na kuona ni jambo la ajabu sana kutokana na yale mambo yote maovu aliyofanyiwa na hao ndugu wa baba yake.

Sura ya Kumi na Moja

Baada ya majadiliano mafupi Ipanga akasema, “Kwa kweli Masha, siwezi kuonana naye kwani ninamuogopa na pia nina hasira naye. Asithubutu tena kunipigia simu kwani sitaipokea.” Ipanga alihitimisha kwa kusema kuwa hataki uhusiano wala ukaribu wowote ule toka kwao kisha akarudi ofisini kwake kuendelea na kazi aliyokuwa akiifanya. Baada ya siku chache Ipanga akiwa nyumbani usiku aliona ndege aina ya kasuku sebuleni. Alishangaa sana kumwona ndege huyo asijue ametoka wapi. Wakati akiendelea kujiuliza, ndege huyo alitoa sauti nzito na kumwambia, “Ipanga hujambo?” Ipanga alisita kidogo kujibu huku akitetemeka kwa hofu.

Yule ndege aliendelea, “Usiogope Ipanga, ni mimi Amani. Ninajua umezoea kuniona katika umbo la mamba.” Baada ya kusikia hivyo, Ipanga akapata ahueni. Kasuku akaendelea, “Kwanza ninaomba uketi kisha tuzungumze vizuri.” Ipanga akaketi kwenye kochi na kuanza kusikiliza. Kasuku akamwuliza, “Habari ya miaka mingi Ipanga?” Baada ya Ipanga kugundua kuwa ni yule mamba, ghafla alipata ujasiri na kuanza kumjibu. Ipanga akajibu, “Ni nzuri sana. Habari ya huko pia?”

Kasuku akajibu, “Mungu ni mwema sana. Ninafurahi kuona unaendelea vizuri kiafya na kimaendeleo wewe pamoja na rafiki yako Masha.” Ipanga akamshukuru, akisema “Ahsante sana.” Kasuku akaendelea, “Niliahidi hatutaonana tena lakini imebidi nije nionane nawe kwa jambo moja tu. Ulipigiwa simu na ndugu wa baba yako kuwa anahitaji sana kuonana na wewe. Lakini huna utayari kabisa wa kuonana naye. Hilo ni jambo jema kwa mtu yeyote yule mwenye akili timamu na mwenye moyo wa nyama. Ila unaamini kuwa binadamu hubadilika?” Ipanga akajibu, “Ndiyo! Kabisa! Ninaamini kuwa binadamu hubadilika lakini siyo yule na wadogo zake.” Kasuku akauliza, “Utajuaje kuwa binadamu kabadilika kutoka kwenye uovu kwenda kwenye wema ama kutoka kwenye wema kwenda kwenye uovu?” Ipanga akajibu, “Mara nyingi matendo yake na kauli imtokayo kinywani ndio huthibitisha kuwa kabadilika.”

Kasuku akasema, “Umenena vema Ipanga. Matendo yake ya kichawi ni vigumu kuyapima ila maneno yatakayomtoka kinywani mwake ndiyo utakayoyapima. Sasa ipo hivi. Huyo Kuchi, baada ya kuhangaika huku na kule ili akupeleke kuzimu

ama wazazi wako, amejikuta inashindikana na mwisho wake yeye mwenyewe ndiye aliyekuwa anaumia. Lakini pia baada ya kuwafuatilia zaidi akagundua kuwa mnalindwa na nguvu kubwa sana za Kimungu. Alichokitarajia kimekwenda tofauti. Hapo alipo anaona aibu sana juu yako na wazazi wako. Hivyo shida yake kubwa ya kuonana na wewe ni kwamba anataka akuombe msamaha kwa yale yote aliyokutendea. Baada ya kukuomba wewe msamaha, endapo atapata nguvu, atafunga safari tena kwenda kijijini kwa wazazi wako ili kuwaomba msamaha pia. Ili kuonyesha msamaha atakao uomba unatoka moyoni mwake, atataja kila aina ya kosa na matendo aliyowafanyia. Hivyo nimejitokeza kwako kukwambia kuwa usiogope. Nenda kaonane naye ukapate baraka za msamaha wake na pia za wadogo zake kupitia kwake kwani wadogo zake kwa sasa hawajiwezi kabisa." Ipanga akasema, "Uliwahi kuniambia kuwa mtu mchawi ni vigumu kuuacha. Hivyo simwamini kabisa kuwa ameacha uchawi na amekuwa na roho nzuri kwa sasa."

Kasuku akaendelea, "Ipanga, kwa Mungu hakuna kinachoshindikana na pia humpokea na kumsamehe kila mmoja pindi anapoamua kukiri,

kutubu dhambi zake na kumrejea yeye aliye mkuu wa kila kitu." Ipanga akasema, "Sawa nimekuelewa. Pia nitamwuliza kwa nini alikuwa ananisingizia mambo maovu kiasi hicho yakiwemo wizi, uvutaji bangi na mengine mengi tu." Kasuku akasema, "Hakuna shaka Ipanga, ila kabla hujamwuliza yote hayo yeye atakuwa wa kwanza kukueleza sababu za kukufanyia hivyo. Kikubwa, nenda na ikiwezekana nenda kesho ukamsikilize na wala usiogope." Ipanga akasema, "Sawa nimekuelewa, nitakwenda kumwona kesho." Kasuku akasema, "Nimefurahi kusikia hivyo. Kama hakuna jambo jipya, mimi nikuage, niondoke." Ipanga akasema, "Kwa kweli hakuna jipya." Kasuku, "Ninajua huna jambo jipya kwa sababu akili yako yote iko kwa Kuchi. Niendelee kukusihi, umefikia hapo ulipo kupitia maombi na sala kwa Mungu aliye juu mbinguni. Ni Mungu huyu huyu ataendelea kukupa majibu ya kila hitaji lako la maisha yako ya sasa na kwa siku za usoni. Hivyo usichoke kumwomba na kuendelea kuwasaidia wenye uhitaji." Ipanga akasema, "Ninashukuru sana na pia ahsante kwa kuendelea kunishauri katika mambo yanayonitatiza." Kasuku akasema, "Usijali Ipanga, moyo wako pamoja na wema wako ndivyo vinapaswa kushukuriwa kwani

vinampendeza Mungu. Nikuache upumzike, kwa heri na sasa hutaniona tena." Wakati Ipanga anataka kusema neno, kasuku hakujali tena bali alipaa na kupotelelea darini.

Kesho yake Ipanga aliamka na kuelekea ofisini kwake na baada ya kumaliza shughuli zake alielekea ofisini kwa Masha kisha akamwambia kuwa amebadilisha mawazo. Baada ya chakula cha mchana ataelekea nyumbani kwa baba yake akamsikilize Kuchi anachomitia. Masha hakuwa na pingamizi isipokuwa alimtaka awe makini. Kweli, baada ya chakula cha mchana, Ipanga alipanda gari lake na kuelekea nyumbani kwao. Alipofika alibisha hodi na kuingia ndani na kumkuta Kuchi kalazwa kwenye mkeka, sebuleni. Kuchi alimkaribisha Ipanga na kuanza kuzungumza, "Ipanga mwanangu, kwanza ninaomba unisamehe kwa kukupotezea muda wako." Ipanga akajibu, "Hakuna shaka kabisa." Kuchi akaendelea, "Ninajuta sana kwa mambo mengi ya ajabu niliyowafanyia wewe pamoja na wazazi wako ukiachilia mbali wana jamii." Ipanga alipigwa na butwaa wakati huo Kuchi akionesha kutetemeka huku akijifuta kwa kutumia kanga jasho jembamba lililokuwa likimtoka wakati wote toka Ipanga

alipofika. Kuchi akaendelea, “Nimekusingizia mambo mengi sana yakiwemo kuvuta bangi, wizi, utoro shuleni, n.k. Mbali na hayo, mimi kama kiongozi pamoja na wadogo zangu tumekuwa tukitumia dawa za kila aina ili kukuharibia maisha. Lakini haikuishia hapo tu, tulijitahidi kukuroga kadri tuwezavyo kwa lengo la kukupeleka kuzimu ukatufanyie kazi mbalimbali za huko.” Ipanga aliendelea kumsikiliza Kuchi kwa makini sana huku akiendelea kutuliza hasira aliyokuwa nayo baada ya kusikia mambo mazito aliyokuwa akifanyiwa na Kuchi.

Kuchi akaendelea kueleza, “Mwanangu Ipanga, mimi pamoja na wadogo zangu tunaomba sana utusamehe na hadi sasa tumepata madhara makubwa sana kwa kutaka kuharibu maisha yako.” Ipanga akamwuliza sengi yake Kuchi, “Kwa nini mlinichukia kiasi hicho? Ni kitu gani kilisababisha mpaka mkawa na chuki nami kiasi hicho?” Kuchi akajibu, “Ipanga mwanangu, kwanza chuki ilihamia kwako baada ya kushindwa kutimiza mambo yetu ya kichawi kwa familia yako hasa mama yako. Tuliona wazazi wako watafaidi sana kwani wewe utakuwa msaada mkubwa sana kwao kama ilivyo sasa. Pili tulikuchukia kwa sababu

toka mwanzo tulishindwa kukupeleka kuzimu." Ipanga akauliza, "Wazazi wangu hasa baba alikuwa na kosa gani kwenu ukizingatia kuwa aliwasaidia sana katika maisha yenu na hadi sasa mnaishi kwenye nyumba yake?" Kuchi akajibu, "Mwanangu Ipanga, ninakwambia kuwa ni roho mbaya tu niliyokuwa nayo. Na hiyo roho mbaya niliwaambukiza wadogo zangu pia." Ipanga akauliza, "Kwa hiyo wadogo zako nao ni wachawi?" Kuchi akajibu, "Nikwambie tu mwanangu. Kwetu hakukuwa na uchawi ila nilikuwa nachukia sana maendeleo ya ndugu zangu hasa baba yako. Ingawa alikuwa akitusaidia sana kimaisha lakini mimi nilikuwa namchukia tu kwa mali alizokuwa nazo pamoja na heshima aliyokuwa anapewa na ndugu zetu wengine. Ninasema alikuwa akitusaidia kwani robo tatu ya hao ndugu na marafiki unaowaona walisaidiwa na baba yako na ndio maana wale walio hai hadi leo wanampenda na kumheshimu sana baba yako. Nilitafuta kila aina ya dawa ili kumshusha baba yako kiuchumi na kuivuruga familia yake ikiwemo kuwaua ndugu zako na baba zako wengine ili mimi niwe na sauti katika maamuzi ya ukoo. Hali hiyo ya kuomba omba dawa ili nimharibie baba yako ndio ilipelekea nikakutana na rafiki mmoja ingawa

mwanzoni sikujua kama alikuwa mchawi. Akawa rafiki yangu mkubwa huku nami nikiendelea kumwomba anisaidie niivuruge familia ya baba yako. Hatimaye aliniambia kuwa nafasi pekee iliyobaki ya kuivuruga familia ya baba yako ni kupata nguvu za ziada. Aliponiambia hivyo sikutaka hata kujua mambo mengi nikamwambia nipo tayari na taratibu akaanza kunifundisha uchawi na kuwa mchawi kamili."

Kuchi akaendelea kusimulia, "Sikuishia hapo. Niliwafundisha pia na wadogo zangu kwani mara nyingi walikuwa wakifuata kila ninachosema ama kuamua. Tulifanikiwa hadi kuvunja ndoa zetu na kurudi kukaa tena hapa kwa baba yako kama tulivyo hivi sasa." Ipanga akamwuliza Kuchi, "Kwa nini hasa mliamua kuvunja ndoa zenu?" Kuchi akajibu, "Tuliamua kufanya hivyo ili kuwa huru kwa mambo yetu ya kichawi. Tuliona tukiendelea kukaa katika ndoa zetu tunaweza kugundulika tabia zetu hizo ovu. Na pia tulitaka ukuu katika maamuzi hasa ya kifamilia ndiyo maana tukaamua kuvunja ndoa kila mmoja kwa wakati wake." Ipanga akauliza, "Kitu gani kimesababisha uniite?" Kuchi akajibu, "Kama unavyoniona sasa, nimekuwa kipofu, nimekuwa kiwete na mikono

yote inakufa ganzi mara kwa mara kutokana na ubishi wangu wa kukufuatilia wewe pamoja na familia yako kwani ninyi ni miongoni mwa wale wenye maombi ya kweli na yenye kumpendeza Mungu. Mimi, nikiwa kiongozi wa wadogo zangu, tumeua watu wengi sana wasio na idadi kwa kutumia mbinu mbalimbali za magonjwa na ajali huku tukiwa mstari wa mbele kuwalaghai watu kuwa ni mapenzi ya Mungu. Tumevuruga familia nyingi sana zisizo idadi kwa kuwafanya watu kuwa wehu, vichaa, walevi wa pombe, bangi na madawa mbalimbali ya kulevya. Tumevunja ndoa nyingi zisizohesabika za rika mbalimbali na kusababisha uhasama wa hali ya juu sana kwa wanandoa ikiwemo utelekezaji wa watoto na mengine mengi. Tumewaongopea sana watu mbalimbali kwa lengo la kuwavuruga ama kuharibu uhusiano wao."

Kuchi alisimamisha kidogo maongezi huku akiinua kichwa mithili ya mtu anayetazama juu ya paa la nyumba kisha akataka kuendelea. Kabla hajaendelea Ipanga akamwuliza, "mlikuwa mnafaidika na nini kwa kufanya yote hayo?" Kuchi akajibu, "kibinadamu hakuna faida yoyote ile zaidi ya kusikia raha kuona mtu ama watu wanahangaika, kupata shida na kukosa amani

kutokana na kile tulichowafanyia. Wakati mwingine tulikuwa mstari wa mbele kwenda kutoa ushauri mbovu ili wazidi kuharibikiwa zaidi na zaidi. Ipanga mwanangu, ninasema haya yote kwa kuwa sasa ni muda wa kupata adhabu tena kali kutoka kwa Mungu. Mimi hapa sijiwezi ninasubiri kifo tu. Wenzangu pia hawajiwezi kwani kila mmoja ana maumivu yake tena makali yanayomtesa kwa sasa. Nikuombe sana msamaha na pia kwa niaba ya wadogo zangu kwani kama unavyoona hawawezi hata kuzungumza."

Kibinadamu, moyo wa huruma ulimwingia Ipanga, akaamua kumwuliza Kuchi, "Imekuwaje mmeugua kiasi hiki na kusababisha wote mmekuwa vipofu na wenzako wamekuwa bubu? Na je, mmekwisha kwenda hospitali kutibiwa?" Kuchi akajibu, "Mwanangu Ipanga, mara ya mwisho tulifuatilia maendeleo yako kimaisha na kuona jumba kubwa la ofisi yako na mwenzako Masha. Tukaona jinsi ofisi yenu inavyolisha watu wa mataifa mbalimbali. Tukaona nyumba na gari vyote vya kifahari ulivyonavyo. Tukaona jinsi ulivyowajengea wazazi wako kijijini na maisha mazuri wanayoyaishi. Tukaona jinsi unavyosaidia watu wenye uhitaji wakiwemo wanafunzi, vijana

na wazee mijini na vijijini. Tulishikwa na hasira na kuamua kutafuta dawa ili tukutoe kabisa duniani, nikiwa na maana kukuua moja kwa moja. Baada ya kukamilisha mipango yetu yote, siku iliyofuata ndiyo ilikuwa siku ya kukuua. Tulijiandaa kama ambavyo huwa tunafanya na ilipofika usiku wa manane tukaruka kukufuata, lakini tulipofika mlangoni kwako, ulikuja mwanga mkali sana kutoka juu ambao toka tuzaliwe tulikuwa hatujawahi kuuona. Wote watatu tuliinua macho juu ili kuutazama na hapo hapo tukapata upofu. Mimi nilipata opofu wa jicho moja na tukakosa mwelekeo kisha tukajigonga kwenye miti na kuanguka chini."

Kuchi akaendelea kusimulia, "Wakati tukiwa chini tusijue la kufanya walitokea wachawi wenzetu na kutunyanyua, wakatubeba na kutufikisha nyumbani kisha wakaondoka. Tokea hapo sisi wote tunaumwa sana kama nilivyokueleza hapo awali. Kuanzia kiunoni hadi miguuni sijiwezi lakini mbaya zaidi wenzangu miguu yao yote inawaka moto kama wako kwenye tanuru na kwa sasa wamekuwa mabubu kabisa. Hicho ndicho kilichotukuta mwanangu. Siwezi kusema kuwa kuna dawa tunaweza kuitumia ili

tupone, tuliyoyafanya kwa binadamu wenzetu hasa kwako wewe na wazazi wako ni mengi na sasa tunasubiri kifo tu. Hii ndio sababu ya kukuomba msamaha na pia kuwaombea wenzangu ambao hawawezi hata kutoa sauti." Muda wote huo, Ipanga alikuwa akimsikiliza Kuchi kwa makini sana huku amejishika tama la kulia. Kuchi akaendelea, "Tafadhali nikuombe kitu mwanangu, endelea kuwa na moyo huo huo kwani Mungu atakuzidishia zaidi na zaidi na uwe na uzao mwema na wenye baraka tele kwani kwa Mungu hakuna lililo gumu kwake. Nami pamoja na wenzangu tunakiri kabisa kuwa Mungu ndiye mweza wa yote kwani pamoja na elimu yangu yote ya kichawi na vyeo nilivyokuwa navyo lakini nilishindwa kabisa kuwadhuru watu wa Mungu kwa namna yoyote ile." Baadaye Kuchi alinyamaza kuashiria kuishiwa maneno huku akisubiri kusikia kauli Ipanga.

Ipanga akamwambia, "Mimi sina zaidi la kusema isipokuwa, nitamke kuwa nimewasamehe kwa yote na Mungu azidi kuwasimamia." Kuchi kusikia hivyo alifurahi sana na kusema, "Mwanangu Ipanga, mimi pamoja na wenzangu tunashukuru sana kwa kutusamehe. Pia

ninakuomba utufikishie maombi ya msamaha kwa wazazi wako. Hali zetu ni mbaya sana na hatuna msaada wowote ule kwani kila mmoja katika jamii ikiwemo ndugu zetu wengine ambao wewe hutaweza kuwafahamu wanatuogopa kutokana na tabia zetu mbaya tulizokuwa nazo." Ipanga aliendelea kumsikiliza kwa makini Kuchi. Kuchi alihitimisha kwa kusema, "Mwanangu Ipanga, ninajua una majukumu na inabidi nikuruhusu uende, isipokuwa ninaomba nikueleze maneno yangu ya mwisho, ninajua mimi na wenzangu tutakufa. Siku tukifa nina hakika utapata taarifa kwani msiba haufichwi. Ninakuomba hata kama hutahudhuria mazishi yetu, njoo mara moja msibani na yeyote yule atakayesimamia mazishi yetu awe wa kiume ama wa kike, awe mwanafamilia ama mwanamtaa, mwambie tuzikwe bila kufunikwa nguo zetu. Kama tutafunikwa basi tufunikwe nguo mpya ambazo zitanunuliwa kwa ajili hiyo. Lakini hizi nguo zetu tulizonazo pamoja na vitu vyetu vyote naomba umsisitize sana vichomwe moto. Vichomwe moto kwa sababu hatutaki mtu yeyote yule aambukizwe wala kujifunza tabia hii ya kichawi kwani ni laana kutoka kwa Mungu na kitu alichokilaani Mungu utakifanya kwa muda tu na mwisho wake ni aibu

na kudhalilika mbele ya jamii inayokuzunguka. Nasisitiza tena Ipanga, kila kitu kichomwe moto kiteketee kabisa. Umenielewa vizuri Ipanga?"

Ipanga akajibu, "Ndiyo nimekuelewa." Kuchi akamalizia, "Basi sasa nikuache uende kwenye shughuli zako. Kila la heri na maisha mema kwako, familia yako utakayoipata na kwa wazazi wako. Wala usihangaike nasi wala kuumiza kichwa juu ya ugonjwa wetu kwani tunapata tulichostahili kukipata." Ipanga akasema, "Sawa nimekuelewa na ahsante sana. Uwe na jioni njema." Baada ya mazungumzo hayo, Ipanga alinyanyuka na kuondoka kuelekea nyumbani kwake kwani tayari giza lilikuwa limeanza kutanda. Akiwa njiani kuelekea nyumbani kwake, aliwaza sana hali ya Kuchi na wadogo zake jinsi ambavyo wanaishi bila msaada wowote ule kutoka kwa ndugu wengine wa karibu wala jamii inayowazunguka. Hasira zake zote juu ya Kuchi na wadogo zake ziliisha ghafla akaanza kuingiwa na huzuni. Alipofika nyumbani kwake na kumaliza shughuli zake zote alimpigia simu baba yake na kumwomba aweke mlio mkubwa kwenye simu ili azungumze nao kuwafahamisha maneno aliyoelezwa na Kuchi yakiambatana na msamaha aliouomba kwake na

kwao. Baada ya Ipanga kuwaeleza yote, wote walisikitika sana na kusababisha baba yake kusema, “Sikujua kuwa maisha yangu yote nilikuwa ninawasaidia mashetani waliokuwa wananiangamiza mimi na familia yangu. Kesho nitakuja kuwafukuza kwenye nyumba yangu na wala sitajali wataelekea wapi.” Mama Ipanga akamwambia mume wake, “Hapana mume wangu, usifanye hivyo kwani hao bado ni ndugu zako. Kikubwa wameomba msamaha na kukiri makosa yao.” Mzee Ipanga akakataa, “Hapana, hao ni mashetani kabisa na wala hawastahili kuendelea kuishi kwenye nyumba yangu. Wamenifanya mimi na familia yangu tuishi kwa mateso sana, ugomvi na kila aina ya ghasia humu ndani kumbe chanzo ni wao.”

Mzee Utulivu aliendelea kusema, “Waliyoyafanya yanatosha na ninasema, yatosha. Waende kuishi kwa hao wachawi wenzao ila kwenye nyumba yangu sitaki kuona mtu hata mmoja. Ipanga unanisikia, kesho asubuhi kabla hujaenda kazini kwako, pita kwa hao mashetani na uwaambie kuwa mimi nitafika mchana ila kwa usalama wao, sitaki kukuta chochote kile kinachowahusu ikiwemo wao wenyewe kwenye

nyumba yangu, unanielewa vizuri?" Ipanga akamjibu, "Baba nimekuelewa vizuri lakini ninaomba tuwape kwanza muda kwani hali yao sio nzuri kabisa kiafya na kiuchumi. Mazingira niliyoyaona hapo hata chakula ninadhani ni shida kukipata." Mzee Ipanga akasema, "Hayo yote mimi siyajali kabisa na wala hayaniumizi kichwa, isipokuwa cha msingi kesho mchana sitaki kuwakuta kwenye nyumba yangu pamoja na kila kitu kinachowahusu." Baada ya kuona mume wake amejaa jazba ikabidi Mama Ipanga aanze kumtuliza kwa kusema, "Mume wangu, tatizo limekwisha na tayari wamekiri na kuomba msamaha na kikubwa zaidi wamethibitisha wamekwisha achana na uchawi, nikiwa na maana kuwa hawatatusumbua tena kichawi maisha yetu yote."

Ipanga nae aliendelea kumsihi baba yake, "Baba, anachosema mama kipo sahihi kuwa kwa sasa hawataweza kutusumbua tena kichawi. Wengine wamepata upofu ukiachilia mbali baadhi ya viungo vyao vya mwili kupooza, hawawezi hata kuona." Mama Ipanga akadakia na kusema, "Mume wangu, msikilize kijana wetu anavyosema. Hebu tuwape muda kidogo wa kufanya maandalizi

kisha watatoka." Mzee Utulivu akasema, "Sawa nimewaelewa, lakini Ipanga, ukipata muda kesho, ninaomba upite huko ukawape taarifa hii, kuwa ujumbe wao tumeusikia ila na sisi ujumbe wetu kwao ni kwamba tumewapa siku saba kuanzia hiyo kesho. Baada ya hizo siku nikute vyumba ni vyeupe nikimaanisha nisiwakute hata kwenye mazingira ya hapo nyumbani." Ipanga akaitikia, "Sawa baba nimekuelewa na ninaomba niwatakie usiku mwema." Ipanga alikata simu kisha akalala kwa ajili ya ratiba ya kesho yake. Kesho yake asubuhi alijiandaa kuelekea kazini kwake akiwa na ratiba ya kwamba baadaye atakwenda kununua chakula awapelekee Kuchi na wenzake kwa sababu hali aliyowaacha nayo jana yake haikumridhisha. Vile vile alitaka akamshawishi Kuchi ili awapeleke hospitali wakachunguzwe zaidi.

Alipofika kazini akapigiwa simu na Kuchi. Mara tu alipopokea simu, akasikia sauti ya mtu mwingine wa kiume ikimtaka afike haraka pale nyumbani. Hata kabla hajamsimulia rafiki yake Masha kilichojiri juu ya mazungumzo baina yake na Kuchi, alimuaga tena kuwa kapigiwa simu na anahitajika huko nyumbani mara moja. Masha aliomba waongozane ili kujua ni kwa nini ameitwa

ghafla namna hiyo. Wakiwa njiani kuelekea nyumbani kwa baba yake kuitikia wito, akaanza kumsimulia Masha mwanzo hadi mwisho na hasira za baba yake. Masha alishangaa sana kisha akamwambia Ipanga, “Hali hiyo unaionaje ndugu yangu! Ninaona kama Mungu ameamua kukufunulia kitu juu ya ubaya wao wote kwako pamoja na familia kwa ujumla.” Ipanga akasema, “Huwezi kuamini ndugu yangu, nilikuwa nina hasira nao sana hasa huyo Kuchi. Lakini ghafla jana hasira zangu ziliisha, nikaanza kuwahurumia maisha duni na ya dhiki wanayoishi. Ninamaanisha wamechoka kweli kweli. Wewe mwenyewe utajionea tutakapofika.” Masha akasema, “Kweli, sasa wanahitaji msaada wako na ninafurahi kusikia kuwa umeachilia mbali yale yote yaliyokuumiza dhidi yao.” Waliendelea kuongea na hatimaye wakajikuta wamefika.

Walipofika waliwakuta baadhi ya watu wamesimama nje ya nyumba huku wakizungumza katika makundi makundi. Miongoni mwa wale watu, Ipanga alimfahamu mmoja wao kwani ni jirani na ndiye alimpigia simu. Jirani alipomwona Ipanga akawakaribisha, “Karibuni huku Ipanga.” Ipanga akajibu, “Ahsante sana baba Jitu.

Shikamoo!" Jirani akaitikia, "Marhaba Ipanga, karibuni." Masha naye akamsalimia jirani kisha jirani akawasogeza pembeni kidogo ya watu kisha akawaambia, "Ipanga, tumepatwa na matatizo hapa, Kuchi na ndugu zake wamefariki ingawa haijajulikana ni muda gani hasa. Wamefariki usiku. Asubuhi ndio tumepata taarifa baada ya jirani mwenzetu ambaye huwa anawajulia hali kabla ya kwenda kazini kuona kimya tofauti na siku zote. Ilibidi aingie ndani, ndio akakutana na hali hiyo. Alituita tukaingia ndani lakini kibaya zaidi tukakuta wote watatu wamefariki. Ndiyo maana tukaona tukupigie uje ili uwafahamishe pia ndugu zako wengine hasa baba yako."

Ipanga na Masha walipigwa na butwaa kusikia hivyo ingawa dalili za watu kusimama makundi makundi hapo nyumbani kuliwafanya wahisi kitu. Masha akamshauri Ipanga kuwa kabla ya kufanya chochote kile, wamfahamishe baba yao. Ipanga alitoa simu yake mfukoni kisha akampigia baba yake, "Shikamoo baba, huku siyo kwema, kuna taarifa mbaya." Mzee Utulivu akauliza kwa mshtuko, "Kipi kimekupata mwanangu?" Siyo mimi baba, ila Kuchi na wadogo zake wote wamekutwa wamekufa na hapa niko na Masha

pamoja na majirani hapa nyumbani." Mzee Utulivu akadakia, "Mwanangu, hata sasa ninavumilia sana maumivu niliyoyapata kutokana na hayo waliyonifanyia. Hasira nilizonazo juu yao ninaweza kujikuta naichapa viboko hiyo miili yao. Kwa ufupi tu, sitaki kujihusisha, wala sitajihusisha na chochote kile juu yao. Hivyo kama ndugu wengine watapatikana endeleeni na utaratibu na wakikosekana kabisa basi serikali itawazika."

Baada ya mzee Utulivu kumjibu kijana wake alimtakia wakati mwema kisha akakata simu. Ipanga alichoka kabisa kusikia majibu hayo kutoka kwa baba yake. Ikabidi ampigie mama yake pia, "Shikamoo mama!" Mama yake akaitikia, "Marhaba mwanangu, habari za huko?" Ipanga akajibu, "Mama, huku siyo kwema kwani kuna msiba. Kuchi na wadogo zake wamefariki usiku wa kuamkia leo." Mama akasema kwa huzuni, "Poleni sana mwanangu! Baba yako umekwishampa taarifa hii?" Ipanga akajibu, "Ndiyo mama, ila kasema hataki kusikia chochote kuwahusu na hataweza kufika msibani." Mama akadakia, "Kweli! Kwa matendo waliyotutendea inatia hasira sana. Hata hivyo binadamu tumeumbwa kusamehe, angesamehe tu." Ipanga akasema, "Mama, tangu

nimfahamu baba, sijawahi kumsikia amekasirika kama alivyokasirika jana na leo. Hivyo suala la kusamehe kwake sio la leo. Bado ninafikiri nifanyeje na sijapata suluhisho. Kibaya zaidi ni kwamba miili yao wote bado imo ndani na majirani wananiangalia mimi zaidi. Nipo hapa na Masha ila Masha hawamjui." Mama akauliza, "Kwani baba yako kahitimishaje?" Ipanga akajibu, "Kasema hivi: wakipatikana ndugu wengine washughulike na mazishi ila ndugu wakikosekana basi wazikwe na serikali." Mama akatoa ushauri, "fanya hivi mwanangu, shauriana na Masha na majirani waliopo hapo mkaihifadhi miili yao hospitali ili tuone kama baba yako anaweza kubadilisha mawazo, akaja huko. Ninajua nikifika nyumbani ataniambia habari hizi nami nitajaribu kumsihi nije naye tuwazike ndugu zake." Ipanga akasema, "Sawa mama, nimekuelewa. Ngoja tulishughulikie hili ila jioni nitawapigia simu tena." Mama akaitikia na kushauri, "Sawa mwanangu, kila la kheri na muwe makini." Ipanga akasema, "Ahsante sana mama."

Ipanga alimshikirisha Masha majibu ya baba yake pamoja na mama yake na hatimaye wakakubaliana kutafuta gari lingine ili ipakie miili

hiyo na kuipeleka hospitali mahali wanapohifadhia maiti huku wakisaidiana na baadhi ya majirani. Baada ya kukamilisha walirudi nyumbani na kuwafahamisha majirani kuwa wanaweza kuendelea na majukumu yao na kwamba wangekutana tena jioni wakiwa wamekwisha pata mwafaka kutoka kwa ndugu wengine kwani wao ni wadogo na hawana maamuzi yoyote juu ya utaratibu wa mazishi. Majirani walitawanyika kisha Ipanga na Masha wakarejea ofisini kwako. Ilipofika jioni Ipanga alimpigia tena simu mama yake ili apate kujua mwafaka uliopatikana kati yake na baba yake. Mama akajibu, "Mwanangu, baba yako amesema kuwa hataki kabisa kusikia habari zozote zile kuhusu hao dada zake na wala hatapoteza muda wake kufika huko. Baada ya hayo majibu yake, mimi pia ninaona haina maana kuja huko bila baba yako kuwepo. Ninachoweza kushauri, yoyote yatakayo jadiliwa yafanyieni kazi ili kusaidia kuwastiri." Ipanga akasema, "Sawa mama, nimekuelewa."

Ipanga na Masha wakiongozana na baadhi ya wafanyakazi wao walielekea pale msibani na walipofika waliwakuta baadhi ya majirani wamekaa. Jirani mmoja akasema, "Ipanga, karibu

tupo huku.” Ipanga akamjibu, “Ahsante, tunakuja.” Ipanga alisalimiana na wageni mbalimbali waliokuwa wamefika hapo kisha akaelekea kwa yule jirani aliyemwita. Wakati huo Masha na wafanyakazi wao walianza kuandaa utaratibu kwa ajili ya chakula cha usiku. Jirani akauliza, “Ipanga, mzee hapa unamfahamu?” Ipanga akajibu, “Hapana!Kwa kweli simfahamu.” Jirani akasema, “Amesema anaitwa Mzee Kisosi.” Ipanga akaangalia juu kisha akasema, “Kweli kabisa!Jina hili niliwahi kulisikia kwa baba kipindi cha nyuma akizungumza kuhusu ng’ombe waliokuwa porini.” Mzee Kisosi akakubaliana naye, “Kweli kabisa na wala hujakosea. Niko porini huko. Ninajihusisha na ufugaji wa ng’ombe na pia nina ng’ombe wengi wa baba yako. Nilikuja huku mjini jana, baada ya kukamilisha mambo yangu nikaona nipite kuwasalimia hawa ndugu zetu, nikakutana na taarifa hizi za kuhuzunisha.” Ipanga akasema, “Ndio hivyo, ninadhani umekwishaelezwa jinsi ilivyokuwa.” Mzee Kisosi akajibu, “Ndiyo, nimeelezwa kila kitu. Sasa utaratibu uliopo ni upi?” Ipanga akajibu, “Hapo kwenye utaratibu, labda nikusikilize wewe kwani mimi sijui chochote.” Mzee Kisosi akauliza, “Umekwisha mpigia baba yako na anasemaje?” Ipanga akajibu, “Baba

hakunipa majibu mazuri, labda nimpigie uongee naye." Mzee Kisosi akasema, "Sawa, mpigie niongee naye."

Ipanga alimpigia simu baba yake kisha akampatia Mzee Kisosi wakaanza kuongea. Baada ya maongezi marefu kidogo, Mzee Kisosi akamwambia Ipanga kuwa baba yake hataweza kufika na ikiwezekana waendelee na taratibu za mazishi. Pia akamwambia, "Ipanga, wewe ni mtoto wa ndugu yangu. Sikufahamu vizuri zaidi ya hapa ninapokuona na ninazungumza mbele ya hawa majirani zako kuwa, maisha yetu ni kama santuri inayorekodi muziki. Ukiwa unarekodi mziki, hata sindano ya kushonea nguo ikidondoka chini kwenye sakafu ni lazima mlio wake wa kudondoka utasikika kwenye santuri. Ninasema hivi nikiwa na maana kwamba, unapokuwa hapa duniani kila unachokitenda kiwe cha wema ama uovu kinajirekodi kwenye jamii. Kumbuka kuwa hii jamii inayotuzunguka ndiyo santuri yenyewe inayoturekodi. Katika maisha yako ukitenda mema, jamii itakupenda sana na muda wote itakuwa nawe katika shida ama raha. Lakini ukitenda maovu, jamii hiyo hiyo itajitenga nawe na kukususia kabisa katika maisha yako yote."

Mzee Kisosi akaendelea, “Pia kumbuka, ukiwa unatenda mema katika jamii utapendwa na watu wema pamoja na watu waovu. Ila ukiwa unatenda maovu kwenye jamii utapendwa na watu waovu tu tena nao wakati mwingine watajitenga nawe kwani siku zote watu waovu ni wanafiki. Husubiri watu wema wakupende ili nao wajifanye kukupenda. Leo hii hawa ndugu zetu walikuwa na sifa mbaya yaani ya uovu kwenye jamii. Ndio maana watu wengi walio wema hawapo hapa kwani walikwishajitenga nao. Wewe mwenyewe ni shuhuda jinsi walivyokuwa wanaishi hapa bila ndugu zao utadhani wao ni yatima. Ndugu walio wengi waliwakimbia kutokana na tabia zao mbovu na hata jamii ililitambua hilo. Lakini unadhani walikuwa hawana ndugu, jamaa na marafiki wenye tabia ovu kama za kwao? Wapo ila yawezekana hawapo hapa kwa ajili ya unafiki wao kama nilivyokueleza hapo awali. Nisiwe msemaji sana ila kama kuna uwezekano, kesho tufanye mazishi ili kesho kutwa kila mmoja aendelee na taratibu zake.”

Ipanga na wale waliokuwepo waliona hasia kali kutoka kwa Mzee Kisosi juu ya mambo maovu yaliyotendwa na Kuchi pamoja na wadogo zake enzi za uhai wao. Ipanga akasema, “Sawa mzee,

kesho itabidi tuwazike." Ipanga akisaidiana na Masha, Mzee Kisosi pamoja na majirani waliratibu mazishi na kesho yake mazishi yakafanyika. Wakati wa jioni wakitoka makaburini kuwastiri, mzee Kisosi alimwambia Ipanga kuwa hakuna suala la matanga na kesho yake yeye atasafiri kurudi kuendelea na shughuli zake. Ipanga akamwambia, "Mzee, Kuchi aliniambia endapo yeye na wenzake watafariki, vitu vyao vyote vichomwe moto hadi viteketee." Mzee Kisosi akasema, "Hakuna shaka Ipanga. Ikiwezekana tafuta vijana tuwalipe pesa ili leo hii usiku wavichome. Tukiwanunulia lita ishirini za mafuta ya petroli nadhani zitawatosha kuteketeza kila kitu." Masha akadakia, "Mzee, naona inakuwa haraka sana. Jamii inaweza isituelewe vizuri."

Mzee Kisosi aliendelea, "Kijana, jamii inajua sana kuliko mimi na wewe tunavyojua. Pia maisha ya sasa siyo ya kupambapamba ama kusifiasifia mambo maovu. Kama kuna watu waovu ama jambo ovu likemee kwa nguvu zako zote, moyo wako wote na akili zako zote. Watu wengi wameharibikiwa ama familia nyingi zimeharibikiwa na kuvurugika kwa ajili ya kukumbatia na kupamba pamba mambo maovu.

Siku zote, mapepo hutolewa kwa kukemewa na si kwa ngonjera ama taarabu." Ipanga akasema, "Sawa mzee wetu. Tumekuelewa vizuri. Tutalifanyia kazi hilo ili vitu vyote visombwe vipelekwe kule uwanjani kisha vichomwe moto hadi viteketee."

Ipanga na Masha waliwaandaa vijana kwa kazi ya malipo kuvisomba vitu vyote kuvitoa ndani hadi uwanjani na kisha kuvichoma moto. Vijana waliifanya shughuli hiyo hadi usiku wa manane na kufikia kesho yake asubuhi nyumba ilibaki wazi na vitu vyote uwanjani vikabadilika kuwa majivu. Historia ya Kuchi na wadogo zake ikawa imeishia hapo. Kesho yake mchana Mzee Kisosi akaondoka kurudi kwake kuendelea na majukumu. Ipanga na Masha nao wakaondoka kuendelea na majukumu yao.

Miaka ilivyozidi kusonga mbele, Ipanga na Masha waliendelea kupangiana majukumu kila mmoja akitekeleza majukumu yake bila kuchoka tena kwa weledi mkubwa na hatimaye kufikia malengo yao. Waliendelea kujituma katika kazi yao ya kujiajiri na hatimaye wakawa matajiri wakubwa katika eneo lile. Watu waliwapenda sana na kuwaona ni vijana wa kuigwa katika jamii. Kila

mmoja alifanikiwa kuoa na kupata familia iliyo bora. Taarifa zilizidi kusambaa kijijini kwao Kitale. Watu wote wakashangaa jinsi Ipanga na Masha walivyopiga hatua kubwa kiuchumi na jinsi walivyo boresha makazi ya wazazi wao kijijini Kitale.